# Kiswahili 1

## Mwongozo wa Mwalimu

### Utohozi kwa Walimu wa Wanafunzi wenye Ulemavu wa Kuona



**Tusome Early Literacy Programme**

# Yaliyomo


Utangulizi .................... ii
Dibaji .................... ii
Maelezo .................... iii
Sauti na majina ya herufi za Kiswahili .................... iv
Mapendekezo ya mgawanyiko wa muda wa kila somo .................... v
Kamusi ya Kiswahili .................... vii
Wiki ya 1 .................... 1
Wiki ya 2 .................... 11
Wiki ya 3 .................... 22
Wiki ya 4 .................... 35
Wiki ya 5 .................... 40
Wiki ya 6 .................... 45
Wiki ya 7 .................... 50
Wiki ya 8 .................... 55
Wiki ya 9 .................... 60
Wiki ya 10 .................... 65
Wiki ya 11 .................... 70
Wiki ya 12 .................... 75
Wiki ya 13 .................... 80
Wiki ya 14 .................... 85
Wiki ya 15 .................... 90
Wiki ya 16 .................... 95
Wiki ya 17 .................... 100
Wiki ya 18 .................... 105
Wiki ya 19 .................... 110
Wiki ya 20 .................... 115
Wiki ya 21 .................... 120
Wiki ya 22 .................... 125
Wiki ya 23 .................... 130
Wiki ya 24 .................... 135
Wiki ya 25 .................... 140
Wiki ya 26 .................... 145
Wiki ya 27 .................... 150
Wiki ya 28 .................... 155
Wiki ya 29 .................... 160
Wiki ya 30 .................... 165

# Utangulizi

Tangu kupata uhuru, serikali ya Kenya imetambua elimu kama mojawapo ya haki za kimsingi za binadamu; kwa hivyo imejitolea kuwapa wananchi wake wote elimu bora. Raslimali nyingi zimewekezwa ili kuimarisha upatikanaji, umuhimu, usawa na ubora, vipengee ambavyo vimeboresha miundomsingi na kuongeza idadi ya wanaohudhuria masomo katika nyanja tofauti za elimu na mafundisho.

Serikali inatambua ya kwamba ili kuweza kushindana katika nyanja za kimataifa na kuimarika kiuchumi, taifa linahitaji elimu inayowawezesha wananchi kuwa wabunifu, kupata elimu ya kudumu maishani na wanaoweza kufanya kazi zilizo tata na zenye changamoto. Elimu pia inafaa kuwawezesha wananchi kutatua shida katika jamii, kukata shauri, kufanya kazi bila kufuatiliwa, kuwajibika na pia waweze kusoma, kupiga mambomsasa na kupata ujuzi wa kujidhihirisha. Maendeleo ya kudumu yanahitaji kila binadamu apate maarifa ya karne ya 21, ujuzi, mtazamo na maadili yanayohitajika kudumisha maisha ya siku za usoni. Mkazo unatiliwa kwenye elimu inayowezesha kusoma na kufanya hesabu. Nchi ya Kenya imefanya maendeleo katika kuhakikisha ubora wa elimu. Miradi mbalimbali imewekwa ili kuangazia ubora wa elimu katika madarasa ya chini ya shule za msingi.

Kitabu hiki cha Tusome, bila shaka, kitaimarisha masomo kuanzia darasa la 1 na la 2 ya shule za msingi kwenye somo la kujua kusoma na kuandika. Mpangilio wa masomo unahakikisha ya kwamba wanafunzi wote nchini Kenya wanaweza kusoma na kuelewa ifikapo mwisho wa mwaka. Kwa hivyo, nawahimiza washirika wetu waendelee kusaidia sekta ya elimu katika utekelezaji wa mikakati na mbinu ili kuboresha elimu.

[redacted]

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia

# Dibaji

Lengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni kutoa elimu bora kwa wanafunzi wote bila kuzingatia hali yao ya kuichumi na kijamii. Mabadiliko yamefanywa ili kuimarisha sekta ya elimu. Mabadiliko haya yana mtazamo wa kuifanya nchi ishindane kimataifa. Mipango ya utafiti kama vile Tathmini ya Kitaifa na Ufuatiliaji wa Mafanikio ya Masomo (NASMLA) na Muungano wa Kusini na Mashariki mwa Afrika wa Kufuatilia Ubora wa Elimu (SACMEQ) inaonyesha kuwa kuna umuhimu wa kuboresha mafanikio katika uwezo wa kusoma na kufanya hesabu.

Maendeleo yaliyofanyika hivi karibuni katika nchi ya Kenya yalionyesha kuwa kuna haja zaidi ya kuwa na mfumo wenye kina wa kuhakikisha ubora wa elimu. Mabadiliko haya yamo katika Katiba ya Kenya (2010) na Ruwaza ya Kenya ya 2030. Katiba ya Kenya inahakikishia kila mtoto nchini masomo ya msingi yasiyo na malipo. Vilevile, Ruwaza ya Kenya ya 2030 inatarajia kuhakikisha kuwa kuna mabadiliko ya kimaendeleo nchini na pia ushindani katika nyanja za kimataifa ifikapo mwaka wa 2030. Kati ya matarajio ni kutoa elimu bora na mafundisho ili kuhakikisha wanafunzi wanapata ujuzi wa hali ya juu. Mfumo uwe wa kupatia wanafunzi ujuzi wa kazi utakaounganisha nchi na soko la kimataifa. Nakala ya Kikao Cha Bunge Nambari 14 ya 2012 inaonyesha njia mwafaka na wanafunzi asilimia mia moja waweze kukamilisha masomo katika elimu ya msingi bila kuathiri ubora wa elimu.

Wizara ya elimu inatazamia kuboresha elimu katika madarasa ya chini ya shule za msingi hasa ikizingatia uwezo wa kusoma na kuandika na kufanya hesabu. Mradi wa Kitaifa wa Tusome unaodhaminiwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Amerika (USAID) na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID), unakusudia kuboresha matokeo ya kuweza kusoma na kuandika katika madarasa ya 1 na ya 2. Mradi huu unalenga kuboresha uwezo wa walimu wa kuelekeza darasani, kuhakikisha wanafunzi wamepata vitabu sahihi vya kusoma na vya ziada, na kuwaelekeza walimu kupitia kwa wakufunzi wa mashauri ya walimu (TAC Tutors) na walimu wakuu. Halikadhalika, utaanzisha njia mwafaka za kufuatilia na kutathmini matokeo ambayo itaunganisha mafunzo na matokeo katika kujifunza kusoma na kuandika. Mradi huu utatumia teknolojia ili kuimarisha mafunzo ya kujua kusoma na kuandika na kuongeza uwezo wa sekta ya elimu kuboresha matokeo ya masomo.

Kwa niaba ya Wizara ya Elimu, ninawasihi washikadau wote kushirikiana ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi wa Tusome umefua dafu.

[redacted]

Katibu Mkuu,

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia: Idara ya Elimu

# Maelezo

Mpangilio wa masomo katika hiki kitabu cha mwalimu uliandikwa ukizingatia mwongozo shupavu wa washauri wa kusoma na lugha kutoka hapa nchini Kenya na kimataifa. Katika warsha ya kwanza maafisa kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST) na Taasisi ya Maandalizi ya Mitaala (KICD), walisimamia uandishi wa mwongozo wa masomo ambao umekuwa kielelezo cha mpangilio wa masomo hayo. Mwongozo huo unaeleza kwa kina vipengele vyote vinavyostahili kuwekwa kwenye mpangilio wa masomo haya. Katika warsha hiyo, uamuzi ulifanywa kuhusu jinsi herufi za lugha ya Kiswahili na Kiingereza zitakavyofunzwa na mbinu zitakazotumika kufundisha watoto jinsi ya kusoma.

Mpangilio wa lugha ya Kiswahili unazingatia sauti za herufi zinazotumika mara nyingi katika lugha hiyo. Kwa hivyo herufi zinazotumika mara nyingi hufundishwa kwanza ili kuwawezesha wanafunzi kuanza kusoma maneno na sentensi kwa muda wa wiki mbili hivi. Hadithi pia zimeandikwa kwa makini zikizingatia sauti za herufi ambazo wanafunzi wamesoma tayari. Hadithi hizi pia zinazingatia mada za silabasi ya Taasisi ya Maandalizi ya Mitaala (KICD) pamoja na msamiati wa kiwango cha mwanafunzi ili waweze kusoma na kuelewa maneno na hadithi.

Kila mpangilio wa somo una mbinu mbalimbali zinazotoa mwelekeo wa kipekee wa kufunza kusoma kwa lugha ya Kiswahili. Mbinu hizi pia zinazingatia vipengele vinne vya lugha (kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika). Pia zinafunza waziwazi na kwa mfululizo maalum unaozingatia vipengele vitano muhimu vya kusoma: Utambuzi wa fonimu, utambuzi wa herufi, utambuzi wa maneno, kusoma kwa mtiririko unaozingatia shada na kiimbo na kusoma kwa ufasaha na kuelewa unachokisoma. Vipengele hivi vinazingatia mambo yote muhimu kwa kumsaidia mwanafunzi apate ujuzi wa kujua kusoma mapema.

Mpangilio huu pia unasisitiza wazo kuu kwamba maneno huundwa kwa sauti, na kila herufi ina sauti na sauti hizi zinapounganishwa huunda neno. Wazo lingine ni kuwa maneno yana maana. Maneno yanapounganishwa hutengeneza sentensi, na sentensi huunda taarifa ama hadithi. Kila siku wanafunzi hufanya mazoezi ya herufi, maneno, kusoma hadithi na ufahamu. Siku ya tano ya kila wiki, huwa ya marudio na mazoezi ili walimu waweze kutathmini jinsi wanafunzi wanavyoendelea katika masomo yao.

Kila kipengele kinafunzwa kwa kuzingatia hatua tatu maalum: Ninafanya – Tunafanya– Unafanya. Kwenye hatua ya kwanza (Ninafanya), mwalimu anatoa maelezo na kielelezo cha kipengele kinachofunzwa. Kwenye hatua ya pili (Tunafanya), mwalimu anawahusisha wanafunzi kufanya mazoezi ya kipengele hicho pamoja naye. Kwenye hatua ya tatu (Unafanya), mwanafunzi anapewa nafasi kufanya mazoezi ya kile ambacho amejifunza. Mwanafunzi ataweza kuhusisha yale ambayo amesoma katika maisha yake ya kila siku. Upimaji wa uelewa wa mwanafunzi umepewa kipaumbele kwenye mpangilio huu, kwani unafanyika katika kila kipengele, kila siku, kila juma na kila muhula.

Tunawashauri walimu wajitayarishe kabla ya somo. Ni vyema kutambua msamiati unaoweza kuwatatiza wanafunzi na kutumia kamusi ili kupata maelezo na maana halisi ya maneno.

# Sauti na Majina ya Herufi za Kiswahili

| Herufi | Jina |
|---|---|
| m | Ma |
| a | A |
| u | U |
| k | Ka |
| t | Ta |
| l | La |
| n | Na |
| o | Oo |
| w | Wa |
| e | Ee |
| i | Ii |
| h | Ha |
| s | sa |
| b | ba |
| y | ya |
| z | Za |
| g | Ga |
| d | Da |
| j | Ja |
| r | ra |
| f | Fa |
| v | Va |
| sh | Sha |
| ny | Nya |
| dh | Dha |
| th | Tha |
| ch | Cha |
| gh | Gha |
| ng’ | ng’a |
| ng | Nga |

Mwalimu aeleze matamshi ya herufi alizopewa

# Mapendekezo ya mgawanyiko wa muda wa kila somo

# (Mwaka wa 1, Wiki ya 1-21)

| **Sehemu** | **Siku ya 1 na 3** | **Siku ya 2 na 4** | **Siku ya 5** | **Wiki ya 11 na 21 (Kila siku)** |
|---|---|---|---|---|
| Ufahamu wa fonimu | 3 | | | |
| Ufahamu wa Herufi | 3 | 3 | 3 | 3 |
| Silabi | 3 | 3 | | |
| Kusoma maneno kwa silabi | 4 | | | |
| Kusoma maneno marefu | | 4 | | |
| Sarufi | | 4 | 4 | 4 |
| Jedwali la silabi | | | 5 | 5 |
| **Hadithi** | | | | |
| Kabla ya kusoma hadithi ya wanafunzi | 4 | 3 | 4 | 4 |
| Wakati wa kusoma hadithi ya wanafunzi | 5 | 5 | 4 | 4 |
| Baada ya kusoma hadithi ya wanafunzi | 5 | 5 | 4 | 4 |
| Hadithi ya mwalimu | | | 3 | 3 |
| Kuandika | 3 | 3 | 3 | 3 |
| | 30 | 30 | 30 | 30 |

## Mapendekezo ya mgawanyiko wa muda wa kila somo

## (Mwaka wa 1, Wiki ya 22-30)

| **Sehemu** | **Siku ya 1 na 3** | **Siku ya 2 na 4** | **Siku ya 5** | **Wiki ya 27 (Kila siku)** |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| Ufahamu wa fonimu | | | | |
| Ufahamu wa Herufi | | | | |
| Silabi | 5 | 3 | | 5 |
| Kusoma maneno kwa silabi | 5 | | | 5 |
| Kusoma maneno marefu | | 4 | | |
| Sarufi | | 4 | 4 | 5 |
| Jedwali la silabi | | | 6 | |
| **Hadithi ya mwanafunzi** | | | | |
| Kabla ya kusoma hadithi ya wanafunzi | 5 | 4 | | 6 |
| Wakati wa kusoma hadithi ya wanafunzi | 6 | 6 | | 6 |
| Baada ya kusoma hadithi ya wanafunzi | 6 | 6 | | 7 |
| **Hadithi ya mwalimu** | | | | |
| Kabla ya kusoma hadithi ya mwalimu | | | 6 | |
| Wakati wa kusoma hadithi ya mwalimu | | | 5 | |
| Baada ya kusoma hadithi ya mwalimu | | | 6 | |
| Hadithi | 3 | 3 | 3 | |
| | 30 | 30 | 30 | |

# Kamusi ya Kiswahili

**Utangulizi**

Kamusi hii imewekwa ili kumsaidia mwalimu anayefundisha darasani kupata maneno kwa haraka. Maana ya maneno haya yametolewa kulingana na jinsi maneno yalivyotumiwa katika hadithi zilizoko kwenye kitabu hiki.

| MSAMIATI | | MAANA |
|---|---|---|
| Akaamua | – | Akakata kauli. |
| Akaitwaa | – | Akaichukua. |
| Akakataa katakata | – | Akakataa kabisa. |
| Akamuuma | – | Akashika na kukata kwa meno. |
| Akang'oa | – | Akatoa mmea kutoka kwa mchanga kwa kuivuruta mizizi yake. |
| Akaogelea | – | Akaenda juu ya maji bila kuzama. |
| Akaoka | - | Kuoka ni njia moja ya upishi maalum ambako moto huwekwa chini na juu ya chakula. |
| Akilisugua | – | Akilipitisha juu ya kitu kingine ili kuondoa alama ama uchafu. |
| Alhamisi | – | Siku ya tano ya wiki. |
| Alijikaza | – | Ingawaje alipata matatizo, alitia bidii ili afaulu. |
| Alishtuka | – | Aligutuka. |
| Alisononeka | – | Alijawa na uchungu moyoni. |
| Aliwatesa | – | Aliwatendea maovu ili wahisi uchungu. |
| Amani | - | Hali tulivu. |
| Amenenepa | - | Mwili wake umeongezeka kwa uzito. |
| Bahasha | – | Mfuko mdogo ambao umetengenezwa kwa karatasi. Unatumika kuweka barua ili kuituma. |
| Barafu | - | Maji yaliyoganda kwa baridi na kuwa magumu kama mawe. |
| Bidhaa | – | Vitu au mali ambayo yanauzwa. |
| Birika | – | Kifaa au chombo kinachotumika nyumbani kwa kuweka chai. Kifaa hiki kina mdomo mrefu na mkono wa kushika. |
| Bonde | – | Sehemu ya ardhi iliyo na mteremko mkubwa. |
| Bwawa | – | Eneo kubwa la maji yaliyokusanyika. |
| Chambo | – | Kitu kinachowekwa kwenye ndoana ili kuvutia samaki. |
| Chatu | – | Aina ya nyoka mkubwa. |
| Chomoza | – | Tokea kama vile jua linavyotokea asubuhi upande wa mashariki. |
| Dhania | – | Mmea wenye harufu nzuri ambao hutumika kuongeza ladha kwenye chakula. |
| Dhahabu | – | Aina ya chuma cha kung'ara ambacho hutumiwa kutengeneza mikufu na pete. Bei yake ni ghali sana. |
| Dhati | – | Kuaminika. Wa kweli na haki. |
| Dubu | – | Mnyama anayefanana na simba au paka na huishi sehemu zenye baridi sana. |
| Enea | – | Kuwa au fika kila mahali. |

| | | |
|---|---|---|
| Fedha | – | Jina lingine la pesa. |
| Foleni | – | Watu au vitu kufuatana moja hadi nyingine katika mlolongo. |
| Fyatua | – | Achilia kwa ghafla kitu kilichokazwa. |
| Gauni | – | Vazi refu kama rinda kutoka mabegani hadi miguuni linalovaliwa na wanawake. |
| Ghalani | – | Pahali panapowekwa vyakula hasa nafaka. Ndani ya stoo ya kuweka chakula. |
| Ghali | – | Yenye bei ya juu. |
| Gharama | – | Pesa zinazotolewa ili kununua kitu. |
| Gharika | – | Mafuriko ya maji. |
| Ghasia | – | Fujo. Kelele ya watu wanaopigana. |
| Ghorofa | – | Nyumba iliyo na vyumba vingine katika sehemu ya juu. |
| Gololi | – | Aina ya chombo kidogo cha kuchezea ambacho kina umbo la mviringo. Watoto huiita bano. |
| Gundi | – | Aina ya kitu ambacho huwa majimaji na hushika kwa kuganda. Hutumiwa kushikanisha mbao au vitu viwili. |
| Hadharani | – | Mahali palipo wazi. Waziwazi; bila kujificha; mbele ya watu. |
| Hakimu | – | Mtu anayetoa uamuzi kortini. |
| Hela | – | Pesa pia fedha. |
| Hodari | – | Mtu ambaye ana ujuzi wa kufanya jambo vizuri kuliko wengine. |
| Hufariki | – | Hufa; Huaga dunia. |
| Hukumiwa | – | Fanyiwa uamuzi kwenye kesi na jaji |
| Hushambulia | – | Huvamia mtu au kitu. |
| Hutapakaa | – | Huenea kila mahali |
| Hutuokea | – | Hutupikia kwa kuweka chakula katika jiko au tanuri. Mkate hupikwa kwa njia hii. |
| Ijumaa | – | Siku ya sita ya wiki. |
| Iliparara | – | Ilichakaa, kuwa na rangi nyeupe. |
| Ini | – | Sehemu ya mnyama ya ndani ambayo huwa nyekundu. Watu huipika na kuila. |
| Jangwani | – | Katika eneo kubwa lililo kavu na lenye mchanga na lisiloota nyasi wala miti |
| Jivu | – | Aina ya unga ambao hubaki baada ya kitu (kama kuni) kuchomeka na kuisha kabisa. |
| Joto | – | Hali ya motomoto. |
| Kaimati | – | Aina ya chakula kinachopikwa kwa sukari na unga wa ngano. |
| Kalenda | – | Orodha ya siku na miezi ya mwaka. |
| Kamati | – | Kundi la watu waliochaguliwa ili kusimamia jambo fulani kisha kufanya uamuzi. |
| Kariri | – | Rudia maneno yaleyale kimoyomoyo ama kwa sauti. Kwa mfano kukariri shairi. |
| Kiamshakinywa | – | Chakula cha kwanza asubuhi. |

| | | |
|---|---|---|
| Kiangazi | – | Wakati jua linapokuwa kali sana; wakati wa joto. |
| Kichochoro | – | Njia ndogo katikati ya nyumba mbili au majengo mawili. |
| Kichongeo | – | Kifaa chenye makali kama wembe kinachotumika kufanya ncha. Hutumiwa kuchongea kalamu za makaa au penseli. |
| Kifahari | – | Kilichosifika; Kilicho cha hali ya juu. |
| Kifutio | – | Kifaa kinachotumiwa kuondoa maandishi katika kitabu au kwenye ubao. |
| Kikateleza | – | Kutambaa bila kutumia miguu na badala yake kutumia mwili wote. |
| King'ora | – | Paipu inayolia kwa sauti kali ili kufahamisha hali ya hatari au jambo la dharura. |
| Kinyonga | – | Aina ya mjusi anayebadilika rangi. Pia huitwa lumbwi. |
| Kipaji | – | Sehemu ya mbele ya kichwa ambayo iko juu ya macho. |
| Kiranja | – | Kiongozi wa darasa. |
| Kisiwani | – | Sehemu ya nchi kavu iliyozungukwa na maji kwa mfano Mombasa na Migingo. |
| Kisogo | – | Sehemu ya nyuma ya kichwa. |
| Kitoweo | – | Chakula kinacholiwa na chakula kingine kama vile mboga, nyama au mchuzi. |
| Kiwango | – | Kipimo kama vile kipimo cha juu au cha wastani. |
| Kochi | – | Aina ya kiti kirefu chenye sehemu ya kuwekea mikono. |
| Konokono | – | Mnyama anayefanana na kinyama kidogo kinachoteleza na kutambaa polepole. |
| Kubweka | – | Kilio cha mbwa. |
| Kuchaguliwa | – | Kuteuliwa katika jambo fulani. |
| Kuchana nywele | – | Hali ya kutumia kichana ili kuzifanya nywele kuwa laini. |
| Kudhihaki | – | Kudharau mtu au kukosea mtu heshima. |
| Kufunga safari | – | Kuanza safari |
| Kufura | – | Kunenepa kwa upana ambako kunasababishwa na ugonjwa. |
| Kufyeka | – | Kuondoa kwekwe kama nyasi kwa kukata kwa upanga au kifyekeo. |
| Kujikinga | – | Kujizuia kutokana na madhara au magonjwa. |
| Kukua | – | Kuongezeka kwa kimo au ukubwa. |
| Kumkamata | – | Kumshika mtu,kitu au mnyama. |
| Kumnyima | – | Kutompatia kitu alichonacho. |
| Kumumunya | – | Kuyeyusha kitu mdomoni kama vile peremende. |
| Kung'ara | – | Kumetameta. Kutoa nuru au mwangaza |
| Kupona | – | Kupata nafuu baada ya kupatwa na ugonjwa. |
| Kustaajabisha | – | Kushangaza. |
| Kutabiri | – | Kueleza yale ambayo yatatokea. |
| Kutaga mayai | – | Jina linalotumika kueleza kitendo cha kuku kutoa mayai kwa mwili wake. |
| Kuteka nyara | – | Kumchukua mtu kwa nguvu ili kupata kitu unachokitaka. |

| | | |
|---|---|---|
| Kuukuu | – | Iliyozeeka na kuchakaa. |
| Kuzimia | – | Hali ya mtu kutoweza kupumua kisha kuanguka na kupoteza fahamu. |
| Kwapani | – | Sehemu ya mkono iliyo chini ya bega. |
| Lahaula | – | Tamko la kuonyesha mshangao. |
| Lalamika | – | Toa matamshi ya kujitetea kwa kutoridhika na yaliyofanywa. |
| Likizo | – | Wakati wa likizo ni wakati wa mapumziko baada ya kuwa shule kwa muda mrefu (kama muhula) wa masomo. |
| Limau | – | Aina ya tunda ambalo hufanana na chungwa lakini lina ladha kali sana. |
| Lishe | – | Chakula. |
| Maarufu | – | Hodari, anayesifika sana. |
| Mabawa | – | Sehemu ya mwili wa ndege inayotumika kumwezesha ndege kupaa. |
| Mabuyuni | – | Katika tunda la mti wa mbuyu ama katika buyu litumiwalo kunywea maji; Ndani ya mabuyu. |
| Mahakama | – | Mahali ambapo kesi husikilizwa na kuamuliwa; korti. |
| Majivuno | – | Maringo. Hali ya kupenda kujionyesha kuwa mzuri au hodari kuliko wengine. |
| Mali | – | Vitu vya thamani kubwa alivyo navyo mtu. |
| Mama | – | Mzazi wa kike. |
| Mamba | – | Mnyama anayeishi kwenye maji lakini hutokea wakati wa adhuhuri ili kuota jua. Mnyama huyu hula nyama. |
| Manyoya | – | Malaika ya mwili wa ndege au mnyama. |
| Maridadi | – | Ya kupendeza. |
| Mawaidha | – | Maneno ya kumuelekeza mtu kwenye njia inayofaa; Ushauri. |
| Mayowe | – | Kilio cha mtu aliye hatarini. |
| Mchana kutwa | – | Mchana mzima. |
| Mchicha | – | Aina ya mboga ya kienyeji. |
| Meli | – | Chombo kinachotumiwa kusafirisha watu kwenye ziwa au baharini. Huwa kikubwa kuliko dau au feri. |
| Mhandisi | – | Mtaalamu aliyehitimu kwa kazi ya injinia. |
| Migomba | – | Miti inayozaa ndizi. |
| Minyoo | – | Wadudu warefu na wembamba ambao huishi tumboni mwa binadamu au mnyama. Minyoo husababishwa na kula uchafu. |
| Mjomba | – | Ndugu wa kiume wa mama. |
| Mjusi | – | Mnyama mdogo mwenye umbo la kenge na hula wadudu. |
| Mkorosho | – | Mti mkubwa ambao huzaa korosho na tunda la bibo. Wengine huuita mbibo. |
| Mkuki | – | Chombo ambacho kimetengenezwa kwa chuma au mti na hutumiwa na wawindaji kuchoma na kuua wanyama msituni. |
| Mlafi | – | Mtu anayependa kula chakula kingi kuliko kile ambacho mwili wake unahitaji |

Mola – Jina lingine la Mungu. Pia huitwa Maulana.

Mtihani – Maswali yanayojibiwa kwa kuandika ili kupima maarifa ya mtahiniwa.

Mvivu – Asiyependa kufanya kazi; mzembe.

Mwashi – Anayefanya kazi ya kujenga nyumba kwa mawe.

Mwenge – Kitu kilicho na moto. Hutoa mwangaza kama taa na huchomeka kwa mda mrefu.

Mwewe – Aina ya ndege ambaye hula nyama. Anapenda kula vifaranga wa kuku na ndege.

Nadhifu – Inayopendeza; safi.

Nafuu – Kuhisi vyema, bora. Hutumiwa kuzungumza kuhusu bei rahisi ya vitu.

Navitamani – Navingoja kwa hamu sana.

Ndege – Kiumbe aliye na mabawa, hivyo basi ana uwezo wa kupaa.

Ng’ambo – Nje ya mipaka ya nchi; hasa baada ya kuvuka bahari au mto.

Ng’ang’ania – Fanya lolote unaloweza ili kufaulu.

Ng’ara – Kumetameta. Hali ya kuwa safi zaidi.

Ngao – Kifaa cha kujikinga. Kimetengenezwa kwa mbao au chuma.

Ngozi – Sehemu ya nje ya mwili wa binadamu au mnyama.

Nuka - Toa harufu mbaya au isiyopendeza.

Nyigu – Mdudu anayekaa kwenye miti au nyumba. Anafanana na nyuki. Kiuno chake huwa chembamba sana.

Nyororo – Aina ya kamba ambayo imetengenezwa kwa chuma.

Nyota - Vitu vyenye nuru vilivyo angani na humetameta usiku.

Nzige – Mdudu kama panzi (locust)

Paa – Sehemu ya juu ya nyumba. Pia kwenda juu kama ndege au eropleni.

Panzi – Mdudu mwenye umbo mrefu, mbawa na huruka; ni wa jamii ya nzige au parare.

Papa - Aina ya samaki mkubwa sana.

Pasaka – Sherehe za kikristo ambazo waumini husherehekea kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo.

Pweza – Aina ya mnyama wa baharini ambaye ana mikia au mikono minane (onyesha picha ya pweza- octopus).

Radi – Sauti kubwa inayotoka mawinguni na kusababishwa na umeme wakati wa mvua.

Randa – Kifaa cha chuma ambacho hutumika kulainisha mbao.

Rangi ya machungwa – Kwa Kiingereza huitwa “orange”.

Rangi ya manjano – Kwa Kiingereza huitwa “yellow”.

Runinga – Televisheni; kifaa maalum kinachopeperusha habari na kuonyesha picha.

Saa – Chombo kinachotumika kuhesabu muda kwa masaa, dakika na sekunde (onyesha saa).

| | | |
|---|---|---|
| Samahani | – | Neno ambalo mtu hutumia wakati amemkosea mtu mwingine. |
| Samawati | – | Rangi ya mbingu bila mawingu. Pia huitwa rangi ya bluu. |
| Sebule | – | Sehemu ya nyumba ambako watu huketi kwa mapumziko. |
| Shada | – | Kundi la maua yaliyoshikanishwa. |
| Shairi | – | Utungo ulio na mpangilio fulani. Huwa na beti na kiitikio. |
| Shanga | – | Mkufu unaovaliwa shingoni. |
| Shikamoo | – | Neno la kumuamkua mtu aliyekuzidi umri. Neno hili hutumika sana katika sehemu za pwani. |
| Shwari | – | Mzuri au nzuri. |
| Sikukuu | – | Siku maalum iliyotengwa kwa ajili ya kusherehekea jambo, tukio au watu fulani. |
| Siri | – | Jambo lililofichwa ili wengine wasijue. |
| Soseji | – | Nyama iliyosagwa na kujazwa katika kifuko cha utumbo kutokana na ng’ombe au nguruwe. |
| Sweta | – | Fulana nzito iliyofumwa kwa uzi na hutumiwa kuzuia baridi. |
| Tabia nzuri | – | Tabia inayodhihirisha heshima. Tabia inayofaa na kukubalika. |
| Takataka | – | Uuchafu. |
| Thamani | – | Gharama ya kitu au ubora kutokana na hali ya kuhitajika kwake na jamii. |
| Thubutu | - | Jaribu. |
| Tikiti | – | Aina ya tunda lenye ngozi ya rangi ya kijani na rangi nyekundu ndani. Tunda hili pia huitwa tikiti maji. |
| Timua | – | Kufukuza kwa ghafla. |
| Tulisisitiza | – | Tulitilia mkazo katika habari ili kuonyesha umuhimu wake. |
| Uhuru | – | Hali ya kufanya mambo bila ya kuingiliwa kati au kutawaliwa na mtu mwingine. |
| Ubora | – | Thamani au faida ya kitu. |
| Uongo | – | Habari isiyo ya kweli. Udanganyifu. |
| Upinde wa mvua | – | Kitu kinachoonekana angani chenye rangi saba. Hutokea wakati kuna mvua ndogo. |
| Utaalam | – | Ujuzi. |
| Utamaduni | – | Desturi za kundi la jamii fulani; mila. |
| Utashangaa | – | Utastaajabu. |
| Uyoga | – | Aina ya mmea wenye umbo la mwavuli unaomea katika zizi la wanyama au palipo miti iliyooza. |
| Vibarua | – | Wafanyikazi wa muda wanaoajiriwa kwa kazi isiyo ya mwezi. |
| Viboko | – | Wanyama wakubwa na wanene sana wanaoishi kwenye maji. Hula nyasi. |
| Vifaa | – | Vitu au vyombo vinavyotumika kufanyia kazi fulani. |
| Vigelegele | – | Kitendo cha kupaza sauti za furaha au kusherehekea . Pia huitwa vifijo au nderemo. |
| Vikosi | – | Mikusanyiko ya askari zaidi ya elfu moja. |

| | | |
|---|---|---|
| Viota | – | Nyumba za ndege.Huwa zimetengenezwa kwa nyasi, vijiti au miiba. |
| Vipawa | – | Uwezo fulani alionao mtu unaomwezesha kulifanya jambo fulani vizuri. |
| Virusi | – | Vidudu vinavyosababisha magonjwa katika mwili wa binadamu au wanyama. |
| Vumilia | - | Endelea na jambo ingawa kwa tabu au shida. |
| Wakamvamia | – | Wakamshambulia bila haki ya kufanya hivyo. |
| Wakatoweka | – | Wakatoroka ili wasionekane. |
| Wakikaza | – | Wakishika kwa nguvu. |
| Wakili | – | Mtu anayemtetea mshtaki au mshtakiwa katika kesi kortini. |
| Walimtimua | – | Walimfanya aende kwa ghafla. |
| Wameangua | - | Hali ya vifaranga kutoka kwenye yai. |
| Wavuvi | – | Watu wanaofanya kazi ya kuvua samaki. |
| Waya | – | Uzi unaotengenezwa kutoka kwa chuma. |
| Wilayani | – | Katika sehemu iliyo ndogo kuliko kaunti. |
| Wishwa | - | Mabaki yatokayo katika nafaka zilizotolewa. |
| Yaya | – | Mtu ambaye ameajiriwa ili afanye kazi ya kulea mtoto nyumbani. |
| Zabibu | – | Aina ya matunda ambayo yana rangi ya zambarau. |
| Zamani | – | Kitambo au miaka mingi iliyopita. |
| Ziara | – | Kwenda kutembelea au kuzuru mahali fulani. |
| Zizi | – | Boma ambamo mifugo kama vile ng'ombe au mbuzi hulala. |
| Zulia | – | Kitu kama mkeka kilichotengenezwa kwa pamba kinachotandikwa chini. |

# Nyenzo za kufundishia:

| Somo | Nyenzo za kufundisha |
|---|---|
| Ufahamu wa fonimu | Jedwali la sauti na majina ya herufi za Kiswahili |
| Ufahamu majina ya herufi na sauti | Kadi za herufi, jedwali la sauti na majina ya herufi za Kiswahili, mfuko wa herufi |
| Silabi | Chati za herufi na silabi, jedwali la sauti na majina ya herufi za Kiswahili |
| Kusoma maneno | Chati za herufi na silabi, kadi za maneno, kadi za silabi |
| Msamiati | Chati za picha na michoro, kadi za picha na michoro, Kamusi ya Kiswahili, vifaa halisi au ghushi, chati zenye msamiati |
| Ufahamu | Vitabu vya hadithi, magazeti na jarida |
| Maktaba | Vitabu vya hadithi, magazeti na jarida |

## Namna ya kushughulikia wanafunzi wenye mahitaji maalumu

1. Endapo darasani kuna wanafunzi walio na mahitaji maalumu, mwalimu anapaswa kutafuta mbinu ya kushughulikia mahitaji haya kwa makini. Baadhi ya mahitaji hayo ni kama:
   a) Matatizo ya kusikia
   b) Matatizo ya kuona vyema
   c) Udhaifu wa kusoma, kuandika na kuelewa mambo haraka
   d) Udhaifu wa kuwasiliana, kwa mfano mtoto aweza kuwa na hali ya kugugumiza na kadhalika
   e) Udhaifu au ulemavu wa viungo vya mwili
   f) Walio hodari wa kuelewa mambo haraka kuliko wale wa wastani
2. Ni muhimu kwa mwalimu kutambua uwezo na udhaifu wa kila mwanafunzi kabla ya, wakati wa na baada ya somo. Kufanya hivi kutamwezesha kushughulikia mahitaji hayo kwa njia inayofaa ili yasiathiri fanaka ya somo.
3. Mifano ya mahitaji maalumu na namna ya kuyashughulikia:

| **Mahitaji maalumu** | **Baadhi ya mapendekezo na namna ya kushughulikia mahitaji maalumu** |
|---|---|
| a) Matatizo ya kusikia | - Tumia lugha ya ishara inapowezekana<br>- Mwanafunzi aketi karibu na mwalimu au pale anapoweza kusikia vizuri<br>- Himiza matumizi ya vifaa vya kuongezea sauti<br>- Matumizi ya vifaa halisi kunahimizwa |
| b) Matatizo ya kuona vyema | - Mwanafunzi aketi karibu au mbali na ubao kulingana na mahitaji yake<br>- Himiza matumizi ya braille inapofaa<br>- Jadili na wazazi au walezi matumizi ya miwani au vioo vya kukuza kimo cha maandishi<br>- Epuka vifaa vinavyoathiri uwezo wa kuona<br>- Mwanafunzi aketi karibu au mbali na mwangaza kulingana na mahitaji yake<br>- Matumizi ya vifaa halisi au ghushi kunahimizwa |
| c) Udhaifu wa kusoma, kuandika na kuelewa mambo kwa haraka | - Wape wanafunzi muda wa ziada kuliko wanafunzi wengine<br>- Watengewe muda maalumu wa kurejelea waliyosoma baada ya somo<br>- Gawa somo kwa hatua fupi fupi kuanzia nyepesi hadi hatua tatanishi<br>- Wape mazoezi ya ziada<br>- Mwalimu awakinge wanafunzi walio dhaifu dhidi ya kudunishwa kwa njia yoyote ile |
| d) Udhaifu wa kuwasiliana | - Wape wanafunzi muda wa kuwasilisha mawazo yao<br>- Mwalimu aepukane na vitendo vinavyoweza kuathiri hisia au maono ya mwanafunzi<br>- Mwalimu atumie mbinu tofauti za mawasiliano ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi |
| e) Udhaifu au ulemavu wa viungo vya mwili | - Mwanafunzi apewe muda wa ziada ili kukidhia upungufu (ulemavu) wake<br>- Wapewe vifaa vya teknolojia ikiwezekana au vya kubuniwa kulingana na hali ya ulemavu ili kuongeza uwezo wa utendaji kazi wao<br>- Mwalimu anaweza kushauriana na wahudumu wa walemavu kwa usaidizi zaidi |
| f) Walio hodari wa kuelewa mambo haraka kuliko wale wa wastani | - Wanafunzi wapewe kazi ya ziada ili watumie muda wao vyema<br>- Wanafunzi wapewe nafasi za kukuza vipawa vyao<br>- Wanafunzi wapewe kazi zenye changamoto zaidi ili kufanyisha kazi akili zao na kuwapa fursa ya kutumia uhodari wao. |

Wiki ya 1: Siku ya 1 na 2 **Nyumbani**

Tamka sauti.

m

Soma neno.

**anaona** **paka** **mama**

### Koki na Mugambi

Kuna marafiki wawili. Msichana anaitwa Koki na mvulana anaitwa Mugambi. (Mvulana na msichana wamevaa nguo za shule na wamebeba begi) Koki na Mugambi huenda sh l kila asubuhi na mapema. Njiani, wao huona vitu mbalimbali. Koki anaona p k . Mugambi anaona k nga. Koki anaona mbe. Mugambi anaona m ba. Wanapofika shule, Koki na Mugambi wanaona majengo ya shule. Koki anaona mw l mu. Mugambi anaona s . Koki na Mugambi wanaona m d w t .

1

**WIKI YA 1: SOMO LA 1**

**Ufahamu wa fonimu: Utambuzi wa sauti**

Tutajifunza sauti mpya. Tutaitamka, kisha nitataja maneno. Ikiwa maneno hayo yanaanza kwa sauti hiyo, mwalimu akubaliane na wanafunzi ishara ya kutumia.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Sauti ni **/m/.**

Neno la kwanza ni **mama**. Neno Mama linaanza kwa sauti **/m/** kwa hivyo mwalimu afanye ishara waliokubaliana.

Neno lingine ni **ama**. Neno ama halianzi kwa sauti **/m/** kwa hivyo mwalimu afanye ishara waliokubaliana.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tutaje sauti **/m/** pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi: /m/***

***Mwalimu:*** Neno la kwanza ni **mama**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno la pili ni **ama**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sauti ambayo tumejifunza ni?

***Wanafunzi: /m/***

***Mwalimu:*** Neno la kwanza ni **mama**.

***Wanafunzi:*** Wanafanye ishara waliokubaliana

***Mwalimu:*** Neno la pili ni **ama**.

***Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

*(Tumia hatua ya 3 kufunza: **makaa, kaka, matatu, ama, mti, taa**).*

**Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi ndogo**

Tutajifunza **jina** na **sauti** ya herufi ndogo **ma**. *(Mwalimu awapatie wanafunzi kadi za herufi m katika breli).*

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Kadi za Herufi: (*Onyesha herufi **m** kisha useme*), jina la herufi hii ni ***ma***. Sauti ya herufi hii ni **/m/**.

Wape kadi ya herufi **m**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tutaje pamoja. Jina la herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi: ma***

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi: /m/***

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni?

***Wanafunzi: ma***

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Wanafunzi: /m/***

***Eleza wanafunzi wasome sauti ya herufi (m) kwenye vitabu vyao, ukurasa wa [ukurasa wa breli unaolingana].***

**Msamiati maalum**

Tutajifunza maneno mapya. Maneno mapya huitwa msamiati. Sasa nitasoma msamiati unaopatikana kwenye hadithi nanyi mtarudia kuisoma.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. *(Onyesha kadi zenye maneno '**mama**', '**paka**' na '**anaona**') kisha useme,* **mama, paka, anaona.**

Mwalimu awapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno 'mama' 'paka' anaona.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tusome maneno haya pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **mama, paka, anaona.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa someni peke yenu.

***Wanafunzi:*** **mama, paka, anaona.**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

***Wanafunzi:*** **mama, paka, anaona.**

**Kabla ya kusoma: hadithi**

Sasa ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu baadhi ya maneno au msamiati unaopatikana kwenye hadithi hiyo. Pia, tutasoma kichwa cha hadithi na kusikiliza maelezo. Kisha tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo. **(Waambie wanafunzi kichwa cha hadithi).**

# Wiki ya 1: Siku ya 1

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Neno la kwanza ni **kanga.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia hili neno? *(Wanafunzi waonyeshe ishara waliokubaliana)*. Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya neno hili? *(Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi wanaonyesha ile ishara, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu neno hilo. Waulize wanafunzi wachache kile walichojadiliana. Iwapo maelezo yao ni sahihi au si sahihi, eleza maana ya neno).*

*Ikiwa ni wachache wanaolielewa, wasijadiliane. Sema:* maana ya **kanga** ni **aina ya ndege anayefanana na kuku lakini anayeishi msituni. Ndege huyu huwa wa rangi ya kijivu na madoadoa meupe.**

(*Tumia njia hiyo hiyo kufunza msamiati uliosalia:* ***mwalimu, madawati*** *na* ***saa).***

Mwalimu awaonyeshe wanafunzi rifaa halisi panapowezekana.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tufungue vitabu vyetu ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma kichwa cha hadithi hii. Kichwa cha hadithi ni **Koki na Mugambi**. Je, tunajua nini kuhusu **Koki na Mugambi?** *(Wanafunzi 3 – 4 wapewe nafasi wajibu).*

***Mwalimu:*** Tusikilize maelezo. Ni kitu gani umekisikia kwenye maelezo? *(Wanafunzi 3 – 4 wapewe nafasi wajibu).*

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa tutafikiria kitakachotendeka kwenye hadithi. Mgeukie mwenzako kisha umweleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii. (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao. Kumbuka kutoa utabiri wako kwanza).*

**Wakati wa kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** *(Soma hadithi ya* ***Koki na Mugambi****).*

***Koki na Mugambi***

**Kuna marafiki wawili. Msichana anaitwa Koki na mvulana anaitwa Mugambi. Koki na Mugambi huenda shule kila asubuhi na mapema. Njiani, wao huona vitu mbalimbali. Koki anaona paka. Mugambi anaona kanga. Koki anaona embe. Mugambi anaona miiba.**

**Wanapofika shule, Koki na Mugambi wanaona majengo ya shule. Koki anaona mwalimu. Mugambi anaona saa. Koki na Mugambi wanaona madawati.**

📖 **Baada ya kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** (*Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao ulitimia). Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya* ***Koki na Mugambi.*** *Sema:* Je, utabiri wenu ulitimia? *(Wanafunzi wanajibu).* Hebu tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tutayajibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

◈ **Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Swali la kwanza. ***Je, mvulana anayezungumziwa kwenye hadithi anaitwa nani?*** Hili ni swali langu, ni mimi nitalijibu kwanza.

Jibu la swali hili lapatikana sehemu mbili tofauti: Kwenye kichwa cha hadithi na pia kwenye hadithi yenyewe. Vilevile ninatumia ujuzi wangu kutofautisha majina ya wasichana na wavulana. Kwa hivyo jina la mvulana huyo ni Mugambi. Hebu niwasomee msitari nilipopata jina hilo. (*Soma msitari wenye jibu kwenye hadithi).*

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Swali la pili. Je ***Msichana anayezungumziwa kwenye hadithi anaitwa nani?*** *(Chagua mwanafunzi mmoja kujibu swali hili, kisha aonyeshe msitari wenye jibu na awasomee wenzake. Hatimaye wanafunzi wote wasome msitari huo).*

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Swali la tatu. ***Koki na Mugambi waliona nini walipokuwa wanaenda shuleni?*** *(Chagua mwanafunzi mmoja mmoja kutaja vitu ambavyo Koki na Mugambi waliviona).*

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Hebu tutaje pamoja kitu kimoja walichokiona.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **Paka.** (Vitu vingine kama kanga, embe, miiba, n.k).

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Taja vitu vingine ambavyo waliviona walipofika shule.

***Wanafunzi:*** *(Wanataja vitu kama* ***majengo ya shule, shule, mwalimu, saa na madawati).***

✍ **Kuandika**

Onyesha kadi yenye herufi '**m**' kwa breli. Waagize wanafunzi waandike.

m m m m m

Hakikisha wanafunzi wanaandika huku wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya Ziada**

Wanafunzi waandike herufi '**m**' mara nne na waonyeshe wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kumbuka kufunza kwa utaratibu wiki ya kwanza. Sio haraka sana wala polepole sana.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 1: Siku ya 2 **Nyumbani**

Tamka sauti.

m

Soma neno.

anaona paka mama

**Koki na Mugambi**

Baada ya masomo, Koki na Mugambi hurudi ny mb ni. Wakiwa nyumbani, Mugambi anaona ny ny na vit nguu. Koki anaona p k p k na m nde. Mugambi anaona p p na p nya. Wote wanaona m m .

2

**WIKI YA 1: SOMO LA 2**

■ **Ufahamu wa herufi: majina na sauti za herufi**

Tutajifunza **jina** na **sauti** ya herufi **Ma** tena. (*Wapatie wanafunzi kadi za herufi* ***m*** *katika breli).*

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** (*Onyesha herufi* ***m*** *kisha useme:* jina la herufi hii ni **ma**. Sauti ya herufi hii ni **/m/**).

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tuseme sote. Jina la herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **Ma**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi: /m/***

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **Ma**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Wanafunzi: /m/***

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**Msamiati maalumu**

Tutajikumbusha msamiati maalumu tuliojifunza jana.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. (*Onyesha kadi zenye maneno '**mama**', '**paka**' na '**anaona**'kisha useme*), **mama**, **paka**, **anaona.**

Mwalimu awapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno '**mama**', '**paka**', '**anaona**'.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tusome maneno haya pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **mama**, **paka**, **anaona.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa someni peke yenu.

***Wanafunzi:*** **mama**, **paka**, **anaona.**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao. *(Wanafunzi wanasoma)*

📖 **Kabla ya kusoma: hadithi**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu baadhi ya maneno au msamiati unaopatikana kwenye hadithi hiyo. Pia tutasoma kichwa cha hadithi na kusikiliza maelezo. Baadaye tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Neno la kwanza ni **popo.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia neno hili? *(Wanafunzi wafanye ishara walio kubaliana).* Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya neno hili? *(Wanafunzi wafanye ishara walio kubaliana. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi wataonyesha ishara, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu neno hilo. Waulize wanafunzi wachache kile walichojadiliana. Iwapo maelezo yao ni sahihi au si sahihi, eleza maana ya neno).*

*Ikiwa ni wachache wanaolielewa, wasijadiliane. Sema:* maana ya *Popo* ni ***mnyama mdogo, kipofu, mwenye mabawa na anayefanana na panya. Mnyama huyu hupenda kula matunda na wadudu na kupaa usiku (****Onyesha picha****).***

(*Tumia njia hiyo hiyo kufunza msamiati uliosalia:* ***mende*****).**

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tufungue vitabu vyetu ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma kichwa cha hadithi hii. Kichwa cha hadithi ni **Koki na Mugambi**. Je, tunajua nini kuhusu **Koki na Mugambi?** *(Wanafunzi 3 – 4 wapewe nafasi wajibu).*

***Mwalimu:*** Hebu tusikilize maelezo. Ni kitu gani umekisikia kwenye maelezo? *(Wanafunzi 3 – 4 wapewe nafasi wajibu).*

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi. Kutabiri ni kufikiria na kusema kitakachotendeka. Mgeukie mwenzako kisha umweleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii. (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao).*

📖 **Wakati wa kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** *(Soma hadithi ya* ***Koki na Mugambi****)*

***Koki na Mugambi***

**Baada ya masomo, Koki na Mugambi hurudi nyumbani. Wakiwa nyumbani Mugambi anaona nyanya na vitunguu. Koki anaona pikipiki na mende. Mugambi anaona popo na panya. Wote wanaona mama akipika chakula.**

**Baada ya kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** (*Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao ulitimia au la. Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya* ***Koki na Mugambi.*** *Sema:* Je, utabiri wenu ulitimia au la? *(Wanafunzi wanajibu).* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitajibu swali la kwanza nanyi mnisaidie kuyajibu yale mengine.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Swali la kwanza. ***Koki na Mugambi waliona nini waliporudi nyumbani?*** Jibu la swali hili linapatikana kwenye hadithi ambayo tumeisoma. Kuna vitu mbalimbali ambavyo Mugambi na Koki waliviona waliporudi nyumbani. Hebu nirejelee sehemu hiyo niisome tena. *(Soma).* Kitu kimoja walichokiona ni **pikipiki**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tutaje pamoja kitu kimoja walichokiona waliporudi nyumbani.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **pikipiki**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Taja vitu vingine ambavyo waliviona waliporudi nyumbani.

***Wanafunzi:*** *(Wanataja vitu kama* ***nyanya, pikipiki, mende, popo, panya, mama akipika****).*

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Swali la pili. ***Kwa nini mama anapika chakula?*** Jibu la swali hili linatuhitaji sisi kutumia ujuzi wetu kusema sababu zinazoweza kumfanya mama apike chakula. Kwa vile ni maoni yetu, sababu yoyote yaweza kutolewa. Kwa mfano, **mama anapika kwa sababu ni kawaida yake kupika kila siku**.

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Hebu tutaje pamoja sababu moja ya mama kupika chakula.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **Ni kawaida yake kupika kila siku.**

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Taja sababu nyingine zinazoweza kumfanya mama apike chakula.

***Wanafunzi:*** *(Wanataja sababu kama vile* ***familia yake ipate chakula cha jioni; familia yake walikuwa wanasikia njaa n.k.****).*

**Kuandika**

Onyesha kadi yenye herufi **m** kwa breli.

m m m m m

M M M M M


Hakikisha wanafunzi wanaandika huku wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya Ziada**

Wanafunzi waendelee kuandika herufi **m** mara tano na waonyeshe wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Ni wajibu wa mwalimu kuhakikisha kuwa anawapongeza wanafunzi kila wakati wanapojibu maswali sahihi. Pia ni muhimu kusaidia wale wanaokosa kutoa jibu sahihi na kuwatia moyo.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________



Wiki ya 1: Siku ya 3 na 4 **Nyumbani**

Tamka sauti.

a m

Tamka sauti ya herufi na silabi.

m a a

ma a

Soma silabi na maneno.

ma ma a ma

**mama** **ama**

Tamka sauti.

a

Tamka sauti ya herufi na silabi.

m a a m aa

ma a maa

Soma silabi na maneno.

ma ma a ma

**mama** **ama**

3

**WIKI YA 1: SOMO LA 3**

**Ufahamu wa fonimu: Utambuzi wa sauti**

Tutajifunza sauti mpya **/a/**. Tutaitamka, kisha nitataja maneno. Ikiwa maneno hayo yanaanza kwa sauti hiyo, mwalimu akubaliane na wanafunzi ishara ya kutumia.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Sauti ni /**a**/. Neno la kwanza ni **ama**. Neno **ama** linaanza kwa sauti **/a/** kwa hivyo mwalimu afanye ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno lingine ni **mama**. Neno **mama** halianzi kwa sauti **/a/** kwa hivyo mwalimu afanye ishara waliokubaliana.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tutaje sauti **/a/** pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:* /a/.**

***Mwalimu:*** Neno la kwanza ni **ama**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno la pili ni **mama**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sauti ambayo tumejifunza ni?

***Wanafunzi:* /a/**

***Mwalimu:*** Neno la kwanza ni **ama**.

***Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana..

***Mwalimu:*** Neno la pili ni **mama**.

***Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno lingine ni **acha**.

***Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno lingine ni **ona**.

***Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

Endelea na: **angu, letu, apa, linda, amua, anza.**

■ **Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Tutajifunza **jina** na **sauti** ya herufi ndogo **aa**. Mwalimu awapatie wanafunzi kadi za herufi **a** katika breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** (*Onyesha herufi **a** kisha useme*), jina la herufi hii ni **aa**. Sauti ya herufi hii ni **/a/**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tutaje sote. Jina la herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:* aa**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:* /a/**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa fanyeni peke yenu. Jina la herufi hii ni?

***Wanafunzi:* aa**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Wanafunzi:* /a/**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

● **Silabi: Kusoma na kuandika**

Tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi. Silabi ni sehemu ya neno ambayo hutamkika kwa kuchanganya sauti mbili au zaidi.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **/m/ /a/– ma**. Silabi hii ni **ma**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tusome pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:* /m/ /a/ – ma**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa mtasoma peke yenu.

***Wanafunzi:* /m/ /a/ – ma.**

*Tumia hatua ya 1-3 kufunza silabi hii:* **a**

***Eleza wanafunzi wasome silabi kwenye vitabu vyao ukurasa wa [ukurasa wa breli unaolingana].***

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Nitatamka kila sauti huku nikiiandika silabi **ma**.

Nisikilize. **/m/ /a/ – ma.**

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** *(Tamka sauti pamoja na wanafunzi huku wakiiandika silabi **ma**)*

***Mwalimu na Wanafunzi:* /m/ /a/ – ma.**

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** *(Tamka sauti pamoja na wanafunzi huku wakiiandika.*

***Wanafunzi:* /m/ /a/ - ma.**

**▬ Kusoma na kuandika maneno kwa kutumia silabi**

Tutatumia silabi tulizozisoma kusoma na kuandika maneno.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize: **ma ma - mama**. Neno hili ni **mama.**

*(Soma pamoja na wanafunzi kisha wanafunzi wasome peke yao).*

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa nitatamka kila silabi huku nikiliandika neno **mama** ubaoni. Nisikilize. **ma ma - mama**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** *(Tamka silabi pamoja na wanafunzi huku wakiliandika neno **mama**).*

***Mwalimu na Wanafunzi:* ma ma – mama.**

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** *(Tamka silabi pamoja na wanafunzi huku wakiliandika neno **ama**).*

***Wanafunzi:* a ma – ama.**

**Hadithi ya mwanafunzi**

**🕮 Kabla ya kusoma: hadithi**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu baadhi ya maneno au msamiati unaopatikana kwenye hadithi hiyo. Pia tutasoma kichwa cha hadithi na kusikiliza maelezo. Baadaye tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. Neno la kwanza ni **paka.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia hili neno **paka**? *(Wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana).* Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya neno hili? *(Wanafunzi wanafanya ishara. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi wanafanya ishara, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu neno hilo. Ikiwa ni wachache wanaolielewa sema:* maana ya hili neno **paka** ni **mnyama anayekaa nyumbani. Paka hunywa maziwa na kula panya**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** (*Waambie wanafunzi kichwa cha hadithi na maelezo kisha useme),* tusome kichwa cha hadithi na maelezo iliyo kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Kichwa cha hadithi ni **Mama na Paka**. Je, tunajua nini kuhusu **Mama na Paka**? (*Wanafunzi 3-4 wapewe nafasi kujibu swali).*

***Mwalimu:*** Hebu tusikilize maelezo. Ni kitu gani umekisikia kwenye maelezo? *(Wanafunzi 3 – 4 wapewe nafasi wajibu).*

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Mgeukie mwenzako kisha umweleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao).*

**🕮 Wakati wa kusoma**

***Mwalimu:*** Hakikisha umefungua ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye kitabu chako. Weka kidole kwenye kichwa cha hadithi. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

*(Soma hadithi huku wanafunzi wakifuatilia kwa vidole. Soma pamoja na wanafunzi kisha wanafunzi wasome peke yao).*

**Hadithi: Mama na Paka**

**Mama anaona paka. Paka anaona mama.**

**◈ Baada ya kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** (*Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao ulitimia. Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya **Mama na Paka)*** *Sema:* Je, utabiri wenu ulitimia? *(Wanafunzi wanajibu.)* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Swali la kwanza. ***Mama anaona nini?*** Jibu la swali hili linapatikana moja kwa moja kwenye mstari wa kwanza unaosema: **Mama anaona paka**.

*(Soma jibu pamoja na wanafunzi kisha wanafunzi wasome peke yao).*

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Swali la pili. ***Paka anaona nani?***

*(Chagua mwanafunzi mmoja kujibu swali kisha asome mstari wenye jibu. Soma mstari huo pamoja na wanafunzi, hatimaye wanafunzi wote wasome mstari huo).*

***Wanafunzi:*** Paka anaona mama.

**✍ Kuandika**

Onyesha kadi yenye herufi **a** kwa breli. Waagize wanafunzi waandike.

a a a a a

Hakikisha wanafunzi wanaandika huku wakizingatia sheria za breli.

**🗍 Kitabu cha Kazi ya Ziada - *Wiki ya 1 Siku ya 3***

Wanafunzi waandike herufi 'a' mara tatu na waonyeshe wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Utabiri usipotimia haimaanishi mwanafunzi amekosea.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 1: Siku ya 3 na 4 Nyumbani

Paka yuko kwa dirisha. Mama amesimama mlangoni mwa kabati.

Mama na Paka

Mama anaona paka.

Paka anaona mama.

4

**WIKI YA 1: SOMO LA 4**

■ **Ufahamu wa herufi: majina na sauti za herufi kubwa**

Jana tulijifunza jina na sauti ya herufi **/a/**. Tutajifunza jina na sauti ya herufi **a** tena.

Waonyeshe kadi yenye herufi 'a' kwenye breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** (*Onyesha herufi **a** kisha useme*), jina la herufi bado ni **aa.** Sauti ya herufi hii ni **/a/.**

Mwalimu awapatie wanafunzi kadi za herufi **a** katika breli.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tutaje pamoja. Jina la herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **Aa**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/a/**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **Aa**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **/a/**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

● **Silabi: Kusoma**

Tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma silabi.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **/m/, /a/–** silabi hii ni **ma**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tusome pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/m/, /a/– ma.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa ni zamu yenu.

***Wanafunzi:*** **/m/, /a/– ma.**

*Tumia hatua ya 1-3 kufunza silabi hizi: **a, maa.***

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

▬ **Maneno: Kusoma na kuandika maneno kwa kutumia silabi**

Tutatumia silabi kusoma na kuandika maneno.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **ma ma – mama**. Neno hili ni **mama**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tusome pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **ma ma – mama**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa.

***Wanafunzi:*** **ma ma – mama**.

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza neno:* **ama.***)*

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana] bila kusema au kutamka silabi.***

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Nitatamka kila silabi huku nikiliandika neno **ama.** Nisikilize. **a ma – ama.**

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Nitatamka kila silabi huku nikiliandika neno **ama.**

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **a ma – ama**.

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Nitatamka kila silabi huku nikiliandika neno **mama.**

***Wanafunzi:*** **ma ma – mama**

**Hadithi ya mwanafunzi**

🕮 **Kabla ya kusoma: hadithi**

***Mwalimu:*** Tutasoma tena hadithi tuliyoisoma jana ya **Mama na Paka.** Hakikisha umefungua ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi hiyo kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

**Wakati wa kusoma hadithi**

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nasoma sasa. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuisome hadithi hii pamoja sasa.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** *(Wanaisoma hadithi).*

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii peke yenu.

***Wanafunzi:*** *(Wanaisoma hadithi peke yao).*

**Mama na Paka**

**Mama anaona paka. Paka anaona mama.**

**Baada ya kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Kwanza, nitawaonyesha jinsi ya kujibu maswali hayo. Kisha tutashirikiana kuyajibu. Baadaye mtashirikiana kuyajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Swali la kwanza. ***Unafikiri mama na paka wako wapi?*** Jibu la swali hili halipo kwenye hadithi. Hivyo inabidi tutumie ujuzi wetu kutoa jibu. ***Huenda mama na paka wako jikoni. Hii ni kwa sababu paka anapenda sana kukaa jikoni.***

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi: Huenda mama na paka wako jikoni.***

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Taja mahali pengine ambapo mama na paka wanaweza kupatikana.

***Wanafunzi:*** *(Wanajibu.* ***Wanaweza kutaja sebuleni, nyumbani, kwenye bustani, chini ya mti n.k.).***

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Swali la pili. ***Umuhimu wa paka ni nini?*** Jibu la swali hili halipo kwenye hadithi. Hivyo inabidi tutumie ujuzi wetu kutoa jibu. ***Paka wetu anapenda kucheza nami. Hivyo umuhimu wa paka ni kucheza nami.***

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi: Umuhimu wa paka ni kucheza nami.***

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Taja umuhimu mwingine wa paka.

***Wanafunzi:*** *(Wanajibu. Wanaweza kutaja yafuatayo:* ***Paka hutusaidia kuwafukuza/kuwala panya; paka ni rafiki wa binadamu n.k.)***

**Kuandika**

Onyesha kadi yenye herufi **a** kwa breli. Waagize wanafunzi waandike.


a a a a a

Hakikisha wanafunzi wanaandika huku wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya Ziada**

Wanafunzi waandike herufi '**c**' mara tano na waonyeshe wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Wiki ya 1: Siku ya 5 **Nyumbani**

Tamka sauti.

m a

Tamka sauti ya herufi na silabi.

m a a

ma a

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano a ma - ama.

| ma | a | ma | a |
| --- | --- | --- | --- |

5

**WIKI YA 1: SOMO LA 5**

■ **Marejeo: Ufahamu wa herufi**

Leo tutarejelea herufi tulizojifunza wiki hii. Tutajikumbusha herufi **Ma** na **Aa**. Tutatamka sauti za herufi hizo.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** *(Mwalimu awapatie wanafunzi kadi za breli zenye herufi **m** na **a**),* Nisikilize. **ma** Sauti ya herufi hii ni **/m/.**

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tuseme pamoja jina la herufi hii ni.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **ma**

***Mwalimu:*** Sasa tutamke pamoja sauti ya herufi hii.

***Mwalimu na Wanafunzi:* /m/.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni:

***Wanafunzi:*** **ma**

***Mwalimu:*** Sasa tamkeni sauti ya herufi hii.

***Wanafunzi:* /m/.**

***Tumia hatua ya 1-3 kufunza aa.***

***Eleza wanafunzi wasome sauti kwenye vitabu vyao ukurasa wa [ukurasa wa breli unaolingana].***

● **Silabi Kuandika**

Tutatumia silabi kadhaa tulizopewa.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Tumepewa silabi nne tofauti. **ma, a, ma** na **a**. Hebu tusome silabi hizi pamoja. ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

Mwalimu na mwanafunzi: **ma, a, ma, a**

***Mwalimu:*** Nisikilize. Naweza kutumia silabi **ma** na **ma** kuunda neno ***mama***. *Pia naweza kutumia silabi **ma** mara mbili kuunda neno lile **mama.***

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tuseme neno hili pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **mama**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Tumia silabi iliyoko kwenye jedwali la sailabi liliyoko kwenye breli kuunda maneno mengine yenye maana.

*(Wanafunzi waunde neno, kama vile: **ama**)*

**Hadithi ya mwalimu**

📖 **Kabla ya kusoma: hadithi**

***Mwalimu:*** Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu baadhi ya maneno au msamiati unaopatikana kwenye hadithi hiyo. Pia tutasoma kichwa cha hadithi na kusikiliza maelezo. Kisha tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. Neno la kwanza ni **alialikwa.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia hili neno **alialikwa**? *(Wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana).* Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya neno hili? *(Wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana). Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu neno hilo. Ikiwa ni wachache waliolielewa sema:* maana ya hili neno **alialikwa** ni **kukaribishwa kwa karamu au sherehe.** *(Tumia hatua hii kufunza **karamu-neno lingine la sherehe. Ulafi-hali ya mtu kupenda kula chakula sana**).*

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** *(Soma kichwa cha hadithi na kisha wanafunzi wasikilize maelezo),* hebu tusome kichwa cha hadithi na maelezo yaliyo kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Kichwa cha hadithi ni **Katumbo**. Hebu sikiliza maelezo. Umesikia nini katika maelezo? *(Wanafunzi 3 -4 wapewe nafasi kujibu swali).*

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Mgeukie mwenzako kisha umweleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii. (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao*).

📖 **Wakati wa kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** Nitasoma hadithi ya Katumbo. Sikiza kwa makini. (*Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

📖 **Hadithi: Katumbo**

Siku moja Katumbo alialikwa kwenye karamu. Baada ya wageni kuketi, chakula kikapakuliwa na wakaanza kula. (***Nani alialikwa kwa karamu***?)

# Wiki ya 1: Siku ya 5

Katumbo akala ugali, kabeji, sukumawiki, mchuzi wa maharagwe na nyama. Baadaye akala wali kwa kuku wa kuchoma. Aliposikia kuna matunda akakimbia huko. Alikula maembe, ndizi, mapera na machungwa. Baadaye, tumbo la Katumbo likaanza kuuma na kunguruma.(***Katumbo alikunywa supu ya nini****?*)

Tumbo la Katumbo lilifura na kupanuka kama jungu la maji. Mara Katumbo akaanza kutapika. Matapiko yake yalikuwa mengi. Mwishowe kukawa ni kama mto mkubwa uliojaa vyakula vya kila aina. Baba yake akampeleka hospitali. Katumbo akapona. Kutoka siku hiyo, Katumbo aliacha ulafi na kuwa mtoto mzuri. (***Unafikiri nini kilimfanya Katumbo kuumwa na tumbo?***)

✍ **Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi zenye silabi **ma** katika breli. Wanafunzi waandike.

| | |
|---|---|
| ma ma | ma ma |
| mama | mama |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Vidokezo vya Mwalimu**

Wakati wa kuunda maneno kutoka kwa jedwali, wakumbushe wanafunzi kuwa wanaweza tu kutengeneza haya maneno wakitumia sauti au silabi zilizo kwenye jedwali. Maneno hayo ni sharti yawe maneno halisi yenye maana.

**Kazi ya Ziada**

Wanafunzi waandike neno **mama** mara mbili kisha waonyeshe wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 2: Siku ya 1 na 2 — Nyumbani

Tamka sauti.

u a m

Tamka sauti ya herufi na silabi.

u | m u | a | m a

u | mu | a | ma

Soma silabi na maneno.

ma ma | ma u a | u a | u ma

**mama** **maua** **ua** **uma**

Tamka sauti.

u

Tamka sauti ya herufi na silabi.

u u | mu u | a a | ma a

uu | muu | aa | maa

Soma neno zima.

anaona paka na

6

**WIKI YA 2: SOMO LA 1**

***Mwalimu:*** Fungua kitabu ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Weka kalamu kisha funga.

**Ufahamu wa fonimu: Utambuzi wa sauti**

Wiki iliyopita tulijifunza sauti **/m/** na **/a/**. Leo tutajifunza sauti mpya **/u/**. Tutaitamka, kisha nitataja maneno. Mtasema ikiwa maneno hayo yanaanza kwa sauti **/u/**. Ikiwa yanaanza kwa sauti hiyo, mwalimu akubaliane na wanafunzi ishara ya kutumia. Iwapo hayaanzi kwa sauti hiyo, mwalimu akubaliane na wanafunzi ishara ya kutumia.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Sauti ni **/u/**. Neno la kwanza ni **ukuta**. Neno **ukuta** linaanza kwa sauti **/u/** kwa hivyo mwalimu afanye ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno lingine ni **tatu**. Neno hili halianzi kwa sauti **/u/** kwa hivyo mwalimu afanye ishara waliokubaliana.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tutaje sauti **/u/** pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/u/**

***Mwalimu:*** Neno la kwanza ni **ukuta**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno la pili ni **tatu**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sauti ambayo tumejifunza ni?

***Wanafunzi:*** **/u/**

***Mwalimu:*** Neno la kwanza ni **ukuta**.

***Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno la pili ni **tatu**.

***Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana. *(Tumia hatua ya 3 kufunza ukitumia maneno haya: **uta, tatu, uki, kuku**).*

■ **Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Tutajifunza **jina** na **sauti** ya herufi **uu.** Mwalimu awapatie wanafunzi kadi za herufi **u** katika breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Jina la herufi hii ni **uu**. Sauti ya herufi hii ni **/u/**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tutaje hii herufi pamoja. Jina la herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **uu**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/u/**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **uu**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **/u/**

***Eleza wanafunzi wasome sauti kwenye vitabu vyao ukurasa wa [ukurasa wa breli unaolingana].***

● **Silabi: Kusoma na kuandika**

Juma lililopita tulijifunza silabi **ma** na **a.** Leo tutajifunza silabi zifuatazo: **mu, u, ma** na **a.** Nitatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **/m/ /u/–mu**. Silabi hii ni **mu**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tuseme pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/m/ /u/ – mu**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa mtasema peke yenu.

***Wanafunzi:*** **/m/ /u/ – mu**.

*(Tumia hatua ya 1–3 kufunza silabi hizi: **u, ma, a**)*. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**Hatua ya 4:**

Sasa nitatamka kila sauti huku nikiiandika silabi **mu**. Nisikilize. **/m/ /u/ – mu.**

**Hatua ya 5**

***Mwalimu:*** Sasa tutamke kila sauti huku mkiiandika silabi **mu**. *(Wanafunzi wanaiandika silabi huku wakiitamka).*

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/m/ /u/ – mu.**

**Hatua ya 6**

***Mwalimu:*** Sasa tamkeni kila sauti huku mkiiandika silabi **ma**.

***Wanafunzi:*** **ma**

▬ **Maneno: Kusoma maneno kwa kutumia silabi**

Wiki iliyopita tulijifunza haya maneno: **mama**, **ama**, **anaona**, **paka** na neno **na.** Leo tutatumia silabi kusoma maneno mengine.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **ma ma – mama**. Neno hili ni **mama.**

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Wanafunzi, tuseme pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **ma ma – mama.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa mtasema peke yenu.

***Wanafunzi:*** **ma ma – mama.**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno **maua, ua, uma.**)*

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Sasa nitatamka kila silabi huku nikiliandika neno **uma**. Nisikilize. **u ma – uma**.

**Hatua ya 5**

***Mwalimu:*** Sasa tutamke kila silabi huku mkiliandika neno **uma**. Tuanze.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **u ma – uma**

**Hatua ya 6**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila silabi huku mkiliandika neno **maua**.

***Wanafunzi:*** **ma u a - maua**.

**Hadithi ya mwanafunzi**

**Kabla ya kusoma: hadithi**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu baadhi ya maneno yanayopatikana kwenye hadithi hiyo. Pia tutasoma kichwa cha hadithi na kusikiliza maelezo. Baadaye tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. Neno la kwanza ni **uma.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia hili neno **uma**? *(Wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana).* Ni wangapi kati yenu wanaojua maana ya neno hili? *(Wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi watafanya ishara, waambie wajadiliane na wenzao. Ikiwa ni wachache wanaolielewa sema* - maana ya neno **uma** ni ***kushika kwa meno*** au ***kifaa cha kulia chakula.*** *(Igiza na wanafunzi neno **uma** kwa kushika kwa meno na uonyeshe kifaa uma).*

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme maana ya neno uma pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Kushika kwa meno.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Semeni maana ya neno uma pamoja.

***Wanafunzi:*** Kushika kwa meno kifaa kama kijiko chenye menomeno cha kulia chakula. *(Tumia hatua ya 1-3 kufunza neno **maua.**) Onyesha maua.*

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Hebu tusome kichwa cha hadithi na kusikiza maelezo kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Kichwa cha hadithi hii ni **Paka na ua**. Je, tunajua nini kuhusu **Paka na ua**?
***Mwalimu na Wanafunzi:*** (*Wajibu swali).*

***Mwalimu:*** Ni vitu gani umezisikia kwenye maelezo? (Wanafunzi wataje vitu mbalimbali walivyovisikia). ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Mgeukie mwenzako kisha umweleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii. (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao).*

**Wakati wa kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** Hakikisha umefungua ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu. Kumbuka kufuatilia kidole. Sikiliza kwa makini.

**Paka na Ua**

Mama anaona uma na maua. Paka anaona ua. Paka, uma ua.

**Baada ya kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** (*Waulize wanafunzi wachache ikiwa utabiri wao ulitimia au la. Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya **Paka na Ua**. Sema),* je utabiri wenu ulitimia? *(Wanafunzi wanajibu.)* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Swali la kwanza. ***Taja kitu kimoja ambacho mama anakiona.*** Jibu la swali hili lapatikana moja kwa moja kwenye mstari wa kwanza unaosema: Mama anaona uma na maua. **Kitu kimoja ambacho mama anaona ni uma**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Swali la pili. ***Taja kitu kingine ambacho mama anakiona***. Tuangalie jibu kwenye hadithi pamoja. Hebu tusome sentensi ya kwanza pamoja. **Kitu kingine ambacho mama anaona ni maua**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Swali la tatu. ***Je, paka anaona nini?*** Wape wanafunzi muda wa kutafuta jibu. Chagua mwanafunzi mmoja kujibu swali huku akisoma sentensi katika hadithi.

**Kuandika na kusoma**

Sasa tutafanya mazoezi ya kuandika maneno tuliyojifunza. Baadaye nitawapatia kazi ya ziada.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Leo tutaandika maneno matano tuliyojifunza. Maneno haya ni **uma, ua, maua, paka na mama**. Nitasema neno, nanyi mtaliandika vizuri na kwa usahihi.

Hebu Nisikilize. Nitalisema neno **uma** kisha niliandike. Ninapoandika, ni lazima nisikilize sauti, nitatamka kila silabi kwa makini huku nikiandika neno.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tufanye pamoja. Nitalitamka neno mara mbili, kisha mtaliandika nami nitaliandika. Neno lingine ni **ua, ua.** Hebu tuandike neno **ua**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** *(Wanaandika)*

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa ni zamu yenu. Nitalitamka neno mara mbili nanyi mtaliandika.

Neno ni **maua, maua**.

Neno lingine ni **paka, paka**.

Neno la mwisho ni **mama, mama**.

**Kazi ya Ziada**

Leo tumesoma neno **ua** na **maua**. Mtaandika kila neno mara mbili kisha uonyeshe wenzako.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 2: Siku ya 1 na 2 | Nyumbani

Tamka sauti.

u a m

Tamka sauti ya herufi na silabi.

u | m u | a | m a
u | mu | a | ma

Soma silabi na maneno.

ma ma | ma u a | u a | u ma
mama | maua | ua | uma

Tamka sauti.

u

Tamka sauti ya herufi na silabi.

u u | mu u | a a | ma a
uu | muu | aa | maa

Soma neno zima.

anaona | paka | na

6

**WIKI YA 2: SOMO LA 2**

▲ **Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Jana tulijifunza jina na sauti ya herufi **/u/.** Leo tutajifunza **jina** na **sauti** ya herufi **u** tena.

Wapatie wanafunzi kadi ya herufi **u** katika breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** (*Onyesha herufi **u** kisha useme*), jina la herufi hii ni **uu.** Sauti ya herufi hii ni **/u/**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tuseme sote. Jina la herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **uu**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi: /u/***

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **uu**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Wanafunzi: /u/***

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

⬬ **Silabi: Kuzisoma**

Jana tulijifunza silabi: **a, ma, mu** na **u**. Leo tutatumia sauti tulizozisoma kusoma silabi.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **/u/ /u/- uu**. Silabi hii ni **uu**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tusome pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi: /u/ /u/*** - **uu**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Someni peke yenu.

***Wanafunzi: /u/ /u/*** - **uu**.

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza silabi hizi: **muu, aa,** na **maa**).* Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

★ **Maneno: Kusoma na kuandika maneno mazima**

Sasa tutasoma maneno tuliyoyasoma wiki iliyopita. Maneno haya tutayasoma bila silabi.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **anaona**. Neno hili ni **anaona**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tuseme pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **anaona**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa.

***Wanafunzi:*** **anaona**.

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno: **paka, na).***

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Nitasoma neno paka huku nikiliandika neno hilo. Nisikilize. **paka.**

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme neno **paka** huku tukiliandika.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **paka.**

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Semeni neno **paka** huku mkiliandika tena.

***Wanafunzi:*** **paka.**

**Hadithi ya mwanafunzi**

Wiki ya 2: Siku ya 1 na 2 | Nyumbani

Meza imefunikwa kwa kitambaa. Kuna viti vinne. Sahani na uma ziko juu ya meza. Pia kuna maua juu ya meza. Paka yuko chini.

Paka na Ua

Mama anaona uma na maua.
Paka anaona ua.
Paka uma ua.

7

### 🕮 Kabla ya kusoma: hadithi

Ni wakati wa kuisoma tena hadithi tuliyoisoma jana.

### 🕮 Wakati wa kusoma

***Mwalimu:*** Hakikisha umefungua ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Ninasoma sasa. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuisome hadithi hii pamoja huku tukiifuatilia kwa kidole.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** *(Wanaisoma hadithi).*

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii pamoja huku mkiifuatilia kwa kidole.

***Wanafunzi:*** *(Wanaisoma hadithi peke yao).*

**Paka na Ua**

**Mama anaona uma na maua. Paka anaona ua. Paka, uma ua.**

### ⟐ Baada ya kusoma hadithi

***Mwalimu:*** Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Swali la kwanza. ***Unafikiri paka alikuwa wapi? Tetea jibu lako.*** Jibu la swali hili halipatikani moja kwa moja kwenye hadithi. Inabidi tutumie taarifa tuliyoisoma na maarifa yetu kulijibu. **Huenda paka alikuwa jikoni. Hii ni kwa sababu sentensi ya kwanza inasema, mama anaona uma na maua.** Kumbuka jana tulisema uma ni kifaa cha kulia. Pengine basi paka alikuwa jikoni kwa sababu uma huwa jikoni.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu sasa tuseme jibu kuhusu alikokuwa paka.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Huenda paka alikuwa jikoni.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Taja mahali pengine unapofikiria alikuwa yule paka.

***Wanafunzi:*** *(Wajibu. Wanaweza kusema huenda ndani ya nyumba kulikuwa na maua au alikuwa kwenye bustani au alikuwa nje n.k.).*

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Swali la pili. ***Unafikiri maua ni ya nani?*** Jibu la swali hili halimo kwenye hadithi. Inabidi tutumie maarifa yetu kujibu maswali. Kwa kawaida maua huwa ya familia.

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Hebu tusome jibu pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Huenda maua yalikuwa ya familia.

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Je, unafikiria maua yanaweza kuwa ya nani mwingine?

***Wanafunzi:*** *(Wajibu. Yaweza kuwa ya mama, kaka n.k.).*

**Hatua ya 7:**

***Mwalimu:*** Swali la tatu. ***Je, unafikiri paka atauma ua?*** Jibu la swali hili halijitokezi waziwazi kwenye hadithi. Inabidi tutumie maarifa yetu kutoa jibu. Sentensi ya mwisho inasema: paka, uma ua. Hii inamaanisha kuna anayemwambia afanye kitendo cha kuuma. Huenda paka hakusikia alichoambiwa kwa hivyo hakuuma ua.

**Hatua ya 8:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Huenda paka hakusikia alichoambiwa kwa hivyo hakuuma ua.

**Hatua ya 9:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Toa maoni yako kuhusu alichofanya paka alipoambiwa aume ua. ***Wanafunzi:*** (Wanajibu. Wanaweza kusema aliuma ua, alitoroka, alisema miau bila kufanya chochote n.k.)

### ✍ Kuandika na kupanga maneno

Sasa tutafanya mazoezi ya kuandika maneno kwa kutumia silabi na herufi zilizochanganywa. Baadaye nitawapatia kazi ya ziada.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Leo tutapanga silabi ili tuunde na kuandika maneno ambayo tumejifunza. Kwa mfano kutokana na silabi hizi **aum** tunapanga silabi na herufi ili tuunde neno **uma**. Nitasema silabi hizi kisha nizipange vizuri ili niunde neno **uma**. Nitaandika neno **uma**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tufanye pamoja. Tutapanga silabi na herufi **kapa** ili tuunde na kuandika neno. Kutokana na silabi hizi **ka pa** tunaweza kuunda neno **paka**. Hebu tuandike neno **paka** kwa kupanga silabi na herufi hizi vizuri.Sasa andikeni neno **paka**. Nitaandika neno hili pia.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** (Wanafunzi waandike).

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa ni zamu yenu. Mtapanga silabi na herufi ninazozitamka, kisha mtazipanga na kuandika neno. Silabi hizi ni **ma u**. Sasa mtapanga silabi hizi ili muunde neno. Andikeni neno hilo.

### 🗒 Kazi ya Ziada

Mwalimu awapatie wanafunzi kadi zenye changanyiko wa silabi zifuatazo katika breli

- ma u        - ma am
- ka pa

Wanafunzi waende na waandike maneno halisi na wonyeshe wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

Wiki ya 2: Siku ya 3 na 4 Nyumbani

Tamka sauti.

k m a u

Tamka sauti ya herufi na silabi.

k a | k u | ka a | ku u

**ka** | **ku** | **kaa** | **kuu**

Soma silabi na maneno.

ku ku | u ku ta | ka ka | a mu a

**kuku** | **ukuta** | **kaka** | **amua**

Tamka sauti.

k

Tamka sauti ya herufi na silabi.

k a | k u | m a | m u

**ka** | **ku** | **ma** | **mu**

Soma sehemu za neno na neno lote.

a ka amua | a ka mu uma

**akaamua** | **akamuuma**

ku kaa

**kukaa**

8

**WIKI YA 2: SOMO LA 3**

***Mwalimu:*** Fungua kitabu ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Weka kalamu kisha funga.

**Ufahamu wa fonimu: Utambuzi wa sauti**

Tutajifunza sauti mpya **/k/**. Tutaitamka, kisha nitataja maneno. Mtasema ikiwa maneno hayo yanaanza kwa hiyo sauti. Ikiwa yanaanza kwa sauti hiyo, mwalimu akubaliane na wanafunzi ishara ya kutumia. Ikiwa hayaanzi kwa hiyo sauti, mwalimu akubaliane na wanafunzi ishara ya kutumia.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Sauti ni **/k/**. Neno la kwanza ni **kaka**. Neno **kaka** linaanza kwa sauti **/k/** kwa hivyo mwalimu afanye ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno lingine ni **mama**. Neno **mama** halianzi kwa sauti **/k/** kwa hivyo mwalimu afanye ishara waliokubaliana.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tutaje sauti **/k/** pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:* /k/**

***Mwalimu:*** Neno la kwanza ni **kaka**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno la pili ni **mama**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sauti ambayo tumejifunza ni?

***Wanafunzi:* /k/**

***Mwalimu:*** Neno la kwanza ni **kaka**.

***Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno la pili ni **mama**.

***Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

*(Tumia hatua ya 3 kufunza maneno:* ***kama, tatu, ukuta, kuku, kiko****).*

■ **Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Leo tutajifunza **jina** na **sauti** ya herufi **ka**.

Wapatie wanafunzi kadi zenye herufi **k** katika breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** *Onyesha herufi* ***k*** *kisha useme:* Jina la herufi hii ni **ka**. Sauti ya herufi hii ni **/k/**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Jina la herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:* ka**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:* /k/**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

***Wanafunzi:* ka**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Wanafunzi:* /k/**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

● **Silabi: Kusoma na kuandika**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

Katika kipindi kilichopita, tulijifunza silabi **a, u, mu** na **ma**. Leo tutatumia sauti **/k/** ambayo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **/k/ /a/– ka**. Silabi hii ni **ka**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tuseme pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:* /k/ /a/ – ka**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

***Wanafunzi:* ka**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Wanafunzi:* /k/**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao (breli).

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Sasa nitatamka kila sauti huku nikiiandika silabi **ka**. Nisikilize. **/k/ /a/ –ka.**

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Tutamke sauti hii huku tukiiandika silabi **ka**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** *(Wanaiandika silabi* **ka** *huku wakiitamka.)*

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Sasa mtatamka kila sauti huku mkiiandika silabi **ku, u**.

***Wanafunzi:*** *(Wanaiandika silabi* **ku – u** *huku wakiitamka).*

**Maneno: Kusoma na Kuandika kwa Silabi**

Katika kipindi kilichopita, tulijifunza maneno yafuatayo: **uma, mama, amu, au, ua.** Leo tutatumia silabi kusoma maneno mengine.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **ku ku – kuku**. Neno hili ni **kuku.**

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tuseme pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **ku ku – kuku.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa semeni peke yenu.

***Wanafunzi:*** **ku ku - kuku**. *(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno,* ***kaka, ukuta, amua****).*

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Sasa nitatamka kila silabi huku nikiliandika neno **kuku** ubaoni**.** Nisikilize **ku ku – kuku**.

**Hatua ya 5**

***Mwalimu:*** Sasa tutatamka kila silabi huku tukiliandika neno **kuku**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** *(Wanaliandika neno* **kuku** *huku wakilitamka.)*

**Hatua ya 6**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Mtatamka kila silabi huku mkiliandika neno **kaka**.

***Wanafunzi:*** **ka ka – kaka.**

**Kabla ya kusoma: hadithi**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu kifungu cha maneno ambacho kinapatikana kwenye hadithi hiyo. Pia tutasoma kichwa cha hadithi na kusikiliza maelezo. Kisha tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. Kifungu chenyewe ni **Akaamua kukaa.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kukisikia kifungu hiki **akaamua kukaa**? *(Wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana).* Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya kifungu hiki? *(Wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana, waambie wajadiliane na wenzao kisha waeleze darasa lote. Ikiwa ni wachache wanaolielewa sema),* maana ya kifungu hiki **akaamua kukaa** ni **kukubali kukaa**

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme maana ya hiki kifungu **akaamua kukaa** pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Kukubali kukaa.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Semeni peke yenu maana ya hiki kifungu **akaamua kukaa**.

***Wanafunzi:*** Kukubali kukaa.

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** (*Onyesha wanafunzi kichwa cha hadithi na wasikize maelezo kwenye ukurasa wa* ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** *kisha useme),* tutazame kichwa cha hadithi.

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Hebu tutazame kichwa cha hadithi. Kichwa cha Hadithi hii ni **Paka na Kaka**. Je, tunajua nini kuhusu **Paka na Kaka**?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** (*Wajibu swali).*

***Mwalimu:*** Hebu tusikilize maelezo. Ni kitu gani umesikia kutokana na maelezo? *(Wanafunzi 3 – 4 wapewe nafasi wajibu).*

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Mgeukie mwenzako kisha umueleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii. *(Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao).*

**Wakati wa kusoma hadithi**

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Fungua ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuisome hadithi hii pamoja huku tukiifuatilia kwa kidole.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** *(Wanaisoma hadithi).*

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii pamoja huku mkiifuatilia kwa kidole.

***Wanafunzi:*** *(Wanaisoma hadithi peke yao).*

**Paka na kaka**

**Paka akaamua kukaa. Mama akaamua kukaa. Kaka akaamua kukaa. Paka akamuuma kaka. Paka akamuuma mama.**

**Baada ya kusoma hadithi**

*(Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao ulitimia au la. Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya* ***Paka na Kaka****.) Sema,* je utabiri wenu ulitimia? *(Wanafunzi wanajibu.)* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Swali la kwanza. ***Taja watu wawili walioamua kukaa.*** Jibu la swali hili lapatikana kwenye hadithi. Hebu tusome tena sentensi ya tatu na ya nne. **Mtu mmoja aliyeamua kukaa ni mama.**

# Wiki ya 2: Siku ya 3

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **Mtu mmoja aliyeamua kukaa ni mama.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Je, nani mwingine aliyeamua kukaa.

***Wanafunzi:*** **Kaka aliamua kukaa.**

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Swali la pili. ***Paka alimuuma nani?*** Jibu la swali hili lapatikana kwenye hadithi. *(Soma)* hadithi tena. Kutokana na sehemu niliyosoma, **Paka alimuuma kaka.**

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **Paka alimuuma kaka.**

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Je, ni nani mwingine aliyeumwa na paka?

***Wanafunzi:*** **Paka alimuuma mama.**

### Kuandika na kusoma

Sasa tutafanya mazoezi ya kuandika maneno tuliyojifunza. Baadaye nitawapatia kazi ya ziada.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Leo tutaandika maneno matano tuliyojifunza. Maneno haya ni **kaka**, **kuku**, **kukaa**, **akaamua** na **akamuuma**. Nitasema neno, nanyi mtaliandika vizuri na kwa usahihi.

Hebu nisikilize. Nitalisema neno **kaka** kisha niliandike. Ninapolisema, ni lazima msikilize sauti, nitatamka kila silabi makini huku nikiandika neno.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tufanye pamoja. Nitalitamka neno mara mbili, kisha mtaliandika nami pia nitaliandika huku tukitamka silabi za neno. Hebu tuandike neno **kuku**. Neno lingine ni **kuku, kuku**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa ni zamu yenu. Nitalitamka neno mara mbili nanyi mtaliandika.

Neno ni **kukaa, kukaa.**

Neno lingine ni **akaamua, akaamua.**

Neno la mwisho ni **akamuuma, akamuuma.**

### Kazi ya Ziada

Mkienda nyumbani mtaandika neno **kuku** mara tatu na umuonyeshe mwenzako.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kabla ya kusoma hadithi mwalimu huzungumza kuhusu msamiati, husoma kichwa cha hadithi, hujadili picha na wanafunzi hatimaye hutoa utabiri.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 2: Siku ya 3 na 4 **Nyumbani**

**Mvulana anatokwa na damu kwa mguu. Paka anakimbia.**

**Paka na Kaka**

Paka akaamua kukaa.
Mama akaamua kukaa.
Kaka akaamua kukaa.
Paka akamuuma kaka.
Paka akamuuma mama.

9

**WIKI YA 2: SOMO LA 4**

**▲ Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Jana tulijifunza jina na sauti ya herufi **ka**. Leo tutajifunza jina na sauti ya herufi kubwa **ka** tena. Wapatie wanafunzi kadi yenye herufi **k** katika breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** *(Onyesha herufi **k** kisha useme),* jina la herufi hii ni **ka**. Sauti ya herufi hii ni **/k/**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tutaje sote. Jina la herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **Ka**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** /k/

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **Ka**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** /k/

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

**⬬ Silabi: Kuzisoma**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

Tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma silabi.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **/k/ /a/**. Silabi hii ni **ka**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tuseme pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/k/ /a/- ka.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu. Sasa someni peke yenu.

***Wanafunzi:*** **/k/ /a/- ka.**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza silabi hizi: **ma, ku, mu**)*

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

**★ Kusoma maneno marefu**

Tutajifunza jinsi ya kusoma neno kwa kutumia sehemu ya neno yenye maana. Sehemu hii wakati mwingine huwa kubwa kuliko silabi.

Mwalimu awapatie wanafunzi kadi zenye maneno katika breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** (Onyesha neno **akaamua**)

Nisikilize. **a ka amua - akaamua.**

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tusome pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **a ka amua – akaamua.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa mtafanya peke yenu.

***Wanafunzi:*** **a ka amua - akaamua**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno haya: **a ka mu uma - akamuuma; ku kaa - kukaa**)*

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

**Hadithi ya mwanafunzi**

**🕮 Kabla ya kusoma: hadithi**

Ni wakati wa kusoma tena hadithi tuliyoisoma jana.

**Wakati wa kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** Hakikisha umefungua ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma. Nasoma sasa.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Hebu tuisome hadithi hii pamoja huku tukiifuatilia kwa kidole.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** *(Wanaisoma hadithi).*

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii pamoja huku mkiifuatilia kwa kidole.

***Wanafunzi:*** *(Wanaisoma hadithi peke yao).*

🕮 **Paka na Kaka**

**Paka akaamua kukaa. Mama akaamua kukaa. Kaka akaamua kukaa. Paka akamuuma kaka. Paka akamuuma mama.**

◈ **Baada ya kusoma hadithi**

Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Swali la kwanza. ***Unafikiri walikalia nini?*** Jibu la swali hili halipatikani kwenye hadithi. Inabidi tutumie ujuzi wetu kujibu. Kwa kawaida watu hukaa kwenye viti. Je, wanyama? Wao pia wanaweza kukalia viti. Hivyo basi tunaweza kusema walikalia viti.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **Walikalia viti.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Je, unafikiri walikalia nini?

***Wanafunzi:*** *(Wajibu. Wanaweza kusema mkeka, chini sakafuni n.k.)*

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Swali la pili. ***Kama ungelikuwa kaka ungelifanya nini?*** Jibu la swali hili halipatikani kwenye hadithi. Inabidi tutumie ujuzi wetu kujibu. Mtu akiumwa na paka, huenda kwa daktari. Pengine kaka angeenda kumwona daktari.

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Kama ni wewe ungefanya nini?

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Taja kile ungelifanya kama ungelikuwa kaka.

***Wanafunzi:*** *(Wajibu. Ningelia/ningempiga yule paka n.k).*

✍ **Kuandika na kupanga maneno**

Sasa tutafanya mazoezi ya kuandika maneno kwa kutumia silabi na herufi zilizochanganywa. Baadaye nitawapatia kazi ya ziada.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Leo tutapanga silabi ili tuunde na kuandika maneno ambayo tumejifunza. Kwa mfano kutokana na silabi hizi **ukuk** tunapanga silabi na herufi ili tuunde neno **kuku**. Nitasema silabi hizi kisha nizipange vizuri ili niunde neno **kuku**. Nitaandika neno **kuku**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tufanye pamoja. Tutapanga silabi na herufi **kaaku** ili tuunde na kuandika neno. Kutokana na silabi hizi **kaaku** tunaweza kuunda neno **kukaa**. Hebu tuandike neno **kukaa** kwa kupanga silabi na herufi hizi vizuri.Sasa andikeni neno **kukaa**. Nitaandika neno hili pia.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa ni zamu yenu. Mtapanga silabi na herufi ninazozitamka, kisha mtazipanga na kuandika neno. Silabi hizi ni **amam**. Sasa mtapanga silabi hizi ili muunde neno. Andikeni neno hilo.

🗒 **Kazi ya Ziada**


Mwalimu awapatie wanafunzi kadi zenye mchanganyiko wa silabi zifuatazo katika breli.

- uk uk
- amam
- kaaku

**Vidokezo vya Mwalimu**

Sauti za herufi ni muhimu kwa kusaidia mwanafunzi kusoma kwa haraka. Ni wajibu wako kuhakikisha umefanya mazoezi ya kutamka sauti za herufi kabla ya kuzifunza na kuzisema darasani.

Tarehe: ________________________ Muda: ________________ Idadi: ________________



Wiki ya 2: Siku ya 5 **Nyumbani**

Tamka sauti.

u k

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: ma ka a – **makaa**

| | | | |
|---|---|---|---|
| ma | ka | u | ka |
| kaa | mu | k | a |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

paka **na** uma. mama **na** kaa.
uma **na** makaa. kaka **na** mama.

**Mama na Paka**

Mama anaona paka na ua.
Kaka anaona uma na makaa.
Paka anaona mama na kaa.
Kaka akaamua kukaa na paka.

10

**WIKI YA 2: SOMO LA 5**

■ **Marejeo: Ufahamu wa herufi**

Leo tutarejelea herufi tulizojifunza wiki hii. Tutajikumbusha herufi **uu** na **ka**. Tutatamka sauti za herufi hizo.

Wanafunzi wapatiwe kadi zenye herufi **u** na **k** katika breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** *(onyesha **u**, kisha useme),* Nisikilize. **uu**. Sauti ya herufi hii ni **/u/**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tuseme pamoja jina ya herufi hii ni.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **uu**

***Mwalimu:*** Sasa tutamke pamoja sauti ya herufi hii.

***Mwalimu na Wanafunzi:* /u/**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni:

***Wanafunzi:*** **uu**

***Mwalimu:*** Sasa tamkeni sauti ya herufi hii.

***Wanafunzi:* /u/**

*Tumia hatua ya 3 kufunza ka **(k)** na sauti yake.*

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

★ **Silabi: Kuandika**

Tutatumia silabi kadhaa tulizopewa kuandika maneno.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. *(Mwalimu asome silabi zote zilizopeanwa)*

Naweza kutumia silabi **ma** na **kaa** kuunda neno **makaa.**

**Hatua ya 2:**

Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

***Mwalimu:*** Tusome silabi hizi zote pamoja. *(Mwalimu na wanafunzi wasome silabi zote).*

***Mwalimu:*** Hebu tuunde neno lingine pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:* a mu–amu.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Soma silabi huku mwenzako akisikiliza.

***Mwalimu:*** Tumieni silabi hizo kuunda maneno mawili pamoja.

***(Wanafunzi watoe maneno waliyoyaunda katika vikundi vyao). Kwa mfano: amu, mkuu, kama, uma, ua, maua, kukaa.***

● **Sarufi**

Soma sentensi zilizo kwenye kitabu ukurasa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma pamoja na wanafunzi. Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

**Paka na uma. Mama na kaka. Uma na makaa. Kaka na mama.**

**Hadithi ya mwanafunzi**

📖 **Kabla ya kusoma: hadithi**

***Mwalimu:*** Leo tutasoma hadithi nyingine. Nitaisoma kisha tutajibu maswali.

**Wakati wa kusoma hadithi**

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Hakikisha umefungua ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma. Nasoma sasa.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuisome hadithi hii pamoja huku tukiifuatilia kwa kidole.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** *(Wanaisoma hadithi).*

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii pamoja huku mkiifuatilia kwa kidole.

***Wanafunzi:*** *(Wanaisoma hadithi peke yao).*

📖 **Mama na Paka**

**Mama anaona paka na uma. Kaka anaona uma na makaa. Paka anaona mama, kaa na kuku. Kaka akaamua kukaa na paka.**

◈ **Baada ya kusoma hadithi**

Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Swali la kwanza. ***Hadithi hii inazungumza kuhusu nani?*** Jibu la swali hili linapatikana kwenye kichwa cha hadithi kinachosema, mama na paka. Vilevile, sehemu tofauti tofauti za hadithi zinazungumzia wawili hao. Hivyo basi, hadithi hii inahusu mama na paka.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Hadithi hii inahusu mama na paka.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Je, hadithi hii inahusu nani?

***Wanafunzi:*** **Hadithi hii inahusu mama na paka.**

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Swali la pili. ***Mama anaona mnyama gani?*** Jibu la swali hili lapatikana kwenye hadithi. Nalo ni paka. Lakini inabidi uelewe kuwa paka ni aina ya mnyama ili uweze kujibu hili swali. Hivyo basi mama anamwona mnyama aitwaye paka.

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **Mama anamwona mnyama aitwaye paka.**

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Je, mama anaona mnyama gani?

***Wanafunzi:*** **Mama anamwona mnyama aitwaye paka.**

**Hatua ya 7:**

***Mwalimu:*** Swali la tatu. ***Paka anamwona nani?*** Jibu la swali hili lapatikana kwenye hadithi. Nalo ni mama. Lakini inabidi uelewe kuwa mama ni mtu ili uweze kujibu swali hili. Hivyo basi paka anamwona mtu ambaye ni mama.

**Hatua ya 8:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Paka anamwona mtu ambaye ni mama.

**Hatua ya 9:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. **Je, paka anamwona nani?**

***Wanafunzi:*** **Paka anamwona mtu ambaye ni mama.**

**Hadithi ya mwalimu**

**Wakati wa kusoma**

***Mwalimu:*** Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu lakini muwe tayari kwa sababu nitawauliza maswali baada ya hadithi. Sikiza kwa makini. (*Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali).*

**Jamii ya Kilemi**

Jamii ya Babu Kilemi ina watu wengi. Kila Desemba wao huenda kijijini kusherehekea sikukuu ya krisimasi. (***Jamii ya kilemi iliienda wapi kusherehekea Krismasi?***) Baba, mama na watoto hufurahia.

Ndugu, dada na shangazi wote hualikwa. Wajomba na amu wote huja. Wao huchinja mbuzi na kufurahia. Wajukuu na vitukuu husherehekea pia. Koki na Mugambi hucheza na babu na bibi yao. Vile vile wao hupenda kuogelea na kupanda juu ya miti.(***Katika sherehe hii wao huchinja nini?***)

**Kazi ya ziada**

**Kuandika maneno kwa silabi**

Nitawapa kazi ya ziada ya kuandika maneno tuliyojifunza na mengine kutumia silabi.

Wapatie wanafunzi kadi zenye silabi katika breli. Waunde na wayaandike maneno matano kutoka kwa silabi walizopewa.


'ma' 'ka' 'u' 'ka' 'kaa' 'mu' 'k' 'a'

**Kitabu cha Kazi ya Ziada - *Wiki ya 2 Siku ya 5***

**Vidokezo vya Mwalimu**

Kipindi cha somo la Kiswahili kina urefu wa dakika 30. Hakikisha unafunza kwa utaratibu ndio uweze kumaliza kufunza somo kwa muda uliopewa. Ukurasa wa v una mpangilio wa kila sehemu na vile unavyostahili kufunza na muda wake.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Wiki ya 3: Siku ya 1 na 2 **Nyumbani**

Tamka sauti.

t k u

Tamka sauti ya herufi na silabi.

t a ta a t u tu u

**ta** **taa** **tu** **tuu**

Soma silabi na maneno.

ta ka ta ka a ta ka

**takataka** **ataka**

a ka ta ka a mu

**akataka** **amu**

Tamka sauti.

t

Tamka sauti ya herufi na silabi.

tu u ku u mu u k u

**tuu** **kuu** **muu** **ku**

Soma sehemu za neno na neno lote.

ku mu ua a ka taka

**kumuua** **akataka**

ku mu uma a ka kataa

**kumuuma** **akakataa**

11

**WIKI YA 3: SOMO LA 1**

**Ufahamu wa fonimu: Utambuzi wa sauti**

Wiki iliyopita tulijifunza sauti **/u/** na **/k/**. Leo tutajifunza sauti mpya **/t/**. Tutaitamka, kisha nitataja maneno. Mtasema ikiwa maneno hayo yanaanza kwa sauti hiyo. Ikiwa yanaanza kwa sauti hiyo, mwalimu akubaliane na wanafunzi ishara ya kutumia. Ikiwa hayaanzi kwa sauti hiyo, mwalimu akubaliane na wanafunzi ishara ya kutumia.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Sauti ni **/t/**. Neno la kwanza ni **tatu**. Neno **tatu** linaanza kwa sauti **/t/** kwa hivyo mwalimu afanye ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno lingine ni **matatu**. Neno **matatu** halianzi kwa sauti **/t/** kwa hivyo mwalimu afanye ishara waliokubaliana.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tutaje sauti **/t/** pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/t/**

***Mwalimu:*** Neno la kwanza ni **tatu**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno la pili ni **matatu**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Sauti ni?

***Wanafunzi:*** **/t/**

***Mwalimu:*** Neno la kwanza ni **tatu**.

***Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno la pili ni **matatu**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

*(Tumia hatua ya 3 kufunza maneno haya: **mataa, tamaa, taa, kitabu, mtoto, tama, makaa, tamu, mti**).*

**Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Ni wakati wa kujifunza **jina** na **sauti** ya herufi **ta**. Wapatie wanafunzi kadi zenye herufi **t** katika breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** *(Onyesha herufi **t** kisha useme),* jina la herufi hii ni **ta**. Sauti ya herufi hii ni **/t/**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tutaje sote. Jina la herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **ta**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/t/**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa jaribuni peke yenu. Jina la herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **ta**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **/t/**

***Mwalimu:*** Sasa nitauliza. Herufi au sauti? Nanyi mtasema herufi au sauti.

***Mwalimu:*** **ta?**

***Wanafunzi:*** herufi.

***Mwalimu:*** **/t/**

***Wanafunzi:*** sauti.

***Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao, ukurasa wa [ukurasa wa breli unaolingana].***

**Silabi: Kusoma na kuandika**

Tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **/t/ /a/- ta**. Silabi hii ni **ta**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/t/ /a/ - ta**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa.

***Wanafunzi:*** **/t/ /a/ - ta**.

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza silabi hizi: **taa ,tu, tuu**)*

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Nitatamka kila sauti huku nikiiandika silabi **ta**. Nisikilize. **/t/ /a/- ta.**

Tamka sauti huku ukiandika silabi.

Tamka ukiandika sauti na wanafunzi huku wakiandika.

Wanafunzi wasome sauti peke yao huku wakiandika kwenye madaftari yao.

**Hatua ya 5**

***Mwalimu:*** Sasa tutatamka kila sauti huku tukiiandika silabi **ta**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/t/ /a/ - ta**.

**Hatua ya 6**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti huku mkiiandika silabi **tuu**.

***Wanafunzi:*** **/t/ /u/ /u/ - tu u**.

**Maneno: Kusoma maneno kwa kutumia silabi**

Hebu sasa tutumie silabi kusoma maneno.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **ta ka ta ka - takataka**. Neno hili ni **takataka**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tuseme pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **ta ka ta ka – takataka**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni wakati wenu sasa. Hebu semeni peke yenu.

***Wanafunzi:*** **ta ka ta ka - takataka**.*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno haya:* ***ataka, akataka,*** *na* ***amu****)*. ***Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao. Ukurasa wa [ukurasa wa breli unaolingana].***

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Nitatamka kila silabi huku nikiliandika neno **amu**. Nisikilize. **a mu – amu.**

**Hatua ya 5**

***Mwalimu:*** Sasa tutatamka kila silabi huku tukiliandika neno **amu**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **a mu – amu**.

**Hatua ya 6**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila silabi huku mkiliandika neno **ataka**.

***Wanafunzi:*** ***a*** **ta ka – ataka**.

**Hadithi ya mwanafunzi**

**Kabla ya kusoma: hadithi**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu maneno ambayo yanapatikana kwenye hadithi hiyo. Pia tutasoma kichwa cha hadithi na kusikiliza maelezo. Kisha tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. Neno la kwanza ni **takataka.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia neno hili **takataka**? *(Wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana).* Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya neno hili? *(Wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu neno hilo. Ikiwa ni wachache wanaolielewa sema),* maana ya neno **takataka** ni **uchafu**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme maana ya neno **takataka** pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **uchafu**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. maana ya neno **takataka**

***Wanafunzi:*** **uchafu**.

*(Tumia hatua 1-3 kufunza maneno haya:* ***amu-ndugu mdogo wa baba, kaa-aina ya mnyama mdogo anayeishi majini.****)*

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** (*Onyesha wanafunzi kichwa cha hadithi na maelezo yaliyo kwenye ukurasa wa* ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** *kisha useme),* tutazame kichwa cha hadithi. Kichwa cha Hadithi hii ni **Kaka na Amu**. Je, tunajua nini kuhusu **Kaka na Amu**? Nafikiri hadithi hii inahusu **kaka**. Pengine ni kaka ana amu.

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Hebu tutazame kichwa cha hadithi. Kichwa cha Hadithi hii ni **Kaka na Amu**. Je, tunajua nini kuhusu **Kaka na Amu**?
***Mwalimu na Wanafunzi:*** (*Wajibu swali).*

***Mwalimu:*** Ni vitu gani umevisikia kwenye maelezo? (***wanafunzi wataje vitu mbalimbali walivyovisikia)***.

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Mgeukie mwenzako kisha umweleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii. (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao).*

**Wakati wa kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** Hakikisha umefungua ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

***Soma hadithi kwa ufasaha huku wanafunzi wakifuatilia kwa vidole. Soma pamoja na wanafunzi kisha wanafunzi wasome peke yao.***

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nasoma sasa. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma.

**Kaka na Amu**

**Kaka anaona takataka. Mama anaona takataka na makaa. Amu anaona takataka, makaa na kaa.Kaa akataka kumuuma amu. Amu akakataa kumuua kaa.**

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuisome hadithi hii pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** *(Wanaisoma hadithi).*

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii pamoja.

***Wanafunzi:*** *(Wanaisoma hadithi peke yao).*

**Baada ya kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** (*Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao ulitimia au la. Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya* ***Kaka na Amu****. Sema),* je utabiri wenu ulitimia au la? *(Wanafunzi wanajibu.)* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Swali la kwanza. ***Taja watu walio kwenye hadithi hii.*** Jibu la swali hili lapatikana kwenye hadithi. Sentensi ya kwanza hadi ya tatu inaanza kwa kutaja watu. Mtu mmoja aliye kwenye hadithi ni kaka. Soma sentensi yenye jibu. Kisha soma na wanafunzi sentensi hiyo.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Mtu mmoja aliye kwenye hadithi ni kaka.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. ***Je, ni nani mwingine aliyetajwa kwenye hadithi hii?***

***Wanafunzi:*** *(Wajibu: Wanaweza kusema mama au amu. Lakini si kaa au takataka. Waeleze kwa nini).*

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Swali la pili. ***Taja vitu vitatu ambavyo amu anaona.*** Chagua mwanafunzi mmoja kujibu swali. Aonyeshe sentensi yenye jibu kisha asome na wanafunzi wenzake.

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Kitu kimoja anachoona amu ni takataka.

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Je, ni vitu vingine vipi anavyoviona amu?

***Wanafunzi:*** *(Wajibu. Wanaweza kutaja makaa au kaa).*

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Leo tutaandika maneno matano tuliyojifunza. Maneno haya ni **kaa, kata, takataka, amu na ataka.** Nitasema neno, nanyi mtaliandika vizuri na kwa usahihi. Hebu nisikilize. Nitalisema neno **kaa** kisha niliandike. Ninapoandika, ni lazima nisikilize sauti, nitatamka kila silabi kwa makini huku nikiandika neno.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tufanye pamoja. Nitalitamka neno mara mbili, kisha mtaliandika nami pia nitaandika huku tukitamka silabi za neno. Neno lingine ni **kata, kata**. Hebu tuandike neno **kata**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** *(Wanafunzi waandike)*

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa ni zamu yenu. Nitalitamka neno mara mbili nanyi mtaliandika.

*(Tamka kila neno mara mbili huku wanafunzi wakiliandika.)*

✍ **Kuandika**

Andika herufi **t**. Waagize wanafunzi waandike.

t t t t t

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya Ziada**

Wanafunzi waandike maneno **kaa** mara tatu na waonyeshe wenzake.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 3: Siku ya 1 na 2 **Nyumbani**

Tamka sauti.

t k u

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| t a | ta a | t u | tu u |
| **ta** | **taa** | **tu** | **tuu** |

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| ta ka ta ka | a ta ka |
| **takataka** | **ataka** |
| a ka ta ka | a mu |
| **akataka** | **amu** |

Tamka sauti.

t

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| tu u | ku u | mu u | k u |
| **tuu** | **kuu** | **muu** | **ku** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku mu ua | a ka taka |
| **kumuua** | **akataka** |
| ku mu uma | a ka kataa |
| **kumuuma** | **akakataa** |

11

**WIKI YA 3: SOMO LA 2**

▲ **Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Jana tulijifunza jina na sauti ya herufi **ta.** Leo tutajifunza **jina** na **sauti** ya herufi **ta**.

Wapatie wanafunzi kadi yenye herufi **'ta'** katika breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** *(Onyesha herufi **t** kisha useme),* jina la herufi hii ni **ta.** Sauti ya herufi hii ni **/t/**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tuseme sote. Jina la herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **ta**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/t/**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **ta**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **/t/**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

⬬ **Silabi: Kuzisoma**

Tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **/t/ /u/ /u/ - tuu**. Silabi hii ni **tu - u**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tusome pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/t/ /uu/ - tuu**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa someni peke yenu.

***Wanafunzi:*** **/t/ /uu/ - tuu**.

*(Tumia hatua ya 3 kufunza silabi hizi: **kuu, muu, ku**).*

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Nitatamka kila sauti huku nikiiandika silabi **tuu**. Nisikilize. **/t/ /uu/- tuu.**

**Hatua ya 5**

***Mwalimu:*** Sasa tutatamka kila sauti huku tukiiandika silabi **tu, u**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/t/ /u/ /u/ - tuu**.

**Hatua ya 6**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti huku mkiiandika silabi **mu** na **u** kwenye madaftari.

***Wanafunzi:*** **/m/ /u/ /u/ - mu - u**.

★ **Maneno: Kusoma na kuandika maneno kwa kutumia silabi**

Nitawafunza jinsi ya kusoma maneno marefu.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **a taka- ataka**. Neno hili ni **ataka**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tufanye pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** a**taka–** a**taka.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Hebu msome peke yenu.

***Wanafunzi:*** **ataka– ataka.**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno haya: **ku mu uma-kumuuma, a ka taka-akataka, a ka kataa (akakataa)**)*

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

**Hadithi ya mwanafunzi**

Wiki ya 3: Siku ya 1 na 2 — **Nyumbani**

**Nje kuna makaa kwa gunia. Kuna takataka za chupa, mifupa, mikebe na makaratasi. Pia kuna kaa.**

**Kaka na Amu**

Kaka anaona takataka.

Mama anaona takataka na makaa.

**Amu anaona takataka, makaa na kaa.**

Kaa akataka kumuuma amu.

Amu akakataa kumuua kaa.

12

### Kabla ya kusoma: hadithi

Tutasoma tena hadithi tuliyoisoma jana kisha tujibu maswali.

### Wakati wa kusoma hadithi

***Mwalimu:*** Hakikisha umefungua ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

Soma hadithi huku wanafunzi wakifuatilia kwa vidole. Soma na wanafunzi kisha wasome peke yao.

### Baada ya kusoma hadithi

***Mwalimu:*** Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Swali la kwanza. ***Eleza kilichomfanya kaa kutaka kumuuma Amu.*** Jibu la swali hili halipatikani kwenye hadithi. Inabidi tufikirie sababu ambazo zingemfanya kaa atake kumuuma Amu. Huenda Amu alimkanyaga.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Swali la pili. ***Takataka hutoka wapi?*** Jibu la swali hili halipatikani kwenye hadithi. Inabidi tutumie maarifa yetu kueleza kunakotoka takataka. Chagua mwanafunzi kujibu swali.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Swali la tatu. ***Rafiki yako anapokutembelea nyumbani kwenu, nyinyi hufanya nini?*** Jibu la swali hili halipatikani kwenye hadithi. Inabidi tutumie maarifa yetu kulijibu. Chagua mwanafunzi mmoja kujibu swali.

### Kuandika na kupanga maneno

Sasa tutafanya mazoezi ya kuandika maneno kwa kutumia silabi na herufi zilizochanganywa. Baadaye nitawapatia kazi ya ziada.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Tamka **atak**. Leo tutapanga silabi ili tuunde na kuandika maneno ambayo tumejifunza. Kwa mfano kutokana na silabi hizi **atak** tunapanga silabi na herufi ili tuunde neno **kata**. Nitasema silabi hizi kisha nizipange vizuri ili niunde neno **kata**. Nitaandika neno **kata**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa ni zamu yenu. Mtapanga silabi na herufi ninazotamka, kisha mtazipanga na kuandika neno. Silabi au herufi hizi ni **aak**. Sasa mtapanga silabi hizi ili muunde neno. Andikeni neno hilo.

### Kazi ya Ziada

Wapatie wanafunzi kadi zenye mchanganyiko wa silabi. Wanafunzi waandike maneno halisi kisha wawaonyeshe wenzao.

Silabi hizi ni:

atak

atak

**Vidokezo vya Mwalimu**

Mwalimu mzuri ni yule anayechukua muda kujiyatarisha kabla ya somo. Ni vizuri kuliangalia somo kabla ya kulifunza. Kujitayarisha vyema kunafanya somo liwe zuri na la kupendeza.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 3: Siku ya 3 na 4 **Nyumbani**

Tamka sauti.

l t k

Tamka sauti ya herufi na silabi.

t i m i k i i

**ti** **mi** **ki** **i**

Soma silabi na maneno.

ti ki ti ki ma m ku u ma ka a

**tikiti** **kima** **mkuu** **makaa**

Tamka sauti.

l i

Tamka sauti ya herufi na silabi.

ti i mi i ki i i i

**tii** **mii** **kii** **ii**

Soma sehemu za neno na neno lote.

a ka kaa a ka taka

**akakaa** **akataka**

a ka ka taa ku kaa

**akakataa** **kukaa**

13

**WIKI YA 3: SOMO LA 3**

**Ufahamu wa fonimu: Utambuzi wa sauti**

Jana tulijifunza sauti /t/. Leo tutajifunza sauti mpya **/i/**. Tutaitamka, kisha nitataja maneno. Mtasema ikiwa maneno hayo yanaanza kwa hiyo sauti. Ikiwa yanaanza kwa sauti hiyo, mwalimu akubaliane na wanafunzi ishara ya kutumia. Ikiwa hayaanzi kwa hiyo sauti, mwalimu akubaliane na wanafunzi ishara ya kutumia.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Sauti ni /**i**/. Neno la kwanza ni **ita**. Neno hili linaanza kwa sauti **/i/** kwa hivyo mwalimu afanye ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno lingine ni **kiti**. Neno kiti halianzi kwa sauti **/i/** kwa hivyo mwalimu afanye ishara waliokubaliana.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tutaje sauti **/i/** pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** /i/

***Mwalimu:*** Neno la kwanza ni **ita**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno la pili ni **kiti**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa ni zamu yenu. Sauti ni?

***Wanafunzi:*** /i/

***Mwalimu:*** Neno la kwanza ni **ita**.

***Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

***Mwalimu:*** Neno la pili ni **kiti**.

***Wanafunzi:*** Wanafanya ishara waliokubaliana.

*(Tumia hatua ya 3 kufunza maneno haya:* ***inuka, nia, kima, itika, kitu****.)*

■ **Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Ni wakati wa kujifunza **jina** na **sauti** ya herufi **i**. Wapatie wanafunzi kadi zenye herufi **i** katika breli..

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** *(Onyesha herufi **i** kisha useme),* jina la herufi hii ni **i.** Sauti ya herufi hii ni **/i/**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tutaje pamoja. Jina la herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **i**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/i/**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **i**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **/i/**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

● **Silabi: Kusoma na kuandika**

Hebu sasa tutumie sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **/t/ /i/- ti**. Silabi hii ni **ti**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tuseme pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** /t/ /i/ - **ti**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa someni peke yenu.

***Wanafunzi:*** /t/ /i/ - **ti**.

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza silabi hizi:* ***mi, ki, i*** *na* ***i****.)* Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Sasa nitatamka kila sauti huku nikiiandika silabi **ti**. Nisikilizeni. **/t/ /i/- ti.**

**Hatua ya 5**

***Mwalimu:*** Tutatamka kila sauti huku tukiiandika silabi **ti**. ***Mwalimu na Wanafunzi:*** /t/ /i/ - **ti**.

**Hatua ya 6**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti huku mkiiandika silabi **ki**.

***Wanafunzi:*** **/k/ /i/ - ki**.

**Maneno: Kusoma maneno kwa kutumia silabi**

Ni wakati wa kutumia silabi kusoma maneno.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **ti ki ti** - **tikiti**. Neno hili ni **tikiti**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tusome pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **ti ki ti - tikiti.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Mtafanya peke yenu sasa.

***Wanafunzi:*** **ti ki ti - tikiti.**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno haya:* ***kima, mkuu, makaa****)* Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Nitatamka kila silabi huku nikiliandika neno **kima** ubaoni. Nisikilize. **ki ma – kima**

**Hatua ya 5**

***Mwalimu:*** Sasa tutatamka kila silabi huku tukiliandika neno **kima**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **ki ma - kima**

**Hatua ya 6**

***Mwalimu:*** Sasa mtatamka kila silabi huku mkiliandika neno **tikiti.**

***Wanafunzi:*** **ti ki ti - tikiti**

📖 **Kabla ya kusoma: hadithi**

Wiki ya 3: Siku ya 3 na 4 — **Nyumbani**

**Ndani ya chumba kuna mama ameketi kwenye kiti. Kima ameketi sakafuni. Mama na kima wanaangaliana. Katikati yao kuna meza. Juu ya meza kuna uki na tikiti.**

**Mama na Kima Mkuu**

Mama anaona Kima mkuu.
Kima mkuu anaona mama.
Mama anaona tikiti na uki mtamu.
Kima mkuu akataka kukaa na mama na amu.
Amu akakataa kukaa na kima mkuu na mama.
Mama akakataa kukaa na amu.
Mama akakaa na kima mkuu.

14

Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu baadhi ya maneno au msamiati unaopatikana kwenye hadithi hiyo. Pia tutasoma kichwa cha hadithi na kusikiza maelezo. Kisha tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. Neno la kwanza ni **kata.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia hili neno **kata**? *(Wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana).* Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya neno hili? *(Wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu neno hilo. Ikiwa ni wachache wanaolielewa sema),* maana ya neno **kata** ni **kugawanya kitu kwenye vipande au kifaa cha kubebea vitu kama vyungu**

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme maana ya neno **kata** pamoja.

***Wanafunzi:*** Kugawanya kitu kwenye vipande au kifaa cha kubebea vitu kama vyungu

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Semeni maana ya neno **kata** peke yenu.

***Wanafunzi:*** Kugawanya kitu kwenye vipande au kifaa cha kubebea vitu kama vyungu

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** (*Onyesha wanafunzi kichwa cha hadithi na maelezo kisha useme),* tutazame kichwa cha hadithi. Kichwa cha Hadithi hii ni **Mama na Kima Mkuu**. Je, tunajua nini kuhusu **Mama na Kima Mkuu**? Nafikiri hadithi hii inahusu watu wawili na kima. Huenda huyo kima ni mfalme ama kiongozi kwa vile ameitwa mkuu.

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Hebu tutazame kichwa cha hadithi. Kichwa cha Hadithi hii ni **Mama na Kima Mkuu**. Je, tunajua nini kuhusu **Mama na Kima Mkuu**?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** (*Wajibu swali).*

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Mgeukie mwenzako kisha umueleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao).*

📖 **Wakati wa kusoma hadithi**

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Hakikisha umefungua ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma. Nasoma sasa.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuisome hadithi hii pamoja.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii pamoja.

# Wiki ya 3: Siku ya 3

### ◈ Baada ya kusoma hadithi

***Mwalimu:*** (*Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao ulitimia au la). Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya* ***Mama na Kima Mkuu****. Sema:* Je, utabiri wenu ulitimia au la? *(Wanafunzi wanajibu.)* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Swali la kwanza. ***Mama alimwona nani?*** Jibu la swali hili lapatikana kwenye sentensi ya kwanza ya hadithi. Mama alimwona kima mkuu.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Semeni jibu peke yenu.

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Swali la pili. ***Kima mkuu aliona nini?*** Jibu la swali hili lapatikana kwenye hadithi. Lakini halijitokezi waziwazi. Hebu nisome sentensi ya pili na ya tatu ya hadithi tena. *(Soma).* Kutokana na sehemu niliyosoma, ikiwa kima mkuu alimwona mama, basi aliona pia uki na tikiti. Kwa vile swali liliuliza kima mkuu aliona nini na si nani, jibu ni kima mkuu aliona uki na tikiti.

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu hilo pamoja.

**Hatua Ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Semeni jibu hilo pamoja.

**Hatua ya 7:**

***Mwalimu:*** Swali la tatu. ***Je, mwisho wa hadithi hii, mama alikaa na nani?*** Jibu la swali hili lapatikana kwenye hadithi. Hebu nisome sentensi ya mwisho hadithi tena. *(Soma).* Kutokana na sentensi hii, mama alikaa na kima mkuu.

**Hatuya ya 8:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme hili jibu pamoja.

**Hatua ya 9:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Mama alikaa na nani?

### ✍ Kuandika na kusoma

Sasa tutafanya mazoezi ya kuandika maneno tuliyojifunza. Baadaye nitawapatia kazi ya ziada.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Leo tutaandika maneno matano tuliyojifunza. Maneno haya ni **kima, mkuu, tikiti, uki na mtamu.** Nitasema neno, nanyi mtaliandika vizuri na kwa usahihi.

Hebu nisikilize. Nitalisema neno **kima** kisha niliandike. Ninapoandika, ni lazima nisikilize sauti, nitatamka kila silabi makini huku nikiandika neno.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tufanye pamoja. Nitalitamka neno mara mbili, kisha mtaliandika nami nitaandika huku tukitamka silabi za neno. Neno lingine ni **mkuu, mkuu**. Hebu tuandike neno **mkuu**.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** (Wanafunzi waandike)

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa ni zamu yenu. Nitalitamka neno mara mbili nanyi mtaliandika.

Neno ni **tikiti, tikiti**.

Neno lingine ni **uki, uki**.

Neno la mwisho ni **mtamu, mtamu**.

### Kazi ya Ziada

Wanafunzi waandike neno **tikiti** mara tatu kisha wawaonyeshe wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati wa kufunza msamiati, unaweza kutumia lugha inayoeleweka na wanafunzi. Pia vitu halisi, picha na maelezo pamoja na kutumia neno kwenye sentensi ni mbinu itakayowasaidia wanafunzi kuelewa vyema.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 3: Siku ya 3 na 4 **Nyumbani**

Tamka sauti.

l t k

Tamka sauti ya herufi na silabi.

t i m i k i i

**ti** **mi** **ki** **i**

Soma silabi na maneno.

ti ki ti ki ma m ku u ma ka a

**tikiti** **kima** **mkuu** **makaa**

Tamka sauti.

l i

Tamka sauti ya herufi na silabi.

ti i mi i ki i i i

**tii** **mii** **kii** **ii**

Soma sehemu za neno na neno lote.

a ka kaa a ka taka

**akakaa** **akataka**

a ka ka taa ku kaa

**akakataa** **kukaa**

13

**WIKI YA 3: SOMO LA 4**

**▲ Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Jana tulijifundisha jina na sauti ya herufi **ii.** Leo tutajifunza **jina** na **sauti** ya herufi **i** tena.

Wapatie wanafunzi kadi zenye herufi **i** katika breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** (*Onyesha herufi **i** kisha useme),* jina la herufi hii ni **ii.** Sauti ya herufi hii ni **/i/**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tuseme sote. Jina la herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **ii**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/i/**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **ii**

***Mwalimu:*** Sauti ya herufi hii ni?

***Wanafunzi:*** **/i/**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

**⬬ Silabi: Kuzisoma**

Tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. **/t/ /i/ /i/**. Silabi hizi ni **ti, i**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tuseme pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/t/ /i/ /i/ - ti i**.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa semeni peke yenu.

***Wanafunzi:*** **/t/ /i/ /i/ - ti - i**.

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza silabi hizi: **mii, kii, ii**.)* Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Sasa nitatamka kila sauti huku nikiiandika silabi **tii**. Nisikilize. **/t/ /i/ /i/ - ti - i**.

**Hatua ya 5**

***Mwalimu:*** Tutatamka kila sauti huku tukiiandika silabi **tii**. ***Mwalimu na Wanafunzi:*** **/t/ /i/ /i/ - ti - i**.

**Hatua ya 6**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti huku mkiiandika silabi **mi i**.

***Wanafunzi:*** **/m/ /i/ /i/ - mi - i**.

**★ Kusoma na kuandika maneno marefu:**

Nitawafunza jinsi ya kusoma maneno kwa kutumia sehemu ya neno yenye maana. Sehemu hii wakati mwingine huwa kubwa kuliko silabi.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize: **a ka kaa -akakaa**. Neno hili ni **akakaa**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme pamoja. Neno ni **akakaa.**

***Mwalimu na Wanafunzi:*** **a ka kaa -akakaa.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa mtafanya peke yenu. Neno ni **akakaa.**

***Wanafunzi:*** **a ka kaa -akakaa.**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno haya: **a ka taka - akataka; a ka kataa – akakataa, ku kaa-kukaa**).* Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

# Wiki ya 3: Siku ya 4

**Hadithi ya mwanafunzi**

Wiki ya 3: Siku ya 3 na 4 **Nyumbani**

**Ndani ya chumba kuna mama ameketi kwenye kiti. Kima ameketi sakafuni. Mama na kima wanaangaliana. Katikati yao kuna meza. Juu ya meza kuna uki na tikiti.**

### Mama na Kima Mkuu

Mama anaona Kima mkuu.
Kima mkuu anaona mama.
Mama anaona tikiti na uki mtamu.
Kima mkuu akataka kukaa na mama na amu.
Amu akakataa kukaa na kima mkuu na mama.
Mama akakataa kukaa na amu.
Mama akakaa na kima mkuu.

14

📖 **Kabla ya kusoma:**

***Mwalimu:*** Tutasoma hadithi tuliyoisoma jana kisha tujibu maswali.

📖 **Wakati wa kusoma hadithi**

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Hakikisha umefungua ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma. Nasoma sasa

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuisome hadithi hii pamoja huku tukifuatilia kwa kidole.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii huku mkifuatilia kwa kidole.

◈ **Baada ya kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Swali la kwanza. ***Unafikiria ni kwa nini kima mkuu alitaka kukaa na mama?*** Jibu la swali hili halipatikani kwenye hadithi. Inabidi tutumie maarifa na ujuzi wetu ili kusikia sababu ambazo zingemfanya kima mkuu atake kukaa na mama. Hadithi inatueleza kuwa kima mkuu aliona mama. Mama alikuwa na uki na tikiti. Huenda kima mkuu alitaka kukaa na mama ili ale asali na tikiti.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Huenda kima mkuu alitaka kukaa na mama ili ale asali na tikiti.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Je, nini kingine kingemfanya kima mkuu atake kukaa na mama?

***Wanafunzi:*** *(Wajibu. Watoe jibu lolote mwafaka kama vile alitaka kukaa nyumbani kama binadamu, kulikuwa na kiangazi naye alikuwa anatafuta chakula, kulikuwa na baridi kali naye alitake mahala pa joto n.k.).*

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Swali la pili. ***Kwa nini amu alikataa kukaa na kima mkuu?*** Jibu la swali hili halipatikani kwenye hadithi. Inabidi tutumie maarifa yetu kueleza sababu zinazoweza kumfanya mtu asitake kukaa na kima. Huenda hakutaka kukaa na mnyama.

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Toa sababu nyingine ambayo ingemfanya amu akatae kukaa na kima mkuu.

***Wanafunzi:*** *(Wajibu. Wanaweza kusema Aliogopa kukaa na kima mkuu; Kima mkuu alitaka chakula n.k.).*

✍ **Kuandika na kupanga maneno**

Sasa tutafanya mazoezi ya kuandika maneno kwa kutumia silabi na herufi zilizochanganywa. Baadaye nitawapatia kazi ya ziada.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Kwa mfano kutokana na silabi hizi **kuum** tunapanga silabi na herufi ili tuunde neno **mkuu**. Nitasema silabi hizi kisha nizipange vizuri ili niunde neno **mkuu**. Nitaandika neno **mkuu**.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tufanye pamoja. Tutapanga silabi na herufi **itikit** ili tuunde na kuandika neno. Kutokana na silabi hizi **itikit** tunaweza kuunda neno **tikiti**. Hebu tuandike neno **tikiti** kwa kupanga silabi na herufi hizi vizuri.Sasa andikeni neno **tikiti**. Nitaandika neno hili pia.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Sasa ni zamu yenu. Mtapanga silabi na herufi ninazozitamka, kisha mtazipanga na kuandika neno. Silabi au herufi hizi ni **maki, mua, ata**.

🗒 **Kazi ya Ziada**

Wapatie wanafunzi kadi zenye mchanganyiko wa silabi '**maki**' '**mua**' '**ata**'. Waandike maneno halisi kisha wawaonyeshe wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 3: Siku ya 5 **Nyumbani**

Tamka sauti.

t i

Tumia silabi kuunda maneno. Kwa mfano: ta tu - **tatu**

| | | | |
|---|---|---|---|
| ma | mi | mu | ta |
| tu | ki | ku | ka |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| wakati uliopo | wakati ujao |
|---|---|
| mama anakaa | mama atakaa. |
| mama anataka | mama atataka. |
| mama anakataa | mama atakataa. |

Amu na Matatu

Amu ataka matatu kuukuu na taa.
Kaka ataka takataka na makaa.
Kama amu atataka takataka na makaa, kaka atakataa katakata.

15

WIKI YA 3: SOMO LA 5

■ **Marejeo: Ufahamu wa herufi**

Leo tutarejelea herufi tulizojifunza wiki hii. Tutajikumbusha **ta** na **ii**. Tutatamka sauti za herufi hizo.

Wapatie wanafunzi kadi zenye herufi **t** na **ii** katika breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** *(onyesha **t**, kisha useme),* **ta**. Sauti ya herufi hii ni **/t/**

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tutaje sote.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** ta

***Mwalimu:*** Sasa tutamke pamoja sauti ya herufi.

***Mwalimu na Wanafunzi:* /t/**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa.

***Wanafunzi:*** **ta**

***Mwalimu:*** Sasa mtamke sauti ya herufi hizi.

***Wanafunzi:* /t/**

***Tumia hatua ya 1-3 kufunza ii na sauti yake.***

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

★ **Silabi: Kuandika maneno**

Tutatumia silabi tulizopewa kuandika maneno.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize *(mwalimu asome silabi zote).*

Naweza kuunganisha silabi **ta** na **tu** kuunda neno: ***tatu***

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tusome silabi hizi zote pamoja. *(Mwalimu na wanafunzi wasome silabi zote kwenye vitabu* ***[ukurasa wa breli unaolingana])***

***Mwalimu:*** Hebu tuunde neno lingine pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:* ki tu-kitu.**

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Soma silabi hizo zote huku mwenzako akisikiliza.

***Mwalimu:*** Tumieni silabi hizo kuunda maneno mawili pamoja.

***(Wanafunzi watoe maneno waliyoyaunda katika vikundi vyao).*** Kwa mfano: **matatu, kata, tamu, tuma, taka, kitu, kuta, miti, kima, n. k.**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana].***

● **Sarufi**

Tutajifunza jinsi ya kutumia wakati uliopo na ujao kwenye sentensi.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize: Mama anakaa - Mama atakaa

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Tusome pamoja.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** Mama anakaa - Mama atakaa

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa.

***Wanafunzi:*** Mama akakaa - Mama atakaa.

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza:*

Mama anataka - Mama atataka.

Mama anakataa - Mama atakataa).

**Hadithi ya wanafunzi**

📖 **Kabla ya kusoma: hadithi**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu baadhi ya maneno au msamiati unaopatikana kwenye hadithi hiyo. Pia tutasoma kichwa cha hadithi na kusikiza maelezo. Kisha tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nisikilize. Neno la kwanza ni **kuukuu.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia hili neno **kuukuu**? *(Wanafunzi wanafanya ishara waliokubaliana).* Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya neno hili? *(Wanafunzi wanaonyesha*

*ishara waliokubaliana. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi wanaonyesha ishara waliokubaliana, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu neno hilo kisha waeleze darasa lote. Ikiwa ni wachache wanaolielewa sema:* Maana ya neno **kuukuu** ni **kitu ambacho kimezeeka ama kuchakaa.**

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme maana ya neno **kuukuu** pamoja.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Semeni maana ya neno **kuukuu** peke yenu.

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza kifungu akakataa katakata – kinachomaanisha **kukataa kabisa**.)*

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** (*Onyesha wanafunzi kichwa cha hadithi na maelezo kisha useme),* tutazame kichwa cha hadithi. Kichwa cha Hadithi hii ni **Amu na Matatu**. Je, tunajua nini kuhusu **Amu na Matatu**? Nafikiri hadithi hii inahusu mtu mmoja - **amu** na gari aina ya matatu. Huenda huyo Amu ni dereva wa matatu.

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Hebu tutazame kichwa cha hadithi. Hadithi hii inahusu **Amu na Matatu**. Je, tunajua nini kuhusu **Amu na Matatu**?

***Mwalimu na Wanafunzi:*** (*Wajibu swali).*

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Mgeukie mwenzako kisha umueleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii (*Chagua mwanafunzi kutoka katika vikundi kadha azungumze kuhusu utabiri wao).*

📖 **Wakati wa kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** Hakikisha umefungua ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Nasoma sasa. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuisome hadithi hii pamoja huku tukifuatilia kwa kidole.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii pamoja huku mkifuatilia kwa kidole.

**Amu na Matatu**

**Amu ataka matatu kuukuu na taa. Kaa ataka takataka na makaa. Kama amu atataka takataka na makaa, kaka atakataa katakata.**

◇ **Baada ya kusoma hadithi**

***Mwalimu:*** *(Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao ulitimia au la).* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Swali la kwanza. ***Amu anataka nini?*** Jibu la swali hili lapatikana kwenye sentensi ya kwanza ya hadithi. Hebu nisome tena sehemu hiyo. *(Soma)*. Kutokana na sentensi hiyo, tunaona kuwa Amu alitaka matatu kuukuu.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

**Hatua ya 3:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Amu anataka nini kingine?

***Wanafunzi:*** Amu alitaka matatu kuukuu na taa.

**Hatua ya 4:**

***Mwalimu:*** Swali la pili. ***Kaa anataka vitu gani?*** Jibu la swali hili lapatikana kwenye sentensi ya pili ya hadithi. Hebu nisome tena sehemu hiyo. *(Soma)*. Kutokana na sentensi hiyo, kaa alitaka takataka

**Hatua ya 5:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

**Hatua ya 6:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Kaa ataka nini kingine?

***Wanafunzi:*** Kaa alitaka makaa.

**Hatua ya 7:**

***Mwalimu:*** Swali la tatu. ***Ni nini kitamfanya kaka kukataa katakata?*** Jibu la swali hili linapatikana kwenye sentensi ya mwisho ya hadithi. Hebu nisome sehemu hiyo tena. *(Soma).* Kutokana na sehemu niliyosoma, tunaambiwa kuwa kaka atakataa katakata ikiwa amu atataka takataka na makaa.

**Hatuya ya 8:**

***Mwalimu:*** Hebu tuseme jibu pamoja.

**Hatua ya 9:**

***Mwalimu:*** Ni zamu yenu sasa. Someni sehemu ya hadithi iliyo na jibu.

**Hadithi ya mwalimu**

📖 **Wakati wa kusoma**

***Mwalimu:*** Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu lakini muwe tayari kwa sababu nitawauliza maswali baada ya hadithi. Nasoma sasa. Sikiza kwa makini. (*Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

**Maneno ya heshima**

Wiki iliyopita tulienda kijijini kwa babu. Babu alikuwa anasherehekea miaka hamsini tangu azaliwe. Babu alichukua nafasi

# Wiki ya 3: Siku ya 5

hiyo kutufundisha maneno ya heshima kama vile'tafadhali' na 'asante'. ***(Babu alikuwa na sherehe gani?)*** Babu alitwambia, "Ukiwa unahitaji chochote, ni vizuri kuomba. Watu wengi husema nataka hiki, nataka kile. Hiyo si lugha ya heshima. Mtoto mwenye heshima husema samahani au tafadhali anapohitaji kitu." ***(Mtoto mwenye heshima husemaje akitaka kitu?)*** Babu akaendelea, "Pia mtu kwa ukarimu wake akikupa kile ulichoomba ni vyema kumshukuru kwa kusema asante au shukrani."

Baada ya kumsikiliza babu, tuliamua kuanza kuyatumia maneno hayo ya heshima. Tulipoenda mezani, nikamwambia bibi, "Bibi, tafadhali naomba mchuzi." Bibi alinipa bakuli la mchuzi. Baada ya kulipokea nilisema, "Asante bibi."

Tulipomaliza kula, tuliwaaga na kurudi nyumbani. ***(Maneno gani mengine huonyesha heshima?)***

### Kazi ya ziada Kuandika na Kujaza pengo

Sasa tutafanya mazoezi ya sarufi tulizojifunza hapo awali. Baadaye nitawapatia kazi ya ziada.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Hatua ya 1:**

***Mwalimu:*** Leo tutaandika sentensi kwa wakati wa sasa kisha tutaandika sentensi hiyo kwa wakati ujao. Kwa mfano, **mama anakaa.** Kwa wakati ujao tutasema **mama atakaa.** Neno anakaa linabadilika kuwa atakaa.

**Hatua ya 2:**

***Mwalimu:*** Sasa tufanye pamoja. Tuandike sentensi hizo.

***Mwalimu na Wanafunzi:*** (Wanafunzi waandike)

Mama anakaa   Mama atakaa

### Kazi ya Ziada

***Mwalimu:*** Sasa ni zamu yenu. Nitawapatia sentensi moja ambayo ni ya wakati wa sasa au uliopo. Kisha mtaenda na kuandika kwa wakati ujao. Kisha mtasomea wenzenu. Sentensi ni: mama anakataa.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kiswahili ni lugha ya kupendeza sana. Mwalimu lazima ajifunze kutamka maneno sawasawa ili aweze kuongoza wanafunzi kuyatamka vyema.

Tarehe: ________________________   Muda: ________________   Idadi: ________________

Wiki ya 4: Siku ya 1 na 2 **Mazingira**

Tamka sauti.

n i t

Soma sauti ya herufi na silabi.

| n a | n u | n i | t u |
|---|---|---|---|
| **na** | **nu** | **ni** | **tu** |

Soma silabi na maneno.

| m ti ni | ki ti ni | a na ka a | a na o na |
|---|---|---|---|
| **mtini** | **kitini** | **anakaa** | **anaona** |

Tamka sauti.

n

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| n a | k a | m a | t a |
|---|---|---|---|
| **na** | **ka** | **ma** | **ta** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

a na taka **anataka** a na ona **anaona**

a na kataa **anakataa** a na tamani **anatamani**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mkate unanukia | mikate inanukia. |
| mti unanukia | miti inanukia. |

16

Wiki ya 4: Siku ya 1 na 2 **Mazingira**

**Kuna mti mkubwa. Tai mkuu amesimama juu ya mti huo.**

### Tai Mkuu

Tai mkuu anakaa mtini.
Paka anakaa na kuku kitini.
Tai mkuu anaona paka na kuku.
Tai mkuu anataka kukaa na kuku.
Paka anakataa.
Tai mkuu anatamani kukaa na paka.
Kuku anakataa.
Tai mkuu ana...

17

**Ufahamu wa fonimu**

N/T/U: Tamka sauti **/n/**. Taja maneno (**nanasi, ini)** huku wanafunzi wakionyesha ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea na maneno: **nini, kana, nani, ina.**

**Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi ni **n**. Tamka sauti **/n/**. Waagize wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **na**. Sema kila sauti /**n**//**a**/ kisha uunganishe na kusema silabi **na**. **[U]** Endelea na silabi: **nu, ni, tu**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U: Andika neno **mtini**. Tamka silabi **m ti ni** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mtini**. **[U]** Endelea na maneno **kitini, anakaa** na **anaona.**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**Kabla ya kusoma::**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **tai, kuku** na **anatamani**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waagize wanafunzi wajadiliane kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Tai mkuu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome hadithi peke yao.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi ya kujibu maswali yafuatayo:

1. ***Tai mkuu anakaa wapi?*** *(mtini)*
2. ***Paka anakaa na nani?*** *(kuku)*

**Kuandika**

Waagize wanafunzi waandike herufi **n**.

n n n n n

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi zenye maneno **anakaa, mtini, kitini, anataka, anakataa** katika breli. Waagize wanafunzi wayanakili. Kisha wawasomee wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati wa kuandika herufi kwa ubao, hakikisha usiandike hivi: **/e/** au **/n/**, lakini uziandike hivi **e** au **n**.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 4: Siku ya 1 na 2 **Mazingira**

Tamka sauti.

n i t

Soma sauti ya herufi na silabi.

| n a | n u | n i | t u |
|---|---|---|---|
| **na** | **nu** | **ni** | **tu** |

Soma silabi na maneno.

| m ti ni | ki ti ni | a na ka a | a na o na |
|---|---|---|---|
| **mtini** | **kitini** | **anakaa** | **anaona** |

Tamka sauti.

n

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| n a | k a | m a | t a |
|---|---|---|---|
| **na** | **ka** | **ma** | **ta** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

a na taka
**anataka**

a na ona
**anaona**

a na kataa
**anakataa**

a na tamani
**anatamani**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mkate unanukia | mikate inanukia. |
| mti unanukia | miti inanukia. |

16

Wiki ya 4: Siku ya 1 na 2 **Mazingira**

Kuna mti mkubwa. Tai mkuu amesimama juu ya mti huo.

**Tai Mkuu**

Tai mkuu anakaa mtini.
Paka anakaa na kuku kitini.
Tai mkuu anaona paka na kuku.
Tai mkuu anataka kukaa na kuku.
Paka anakataa.
Tai mkuu anatamani kukaa na paka.
Kuku anakataa.
Tai mkuu ana...

17

**▲ Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **n** tena. Tamka sauti ya herufi **/n/**.

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**⬬ Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **na**. Sema kila sauti **/n//a/** kisha uunganishe na kusema silabi **na**. **[U]** Endelea na silabi: **ka, ma, ta**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**★ Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **a na taka** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **anataka** kwa upesi. Endelea kwa maneno: **a na tamani (anatamani), a na kataa (anakataa), a na ona (anaona).**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**◆ Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **M**kate **una**nukia | - | **Mi**kate **ina**nukia. |
| **M**ti **una**nukia | - | **Mi**ti **ina**nukia. |

***Eleza wanafunzi wasome kwenye [ukurasa wa breli unaolingana].***

**📖 Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **tai, kuku** na **anatamani**.

**📖 Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Tai mkuu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome katika vikundi vya watu wawili.

**◈ Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Kwa nini paka na kuku walikataa kukaa na tai mkuu?*** *(kwa sababu walimwogopa, tai angemla kuku, n.k.)*
2. ***Unafikiri tai mkuu alifanya nini?*** *(alilia, alikasirika, n.k.)*

**✍ Kuandika**

Tamka neno **miti**. Wanafunzi waandike kuhusu miti.

Wanafunzi wajadiliane wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wana funzi kadi zenye maneno katika breli: **mkate – mikate, mti – miti, mtini – mitini**. Waagize wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati wanafunzi wanaposoma, tembea darasani ndio uweze kujua wanaosumbuka kusoma. Wasaidie wanafunzi hawa kusoma.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 4: Siku ya 3

Wiki ya 4: Siku ya 3 na 4 **Vyakula**

Tamka sauti.

o n i

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| n o | k o | m o | t o |
| **no** | **ko** | **mo** | **to** |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| no no | mo to | mo to ni | m to to |
| **nono** | **moto** | **motoni** | **mtoto** |

Tamka sauti.

o

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| n o | n oo | n i | n ii |
| **no** | **noo** | **ni** | **nii** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a na taka | a na toa |
| **anataka** | **anatoa** |
| a na ota | a na kata |
| **anaota** | **anakata** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| **umoja** | **wingi** |
|---|---|
| kaa | makaa |
| ini | maini |
| tikiti | matikiti |

18

Wiki ya 4: Siku ya 3 na 4 **Vyakula**

**Msichana ameketi karibu na moto. Anachoma ini. Kando yake kuna kuni. Juu ya kuni kuna konokono.**

**Kanini na Katana**

Kanini ni mtoto.
Anakaa na kaka Katana.
Katana anakata kuni. Kanini anaota moto.
Motoni mna ini nono.
Katana anaona konokono.
Anatoa mkuki. Anataka kuua konokono.
Katana anataka kutia konokono motoni.
Kanini anakataa.

19

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/o/**. Taja maneno huku wanafunzi wakionyesha ishara waliokubaliana. (**oga, noti**). **[U]**Endelea na maneno: **omba, toto, ota na tomoko.**

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **o**. Tamka sauti **/o/**.

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **no**. Sema sauti ya kila sauti /**n**//**o**/ kisha uunganishe na kusema silabi **no**. **[U]** Endelea na silabi**: ko, mo, to**.

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Andika neno **nono**. Tamka silabi **/no//no/** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **nono**. **[U]** Endelea na maneno: **moto, motoni, mtoto.**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Waagize wanafunzi waeleze maana ya maneno **konokono, nono** na **mkuki**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Kanini na Katana"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Kanini anakaa na nani?*** *(kaka yake, katana)*
2. ***Katana anafanya nini?*** *(anakata kuni)*

### Kuandika

Tamka sauti **o**. Waagize wanafunzi waandike herufi **o**.

o o o o o

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo:

- i. **Kanini ni mtoto.**
- ii. **Kanini anaota moto.**
- iii. **Katana anaona konokono.**
- iv. **Katana anakataa.**

Waagize wanafunzi wazinakili kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

# Wiki ya 4: Siku ya 4

Wiki ya 4: Siku ya 3 na 4 **Vyakula**

Tamka sauti.

**o** **n** **i**

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| n o | k o | m o | t o |
| **no** | **ko** | **mo** | **to** |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| no no | mo to | mo to ni | m to to |
| **nono** | **moto** | **motoni** | **mtoto** |

Tamka sauti.

**o**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| n o | n oo | n i | n ii |
| **no** | **noo** | **ni** | **nii** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a na taka | a na toa |
| **anataka** | **anatoa** |
| a na ota | a na kata |
| **anaota** | **anakata** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| **umoja** | **wingi** |
|---|---|
| kaa | **ma**kaa |
| ini | **ma**ini |
| tikiti | **ma**tikiti |

18

Wiki ya 4: Siku ya 3 na 4 **Vyakula**

**Msichana ameketi karibu na moto. Anachoma ini. Kando yake kuna kuni. Juu ya kuni kuna konokono.**

## Kanini na Katana

Kanini ni mtoto.
Anakaa na kaka Katana.
Katana anakata kuni. Kanini anaota moto.
Motoni mna ini nono.
Katana anaona konokono.
Anatoa mkuki. Anataka kuua konokono.
Katana anataka kutia konokono motoni.
Kanini anakataa.

19

### ▲ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **O** tena. Tamka sauti ya herufi **/o/**.

### ⬬ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **no**. Sema kila sauti **/n//o/** kisha uunganishe na kusema silabi **no**. **[U]** Endelea na silabi: **noo, ni, nii**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **a na taka** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **anataka** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **a na toa (anatoa), a na ota (anaota), a na kata (anakata).**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

Andika maneno haya ubaoni. N/T/U. Soma maneno haya.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| kaa | - | **ma**kaa |
| ini | - | **ma**ini |
| tikiti | - | **ma**tikiti |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **konokono, nono** na **mkuki**.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Kanini na Katana"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Kwa nini kanini anaota moto?*** *(anahisi baridi, ili apate kuhisi joto, n.k.).*
2. ***Kwa nini kanini anakataa kumruhusu Katana kutia konokono motoni?*** *(kwa sababu konokono atanuka n.k.)*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno **1. taa –** ________, **2. kaa –** ________, **3. Ini –** __________ Waagize wanafunzi waandike wingi wa maneno hayo. Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yaliyochanganywa: **tomto, tomo, nokokono, noon, kukim**. Waagize wanafunzi wayapange ili kuunda maneno kisha wawasomee wenzao. **Mfano:** tomto - mtoto

Tarehe: ____________________________ Muda: ____________________ Idadi: ____________________

Wiki ya 4: Siku ya 5 **Vyakula**

Tamka sauti.

n o

Tumia silabi kuunda maneno. Kwa mfano: mo to - moto

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| m | na | mo | i | kaa | ni |
| a | to | ta | ka | u | no |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| wakati uliopo (sasa) | wakati ujao (kesho) |
|---|---|
| koki analia | koki atalia. |
| kamau ananunua | kamau atanunua. |
| koki anatamani | koki atatamani. |
| kamau anamkatia | kamau atamkatia. |

Mvulana na msichana wamesimama karibu na mlango. Mvulana ameshika chupa ya asali na amebeba kikapu. Msichana analia.

**Kamau na Koki**

Kamau ananunua kaimati, asali na maini.
Koki anatamani asali.
Kamau anakataa kumpatia. Koki anataka maini.
Kamau anakataa kumkatia.
Koki analia,
"Kamau nataka kaimati." Kamau anamkatia kaimati.
Kaimati ni tamu.

20

■ **Majina ya herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi majina ya herufi **(n).** Tamka sauti ya herufi **/n/**. **[U]** Endelea kwa majina na herufi ya herufi **(o).**

★ **Silabi: Kuandika maneno**

Soma silabi zote pamoja na wanafunzi.

**[N]** Tumia silabi **mo** na **to** kuandika neno moto. **[T]** Soma neno **moto** pamoja na wanafunzi. **[U]** wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno matano halisi kwa kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

● **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

N/T/U. Soma sentensi hizi.

| Wakati uliopo | Wakati ujao |
|---|---|
| Koki analia. | Koki atalia. |
| Kamau ananunua. | Kamau atanunua. |
| Koki anatamani. | Koki atatamani. |
| Kamau anamkatia. | Kamau atamkatia. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Waagize wanafunzi waeleze maana ya maneno **maini** na **kaimati**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee Maelezo. **[U]** Waagize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri kuhusu hadithi.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Kamau na Koki"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

*i.* ***Kamau alinunua vyakula gani?*** *(alinunua kaimati, asali na maini).*
*ii.* ***Koki alitamani nini?*** *(alitamani asali, alitaka maini).*
*iii.* ***Kwa nini Koki alilia?*** *(Kamau alikataa kumpa asali na maini).*
*iv.* ***Taja vyakula vingine ambavyo ni vitamu.*** *(ndizi, peremende, n.k).*

**Hadithi ya mwalimu**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. (*Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali).*

**Kacheche na nyuki**

Hapo zamani za kale, Kacheche na ndugu zake waliwinda wanyama mwitu na kutafuta asali ya nyuki. Kila walipoenda kuwinda walibeba vyakula kama vile viazi, mkate, ndizi na maziwa. ***(Kacheche na ndugu zake waliwinda nini?)***

Siku moja walipokuwa msituni, Kacheche alisikia nyuki wakivuma juu ya mti mkubwa. Alienda pale akidhani kuwa nyuki walikuwa na asali. ***(Nyuki walikuwa wakivuma wapi?)***

Ndugu zake wakaja na wakasimama chini ya mti. Ndugu mkubwa akasema, "Hawa nyuki bado wanavuma. Tuendelee kuwinda wanyama." Kacheche hakufurahishwa na wazo hilo.Alirudi na kuwachokoza wale nyuki.

Nyuki walijawa na hasira. Walimvamia na kumuuma. Kacheche alipiga mayowe lakini hapakuwa na wa kumsaidia. Alianguka chini na kuzirai. Ndio maana wahenga wakasema, "Ukicheza na moto, hakika utachomeka." ***(Uzuri wa nyuki ni nini?)***

**Kuandika imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **kaimati, anatamani, anataka, tamu, makaa.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wanafunzi watumie silabi zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kuunda maneno matatu zaidi kisha wasomee wenzao.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada - *Wiki ya 4 Siku ya 5***

**Vidokezo vya Mwalimu**
Hakikisha wanafunzi wameongea na wenzao kuhusu utabiri kabla ya kuuliza wachache waelezee kuhusu utabiri.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 5: Siku ya 1 na 2 — Wanyama

Tamka sauti.

w o n

Tamka sauti ya herufi na silabi.

w a — w i — w u — w o

**wa** **wi** **wu** **wo**

Soma silabi na maneno.

wa tu — wa to to — wa na — wa ta no

**watu** **watoto** **wana** **watano**

Tamka sauti.

w

Tamka sauti ya herufi na silabi.

w a — k o — n a — t o

**wa** **ko** **na** **to**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa ka taka — wa ka wa toa

**wakataka** — **wakawatoa**

a ka wa ona — a ka wa ita

**akawaona** — **akawaita**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mama akamwona mtu | mama wakawaona watu. |
| mama akamtoa kuku | mama wakawatoa kuku. |
| mama akamwita mtoto | mama wakawaita watoto. |

21

Wiki ya 5: Siku ya 1 na 2 — Wanyama

Kuna shamba la mtama. Mtoto wa kima amekata mtama.

### Watoto wa Kima

Kima ana watoto watano.
Watoto wa kima wana mikia mirefu.
Watoto wanataka mtama mtamu wa mama.
Mama anawaona watoto wa kima mtamani.
Mama anawaita watu.
Watu wanawatoa watoto wa kima mtamani.
Ungetaka kuwaona watoto wa kima wenye mikia mirefu?

22

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti /**w**/. Taja maneno (watu, awamu) halafu wanafunzi waonyeshe ishara mliokubaliana. Endelea na maneno **[U] wanyama, awamu, watoto, mabawa, wote, kote**.

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **w**. Tamka sauti /**w**/. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **wa**. Sema sauti /**w**/ /**a**/ kisha uunganishe na kusema silabi **wa**. **[U]** Endelea na silabi **wi, wu, wo.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **wa** na **tu** kisha uunganishe silabi hizo na useme upesi neno **watu**. **[U]** Endelea na maneno **watoto, wana** na **watano.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mkia/mikia** na **mtamu**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo.

Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Watoto wa Kima"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

*i.* ***Kima ana watoto wangapi?*** *(watano)*
*ii.* ***Watoto wa kima wataka nini?*** *(mtama)*

### Kuandika

Tamka herufi **w**. Waagize wanafunzi waandike.

w w w w w

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **watoto, watano, wakataka, watu, kuwaona**. Waagize wanafunzi wayaandike kisha wawasomee wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Ufahamu wa fonimu huzingatia kufunza sauti za herufi. Wakati wa kufunza sauti, mwalimu hapaswi kuandika herufi hizi ubaoni. Kipindi hiki ni cha mazungumzo pekee.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 5: Siku ya 1 na 2 — Wanyama

Tamka sauti.

w o n

Tamka sauti ya herufi na silabi.

w a — w i — w u — w o

wa — wi — wu — wo

Soma silabi na maneno.

wa tu — wa to to — wa na — wa ta no

watu — watoto — wana — watano

Tamka sauti.

w

Tamka sauti ya herufi na silabi.

w a — k o — n a — t o

wa — ko — na — to

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa ka taka — wa ka wa toa

wakataka — wakawatoa

a ka wa ona — a ka wa ita

akawaona — akawaita

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mama akamwona mtu | mama wakawaona watu. |
| mama akamtoa kuku | mama wakawatoa kuku. |
| mama akamwita mtoto | mama wakawaita watoto. |

21

Wiki ya 5: Siku ya 1 na 2 — Wanyama

Kuna shamba la mtama. Mtoto wa kima amekata mtama.

Watoto wa Kima

Kima ana watoto watano.
Watoto wa kima wana mikia mirefu.
Watoto wanataka mtama mtamu wa mama.
Mama anawaona watoto wa kima mtamani.
Mama anawaita watu.
Watu wanawatoa watoto wa kima mtamani.
Ungetaka kuwaona watoto wa kima wenye mikia mirefu?

22

### ▲ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **W**. Tamka sauti /**W**/.

### ⬬ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **wa**. Sema sauti **/w/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi **wa**. **[U]** Endelea na silabi: **ko, na to**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa ka taka** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **wakataka**. **[U]** Endelea na: **a ka wa ona (akawaona), wa ka wa toa (wakawatoa)** na **a ka wa i ta (akawaita).** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***

N/T/U: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Mama **a**kamwona mtu | - | Mama **wa**kawaona watu. |
| Mama **a**kamtoa kuku | - | Mama **wa**kawatoa kuku. |
| Mama **a**kamwita mtoto | - | Mama **wa**kawaita watoto. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **mkia, tamu.**

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Watoto wa kima"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome kwa vikundi vya wawili wawili.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

i. ***Je, kati ya mtama na kima unafikiri mama alipenda nini?*** *(mtama kwa sababu alitaka watoto wa kima waondolewe mtamani).*

ii. ***Ukiona watoto na kima utafanya nini?*** *(wanafunzi wapeane majibu mbalimbali kama vile (nitatoroka).*

### ✍ Kuandika

Tamka maneno haya. Wanafunzi wayaandike kisha wajadiliane kuhusu matatu.

**Mtoto – watoto**

**Mtu - watu**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **mtoto - watoto, mtu - watu**. Waagize wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

Wiki ya 5: Siku ya 3 na 4 — Wanyama

Tamka sauti.

e w o

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| n e | t e | w e | m we |
| ne | te | we | mwe |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| te na | ne e ma | m ke ka ni | ma we |
| tena | neema | mkekani | mawe |

Tamka sauti.

e

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| w e | k e | w i | w o |
| we | ke | wi | wo |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a ka muona | a ka muita |
| akamuona | akamuita |
| a ka m timua | a ki m kamata |
| akamtimua | akimkamata |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mtoto anataka | watoto wanataka. |
| mtoto anaona | watoto wanaona. |
| mtoto anatamani | watoto wanatamani. |
| mtoto anaokota | watoto wanaokota. |

23

Wiki ya 5: Siku ya 3 na 4 — Ndege na Wanyama

Nje ya nyumba kuna kuku, vifaranga na mwewe. Mwewe anataka kumkamata kuku.

Neema na Mwewe

Amina akaketi mkekani akiota moto.
Akamuona mwewe akimkamata kuku.
Akamuita Neema, "Neema, Neema!"
Neema akaitika, "Naam, Amina."
Amina akaita tena, "Neema! Ona mwewe."
Neema akaokota mawe na kumtimua mwewe.
Mwewe akatua mtini.
Amina na Neema wakaketi mkekani wakiota moto na kukata mkate.

24

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/e/**. Taja maneno **(embe** na **mwewe)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. Endelea na maneno **[U] eka, debe, ewe, keki, enda, keti.**

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **e**. Tamka sauti /e/. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma silabi

Andika silabi **ne**. N/T/U: Sema sauti **/n/ /e/** kisha uunganishe na kusema silabi **ne**. **[U]** Endelea na silabi **te, we, m we.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **te** na **na** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **tena**. **[U]** Endelea na maneno **Neema, mkekani** na **mawe**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **akiota/ota** na **akamtimua/timua**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo.

Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Neema na Mwewe"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kusoma peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

- ***i.*** ***Amina aliketi mkekani akifanya nini?*** *(Aliketi mkekani akiota moto).*
- ***ii.*** ***Amina alimuita nani?*** *(Amina alimuita Neema).*
- ***iii.*** ***Amina na Neema walikata nini?*** *(Amina na Neema walikata mkate).*

### Kuandika

Tamka jina la herufi **e**. Waagize wanafunzi waandike.

e e e e e

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo.

- **i. Amina akaketi mkekani.**
- **ii. Neema akatoka na mawe.**
- **iii. Mwewe akatua mtini.**

Waambie wanafunzi wanakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 5: Siku ya 3 na 4 — Wanyama

Tamka sauti.

e w o

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| n e | t e | w e | m we |
| **ne** | **te** | **we** | **mwe** |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| te na | ne e ma | m ke ka ni | ma we |
| **tena** | **neema** | **mkekani** | **mawe** |

Tamka sauti.

e

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| w e | k e | w i | w o |
| **we** | **ke** | **wi** | **wo** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a ka muona | a ka muita |
| **akamuona** | **akamuita** |
| a ka m timua | a ki m kamata |
| **akamtimua** | **akimkamata** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mtoto anataka | watoto wanataka. |
| mtoto anaona | watoto wanaona. |
| mtoto anatamani | watoto wanatamani. |
| mtoto anaokota | watoto wanaokota. |

23

Wiki ya 5: Siku ya 3 na 4 — Ndege na Wanyama

Nje ya nyumba kuna kuku, vifaranga na mwewe. Mwewe anataka kumkamata kuku.

**Neema na Mwewe**

Amina akaketi mkekani akiota moto.
Akamuona mwewe akimkamata kuku.
Akamuita Neema, "Neema, Neema!"
Neema akaitika, "Naam, Amina."
Amina akaita tena, "Neema! Ona mwewe."
Neema akaokota mawe na kumtimua mwewe.
Mwewe akatua mtini.
Amina na Neema wakaketi mkekani wakiota moto na kukata mkate.

24

▲ **Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **E**. Tamka sauti /**e**/.

⬬ **Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **we**. Sema sauti **/w/ /e/** kisha uunganishe na kusema silabi **we**. **[U]** Endelea na silabi **ke, wi, wo**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **a ka muona** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **akamuona**. **[U]** Endelea kwa: **a ka muita (akamuita), a ka m timua (akamtimua), a ka m kamata (akamkamata).** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

◆ **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

N/T/U. Soma sentensi hizi:

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Mtoto **a**nataka | - | **Wa**toto **wa**nataka. |
| Mtoto **a**naona | - | **Wa**toto **wa**naona. |
| Mtoto **a**natamani | - | **Wa**toto **wa**natamani. |
| Mtoto **a**naokota | - | **Wa**toto **wa**naokota. |

📖 **Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **akiota/ota** na **akamtimua/timua** na **akatua/tua**.

📖 **Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Neema na Mwewe"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome kwa vikundi vya wawili wawili.

◈ **Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

*i.* ***Je, unafikiri mwewe alikuwa mtini akifanya nini?*** *(akipumzika/akiangalia kuku n.k)*

*ii.* ***Je, unafikiria ni kwa nini mwewe alitaka kumshika kuku?*** *(ili amle)*

✍ **Kuandika**

Tamka maneno haya ubaoni. Waambie wanafunzi waandike wingi wa maneno hayo.

| | **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|---|
| Kwa mfano: | **ana**taka | - | **wana**taka |
| | **ana**ona | - | __________ |
| | **ana**tamani | - | __________ |
| | **ana**okota | - | __________ |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yaliyochanganywa: **wema, temka, kanimke, nate**. Kisha wayaandike kwa usahihi na wawasomee wenzao.

**Kwa mfano:** wemwe - mwewe

Tarehe: __________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 5: Siku ya 5 — **Chakula**

Tamka sauti.

e w

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: wa tu **watu**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ka | tu | m | wa | te | we |
| i | a | to | ma | mi | ta |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

wewe **una**taka - mtoto **ana**taka.
wewe **una**ona - mtoto **ana**ona.
wewe **una**ita - mtoto **ana**ita.
wewe **una**okota - mtoto **ana**okota.

Wavulana wawili na msichana wanacheza na mtoto wa paka.

**Tai na mtoto wa paka**

Owino ana watoto watatu: Wata, Wakio na Waki.
Watoto wa Owino wana mtoto wa paka.
Tai mtini anamuona mtoto wa paka.
Anatamani kumkamata mtoto wa paka.
Watoto wanaita Owino.
Owino anamuona tai na mtoto wa paka.
Owino anaokota tawi.

25

### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina ya herufi (**w**). Tamka sauti ya herufi **/w/**. **[U]** Eleza wanafunzi jina na itamke sauti ya herufi (**e**).

### ★ Silabi: Kuandika

Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi.

**[N]** Tumia silabi **wa** na **tu** kuunda neno **watu**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi zilizo kwenye vitabu vyao ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

Soma sentesi ya kwanza. Soma pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| wewe | yeye |
|---|---|
| Wewe **una**taka | Mtoto **ana**taka |
| Wewe **una**ita | Mtoto **ana**ita |
| Wewe **una**ona | Mtoto **ana**ona |
| Wewe **una**okota | Mtoto **ana**okota |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kumkamata** na **anaokota**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Tai na mtoto wa paka"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

*i.* ***Owino alikuwa na watoto wangapi?*** *(Watatu).*
*ii.* ***Watoto wa Owino walikuwa na nini?*** *(Mtoto wa paka).*
*iii.* ***Je, unafikiri kwa nini tai alishika mtoto wa paka?*** *(Kumla).*
*iv.* ***Owino alifanyia nini tawi aliloliokota?*** *(Alimrushia tai).*

### 🕮 Hadithi ya mwalimu

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. *(Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

**Fisi na Sungura**

Hapo zamani za kale Fisi alitoka kwenda kutafuta chakula. Baada ya kutembea kwa muda mrefu alikutana na mnyama wa kwanza na kumuuliza, "Jina lako ni nani?"
"Jina langu ni Kondoo." ***(Fisi alikutana na mnyama gani kwanza?)***
"Nitakula," Fisi akasema.
Kondoo alijibu, "Usinile. Wacha nimuite ng'ombe."
Fisi alimuuliza ng'ombe, "Jina lako ni nani?"
Ng'ombe alijibu, "Jina langu ni ng'ombe."
Fisi akasema, "Nitakula."
"Usinile. Wacha nimuite nguruwe." (***Ng'ombe alimuita mnyama gani?***)
Nguruwe akaja. Fisi akamuuliza, "Jina lako ni nani?"
"Jina langu ni nguruwe," Nguruwe akajibu.
"Nitakula," Fisi akamtisha Nguruwe.
"Usinile. Wacha nimuite Sungura." Nguruwe akaomba.
Sungura alipokuja, Fisi akamuuliza, "Jina lako ni nani?"
"Jina langu ni Sungura," Sungura akajibu.
"Nitakula."
"Kabla ya kunila hebu fungua macho yako wazi."
Fisi alikodoa macho. Sungura alitupa mchanga kwenye macho ya Fisi. Sungura alitoroka mbio, huku akicheka na kumwacha fisi akilia. ***(Je, Sungura alifanya jambo zuri?)***

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **watu, watoto, paka, wanaita, tai.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wanafunzi watumie silabi zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kuunda maneno zaidi kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 6: Siku ya 1 na 2 — **Chakula**

Tamka sauti.

l e w

Tamka sauti ya herufi na silabi.

l e — **le**   l i — **li**   l u — **lu**   l o — **lo**

Soma silabi na maneno.

lo la ni — **lolani**   li ma u — **limau**   ne li ma — **nelima**   la ki ni — **lakini**

Tamka sauti.

l

Tamka sauti ya herufi na silabi.

l a — **la**   w e — **we**   n e — **ne**   k e — **ke**

Soma sehemu za neno na neno lote.

a ka m letea — **akamletea**   a ka litema — **akalitema**

a ki li tema — **akilitema**   li li kuwa — **lilikuwa**

Sarufi: Soma maneno haya.

| wakati uliopita | wakati ujao |
|---|---|
| aliona | ataona |
| alilala | atalala |
| alilia | atalia |
| alitamani | atatamani |
| aliwaletea | atawaletea |

26

Wiki ya 6: Siku ya 1 na 2 — **Chakula**

Mtoto mvulana amelala kitini ndani ya nyumba.

### Lolani na Nelima

Lolani alilala kitini.
Nelima akamletea limau.
Lolani akala.
Lo! Limau lilikuwa kali.
Lolani akalitema limau na kulia.
Nelima akaona Lolani akilitema limau.
Nelima akamletea Lolani muwa.
Lakini Lolani hakula muwa.
Nelima akamletea asali.
Lolani akala asali.
Asali ni tamu.

27

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/l/**. Taja maneno **(lala** na **ala)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea kwa maneno: **lakini, Lolani, Nelima, limau.**

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **l**. Tamka sauti **/l/**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **le** ubaoni. Sema kila sauti /l//e/ kisha uunganishe na kusema silabi **le**. **[U]** Endelea na silabi: **li, lu, lo.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **/Lo//la//ni/** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **Lolani**. **[U]** Endelea na maneno **limau, Nelima** na **lakini.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **Limau, akalitema** na **muwa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Lolani na Nelima**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

i. ***Lolani alilala wapi?*** *(Lolani alilala kitini).*
ii. ***Kwa nini Lolani alilitema limau?*** *(Limau lilikuwa kali).*

### Kuandika

Tamka jina la herufi **l**. Waagize wanafunzi waandike.

l l l l l

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **limau, lilikuwa, akalitema, akala, alilala**. Waagize wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 6: Siku ya 1 na 2 **Chakula**

Tamka sauti.

l e w

Tamka sauti ya herufi na silabi.

l e    l i    l u    l o

**le**    **li**    **lu**    **lo**

Soma silabi na maneno.

lo la ni    li ma u    ne li ma    la ki ni

**lolani**    **limau**    **nelima**    **lakini**

Tamka sauti.

l

Tamka sauti ya herufi na silabi.

l a    w e    n e    k e

**la**    **we**    **ne**    **ke**

Soma sehemu za neno na neno lote.

a ka m letea    a ka litema

**akamletea**    **akalitema**

a ki li tema    li li kuwa

**akilitema**    **lilikuwa**

Sarufi: Soma maneno haya.

| wakati uliopita | wakati ujao |
|---|---|
| aliona | ataona |
| alilala | atalala |
| alilia | atalia |
| alitamani | atatamani |
| aliwaletea | atawaletea |

26

Wiki ya 6: Siku ya 1 na 2 **Chakula**

Mtoto mvulana amelala kitini ndani ya nyumba.

Lolani na Nelima

Lolani alilala kitini.
Nelima akamletea limau.
Lolani akala.
Lo! Limau lilikuwa kali.
Lolani akalitema limau na kulia.
Nelima akaona Lolani akilitema limau.
Nelima akamletea Lolani muwa.
Lakini Lolani hakula muwa.
Nelima akamletea asali.
Lolani akala asali.
Asali ni tamu.

27

### ▲ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **L**. Tamka sauti ya herufi **/l/**.

### ⬬ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **la**. Sema kila sauti **/l/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi **la**. **[U]** Endelea na silabi: **we, ne, ke.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **a ka m letea** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **akamletea**. **[U]** Endelea kwa maneno: **A ka litema (akalitema), li li kuwa (lilikuwa).** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

N/T/U. Soma maneno haya katika nyakati mbalimbali.

| Wakati uliopita | | Wakati ujao |
|---|---|---|
| **ali**ona | - | **ata**ona |
| **ali**lala | - | **ata**lala |
| **ali**lia | - | **ata**lia |
| **ali**tamani | - | **ata**tamani |
| **ali**waletea | - | **ata**waletea |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **limau, akalitema** na **muwa**.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Lolani na Nelima"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### ⟐ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

- ***i.*** ***Kwa nini Lolani alilala kitini?*** *(alikuwa mgonjwa, kwa sababu alikuwa amechoka, alihisi njaa n.k.).*
- ***ii.*** ***Hebu onyesha na ueleze jinsi Lolani alivyofanya baada ya kula limau*** *(wanafunzi waonyeshe jinsi ya kutema kitu).*

### ✍ Kuandika: Imla

Tamka maneno haya: **i. limau, ii. muwa**. Waagize wanafunzi wayaandike.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno haya: **aliona - ataona, alilia - atalia, alilala - atalala**. Waambie wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao:

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 6: Siku ya 3 na 4 — Nyumbani

Tamka sauti.

h l e

Tamka sauti ya herufi na silabi.

h a h o h u h e

ha ho hu he

Soma silabi na maneno.

ha mu ka ha wa ho te li ni He le na

hamu kahawa hotelini Helena

Tamka sauti.

h

Tamka sauti ya herufi na silabi.

h i w i l i k i

hi wi li ki

Soma sehemu za neno na neno lote.

a li nunua a ka m letea

alinunua akamletea

a ka tokea ha ku taka

akatokea hakutaka

Sarufi: Soma sentensi zifuatazo.

1. mama mfupi
2. mtoto mrefu
3. amu mnene
4. paka mkubwa

28

Wiki ya 6: Siku ya 3 na 4 — Nyumbani

Mpishi yuko hotelini akitia chai kwa kikombe. Watu wanakunywa chai kwa hoteli.

**Hotelini**

Helena alinunua kaimati, mkate na kahawa hotelini.
Alikuwa na hamu ya kahawa tamu.
Mama akatokea na kuketi kitini.
Helena akamletea kahawa tamu, kaimati na mkate.
Lakini mama alitaka kula wali kwa maini.
Hakutaka kahawa tamu, kaimati na mkate kama Helena.

29

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/h/**. Taja maneno **(hana** na **wahi)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea na maneno **hema, kahawa, hawa** na **kahama**.

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **h**. Tamka sauti **/h/**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **ha**. Sema kila sauti /**h**//**a**/ kisha uunganishe na kusema silabi **ha**. **[U]** Endelea na silabi: **ho, hu, he.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **/ha//mu/** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **hamu**. **[U]** Endelea na maneno **kahawa, hotelini** na **Helena.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **hotelini, hamu** na **kaimati**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **Hotelini** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kusoma peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Helena alinunua nini hotelini?*** *(kaimati, mkate, kahawa)*
2. ***Mama alitaka kula nini?*** *(wali, maini)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **h** mara tatu.

h h h h h

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo:

i. **Helena alinunua kaimati.**
ii. **Helena alinunua kahawa.**
iii. **Mama hakutaka kahawa tamu.**
iv. **Mama alitaka wali.**

Waambie wanafunzi wazinakili kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ____________________ Idadi: ____________________

Wiki ya 6: Siku ya 3 na 4 — **Nyumbani**

Tamka sauti.

h l e

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| h a | h o | h u | h e |
| ha | ho | hu | he |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ha mu | ka ha wa | ho te li ni | He le na |
| hamu | kahawa | hotelini | Helena |

Tamka sauti.

h

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| h i | w i | l i | k i |
| hi | wi | li | ki |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li nunua | a ka m letea |
| alinunua | akamletea |
| a ka tokea | ha ku taka |
| akatokea | hakutaka |

Sarufi: Soma sentensi zifuatazo.

1. mama mfupi
2. mtoto mrefu
3. amu mnene
4. paka mkubwa

28

Wiki ya 6: Siku ya 3 na 4 — **Nyumbani**

**Mpishi yuko hotelini akitia chai kwa kikombe. Watu wanakunywa chai kwa hoteli.**

**Hotelini**

Helena alinunua kaimati, mkate na kahawa hotelini.
Alikuwa na hamu ya kahawa tamu.
Mama akatokea na kuketi kitini.
Helena akamletea kahawa tamu, kaimati na mkate.
Lakini mama alitaka kula wali kwa maini.
Hakutaka kahawa tamu, kaimati na mkate kama Helena.

29

### ▲ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **h**. Tamka sauti ya herufi **/h/**.

### ⬬ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **hi** ubaoni. Sema kila sauti **/h//i/** kisha uunganishe na kusema silabi **hi. [U]** Endelea na silabi: **wi, li** na **ki.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **a li nunua** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **alinunua** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **a ka tokea (akatokea), a ka m letea (akamletea), ha ku taka (hakutaka).** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

Eleza wanafunzi maana na matumizi ya vivumishi vya sifa.

Andika vifungu hivi ubaoni. N/T/U. Soma vifungu hivi.

1. mama **mfupi**
2. mtoto **mrefu**
3. amu **mnene**
4. paka **mkubwa**

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **hotelini, hamu kaimati**.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Hotelini"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Taja vyakula vingine ambavyo huuzwa hotelini.*** *(chapati, chai, maharagwe, samaki n.k.)*
2. ***Taja chakula unachokipenda sana.*** *(nyama, viazi, n.k.)*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye vifungu hivi:

**Godoro zito**
**Kahawa tamu**
**Viatu safi**

Waagize wanafunzi waviandike.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno haya yaliyochanganywa: **mauli, liaku, liasa, wamu**. Waambie wanafunzi waandike maneno halisi kisha wawasomee wenzao. Kwa mfano: **mauli - limau**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 6: Siku ya 5 **Nyumbani**

Tamka sauti.

h l

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: **hoteli**.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| te | ho | ta | la | li | na |
| te | we | ti | ma | ni | le |

Sarufi: Soma maneno haya.

| umoja | wingi |
|---|---|
| **aka**mletea | **wakawa**letea |
| **aka**muona | **wakawa**ona |
| **aka**muita | **wakawa**ita |
| **aka**lia | **waka**lia |

Mvulana na msichana wanaongeleshana. Msichana ameshika kitu. Mvulana anamuomba.

**Halake na Lina**

**Halake:** Niliokota lulu. Nikaiweka katika taulo.
**Lina:** Niliona taulo kitini.Nikaitoa na kuiweka uani. Niliona lulu na kuiokota.
**Halake:** (*Akimwambia Ali*) Nimemwona Lina na ile lulu.
**Ali:** Ninaitaka lulu. (*Lina anakataa*)
**Halake:** (*Akilia*) Mama! Mama!
**Lina:** Nimeiweka lulu kitini.
**Ali:** Lina ameiweka lulu kitini. (*Halake anaiokota ile lulu.*)

30

### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(l)**. Tamka sauti ya herufi **/l/**. **[U]** Endelea na herufi **(h)**.

### ★ Silabi: Kuandika

Soma silabi zote katika ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. **[N]** Tumia silabi **ho, te** na **li** kuandika neno **hoteli**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

N/T/U. Soma maneno haya.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **aka**mletea | **wakawa**letea |
| **aka**muona | **wakawa**ona |
| **aka**muita | **wakawa**ita |
| **aka**lia | **waka**lia |

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **lulu**, **taulo** na **akaiokota**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha mchezo. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma mchezo wa **"Halake na Lina"** huku wanafunzi wakifwatilia kwa kidole. **[T] [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao. Kwa zamu kama Halake, Lina na Ali.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Halake aliokota nini?*** *(lulu)*
2. ***Halake aliweka lulu wapi?*** *(katika taulo)*
3. ***Kwa nini Halake alilia?*** *(Alimuona Lina na lulu, alidhani lina hangemrudishia lulu)*
4. ***Kama ungelikuwa Halake ungelifanya nini?*** *(ningeificha lulu kwenye kichaka, n.k)*

### Hadithi ya mwalimu

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. (*Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.*)

**NJIWA WA AJABU**

Baba ya Baraka alimnunulia njiwa wawili. Njiwa hawa walikuwa wa kike na wa kiume. (***Baba ya Baraka alinunua njiwa wangapi?***)

Baraka aliwalisha njiwa wake vizuri sana. Kila mara aliwaletea mbegu za aina tofauti.

Baada ya miezi miwili njiwa wa kike akataga mayai kumi. Njiwa wa kike alilalia mayai kwa siku kumi na saba kisha mayai yakaangua. (***Njiwa wa kike alitaga mayai baada ya muda gani?)***

Baraka akawa na njiwa kumi na wawili. Alicheza na njiwa wake kila asubuhi na jioni.

Baraka alipowaambia wanafunzi wenzake kuhusu njiwa wake hawakuamini. Mwalimu pia alishangazwa na njiwa hawa.(***Kwa nini wanafunzi na walimu walishangaa?***)

### Kuandika-Imla

Soma maneno haya mara mbili au tatu huku wanafunzi wakiyaandika: **limau, muwa, alilala, lilikuwa, akalitema.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waendelee kuunda maneno zaidi kutoka kwa silabi walizopewa katika ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

Tamka sauti.

s h l

Tamka sauti ya herufi na silabi.

s a s i s o s e

**sa** **si** **so** **se**

Soma silabi na maneno.

sa u mu so ko a su bu hi Sa ra

**saumu** **soko** **asubuhi** **Sara**

Tamka sauti.

s

Tamka sauti ya herufi na silabi.

s u h u l u w u

**su** **hu** **lu** **wu**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa li kutana wa li wa tesa

**walikutana** **waliwatesa**

ni ta wa sema a li sononeka

**nitawasema** **alisononeka**

Sarufi: Soma maneno haya.

| umoja | wingi |
|---|---|
| aliwatesa | waliwatesa |
| aliwasema | waliwasema |
| alikutana | walikutana |
| alisononeka | walisononeka |





Wasichana wawili. Msichana mkubwa amekalia mkeka sakafuni. Anamwongelesha msichana mdogo ambaye amesimama na analia.

## Sara na Saumu

Sara na Saumu wanakaa Masii karibu na soko la Sokomoko.
Asubuhi walikutana na watoto sita wa mtaani.
Watoto hawa waliwatesa na kuwatusi Sara na Saumu.
Saumu alisononeka sana. Sara alikuwa na wasiwasi sana.
Sara akasema, "Msinitese wala kunitusi. Nitawasema kwa baba na mama."
Wale watoto wakatoroka.



### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/s/**. Taja maneno **(sikio, usiku)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea na maneno **sukuma**, **makasi**, **simu** na **masika**.

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **s**. Tamka sauti **/s/**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **sa**. Sema kila sauti **/s/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi **Sa**. **[U]** Endelea na silabi: **si**, **so**, **se.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Andika neno **Saumu** ubaoni. Tamka silabi **/sa/ /u//mu/** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **Saumu**. **[U]** Endelea na maneno: **soko, asubuhi** na **Sara.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mtaani**, **waliwatesa** na **alisononeka**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Sara na Saumu**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Sara na Saumu wanakaa wapi?*** *(Wanakaa Masii karibu na soko la Sokomoko.)*
2. ***Saumu alisema angewasema wale watoto wa mtaani kwa nani?*** *(baba na mama)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **s** mara tatu.

s s s s s

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **Saumu, soko, asubuhi, mtaani, waliwatesa**. Waambie wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 7: Siku ya 1 na 2 **Nyumbani**

Tamka sauti.

s h l

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| s a | s i | s o | s e |
|---|---|---|---|
| **sa** | **si** | **so** | **se** |

Soma silabi na maneno.

| sa u mu | so ko | a su bu hi | Sa ra |
|---|---|---|---|
| **saumu** | **soko** | **asubuhi** | **Sara** |

Tamka sauti.

s

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| s u | h u | l u | w u |
|---|---|---|---|
| **su** | **hu** | **lu** | **wu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li kutana | wa li wa tesa |
|---|---|
| **walikutana** | **waliwatesa** |
| ni ta wa sema | a li sononeka |
| **nitawasema** | **alisononeka** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| umoja | wingi |
|---|---|
| aliwatesa | waliwatesa |
| aliwasema | waliwasema |
| alikutana | walikutana |
| alisononeka | walisononeka |

31

Wiki ya 7: Siku ya 1 na 2 **Nyumbani**

**Wasichana wawili. Msichana mkubwa amekalia mkeka sakafuni. Anamwongelesha msichana mdogo ambaye amesimama na analia.**

## Sara na Saumu

Sara na Saumu wanakaa Masii karibu na soko la Sokomoko.
Asubuhi walikutana na watoto sita wa mtaani.
Watoto hawa waliwatesa na kuwatusi Sara na Saumu.
Saumu alisononeka sana. Sara alikuwa na wasiwasi sana.
Sara akasema, "Msinitese wala kunitusi. Nitawasema kwa baba na mama."
Wale watoto wakatoroka.

32

### ▲ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **s**. Tamka sauti ya herufi **/s/**.

### ⬬ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **su**. Sema kila sauti **/s/ /u/** kisha uunganishe na kusema silabi **su**. **[U]** Endelea na silabi: **hu, lu, wu.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa li kutana** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **walikutana** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **wa li wa tesa (waliwatesa), ni ta wa sema (nitawasema), a li sononeka (alisononeka)**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

N/T/U. Soma maneno haya.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **ali**watesa | **wali**watesa |
| **ali**wasema | **wali**wasema |
| **ali**kutana | **wali**kutana |
| **ali**sononeka | **wali**sononeka |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **mtaani, waliwatesa** na **alisononeka**.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi "**Sara na Saumu**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

*i.* ***Watoto wa mtaani wana tabia gani?*** *(wana tabia mbaya)*

*ii.* ***Kwa nini watoto wa mtaani walitoroka?*** *(waliogopa kushikwa n.k)*

### ✍ Kuandika: Imla

Soma maneno haya **(Sara, Saumu)** kisha wanafunzi waandike.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sarufi hizi:

| | | |
|---|---|---|
| **alitutesa** | - | **walitutesa** |
| **alisononeka** | - | **walisononeka** |
| **aliwasema** | - | **waliwasema** |

Waagize wanafunzi wazinakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

Tarehe: ________________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Wiki ya 7: Siku ya 3 na 4 **Nyumbani**

Tamka sauti.

b s h

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| b a | b e | b u | b o |
|---|---|---|---|
| **ba** | **be** | **bu** | **bo** |

Soma silabi na maneno.

| bi s ku ti | ba ku li | bi ri ka | m ke be |
|---|---|---|---|
| **biskuti** | **bakuli** | **birika** | **mkebe** |

Tamka sauti.

b

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| b i | s i | k i | h i |
|---|---|---|---|
| **bi** | **si** | **ki** | **hi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa li amka — **waliamka**

wa ka tamani — **wakatamani**

wa ka toa — **wakatoa**

wa ka tabasamu — **wakatabasamu**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mtoto aliamka | watoto waliamka. |
| mtoto alitoa | watoto walitoa |
| mtoto alitamani | watoto walitamani. |
| mtoto alitabasamu | watoto walitabasamu. |

33

Wiki ya 7: Siku ya 3 na 4 **Nyumbani**

Dada wawili na kaka wamesimama mbele ya kabati. Wanatoa biskuti kwa kabati.

**Biskuti**

Asubuhi baba, mama na watoto waliamka.
Watoto wakatamani kula biskuti.
Kulikuwa na bakuli, birika, bilauri na mkebe kabatini.
Mama akatoa birika akaona bilauri.
Watoto wakatoa bilauri wakaona buibui.
Baba, akamtoa buibui.
Watoto wakatoa mkebe, wakaona biskuti.
Watoto wakatabasamu.

34

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/b/**. Taja maneno **(baba, kabati)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]**Endelea na maneno **beba, mama, bibi, hema, babu** na **kabati.**

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **b**. Tamka sauti **/b/**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **ba**. Sema kila sauti **/b//a/** kisha uunganishe na kusema silabi **ba**. **[U]** Endelea na silabi**: be, bu, bo.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **bi s ku ti** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **biskuti**. **[U]** Endelea na maneno **bakuli, birika** na **mkebe.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **buibui, bilauri** na **wakatabasamu**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Biskuti"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Taja vyombo vilivyokuwa kabatini?*** *(Kabatini kulikuwa na bakuli, birika, bilauri na mkebe.)*
2. ***Watoto waliona nini walipotoa mkebe?*** *(Waliiona biskuti.)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **b** mara tatu.

b b b b b

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi hizi:

i. **Baba aliamka asubuhi.**
ii. **Mama akatoa birika.**
iii. **Watoto walitamani kula biskuti.**
iv. **Mama aliona bilauri.**

Waagize wanafunzi wazinakili. Kisha wawasomee wenzao.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 7: Siku ya 3 na 4 **Nyumbani**

Tamka sauti.

b s h

Tamka sauti ya herufi na silabi.

b a — **ba**; b e — **be**; b u — **bu**; b o — **bo**

Soma silabi na maneno.

bi s ku ti — **biskuti**; ba ku li — **bakuli**; bi ri ka — **birika**; m ke be — **mkebe**

Tamka sauti.

b

Tamka sauti ya herufi na silabi.

b i — **bi**; s i — **si**; k i — **ki**; h i — **hi**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa li amka — **waliamka**; wa ka tamani — **wakatamani**

wa ka toa — **wakatoa**; wa ka tabasamu — **wakatabasamu**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mtoto aliamka | watoto waliamka. |
| mtoto alitoa | watoto walitoa |
| mtoto alitamani | watoto walitamani. |
| mtoto alitabasamu | watoto walitabasamu. |

33

Wiki ya 7: Siku ya 3 na 4 **Nyumbani**

Dada wawili na kaka wamesimama mbele ya kabati. Wanatoa biskuti kwa kabati.

**Biskuti**

Asubuhi baba, mama na watoto waliamka.
Watoto wakatamani kula biskuti.
Kulikuwa na bakuli, birika, bilauri na mkebe kabatini.
Mama akatoa birika akaona bilauri.
Watoto wakatoa bilauri wakaona buibui.
Baba, akamtoa buibui.
Watoto wakatoa mkebe, wakaona biskuti.
Watoto wakatabasamu.

34

### ▲ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **b**. Tamka sauti ya herufi **/b/**.

### ⬬ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **bi**. Sema kila sauti **/b//i/** kisha uunganishe na kusema silabi **bi**. **[U]** Endelea na silabi: **si, ki** na **hi.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa li amka** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **waliamka** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **wa ka tamani (wakatamani), wa ka toa (wakatoa), wa ka tabasamu (wakatabasamu).** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

N/T/U. Soma senetensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Mtoto **ali**amka | Watoto **wali**amka. |
| Mtoto **ali**toa | Watoto **wali**toa. |
| Mtoto **ali**tamani | Watoto **wali**tamani. |
| Mtoto **ali**tabasamu | Watoto **wali**tabasamu. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **buibui, bilauri** na **wakatabasamu**.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Biskuti"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Nini kinaonyesha watoto walifurahi kuona biskuti?*** *(walitabasamu)*
2. ***Kwa nini buibui alikuwa kabatini?*** *(alikuwa anaishi kule; kulikuwa na giza kabatini na buibui anapenda giza; kulikuwa na chakula na buibui angewapata wadudu kule ambao ni chakula chake kule n.k.)*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno haya. Wanafunzi waandike wingi wa maneno haya. Kwa mfano **alitoa - walitoa**.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **a**litoa | **wa**litoa |
| **a**liamka | ____________ |
| **a**litamani | ____________ |
| **a**litaka | ____________ |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yaliyochanganywa: **kebem, biuibu, karibi, kuliba, tiskubi**. Waambie wanafunzi wayaandike kwa uhalisi. Baadaye wawasomee wenzao. **Mfano:** kebem - mkebe

Tarehe: ________________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Wiki ya 7: Siku ya 5 Nyumbani

Tamka sauti.

b s

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: u si ku **usiku**.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ma | ku | u | sa | ki | ba |
| si | li | na | bu | i | ha |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mtu **a**ka**mu**ona kuku | watu **waka**wa**ona kuku. |
| mtu **a**ka**m**kamata kuku | watu **waka**wa**kamata kuku. |
| mtoto **a**ka**mu**ona buibui | watoto **waka**wa**ona buibui. |

Babu ameketi kwenye kiti. Anazungumza na mvulana na wasichana wawili. Wamekaa chini wakimsikiliza babu.

Wasia wa babu

Babu: Njooni hapa. Sikieni wasia huu. Nawasihi msome. Masomo ni muhimu sana. Masomo huleta hekima. Hekima huleta mali.

Watoto: Naam Babu. Sisi sote tutasoma.Usiwe na wasiwasi.

Babu: Msisahau kuwasiliana na walimu wenu.

Watoto: Naam Babu. Hatutasahau. Asante kwa wasia wako.

35

■ **Majina ya herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(b)**. Tamka sauti ya herufi **/b/**. **[U]** Endelea na herufi **(s)**.

★ **Silabi: Kuandika**

Soma silabi zote zilizo ukurasa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. **[N]** Tumia silabi **u si** na **ku** kuandika neno **usiku**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

● **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

N/T/U. Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Mtu **a**ka**mu**ona kuku | Watu **waka**wa**ona kuku. |
| Mtu **a**ka**m**kamata kuku | Watu **waka**wa**kamata kuku. |
| Mtoto **a**ka**mu**ona buibui | Watoto **waka**wa**ona buibui. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **wasia, nawasihi** na **kuwasiliana**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Wasia wa Babu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

◇ **Maswali**

1. ***Babu aliwasihi watoto wafanye nini?*** *(wasome)*
2. ***Babu alisema masomo huleta nini?*** *(hekima)*
3. ***Je, ungependa kufanya kazi gani ukiwa mkubwa?*** *(watoto waeleze kazi ambayo wangependa kufanya)*
4. ***Unafikiri ni kwa nini babu aliwasihi watoto wawasiliane na walimu wao?*** *(kwa sababu walimu ndio wanaowafundisha watoto/watawasaidia)*

**Hadithi ya mwalimu**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. *(Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

**Wekesa hospitalini**

Wekesa alikuwa na shida ya kupumua. Babake akambeba na kumpeleka hospitalini. Walipofika, muuguzi alimpima Wekesa joto na mapigo ya moyo. Muuguzi alimpeleka kwa daktari. ***(Wekesa alikuwa na shida gani?)*** Daktari alimwambia muuguzi aweke dawa kwenye sindano ili amdunge Wekesa. Alimwambia muuguzi pia aweke kifaa cha kumsaidia kupumua kwenye pua. Mara tu, akaanza kuhisi vyema tena.
Alipoanza kupumua vizuri, msaidizi alimpeleka Wekesa kwenye wodi ya watoto. Ilipofika jioni mpishi alimuandalia chakula kitamu sana. (***Msaidizi alimpeleka Wekesa wapi?)***

Siku iliyofuata, Wekesa alihisi amepata nafuu kabisa. Daktari akasema, “Wekesa, unaweza kwenda nyumbani sasa. Lakini usisahau kuchukua dawa zako!” Babake wekesa akamjibu, “Asante sana Bwana Daktari.” Aliwashukuru watu wengi: daktari, muuguzi, mpishi na msaidizi. Akawapungia wote mikono akisema, “Kwaheri!” (***Kati ya watu hawa wote nani alimsaidia Wekesa sana?***)

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **samaki, soko, mkebe, bakuli, buibui.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wanafunzi waandike maneno zaidi kutoka kwa silabi zilizo ukurasa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 8: Siku ya 1 na 2 **Familia**

Tamka sauti.

y b s

Tamka sauti ya herufi na silabi.

y a y e y i y u

**ya ye yi yu**

Soma silabi na maneno.

ma ya i ye ru sa he ka ya ya ya

**mayai yerusa hekaya yaya**

Tamka sauti.

y

Tamka sauti ya herufi na silabi.

y o b o l o h o

**yo bo lo ho**

Soma sehemu za neno na neno lote.

hu tu okea

**hutuokea**

hu tu somea

**hutusomea**

a na ye tii

**anayetii**

a ta ku somea

**atakusomea**

Sarufi: Soma sentensi zifuatazo.

| huyu | yule |
|---|---|
| 1. yaya **huyu** ni mzuri | yaya **yule** ni mzuri. |
| 2. babu **huyu** ni mrefu | babu **yule** ni mrefu. |
| 3. paka **huyu** ni mkali | paka **yule** ni mkali. |
| 4. kuku **huyu** ni mnono | kuku **yule** ni mnono. |

36

Wiki ya 8: Siku ya 1 na 2 **Familia**

Watoto wawili wakiwa vitandani wanasomewa kitabu na msichana mkubwa.

**Yerusa yaya wetu**

Yaya wetu ni Yerusa.

Kila asubuhi Yerusa hutuokea keki na mayai.

Kabla ya kulala, yeye hutusomea hekaya tamu tamu.

Ukiwa mtoto mtiifu, Yerusa hukusomea hekaya nyingi wakati wa kulala. Hekaya huwa tamu.

37

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/y/**. Taja maneno **(yaya, huyu)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea na maneno **yuko, hayo, yeye, pabaya.**

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **y**. Tamka sauti **/y/**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **ya**. Sema kila sauti **/y//a/** kisha uunganishe na kusema silabi **ya**. **[U]** Endelea na silabi: **ye, yi, yu.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **ma ya i** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mayai**. **[U]** Endelea na maneno: **Yerusa, hekaya** na **yaya.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **yaya, hutuokea** na **hekaya**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Yerusa yaya wetu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Yaya Yerusa alifanya kazi zipi?*** *(kupika chakula kama keki na mayai, kusimamia watoto kuelewa masomo, kusomea watoto hadithi n.k.)*
2. ***Yerusa hupika nini kila asubuhi?*** *(Yeye huoka keki na kupika mayai.)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **y** mara tatu.

y y y y y

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **Yaya, mayai, yeye, kuyaelewa, hekaya**. Waagize wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 8: Siku ya 1 na 2 — **Familia**

Tamka sauti.

y b s

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| y a | y e | y i | y u |
|---|---|---|---|
| **ya** | **ye** | **yi** | **yu** |

Soma silabi na maneno.

| ma ya i | ye ru sa | he ka ya | ya ya |
|---|---|---|---|
| **mayai** | **yerusa** | **hekaya** | **yaya** |

Tamka sauti.

y

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| y o | b o | l o | h o |
|---|---|---|---|
| **yo** | **bo** | **lo** | **ho** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu tu okea | hu tu somea |
|---|---|
| **hutuokea** | **hutusomea** |
| a na ye tii | a ta ku somea |
| **anayetii** | **atakusomea** |

Sarufi: Soma sentensi zifuatazo.

| **huyu** | **yule** |
|---|---|
| 1. yaya **huyu** ni mzuri | yaya **yule** ni mzuri. |
| 2. babu **huyu** ni mrefu | babu **yule** ni mrefu. |
| 3. paka **huyu** ni mkali | paka **yule** ni mkali. |
| 4. kuku **huyu** ni mnono | kuku **yule** ni mnono. |

36

Wiki ya 8: Siku ya 1 na 2 — **Familia**

Watoto wawili wakiwa vitandani wanasomewa kitabu na msichana mkubwa.

**Yerusa yaya wetu**

Yaya wetu ni Yerusa.
Kila asubuhi Yerusa hutuokea keki na mayai.
Kabla ya kulala, yeye hutusomea hekaya tamu tamu.
Ukiwa mtoto mtiifu, Yerusa hukusomea hekaya nyingi wakati wa kulala. Hekaya huwa tamu.

37

### ▲ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **y**. Tamka sauti ya herufi **/y/**.

### ⬬ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **yo**. Sema kila sauti **/y//o/** kisha uunganishe na kusema silabi **yo**. **[U]** Endelea na silabi: **bo, lo, ho.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **hu tu okea** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **hutuokea**. **[U]** Endelea kwa maneno: **hu tu somea (hutusomea), a na ye tii (anayetii), a ta ku somea (atakusomea).** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

Eleza wanafunzi jinsi ya matumizi ya vionyeshi **huyu yule**.

[N/T] Soma sentensi kisha uzisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

1. Yaya **huyu** ni mzuri - Yaya **yule** ni mzuri.
2. Babu **huyu** ni mrefu - Babu **yule** ni mrefu.
3. Paka **huyu** ni mkali - Paka **yule** ni mkali.
4. Kuku **huyu** ni mnono - Kuku **yule** ni mnono.

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **yaya, hutuokea** na **hekaya**.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Yerusa yaya wetu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Taja tabia za mtoto mtiifu*** *(kufuata maagizo ya mwalimu na wazazi/kufanya kazi wazazi wanazokutuma n.k.)*
2. ***Yaya mzuri hufanya nini?*** *(hutusaidia kazi/hutuchekesha/hucheza na sisi n.k.)*

### ✍ Kuandika

Soma neno **yaya**. Wanafunzi waliandike. Kisha wajadiliane kuhusu **yaya**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye vifungu vifuatavyo:

**baba huyu** - **baba yule**
**mtoto huyu** - **mtoto yule**
**mtu huyu** - **mtu yule**

Waagize wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao:

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 8: Siku ya 3 na 4 — Familia

Tamka sauti.

z y b

Tamka sauti ya herufi na silabi.

z a — **za** · z i — **zi** · z u — **zu** · z e — **ze**

Soma silabi na maneno.

zi zi ni — **zizini** · za bi bu — **zabibu** · zi wa ni — **ziwani** · wa za zi — **wazazi**

Tamka sauti.

z

Tamka sauti ya herufi na silabi.

z o — **zo** · s o — **so** · y o — **yo** · b o — **bo**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa li elekea — **walielekea** · wa li kula — **walikula**

ku wa bebea — **kuwabebea** · wa ka wa nunulia — **wakawanunulia**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| huu ni mnazi wetu | hii ni minazi yetu. |
| huu ni mzabibu wetu | hii ni mizabibu yetu. |
| huu ni mlimau wetu | hii ni milimau yetu. |
| huu ni mmea wetu | hii ni mimea yetu. |
| huu ni mkebe wetu | hii ni mikebe yetu. |

38

Wiki ya 8: Siku ya 3 na 4 — Familia

Msichana mdogo anavaa miwani. Baba na mama wameketi kwa kiti na wamebeba matunda. Wanamskiliza mvulana akicheza muziki akiwa ameketi kwenye mkeka.

### Zani na Ziki

Ilikuwa wakati wa likizo. Zani na Ziki walikuwa na zamu ya kutazama zizi lao na ziwa.
Kila asubuhi walielekea zizini.
Baadaye walielekea ziwani.
Huko waliona minazi na mizabibu.
Walikula zabibu. Waliwabebea wazazi wao zabibu na nazi.
Wazazi wakawanunulia zawadi. Zani akanunuliwa zawadi ya zeze. Ziki akanunuliwa zawadi ya miwani.

39

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/z/**. Taja maneno (**ziwa, kizungu)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea na maneno: **zizi, wazazi, zamani, mkizi, zawadi, kaza.**

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **z**. Tamka sauti **/z/**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **za**. Sema kila sauti /**z**//**a**/ kisha uunganishe na kusema silabi **za**. **[U]** Endelea kwa silabi**: zi, zu, ze.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Andika neno **zizini**. Tamka silabi **zi zi ni** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **zizini**. **[U]** Endelea na maneno **zabibu, ziwani** na **wazazi.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **likizo, zamu** na **zabibu, zeze**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **Zani na Ziki** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Taja vitu ambavyo Zani na Ziki waliona walipoenda ziwani.*** *(minazi na mizabibu).*
2. ***Taja zawadi ambazo Zani na Ziki walipewa na wazazi wao?*** *(Zani alipewa zeze/Ziki alipewa miwani).*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **z** mara tatu.

z z z z z

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo.

i. **Walielekea zizini.**
ii. **Walikuwa na zamu.**
iii. **Waliona minazi na mizabibu.**
iv. **Walinunua zawadi.**

Waagize wanafunzi wazinakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 8: Siku ya 3 na 4 — **Familia**

Tamka sauti.

**z** **y** **b**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| z a | z i | z u | z e |
|---|---|---|---|
| **za** | **zi** | **zu** | **ze** |

Soma silabi na maneno.

| zi zi ni | za bi bu | zi wa ni | wa za zi |
|---|---|---|---|
| **zizini** | **zabibu** | **ziwani** | **wazazi** |

Tamka sauti.

**z**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| z o | s o | y o | b o |
|---|---|---|---|
| **zo** | **so** | **yo** | **bo** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa li elekea — **walielekea**

wa li kula — **walikula**

ku wa bebea — **kuwabebea**

wa ka wa nunulia — **wakawanunulia**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| huu ni **m**nazi wetu | hii ni **mi**nazi yetu. |
| huu ni **m**zabibu wetu | hii ni **mi**zabibu yetu. |
| huu ni **m**limau wetu | hii ni **mi**limau yetu. |
| huu ni **m**mea wetu | hii ni **mi**mea yetu. |
| huu ni **m**kebe wetu | hii ni **mi**kebe yetu. |

38

Wiki ya 8: Siku ya 3 na 4 — **Familia**

Msichana mdogo anavaa miwani. Baba na mama wameketi kwa kiti na wamebeba matunda. Wanamskiliza mvulana akicheza muziki akiwa ameketi kwenye mkeka.

### Zani na Ziki

Ilikuwa wakati wa likizo. Zani na Ziki walikuwa na zamu ya kutazama zizi lao na ziwa.

Kila asubuhi walielekea zizini.

Baadaye walielekea ziwani.

Huko waliona minazi na mizabibu.

Walikula zabibu. Waliwabebea wazazi wao zabibu na nazi.

Wazazi wakawanunulia zawadi. Zani akanunuliwa zawadi ya zeze. Ziki akanunuliwa zawadi ya miwani.

39

▲ **Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **z**. Tamka sauti ya herufi **/z/**.

⬬ **Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **zo**. Sema kila sauti **/z//o/** kisha uunganishe na kusema silabi **zo**. **[U]** Endelea na silabi: **so, yo** na **bo.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa li elekea** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **walielekea** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **wa li kula (walikula), ku wa bebea (kuwabebea), wa ka wa nunulia (wakawanunulia).** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

◆ **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

[N/T/U] Some sentensi kisha uzisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Huu ni **m**nazi wetu | Hii ni **mi**nazi yetu. |
| Huu ni **m**zabibu wetu | Hii ni **mi**zabibu yetu. |
| Huu ni **m**limau wetu | Hii ni **mi**limau yetu. |
| Huu ni **m**mea wetu | Hii ni **mi**mea yetu. |
| Huu ni **m**kebe wetu | Hii ni **mi**kebe yetu. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **likizo, zamu, zeze** na **zabibu**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Zani na Ziki"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Kwa nini Zani na Ziki walituzwa?*** *(kwa sababu waliwasaidia wazazi, waliwaletea wazazi wao nazi, pengine walifanya vyema shuleni)*
2. ***Wewe hufanya nini wakati wa likizo?*** *(Hutembelea nyanya babu; hucheza na marafiki, husaidia wazazi)*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Waambie wanafunzi wayaandike kwa wingi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| mnazi | - | ___________ |
| mzabibu | - | ___________ |
| mkebe | - | ___________ |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

Kamilisha somo kwa kuimba wimbo: **Kuna mtu shambani**.

**Wimbo**: Kuna mtu shambani ia, ia kuna mtu shambani. Mtu ataka mke.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yaliyochanganywa: **zoliki, muza, wanizi, nizizi, bibumiza**. Waambie wanafunzi wayapange na kwa usahihi kisha wawasomee wenzao.

**Mfano:** zoliki - likizo

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 8: Siku ya 5 **Familia**

Tamka sauti.

z y

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: wa za zi **wazazi**.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| si | ka | za | wa | wa | na |
| zi | ha | i | ma | ti | ki |

Sarufi: Soma maneno haya.

| wakati uliopo | wakati uliopita |
|---|---|
| 1. anakaa | alikaa |
| 2. anaona | aliona |
| 3. analia | alilia |
| 4. anataka | alitaka |

Mzee ameketi kwa kiti akishikilia mashavu akiwa na bakora. Naye msichana ameketi kando ya mzee nje ya nyumba.

Ayoo

Ayoo ni mtoto. Baba yake ni Otieno. Mama yake anaitwa Kanini.

Yeye hukaa na babu yake wilayani Kikuyu. Kila siku Ayoo huletewa mayai na shangazi yake Zainabu.

Bibi humwekea mabuyu kibuyuni. Ayoo hutamani chakula kitamu zaidi ya mabuyu. Yeye huomba ili babu yake awe na mali.

40

### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(y)**. Tamka sauti ya herufi **/y/**. **[U]** Endelea na **(z)**. Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Silabi: Kuandika

**[N]** Soma silabi zote zilizo ukurasa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **wa, za** na **zi** kuandika neno **wazazi**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

[N/T/U] Fuatilia mtindo wa kufundisha nyakati: **Leo – Jana**. Kisha uzisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| Wakati uliopo | Wakati uliopita |
|---|---|
| 1. anakaa | alikaa |
| 2. anaona | aliona |
| 3. analia | alilia |
| 4. anataka | alitaka |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **wilayani, mabuyuni** na **mali**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **Ayoo** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Ayoo na babu yake wanaishi wapi?*** *(Wanaishi wilaya ya kikuyu)*
2. ***Je, Ayoo husali kila siku kwa nini?*** *(ili babu yake awe na mali)*
3. ***Bibi humwekea mabuyu wapi?*** *(Kibuyuni)*
4. ***Unafikiri kama Ayoo na babu yake wangepata mali wangefanya nini?*** *(wangenunua chakula kizuri, wangejenga nyumba n.k.)*

### 🕮 Hadithi ya mwalimu

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi wasikize kwa makini.

**Ndoto ya Wanjiru**

Wanjiru alipokuwa katika darasa la kwanza, alikuwa mtoto wa pekee hakuwa na ndugu. Alihuzunika sana. Wazazi wake walimwambia kuwa siku moja, Mungu angempa ndugu. Siku moja, baba alimsomea hadithi. Baadaye, Wanjiru aliwaona watoto wengi katika chumba chake cha kulala. Akaanza kuwahesabu, "Mmoja, wawili, watatu... kumi." Mara wakaongezeka. Wanjiru akashangaa sana. Akawaweka kwenye makundi ya watoto kumi. Kisha Wanjiru akaendelea kuhesabu, "Kumi, ishirini, thelathini, arobaini, hadi mia moja."

Wanjiru akaogopa sana. Babake akamwambia, "Hawa ni ndugu zako." Wanjiru akaanza kulia akisema,"Chumba changu kimejaa na sitaki kuwapa doli wangu." Mara tu, mama akamwamsha kwenda msalani kabla ya kwenda kulala. Ndipo Wanjiru akatambua kuwa ilikuwa ndoto tu.

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika kwenye vitabu vyao: **mayai, hekaya, zizini, minazi, zawadi**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waendelee kuunda maneno zaidi kutoka kwa silabi walizopewa katika ukurasa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 9: Siku ya 1 na 2 **Sokoni/Dukani**

Tamka sauti.

**g** **z** **y**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

g a — **ga**
g aa — **gaa**
g e — **ge**
g i — **gi**

Soma silabi na maneno.

ki so go — **kisogo**
mi zi go — **mizigo**
ma go ti — **magoti**
gaa gaa — **gaagaa**

Tamka sauti.

**g**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

g u — **gu**
g i — **gi**
g o — **go**
g oo — **goo**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa ka wa samehe — **wakawasamehe**
wa ka wategа — **wakawatega**
wa ka wa ona — **wakawaona**
wa ka gaagaa — **wakagaagaa**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| hili ni bega | haya ni mabega. |
| hili ni goti | haya ni magoti. |
| hili ni sikio | haya ni masikio. |
| hili ni gego | haya ni magego. |

41

Wiki ya 9: Siku ya 1 na 2 **Sokoni/Dukani**

Vijana wawili wanakimbizwa na umati wa watu sokoni.

### Wezi sokoni

Katika soko la Mogotio, kulitokea wezi watatu.
Walitaka kuiba mizigo sokoni.
Watu wakawaona.
Wezi wakataka kutoroka.
Watu wakawatega.
Mtego ukawakamata.
Wezi wakaumia sana.
Kuna wale waliumia visogo. Wengine wakaumia mabega, magoti na miguu.
Wezi wakagaagaa.
Muuguzi akawatibu.
Watu wakawasamehe.
Kutoka siku hiyo wezi hawakuiba tena.

42

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti /**g**/. Taja maneno **(gamba, agiza)** halafu wanafunzi wafanye ishara waliokubaliana. Endelea na maneno **[U] ganga, babu, gari, gogo, gazeti**.

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **g**. Tamka sauti /**g**/. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **ga**. Sema sauti /**g**/ /**a**/ kisha uunganishe na kusema silabi **ga**. **[U]** Endelea kwa silabi **gaa, ge, gi.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **ki so go** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **kisogo**. **[U]** Endelea na maneno: **mizigo, magoti, gaagaa.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mizigo, wakawatega/ tega** na **wakagaagaa/gaagaa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo.

Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Wezi sokoni"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

- *i.* ***Wezi walitokea katika soko gani?*** *(mogotio)*
- *ii.* ***Wezi hao walitaka kuiba nini?*** *(wezi walitaka kuiba mizigo)*
- *iii.* ***Wezi waliumia wapi?*** *(mabega, magoti na miguu)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **g** mara tatu.

g g g g g

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **kisogo, mabega, magoti, miguu, muuguzi.** Wanafunzi wayaandike kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Tamka sauti.

g z y

Tamka sauti ya herufi na silabi.

g a g aa g e g i

**ga** **gaa** **ge** **gi**

Soma silabi na maneno.

ki so go mi zi go ma go ti gaa gaa

**kisogo** **mizigo** **magoti** **gaagaa**

Tamka sauti.

g

Tamka sauti ya herufi na silabi.

g u g i g o g oo

**gu** **gi** **go** **goo**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa ka wa samehe wa ka wa tega

**wakawasamehe** **wakawatega**

wa ka wa ona wa ka gaagaa

**wakawaona** **wakagaagaa**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| hili ni bega | haya ni mabega. |
| hili ni goti | haya ni magoti. |
| hili ni sikio | haya ni masikio. |
| hili ni gego | haya ni magego. |





Vijana wawili wanakimbizwa na umati wa watu sokoni.

**Wezi sokoni**

Katika soko la Mogotio, kulitokea wezi watatu.
Walitaka kuiba mizigo sokoni.
Watu wakawaona.
Wezi wakataka kutoroka.
Watu wakawatega.
Mtego ukawakamata.
Wezi wakaumia sana.
Kuna wale waliumia visogo. Wengine wakaumia mabega, magoti na miguu.
Wezi wakagaagaa.
Muuguzi akawatibu.
Watu wakawasamehe.
Kutoka siku hiyo wezi hawakuiba tena.



▲ **Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **g**. Tamka sauti /**g**/.

⬬ **Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **gu**. Sema sauti **/g/ /u/** kisha uunganishe na kusema silabi **gu**. **[U]** Endelea kwa silabi: **gi, go, goo**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa ka wa samehe** kisha uunganishe sehemu hizo upesi na useme neno **wakawasamehe**. **[U]** Endelea na: **wa ka wa ona (wakawaona), wa ka wa tega (wakawatega), wa ka gaagaa (wakagaagaa).** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

◆ **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

N/T/U. Soma sentensi katika umoja na wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **Hili** ni bega | **Haya** ni **ma**bega. |
| **Hili** ni goti | **Haya** ni **ma**goti. |
| **Hili** ni sikio | **Haya** ni **ma**sikio. |
| **Hili** ni gego | **Haya** ni **ma**gego. |

🕮 **Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **mizigo, tega** na **gaagaa**.

🕮 **Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi **"Wezi sokoni"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome kwa vikundi vya wawili.

◈ **Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

*i.* ***Je, unafikiria kama watu hawangewaona wezi nini kingefanyika?*** *(watu hawangewatega, wangeiba vitu sokoni n.k.)*

*ii.* ***Je, unafikiri watu walifanya vizuri kuwasamehe wezi?*** *(ndio, la)*

*iii.* ***Kwa nini unafikiria hivyo?*** *(kwa sababu waliposamehewa hawakuiba tena, kwa sababu walikuwa wameumia)*

✍ **Kuandika: Imla**

Soma maneno '**bega**' '**goti**' '**sikio**' '**gego**'. Wanafunzi wayaandike kisha wajadiliane kuhusu sehemu za mwili.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno haya:

**bega** - **mabega**
**goti** - **magoti**
**sikio** - **masikio**

Waagize wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao:

Tarehe: ________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Wiki ya 9: Siku ya 3

Wiki ya 9: Siku ya 3 na 4 — **Sokoni/Dukani**

Tamka sauti.

**d** **g** **z**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

d e · d i · d u · d o

**de** · **di** · **du** · **do**

Soma silabi na maneno.

de be · do li · A di di · da ki ka

**debe** · **doli** · **Adidi** · **dakika**

Tamka sauti.

**d** **d**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

d a · b a · d e · b e

**da** · **ba** · **de** · **be**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa ka elekea — **wakaelekea**

ku ni nunulia — **kuninunulia**

tu ta nunua — **tutanunua**

a ka kubali — **akakubali**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| hili ni debe | haya ni madebe. |
| hili ni godoro | haya ni magodoro. |
| hili ni doli | haya ni madoli. |
| hili ni dau | haya ni madau. |

43

Wiki ya 9: Siku ya 3 na 4 — **Sokoni/Dukani**

Kuna watu wengi sokoni. Wengine wanauza na wengine wananunua.

### Adidi na Baba sokoni

Baba aliita, "Adidi! Amka! Leo ni siku ya soko."
Adidi aliamka baada ya dakika kumi.
Wakaelekea soko la Gede.
Baba akasema, "Adidi, leo tutanunua dagaa, dania, debe na godoro."
Adidi akauliza, "Baba, unaweza kuninunulia soda, doli na gololi?"
"Sawa Adidi, nitakununulia." Baba akakubali.

44

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/d/**. Taja maneno **(dada, ada)** halafu wanafunzi wafanye ishara waliokubaliana. Endelea na maneno **[U] dunia, ibada, baba, darasa, gari**.

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **d**. Tamka sauti **/d/**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma silabi

Andika silabi **de**. N/T/U: Sema sauti **/d/ /e/** kisha uunganishe na kusema silabi upesi **de**. **[U]** Endelea kwa silabi **di, du, do.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **de be** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **debe**. **[U]** Endelea na maneno **doli, Adidi** na **dakika**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **dania, gololi** na **dagaa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo.

Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Adidi na Baba sokoni"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

i. ***Baba alimuambia Adidi ilikuwa siku ya nini?*** *(ilikuwa siku ya soko)*
ii. ***Baba na Adidi walielekea soko gani?*** *(Gede)*
iii. ***Adidi alitaka baba amnunulie nini?*** *(soda, doli na gololi)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **d** mara tatu.

d d d d d

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wanafunzi wapatiwe kadi za breli zenye sentensi zifuatazo. Wanafunzi wazinakili kisha wawasomee wenzao.

i. **Leo tutanunua dagaa.**
ii. **Leo tutanunua dania.**
iii. **Unaweza kununua godoro.**
iv. **Unaweza kununua gololi.**

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 9: Siku ya 3 na 4 — Sokoni/Dukani

Tamka sauti.

d g z

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| d e | d i | d u | d o |
|---|---|---|---|
| **de** | **di** | **du** | **do** |

Soma silabi na maneno.

| de be | do li | A di di | da ki ka |
|---|---|---|---|
| **debe** | **doli** | **Adidi** | **dakika** |

Tamka sauti.

d d

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| d a | b a | d e | b e |
|---|---|---|---|
| **da** | **ba** | **de** | **be** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa ka elekea | ku ni nunulia |
|---|---|
| **wakaelekea** | **kuninunulia** |
| tu ta nunua | a ka kubali |
| **tutanunua** | **akakubali** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **umoja** | **wingi** |
|---|---|
| **hili** ni debe | **haya** ni **ma**debe. |
| **hili** ni godoro | **haya** ni **ma**godoro. |
| **hili** ni doli | **haya** ni **ma**doli. |
| **hili** ni dau | **haya** ni **ma**dau. |

43

Wiki ya 9: Siku ya 3 na 4 — Sokoni/Dukani

Kuna watu wengi sokoni. Wengine wanauza na wengine wananunua.

**Adidi na Baba sokoni**

Baba aliita, "Adidi! Amka! Leo ni siku ya soko."
Adidi aliamka baada ya dakika kumi.
Wakaelekea soko la Gede.
Baba akasema, "Adidi, leo tutanunua dagaa, dania, debe na godoro."
Adidi akauliza, "Baba, unaweza kuninunulia soda, doli na gololi?"
"Sawa Adidi, nitakununulia." Baba akakubali.

44

### ▲ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **d**. Tamka sauti **/d/**.

### ⬬ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **da**. Sema sauti **/d/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi kwa upesi **da**. **[U]** Endelea na silabi: **ba, de** na **be**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa ka elekeza** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **wakaelekea**. **[U]** Endelea na: **ku ni nunulia (kuninunulia), tu ta nunua (tutanunua), a ka kubali (akakubali).** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

N/T/U. Soma sentensi hizi katika umoja na wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **Hili** ni debe | **Haya** ni **ma**debe. |
| **Hili** ni godoro | **Haya** ni **ma**godoro. |
| **Hili** ni doli | **Haya** ni **ma**doli. |
| **Hili** ni dau | **Haya** ni **ma**dau. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **dania, gololi** na **dagaa**.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Adidi na Baba sokoni"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome kwa vikundi vya wawili wawili.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

i. ***Je, unafikiri Adidi na babake walienda sokoni saa ngapi?*** *(Asubuhi, mchana, saa tatu, saa kumi, n.k.)*

ii. ***Je, unafikiri Adidi na babake walikula nini siku hiyo?*** *(dagaa)*

iii. ***Je, kwa nini Adidi alitaka gololi?*** *(kwa sababu alitaka kucheza nayo)*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Wanafunzi waandike wingi wa maneno hayo.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| debe | - | madebe |
| godoro | - | ____________ |
| doli | - | ____________ |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yaliyo changanywa: **gaada, niada, lido, bede, rogodo**. Wanafunzi wayaandike maneno halisi. Baadaye wawasomee wenzao. **Mfano:** gaada - dagaa

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 9: Siku ya 5 **Sokoni/Dukani**

Tamka sauti.

g d

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: da ki ka **dakika**.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| m | go | ge | be | de | ki |
| da | ma | ti | ka | te | mu |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

1. kaka ali**enda** shuleni.
2. mtoto ali**lia** kitini.
3. jitu lili**simama** njiani.
4. bibi ali**beba** mzigo.

Wanaume wawili wamebeba mizigo mizito.

**Kazi ya Kogo na Radoli**

Kogo na Radoli walikaa Migori. Kazi yao ilikuwa kubeba mizigo mizito. Kila asubuhi walibeba magunia mazito ya mboga na mihogo. Kila usiku mabega na miguu yao iliuma sana. Walikula ugali kwa uyoga. Walikubaliana kugawana hela baada ya kazi.

45

### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(g)**. Tamka sauti ya herufi **/g/**. **[U]** Endelea na herufi **(d)**.

### ★ Silabi: Kuandika

Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. **[N]** Tumia silabi **da, ki** na **ka** kuandika neno **dakika**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

N/T/U. Soma sentensi hizi.

1. Kaka ali**enda** shuleni.
2. Mtoto ali**lia** kitini.
3. Jitu lili**simama** njiani.
4. Bibi ali**beba** mzigo.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **uyoga, kugawana** na **hela**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Kazi ya Kogo na Radoli"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

- ***i.*** ***Kogo na Radoli walikaa wapi?*** *(Migori)*
- ***ii.*** ***Kogo na Radoli walifanya kazi gani?*** *(kubeba mizigo)*
- ***iii.*** ***Je, unafikiri Kogo na Radoli walifanya kazi yao ofisini au sokoni?*** *(sokoni)*
- ***iv.*** ***Kwa nini unasema hivyo?*** *(kwa sababu mizigo ya mboga na mihogo hupatikana sokoni, n.k.)*

### Hadithi ya mwalimu

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. *(Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

**Gazeti**

Rukia aliishi na wenzake kwenye nyumba ya malezi. Kila jioni walipenda kusoma gazeti la Taifa Leo kwenye maktaba. (***Rukia na wenzake waliishi wapi?***) Kwenye gazeti hilo walipenda kusoma taarifa na kutazama picha.

Siku moja Rukia na Saada wakaamua kusoma sehemu ya matangazo. Kwenye sehemu hiyo kulikuwa na matangazo ya michezo ya watoto. Saada na Rukia wakamuonyesha mama mlezi tangazo hilo la michezo. (***Rukia walimuonyesha nani gazeti?***) Wakamuomba ruhusa ya kushiriki katika michezo hiyo.

Mama mlezi akawaita watoto wote na kuwaambia, "Kesho tutaenda kushiriki katika michezo ya watoto." Watoto walifurahi sana kusikia hivyo.

Asubuhi na mapema watoto wote wakaanza safari ya kwenda uwanjani. Rukia alishinda mbio za mita mia moja na akapewa nishani ya dhahabu. (***Je, wewe umewahi kusoma gazeti? Ni sehemu gani iliyokupendeza?***)

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **walikaa, mboga, kugawana, walibeba, dagaa.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Eleza wanafunzi waendelee kuunda maneno zaidi kutoka kwa silabi walizopewa katika ukurasa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 10: Siku ya 1 na 2 — Siku za Wiki

Tamka sauti.

j d g

Tamka sauti.

j a — ja    j aa — jaa    j e — je    j i — ji

Soma sentensi hizi.

1. kaka alienda shuleni.
2. mtoto alilia kitini.
3. jitu lilisimama njiani.
4. bibi alibeba mzigo.

Tamka sauti.

j

Tamka sauti ya herufi na silabi.

j u — ju    g u — gu    d u — du    j o — jo

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa na kijiji — wanakijiji    wa ka mu amini — wakamuamini

ha wa ku amini — hawakuamini    a ka li patia — akalipatia

Sarufi: Soma sentensi hizi.

1. dada ameketi wapi?
2. paka amesimama wapi?
3. mwalimu ameandika wapi?
4. jiwe liko wapi?

46

Wiki ya 10: Siku ya 1 na 2 — Siku za Wiki

1. kitini
2. dirishani
3. mezani
4. ubaoni

Jitu lenye umbo la binadamu. Lenye pembe mbili, macho matatu kwenye utosi na masikio kama ya popo. Limeshika mfupa mkononi. Lina kucha ndefu za kutisha.

**Jilo na Jitu**

Siku ya Jumatatu jioni, Jilo aliona jitu kijijini.
Akasema, "Nimeliona jitu majanini." Wanakijiji hawakuamini.
Siku ya Jumanne, Jumatano na Alhamisi mchana akaliona jitu tena.
Siku ya Ijumaa asubuhi jitu likasema, "Jilo, nataka kula."
Jilo alijawa na wasiwasi.
Akalipatia jitu jiwe la moto.
Jitu likala jiwe na kuzimia.
Siku ya Jumamosi walilizika jitu. Jumapili ilipofika walifanya sherehe kwa heshima ya Jilo. Wanakijiji wote walimwamini jilo.

47

**Ufahamu wa fonimu**

N/T/U: Tamka sauti **/j/**. Taja maneno **(jamii, Ijumaa)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]**Endelea kwa maneno ***jani, ajali, jogoo, moto, joto, jua, juzi***.

**Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **j**. Tamka sauti **/j/**. Andika herufi **j** hewani. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **ja**. Tamka kila sauti **/j/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi **ja**. **[U]** Endelea na silabi**: jaa, je, ji.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U: Tamka silabi **ji** na **tu** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **jitu**. **[U]** Endelea na maneno: **alijawa, kijijini, Jumatano.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kuzimia, alhamisi** na **ijumaa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Jilo na Jitu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Jilo aliona jitu siku gani?*** *(Jumatatu/Jumanne/Jumatano/Alhamisi/Ijumaa).*
2. ***Jitu lilikaa wapi?*** *(Jitu lilikaa kwenye majani/Jitu lilikaa majanini).*
3. ***Jitu lilikula nini?*** *(jiwe la moto).*

**Kuandika**

Waagize wanafunzi waandike herufi **j** mara tatu.

j j j j j

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wanafunzi wapewe kadi za breli zenye maneno haya: **jitu, kijijini, Jumanne, Jumatatu, Ijumaa**. Waambie wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 10: Siku ya 1 na 2 — Siku za Wiki

Tamka sauti.

j d g

Tamka sauti.

j a — ja
j aa — jaa
j e — je
j i — ji

Soma sentensi hizi.

1. kaka alienda shuleni.
2. mtoto alilia kitini.
3. jitu lilisimama njiani.
4. bibi alibeba mzigo.

Tamka sauti.

j

Tamka sauti ya herufi na silabi.

j u — ju
g u — gu
d u — du
j o — jo

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa na kijiji — wanakijiji
wa ka mu amini — wakamuamini
ha wa ku amini — hawakuamini
a ka li patia — akalipatia

Sarufi: Soma sentensi hizi.

1. dada ameketi wapi?
2. paka amesimama wapi?
3. mwalimu ameandika wapi?
4. jiwe liko wapi?

46

Wiki ya 10: Siku ya 1 na 2 — Siku za Wiki

1. kitini
2. dirishani
3. mezani
4. ubaoni

Jitu lenye umbo la binadamu. Lenye pembe mbili, macho matatu kwenye utosi na masikio kama ya popo. Limeshika mfupa mkononi. Lina kucha ndefu za kutisha.

**Jilo na Jitu**

Siku ya Jumatatu jioni, Jilo aliona jitu kijijini.
Akasema, "Nimeliona jitu majanini." Wanakijiji hawakuamini.
Siku ya Jumanne, Jumatano na Alhamisi mchana akaliona jitu tena.
Siku ya Ijumaa asubuhi jitu likasema, "Jilo, nataka kula."
Jilo alijawa na wasiwasi.
Akalipatia jitu jiwe la moto.
Jitu likala jiwe na kuzimia.
Siku ya Jumamosi walilizika jitu. Jumapili ilipofika walifanya sherehe kwa heshima ya Jilo. Wanakijiji wote walimwamini jilo.

47

▲ **Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **j**. Tamka sauti ya herufi **/j/**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

⬬ **Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **ju**. Sema kila sauti **/j//u/** kisha uunganishe na kusema silabi **ju**. **[U]** Endelea na silabi: **gu, du, jo.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wana ki jiji** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **wanakijiji** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **ha wa ku amini (hawakuamini), wa ka mu amini (wakamuamini), a ka li patia (akalipatia).** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

◆ **Sarufi**

[N/T/U] Wasomee wanafunzi maswali yafuatayo. Kisha wasaidie kupata majibu kwenye maelezo yaliyo kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. **[Majibu ni: kitini, dirishani, ubaoni, mezani]**

1. Dada ameketi wapi?
2. Paka amesimama wapi?
3. Mwalimu ameandika wapi?
4. Jiwe liko wapi?

🕮 **Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **kuzimia, Alhamisi** na **ijumaa**.

🕮 **Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Jilo na jitu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Kwa nini Jilo alijawa na wasiwasi?*** *(kwa sababu jitu lilitaka kumla)*
2. ***Unafikiri ni kwa nini wanakijiji hawakumuamini Jilo?*** *(hawakuwa wameliona jitu, walifikiri Jilo alikuwa anafanya mzaha, n. k.)*

✍ **Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **Jiwe**, **jitu**, **Jumanne**, **majanini**, **jaa**. Waagize wanafunzi wayaandike. Kisha wajadiliane kuhusu jitu.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno **'kitini' 'mezani' 'dirishani' 'ubaoni'**. Wanafunzi wayanakili kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 10: Siku ya 3

Wiki ya 10: Siku ya 3 na 4 Siku za Wiki

Tamka sauti.

**r** **g** **j**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

r e | r a | r i | r o
**re** | **ra** | **ri** | **ro**

Soma silabi na maneno.

ra i s | ga ri | ra di | Ja nu a ri
**rais** | **gari** | **radi** | **Januari**

Tamka sauti.

**r**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

r u | j i | w a | g a
**ru** | **ji** | **wa** | **ga**

Soma sehemu za neno na neno lote.

li li simama — **lilisimama**
tu ka sikia — **tukasikia**
a ki malizia — **akimalizia**
wa ka torokea — **wakatorokea**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **wakati uliopo** | **wakati ujao** |
|---|---|
| rais a**na**kuja kijijini | rais a**ta**kuja kijijini. |
| rais a**na**simama barabarani | rais a**ta**simama barabarani. |
| rais a**na**wasihi watu | rais a**ta**wasihi watu. |
| rais a**na**furahi sana | rais a**ta**furahi sana. |

48

Wiki ya 10: Siku ya 3 na 4 Siku za Wiki

Mtu aliyevalia suti amesimama juu ya gari lililofunguliwa dau. Amezingirwa na askari na anahutubia umati wa watu sokoni akitumia kipaza sauti.

**Ziara ya Rais**

Ilikuwa siku ya Jumatatu mwezi wa Januari Rais alipotutembelea. Rais wetu alikuja kijijini kukutana na raia.
Gari lake lilisimama barabarani.
Rais akasema, "Nawasihi mkae kwa amani na watu wote."
Siku hiyo, wanakijiji walikuwa na furaha sana.
Akimalizia ziara yake, mara tukasikia radi.
Watu wakatorokea madukani.
Kesho yake barabara ilikuwa imejaa maji.

49

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/r/**. Taja maneno **(raia, mpira)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea na maneno: ***radi, mradi, Rais, ziara***.

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **r**. Tamka sauti **/r/**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **re**. Sema kila sauti **/r//e/** kisha uunganishe na kusema silabi **re**. **[U]** Endelea kwa silabi **ra, ri** na **ro.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **/ra/ /i/ /s/** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **rais**. **[U]** Endelea na maneno: **gari, radi** na **Januari.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **ziara, radi** na **amani**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Ziara ya Rais"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**.** **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Ni nani alikuja kijijini?*** *(Ni Rais wetu alikuja kijijini)*
2. ***Rais aliwaambia nini wanakijiji?*** *(alisema wakae kwa amani na watu wote)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **r** mara tatu.

r r r r r

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi hizi. **Rais alikutana na raia; Rais alisimama barabarani; wanakijiji walikuwa na raha; wanakijiji walisikia radi.** Waambie wanafunzi wazinakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Tamka sauti.

r g j

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| r e | r a | r i | r o |
| re | ra | ri | ro |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ra i s | ga ri | ra di | Ja nu a ri |
| rais | gari | radi | Januari |

Tamka sauti.

r

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| r u | j i | w a | g a |
| ru | ji | wa | ga |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| li li simama | tu ka sikia |
| lilisimama | tukasikia |
| a ki malizia | wa ka torokea |
| akimalizia | wakatorokea |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| wakati uliopo | wakati ujao |
|---|---|
| rais anakuja kijijini | rais atakuja kijijini. |
| rais anasimama barabarani | rais atasimama barabarani. |
| rais anawasihi watu | rais atawasihi watu. |
| rais anafurahi sana | rais atafurahi sana. |





Mtu aliyevalia suti amesimama juu ya gari lililofunguliwa dau. Amezingirwa na askari na anahutubia umati wa watu sokoni akitumia kipaza sauti.

### Ziara ya Rais

Ilikuwa siku ya Jumatatu mwezi wa Januari Rais alipotutembelea. Rais wetu alikuja kijijini kukutana na raia.
Gari lake lilisimama barabarani.
Rais akasema, "Nawasihi mkae kwa amani na watu wote."
Siku hiyo, wanakijiji walikuwa na furaha sana.
Akimalizia ziara yake, mara tukasikia radi.
Watu wakatorokea madukani.
Kesho yake barabara ilikuwa imejaa maji.



**▲ Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **r**. Tamka sauti ya herufi **/r/**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**⬬ Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **ru**. Sema kila sauti **/r/ /u/** kisha uunganishe na kusema silabi **ru**. **[U]** Endelea na silabi **ju, wu** na **gu.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**★ Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **li li simama** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **lilisimama** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **a ki malizia (akimalizia), tu ka sikia (tukasikia), wa ka torokea (wakatorokea).** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**◆ Sarufi**

[N/T] Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Eleza wanafunzi jinsi ya kutumia nyakati kueleza vitendo.

| Wakati uliopo | Wakati ujao |
|---|---|
| Rais **ana**kuja kijijni<br>Rais **ana**simama barabarani<br>Rais **ana**wasihi watu<br>Rais **ana**furahi sana | Rais at**a**kuja kijijni.<br>Rais at**a**simama barabarani.<br>Rais at**a**wasihi watu.<br>Rais at**a**furahi sana. |

**🕮 Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **ziara, radi** na **amani**.

**🕮 Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Ziara ya Rais"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

Mwalimu achague wanafunzi wawili wasimulie hadithi waliyoisoma.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Kwa nini wanakijiji walikuwa na furaha?*** *(kwa sababu Rais aliwatembelea/kwa sababu Rais alikuja kijijini).*
2. ***Kwa nini watu walitorokea madukani?*** *(ili wajikinge na mvua n.k.)*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Kisha wanafunzi wayaandike katika wakati ujao.

| | | |
|---|---|---|
| anasimama | - | atasimama |
| anamaliza | - | ____________ |
| anatoroka | - | ____________ |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yaliyochanganywa: **dira, isra, riga, arazi, barabarani**. Waagize wanafunzi wayaandike maneno halisi. Baadaye wawasomee wenzao. **Mfano:** dira - radi

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 10: Siku ya 5 **Siku za Wiki**

Tamka sauti.

j J r R

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: I ju maa Ijumaa.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| tu | no | ji | ki | i | do |
| maa | i | ju | n | ma | ta |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| wakati uliopita | wakati ujao |
|---|---|
| zakayo **ali**lala kitini | zakayo **ata**lala kitini. |
| zakayo **ali**sugua jino | zakayo **ata**sugua jino. |
| mama **ali**muona zakayo | mama **ata**muona zakayo. |
| mama **ali**elekea dukani | mama **ata**elekea dukani. |

Kijana anawasha jiko kama amepiga magoti huku akishika shavu. Anaonekana anahisi uchungu kwenye shavu lake.

Jino la Zakayo

Jumamosi asubuhi, Zakayo alilala kitini.
Jino lake lilikuwa linamuuma.
Alilala huku akilisugua jino kwa kidole.
Mara alijikaza kuelekea jikoni.
Huko aliokota jivu na kuliweka kwenye jino.
Mama yake alimuona ameketi jikoni akilia.
Mama alielekea dukani. Akanunua dawa na kumletea.
Akanywa dawa. Jino likatulia.

50

■ **Majina ya herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(j)**. Tamka sauti ya herufi **/j/**. **[U]** Endelea na herufi **(r)**.

★ **Silabi: Kuandika**

**[N]** Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **ji** na **we** kuandika neno **jiwe**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

● **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome sentensi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U. Soma sentensi, soma pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| Wakati uliopita | Wakati ujao |
|---|---|
| Zakayo **ali**lala kitini | Zakayo **ata**lala kitini. |
| Zakayo **ali**sugua jino | Zakayo **ata**sugua jino. |
| Mama **ali**muona Zakayo | Mama **ata**muona Zakayo. |
| Mama **ali**elekea dukani | Mama **ata**elekea dukani. |

📖 **Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **jivu, akilisugua** na **alijikaza**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

📖 **Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Jino la Zakayo"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

◈ **Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Taja jina la mtu aliyelala kitini*** *(Jina lake ni Zakayo)*
2. ***Zakayo alilala kitini siku gani?*** *(Jumamosi/Jumamosi asubuhi)*
3. ***Kwa nini Zakayo alilia*** *(alikuwa anahisi maumivu/jino lake lilikuwa linauma)*
4. ***Eleza vile ulivyohisi wakati ulikuwa mgonjwa?*** *(maumivu/ kulia n.k.)*

📖 **Hadithi ya mwalimu**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. *(Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

**MIEZI YA MWAKA**

Mwezi wa Januari,mwaka twausherehekea
Februari mwezi wa pili, joto jingi na jasho
**Miezi kumi na miwili, ndipo mwaka hukamilika**

Mwezi wa tatu ni Machi, mvua huanza nyesha.
Mwezi wa nne Aprili, ni likizo twafurahia
**Miezi kumi na miwili, ndipo mwaka hukamilika**

Mwezi wa tano ni Mei, ndo mwezi wa leba dei.
Mwezi wa sita ni Juni, ni mwezi wa madaraka
**Miezi kumi na miwili, ndipo mwaka hukamilika. (*Mwezi wa tano unaitwaje?*)**

Julai, mwezi wa saba, baridi kama barafu
Agosti mwezi wa nane, ndio mwezi wa mavuno
**Miezi kumi na miwili, ndipo mwaka hukamilika. (*Mwezi wa Julai una nini?*)**

Wa tisa ni Septemba, muhula wa tatu kuanza
Mwezi kumi Oktoba, twakumbuka mashujaa
**Miezi kumi na miwili, ndipo mwaka hukamilika**

Novemba kumi na moja, mitihani hukaribia
Desemba kumi na mbili, sherehe za Krismasi
**Miezi kumi na miwili, ndipo mwaka hukamilika. (*Kati ya Miezi hii, ni mwezi gani uupendao?*)**

✍ **Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **kijijini, Ijumaa, jitu, Rais, radi, ziara.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wanafunzi waendelee kuunda maneno zaidi wakitumia silabi zilizo ukurasa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 11: Siku ya 1

## Mazingira

Tamka sauti.

m a u k

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: ma ma - mama.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| kaa | ma | mu | ka | m |
| maa | ku | a | kuu | u |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wakati ujao |
|---|---|
| kaka **aka**amua kuamka | kaka **waka**amua kuamka. |
| kaka **aka**muuma kaa | kaka **wakawa**uma kaa. |

Mvulana ameketi kwa kiti uani. Kaa amemuuma mguu akashtuka.

### Kaka na Kaa

Kuku akaamua kuamka.
Paka akaamua kuamka.
Mama akaamua kuamka.
Kaka akaamua kuamka.
Kaka akaamua kukaa na kaa.
Kaa akamuuma kaka.
Paka akamuuma kaa.

51

**Vidokezo vya Mwalimu**
Je, unakumbuka mpangilio wa "Ninafanya", "Tunafanya", "Unafanya", wakati wa kufunza somo la kusoma?

### ★ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(m)**. Tamka sauti ya herufi **/m/**. **[U]** Endelea na herufi **a, u** na **k.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### ★ Silabi: Kuandika

**[N]** Soma silabi zote zilizo ukurasa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **ma** na **ma** kuandika neno **mama**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

N/T/U. Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Kaka **aka**amua kuamka | - | Kaka **waka**amua kuamka. |
| Kaka **aka**muuma kaa | - | Kaka **waka**wauma kaa. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya neno **akaamua** na **akamuuma**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Kaka na Kaa"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

- ***i.*** ***Kuku aliamua kufanya nini?*** *(aliamua kuamka)*
- ***ii.*** ***Kaka aliamua kufanya nini?*** *(kuamka, kukaa na kaa)*
- ***iii.*** ***Paka alimuuma nani?*** *(kaa)*

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya kwa sauti mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika**: paka, mama, kukaa, matatu, kuku.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Waambie wanafunzi waandike maneno matano zaidi kutokana na silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** na wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 11: Siku ya 2 **Mazingira**

Tamka sauti.

t i n o

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: ta mu - tamu

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ni | m | na | ta | mi |
| mu | ti | i | nu | ma |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| wakati uliopo | wakati ujao |
|---|---|
| tai anakaa | tai atakaa. |
| kima anakataa | kima atakataa. |
| tai anamtuma | tai atamtuma. |
| konokono anakataa | konokono atakataa. |

Tai na konokono wakiwa juu ya mti. Tai anamwangalia konokono. Konokono anamwelekea tai.

### Tai na Kima

Tai anakaa na kima mtini.
Tai anataka kununua asali na ini nono.
Tai akamtuma kima.
Kima akakataa.
Tai akaona konokono mtini.
Akamuita na kumtuma.
Konokono akakataa.
Tai akanuna.

52

**Vidokezo vya Mwalimu**
Iwapo kuna wanafunzi wasioweza kujibu maswali ya ufahamu, waelekeze kwenye mbinu zitakazowapatia jibu kwa urahisi. Usiwapatie jibu papo hapo.

### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(t)**. Tamka sauti ya herufi **/t/.** **[U]** Endelea kwa herufi **i, n, o.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### ★ Silabi

**[N]** Soma silabi zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **ta** na **mu** kuandika neno **tamu**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma sentensi zote.

| Wakati uliopo | Wakati ujao |
|---|---|
| Tai ana**na**kaa | Tai a**ta**kaa |
| Kima a**na**kataa | Kima a**ta**kataa |
| Tai a**na**mtuma | Tai a**ta**mtuma |
| Konokono a**na**kataa | Konokono a**ta**kataa |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya neno **konokono** na **nuna**. Eleza wanafunzi maana ya neno hilo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Tai na Kima"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

- ***i. Tai alikaa na kima wapi?*** *(alikaa na kima mtini).*
- ***ii. Tai alitaka kununua nini?*** *(biskuti na ini nono).*
- ***iii. Kwa nini Tai alinuna?*** *(wote aliowatuma walikataa).*

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiandika: **anakataa, anataka, anamuona, ananunua, anatamani.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Waambie wanafunzi waandike maneno matano zaidi kutokana na silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** na wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 11: Siku ya 3 na 4 **Sokoni**

Tamka sauti.

w e l h

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: mi wi li - **miwili**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ki | a | wi | li | wa |
| ka | mi | tu | ha | wi |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **wakati uliopita** | **wakati ujao** |
|---|---|
| katile a**li**wahukumu | katile a**ta**wahukumu. |
| barasa a**li**lia | barasa a**ta**lia. |
| wakili a**li**lalamika | wakili a**ta**lalamika. |
| hawa a**li**lewa | hawa a**ta**lewa. |

Ndani ya koti kuna hakimu, washtakiwa wawili na makarani wawili.

**Wamiti na Hawa**

Wamiti na Hawa walienda sokoni. Walinunua mboga, nyanya na vitunguu.
Wamiti aliona viatu vizuri vya bei ghali.
Alivitamani lakini hakuwa na pesa. Wamiti alivichukua viatu akampa Hawa.
Walishikwa na kupelekwa katika mahakama. Wote walihukumiwa miaka miwili na hakimu. Wamiti na Hawa waliomba msamaha.

53

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kumbuka kufanya utabiri na wanafunzi siku ya kwanza, ya tatu na ya tano pekee. Hakuna utabiri siku ya 2 na ya 4. Wanafunzi watarejelea msamiati.

■ **Majina ya herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(w)**. Tamka sauti ya herufi **/w/**. **[U]** Endelea kwa herufi **e, l, h**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

★ **Silabi**

**[N]** Soma silabi zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **mi, wi** na **li** kuandika neno **miwili**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

● **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma sentensi zote:

| **Wakati uliopita -li** | **Wakati ujao -ta** |
|---|---|
| Katile a**li**wahukumu | Katile a**ta**wahukumu |
| Wamiti a**li**lia | Wamiti a**ta**lia |
| Wakili a**li**lalamika | Wakili a**ta**lalamika |
| Hawa a**li**lewa | Hawa a**ta**lewa |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **hakimu, mahakama** na **walihukumiwa/hukumiwa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Wamiti na Hawa"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

**Maswali:**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

*i.* ***Wamiti na Hawa walienda wapi?*** *(sokoni)*
*ii.* ***Kwa nini Wamiti alivichukua viatu?*** *(alivitamani, hakuwa na pesa)*
*iii.* ***Ni nani aliwahukumu Wamiti na Hawa?*** *(hakimu)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili kwa sauti huku wanafunzi wakiandika: **mahakama, hakimu, nawasihi, wanakijiji, radi.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Waambie wanafunzi waandike maneno matano zaidi kutokana na silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** na wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 11: Siku ya 4 **Nyumbani**

Tamka sauti.

s b y z

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: sa ba - **saba**.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| wa | mo | sti | sa | mi | zi |
| bi | to | ya | ba | ma | s |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| wakati uliopo | wakati ujao |
|---|---|
| ni**na**sikia mayowe | ni**ta**sikia mayowe. |
| ni**na**tazama moto | ni**ta**tazama moto. |
| ni**na**uzima moto | ni**ta**uzima moto. |
| ni**na**elekea sebuleni | ni**ta**elekea sebuleni. |

Gari kubwa lenye rangi nyekundu la kuzima moto. Gari lina kimulimuli na king'ora.

**Waya wawaka moto**

Tulisikia **mayowe** tukiwa sebuleni.
"Tokeni!" Baba akasema.
Sote tukatoka.
Kutazama tukaona moto ukiwaka sana.
**Waya** wa stima jikoni mwa jirani wetu uliwaka moto.
Sote tukawa na wasiwasi sana.
Wazimamoto wakafika.
Wakauzima moto uliokuwa **umeenea**.
Mioyo yetu ikatulia, tukaelekea sebuleni tena.

54

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kumbuka hatua tatu muhimu za kufunza. Mtindo huu ni: Ninafanya, Tunafanya na Unafanya.

### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(s)**. Tamka sauti ya herufi **/s/**. **[U]** Endelea na herufi **b, y, z**.

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### ★ Silabi

**[N]** Soma silabi zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **sa,** na **ba** kuandika neno **saba**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma sentensi zote:

| Wakati uliopo -na | Wakati ujao -ta |
|---|---|
| Ni**na**sikia mayowe | Ni**ta**skia mayowe |
| Ni**na**tazama moto | Ni**ta**tazama moto |
| Ni**na**uzima moto | Ni**ta**uzima moto |
| Ni**na**elekea sebuleni | Ni**ta**elekea sebuleni |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **waya, mayowe** na **umeenea/enea**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Waya wawaka moto**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### ◈ Maswali:

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

*i.* ***Walisikia mayowe wakiwa wapi?*** *(sebuleni)*

*ii.* ***Waya wa stima ulikuwa ikifanya nini?*** *(uliwaka moto)*

*iii.* ***Ni nani aliuzima moto?*** *(wazima moto)*

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili kwa sauti huku wanafunzi wakiandika: **waya, wawaka, mayowe.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Waambie wanafunzi waandike maneno matano zaidi kutokana na silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** na wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 11: Siku ya 5

Wiki ya 11: Siku ya 5 **Anga**

Tamka sauti.

g d j r

Tumia silabi kuunda maneno. Kwa mfano: Ju ni - Juni

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ni | ma | ju | se | mba |
| go | a | sti | de | mbe |

Sarufi: Soma maneno haya.

| wakati uliopo | wakati uliopita |
|---|---|
| **wana**soma | **wali**soma |
| **wana**furahia | **wali**furahia |
| **wana**rudi | **wali**rudi |
| **wana**saidia | **wali**saidia |

1. Jua limewaka sana.
2. Upepo mkali unavuma na miti inainama.
3. Mawingu mazito na mvua inanyesha.
4. Mawingu mazito hakunyeshi.

### Hali ya Hewa

Januari na Februari kuna joto na jua kali. Watoto wanasoma kwa bidii sana. Aprili ni likizo. Baada ya likizo watoto husoma miezi ya Mei, Juni hadi Julai. Agosti huwa likizo tena. Watoto hufurahia kusaidia wazazi. Wao hurudi kusoma kwa miezi mitatu hadi likizo ya sikukuu ya Disemba.

55

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kumbuka kuwa kusoma hadithi kuna vipengele vitatu. Kusoma maneno vizuri, kwa mwendo mzuri na kuonyesha hisia na kuzingatia alama za uafikishaji.

■ **Majina ya herufi na sauti:**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(g)**. Tamka sauti ya herufi **/g/**. **[U]** Endelea na herufi **d, j, r**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

★ **Silabi**

**[N]** Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **Ju,** na **ni** kuandika neno **juni**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

● **Sarufi**

[N/T] Eleza wanafunzi maneno katika ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Yasome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| Wakati uliopo | Wakati uliopita |
|---|---|
| **wana**soma | **wali**soma |
| **wana**furahia | **wali**furahia |
| **wana**rudi | **wali**rudi |
| **wana**saidia | **wali**saidia |

🕮 **Kabla ya kusoma::**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **joto, sikukuu** na **likizo**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

🕮 **Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Hali ya hewa"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

◈ **Maswali:**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

- ***i.*** ***Kuna joto miezi gani?*** *(miezi ya Januari na Februari)*
- ***ii.*** ***Baada ya likizo wanafunzi husoma miezi gani?*** *(mwezi wa Mei, Juni na Julai)*
- ***iii.*** ***Sikukuu iliyotajwa huwa mwezi gani?*** *(mwezi wa Desemba).*

✍ **Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili kwa sauti huku wanafunzi wakiandika: **kuzimia, madukani, likasema, alijawa, akalia.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Waambie wanafunzi waandike maneno matano zaidi kutokana na silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** na wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 12: Siku ya 1

Wiki ya 12: Siku ya 1 na 2 — Tarakimu

Tamka sauti.

**p** **g** **d**

Soma sauti za herufi na silabi.

| p e | p i | p u | p o |
|---|---|---|---|
| **pe** | **pi** | **pu** | **po** |

Soma silabi na maneno.

| pa sa ka | Pa te | Pe te ro | pa pa |
|---|---|---|---|
| **pasaka** | **Pate** | **Petero** | **papa** |

Tamka sauti.

**p**

Soma silabi.

| e | a |
|---|---|
| **we** | **wa** |
| **pwe** | **pwa** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li ona | wa ki tumia |
|---|---|
| **waliona** | **wakitumia** |
| wa li tumia | i li po wadia |
| **walitumia** | **ilipowadia** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| huyu ni punda mmoja | hawa ni punda wawili. |
| huyu ni papa mmoja | hawa ni papa watatu. |
| huyu ni pweza mmoja | hawa ni pweza wanne. |
| huyu ni samaki mmoja | hawa ni samaki watano. |

56

Wiki ya 12: Siku ya 1 na 2 — Tarakimu

Mwanamume amepanda juu ya punda. Wanatembelea kando ya bahari. Baharini kuna meli. Kando kuna miti ya minazi.

**Sikukuu ya Pasaka**

Sikukuu ya pasaka ilipowadia, Petero na wazazi wake walitoka Pate na kuelekea Faza. Walitumia magari mawili hadi Mpeketoni. Wakatumia dau kuvukia Bahari Hindi hadi kisiwani Faza. Kule kisiwani, waliona watu sita wakitumia punda kubebea mizigo na watu. Pia waliona papa na pweza. Papa walikuwa ishirini na pweza walikuwa kumi na wanne.

57

**Ufahamu wa fonimu:**

N/T/U: Tamka sauti **/p/**. Taja maneno **(paka, kapu)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea na maneno: **kikapu, papa, penseli, pia** na **pipa.**

**Jina la herufi na sauti:**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **p.** Tamka sauti **/p/**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**Kusoma silabi:**

N/T/U: Andika silabi **pe**. Sema kila sauti **/p//e/** kisha uunganishe na kusema silabi **pe**. **[U]** Endelea na silabi **pi, pu** na **po**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U: Tamka silabi **pa sa ka** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **pasaka**. **[U]** Endelea na maneno: **Pate, Petero, papa**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **pasaka, pweza** na **kisiwani**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Sikukuu ya Pasaka"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

**Maswali:**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Ni vyombo gani ambavyo Petero na wazazi wake walitumia kwenda Faza?*** *(gari, dau, punda)*
2. ***Taja aina ya wanyama wa baharini waliowaona walipofika kisiwani Faza.*** *(papa, pweza)*

**Kuandika**

Waagize wanafunzi waandike herufi **p** mara tatu.

p p p p p

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **pasaka, punda, wakapanda, papa, pweza**. Wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 12: Siku ya 1 na 2 — Tarakimu

Tamka sauti.

p g d

Soma sauti za herufi na silabi.

| p e | p i | p u | p o |
|---|---|---|---|
| pe | pi | pu | po |

Soma silabi na maneno.

| pa sa ka | Pa te | Pe te ro | pa pa |
|---|---|---|---|
| pasaka | Pate | Petero | papa |

Tamka sauti.

p

Soma silabi.

| e | a |
|---|---|
| we | wa |
| pwe | pwa |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li ona | wa ki tumia |
|---|---|
| waliona | wakitumia |
| wa li tumia | i li po wadia |
| walitumia | ilipowadia |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| huyu ni punda mmoja | hawa ni punda wawili. |
| huyu ni papa mmoja | hawa ni papa watatu. |
| huyu ni pweza mmoja | hawa ni pweza wanne. |
| huyu ni samaki mmoja | hawa ni samaki watano. |

56

Wiki ya 12: Siku ya 1 na 2 — Tarakimu

Mwanamume amepanda juu ya punda. Wanatembelea kando ya bahari. Baharini kuna meli. Kando kuna miti ya minazi.

Sikukuu ya Pasaka

Sikukuu ya pasaka ilipowadia, Petero na wazazi wake walitoka Pate na kuelekea Faza. Walitumia magari mawili hadi Mpeketoni. Wakatumia dau kuvukia Bahari Hindi hadi kisiwani Faza. Kule kisiwani, waliona watu sita wakitumia punda kubebea mizigo na watu. Pia waliona papa na pweza. Papa walikuwa ishirini na pweza walikuwa kumi na wanne.

57

▲ **Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **p**. Tamka sauti ya herufi **/p/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

⬬ **Kusoma silabi**

N/T/U: Andika herufi **/e/**. Soma sauti **/e/.** Ongeza herufi **w** kisha uunganishe sauti na kusema silabi **we**. Ongeza herufi **p** kisha uunganishe na kusema silabi **pwe**. **[U]** Endelea na silabi: **a, wa, pwa.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa li ona** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **waliona** kwa upesi. Endelea na maneno: **wa li tumia (walitumia), wa ki tumia (wakitumia), i li po wadia (ilipowadia).** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

◆ **Sarufi**

[N/T] Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma sentensi kisha uzisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **Huyu** ni punda **mmoja** | - | **Hawa** ni punda **wawili**. |
| **Huyu** ni papa **mmoja** | - | **Hawa** ni papa **watatu**. |
| **Huyu** ni pweza **mmoja** | - | **Hawa** ni pweza **wanne**. |
| **Huyu** ni samaki **mmoja** | - | **Hawa** ni samaki **watano**. |

📖 **Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **pasaka, pweza** na **kisiwani**.

📖 **Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Sikukuu ya Pasaka"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

◈ **Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Ni njia gani za usafiri ambazo unazijua?*** *(ndege/eropleni, meli, garimoshi n.k)*
2. ***Taja aina ya samaki unayojua.*** *(tilapia, kamongo n.k)*

✍ **Kuandika: Imla**

Soma maneno haya. Wanafunzi wayaandike.

**i.** **punda** **ii.** **papa**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli zenye maneno yafuatayo.

**Kazi ya ziada**

Andika maneno haya ubaoni.

**punda mmoja**
**punda wawili**
**pweza watatu**
**samaki wanne**

Waagize wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao:

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 12: Siku ya 3 na 4 — Tarakimu

Tamka sauti.

f p

Soma sauti za herufi na silabi.

f i — f e — f o — f a

fi — fe — fo — fa

Soma silabi na maneno.

a li fa u lu — fa ra si — pi ki pi ki — fo le ni

alifaulu — farasi — pikipiki — foleni

Tamka sauti.

f

Soma sauti za herufi na silabi.

p e — f e — k e — w e

pe — fe — ke — we

Soma sehemu za neno na neno lote.

ki li furahi — wa m salimie

kilifurahi — wamsalimie

wa li furahi — wa li safiri

walifurahi — walisafiri

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| hii ni pikipiki moja | hizi ni pikipiki mbili. |
| hii ni matatu moja | hizi ni matatu tatu. |
| hii ni baiskeli moja | hizi ni baiskeli nne. |
| hii ni meli moja | hizi ni meli tano. |

58

Wiki ya 12: Siku ya 3 na 4 — Tarakimu

Gari liko barabarani. Kijana anaendesha baiskeli barabarani sehemu iliyotengewa baisikeli. Mzee akiwa juu ya punda wanapitia kando ya barabara huku akishikilia kamba na fimbo.

Matokeo ya Apese

Apese alifaulu mtihani wa darasa la nane. Alipata alama mia nne hamsini.
Kijiji kizima kilifurahi sana.
Wanakijiji walifurahi na kupiga vigelegele.
Walisafiri kwa kutumia farasi wanne, mabasi mawili na pikipiki kumi na mbili. Wengine walisafiri kwa kutumia matatu tano na baiskeli ishirini na tano.
Wakapiga foleni ili wamsalimie Apese.
Wazazi wake walifurahi kwa matokeo ya mtoto wao.

59

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/f/.** Taja maneno **(furaha** na **ufuta)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea kwa maneno: **fimbo, ufuta, fisi, mlafi, funga.**

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **f**. Tamka sauti **/f/**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **fi**. Sema kila sauti /f//i/ kisha uunganishe na kusema silabi **fi**. **[U]** Endelea na silabi**: fe, fo, fa.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **a li fa u lu** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **alifaulu**. **[U]** Endelea na maneno **farasi, pikipiki** na **foleni.** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mtihani, vigelegele** na **foleni**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Matokeo ya Apese"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Kwa nini wanakijiji walisherehekea?*** *(kwa sababu Apese alifaulu mtihani wa darasa la nane)*
2. ***Je, watu walitumia nini kusafiri?*** *(farasi wanne, mabasi mawili, pikipiki kumi na mbili, matatu tano na basikeli ishirini na tano)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **f** mara tatu.

f f f f f

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo: **Apese alifaulu; wanakijiji walifurahi; walipiga foleni; walitumia farasi**. Waagize wanafunzi wazinakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 12: Siku ya 3 na 4 — Tarakimu

Tamka sauti.

f p

Soma sauti za herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| f i | f e | f o | f a |
| fi | fe | fo | fa |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a li fa u lu | fa ra si | pi ki pi ki | fo le ni |
| alifaulu | farasi | pikipiki | foleni |

Tamka sauti.

f

Soma sauti za herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| p e | f e | k e | w e |
| pe | fe | ke | we |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ki li furahi | wa m salimie |
| kilifurahi | wamsalimie |
| wa li furahi | wa li safiri |
| walifurahi | walisafiri |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| hii ni pikipiki moja | hizi ni pikipiki mbili. |
| hii ni matatu moja | hizi ni matatu tatu. |
| hii ni baiskeli moja | hizi ni baiskeli nne. |
| hii ni meli moja | hizi ni meli tano. |

58

Wiki ya 12: Siku ya 3 na 4 — Tarakimu

Gari liko barabarani. Kijana anaendesha baiskeli barabarani sehemu iliyotengewa baisikeli. Mzee akiwa juu ya punda wanapitia kando ya barabara huku akishikilia kamba na fimbo.

Matokeo ya Apese

Apese alifaulu mtihani wa darasa la nane. Alipata alama mia nne hamsini.
Kijiji kizima kilifurahi sana.
Wanakijiji walifurahi na kupiga vigelegele.
Walisafiri kwa kutumia farasi wanne, mabasi mawili na pikipiki kumi na mbili. Wengine walisafiri kwa kutumia matatu tano na baiskeli ishirini na tano.
Wakapiga foleni ili wamsalimie Apese.
Wazazi wake walifurahi kwa matokeo ya mtoto wao.

59

**▲ Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **f**. Tamka sauti ya herufi **/f/**.

**⬬ Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **fe**. Sema sauti **/f//e/** kisha uunganishe na kusema silabi **fe**. **[U]** Endelea na silabi: **pe, ke** na **we**. Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**★ Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **ki li furahi** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **kilifurahi** kwa upesi. Endelea kwa maneno: **[U]** Endelea na maneno: **wa li furahi (walifurahi), wa m salimie (wamsalimie), wa li safiri (walisafiri).** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kwenye vitabu vyao.

**◆ Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma sentensi kisha uzisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Hii ni pikipiki **moja** | - | Hizi ni pikipiki **mbili**. |
| Hii ni matatu **moja** | - | Hizi ni matatu **tatu**. |
| Hii ni baiskeli **moja** | - | Hizi ni baiskeli **nne**. |
| Hii ni meli **moja** | - | Hizi ni meli **tano**. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **mtihani, vigelegele** na **foleni**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Matokeo ya Apese"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Eleza jinsi watu wa kwenu husherehekea?*** *(huimba, hucheza ngoma, hula vyakula mbalimbali)*
2. ***Ni vyombo vipi vingine vya usafiri ambavyo unavijua au umewahi kuvitumia?*** *(meli, mikokoteni, gari la moshi, ndege n.k)*

**Kuandika**

Wanafunzi wapewe kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Waagize wanafunzi wayaandike katika wingi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| kijiji | vijiji |
| kisiwa | ____________ |
| kijiti | ____________ |
| kikapu | ____________ |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yaliyochanganywa: **lenifo, pipikiki, tatuma, siba**. Wanafunzi wayaandike maneno halisi. Kisha wawasomee wenzao. **Mfano:** risafi - safiri

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 12: Siku ya 5 Tarakimu

Tamka sauti.

p f

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: pa sa ka pasaka.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ni | pa | fa | si | ra | fi |
| ba | ha | na | ka | sa | ri |

Sarufi: Soma maneno haya.

| neno | kinyume |
|---|---|
| enda | rudi |
| mchana | usiku |
| baba | mama |
| dada | kaka |

Mama na msichana wanapanda eropleni.

Usafiri

Kila mtu hutamani kusafiri kwa njia za kifahari. Njia hizi ni kama eropleni, magari na meli. Nikiwa na safari fupi, mimi husafiri kwa miguu mara mbili kwa wiki. Kusafiri kwa miguu kuna faida kwenye mwili wa binadamu. Zaidi ya hayo, msafiri hatumii hela zozote kusafiri. Je, wewe husafiri kwa miguu mara ngapi kwa wiki?

60

■ **Majina ya herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(p)**. Tamka sauti ya herufi **/p/**. **[U]** Endelea kwa herufi ndogo na kubwa **(f)**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

★ **Silabi**

**[N]** Soma silabi zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **pa, sa** na **ka** kuandika neno **pasaka**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

● **Sarufi**

Wape wanafunzi nafasi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma maneno haya kisha eleza wanafunzi maana ya kinyume:

| Neno | | Kinyume |
|---|---|---|
| enda | - | rudi |
| mchana | - | usiku |
| baba | - | mama |
| dada | - | kaka |

📖 **Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kifahari, ndege** na **meli**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

📖 **Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Usafiri"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

◈ **Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Taja njia moja ya usafiri wa kifahari*** *(ndege/eropleni)*
2. ***Ni njia gani bora zaidi ya kusafiri kwa safari fupi?*** *(miguu)*
3. ***Eleza umuhimu wa kusafiri kwa miguu.*** *(kuna faida kwa mwili/msafiri ha tumii pesa zozote)*
4. ***Wewe hupenda kusafiri kwa njia gani unapomtembelea babu au bibi yako?*** *(wanafunzi wataje njia mbalimbali za usafiri wanazozitumia)*
5. ***Je, wewe husafiri kwa miguu mara ngapi kwa wiki?***

📖 **Hadithi ya mwalimu:**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. *(Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

**Chura mpenda maua**

Paliishi Chura mmoja aliyependa maua. Siku moja aliamua kupanda maua shambani mwake. Alienda kwa jirani yake kuomba mbegu za maua. (***Chura alienda kwa jirani kuomba nini?)***

Aliporudi nyumbani, alitayarisha shamba lake na kupanda zile mbegu. Mbegu zilipochelewa kumea, Chura akapiga magoti. Alipaaza sauti na kusema, “Mbegu, anza kumea.” (***Je, unafikiri mbegu zilimea kwa kuambiwa zimee?***)

Chura aliinuka na kuangalia chini tena. Mbegu hazikumea. Chura alisema kwa sauti kubwa, “Mbegu, anza kumea.” Bado mbegu hazikumea. Kesho yake mchana kutwa chura aliimbia mbegu zake nyimbo.

Kesho kutwa alikariria mbegu zake mashairi. Mtondo alichezea mbegu zake muziki. Lakini hazikumea. Mtondogoo, Chura alikasirika na alizimwagia maji. Ajabu mbegu zake zilimea vizuri sana. Zikatoa maua ya rangi nyingi za kupendeza. Kweli mbegu huhitaji maji si nyimbo wala mashairi. (***Kutokana na hadithi hii, inaonekana kuwa mbegu huhitaji nini ndipo zimee?)***

✍ **Kuandika - Imla**

Tamka maneno mara mbili, kiisha wanafunzi wayaandike maneno hayo kwa madaftari yao. **punda, pweza, farasi, pikipiki, foleni.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Eleza wanafunzi waendelee kuunda maneno zaidi wakitumia silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 13: Siku ya 1

Wiki ya 13: Siku ya 1 na 2 **Mazingira**

Tamka sauti.

v p f

Soma sauti ya herufi na silabi.

v e v i v u v a

**ve** **vi** **vu** **va**

Soma s labi na maneno.

vi ji to wa vu vi vi bo ko ma de vu

**vijito** **wavuvi** **viboko** **madevu**

Tamka sauti.

v

Tamka sauti ya herufi na silabi.

f o v o f e v e

**fo** **vo** **fe** **ve**

Soma sehemu za neno na neno lote.

ya li malizika a ka wa ita

**yalimalizika** **akawaita**

vi ka haribiwa wa li po kata

**vikaharibiwa** **walipokata**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| hiki ni kijito | hivi ni vijito. |
| hiki ni kilima | hivi ni vilima. |
| hiki ni kiboko | hivi ni viboko. |
| hiki ni kiota | hivi ni viota. |

61

Wiki ya 13: Siku ya 1 na 2 **Mazingira**

Mto umekauka. Wanyama wa majini wamekufa. Ndege wakubwa wanaila mizoga ya wanyama hao.

**Athari za ukataji wa miti**

Kijijini Taita kulikuwa na vijito na vilima.
Vijana wa huko walikuwa wavuvi wa samaki.
Watu walipokata miti, maji yalimalizika vijitoni.
Viboko na samaki wakafa.
Viota vikaharibiwa.
Mzee Madevu akawaita watu na kusema, "Tunahitaji kupanda miti, ili tupate maji visimani."

62

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/v/**. Taja maneno **(vibaya** na **povu)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea kwa maneno: ***vipi, nyavu, kiwavi, vitu, viatu, viti*** na ***fisi.***

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **v**. Tamka sauti **/v/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **ve**. Sema kila sauti **/v/ /e/** kisha uunganishe na kusema silabi **ve**. **[U]** Endelea na silabi **vi, vu** na **va**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **vi ji** na **to** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **vijito**. **[U]** Endelea na maneno: **wavuvi, viboko** na **Madevu.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **wavuvi, viota** na **viboko**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Athari za ukataji wa miti"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

N/T/U: Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Kazi ya vijana wa Taita ilikuwa gani?*** *(walikuwa wavuvi wa samaki)*
2. **Eleza kilichofanyika baada ya watu kukata miti.** *(maji yalimalizika vijitoni/viboko na samaki wakafa/viota viliharibiwa)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **v** mara tatu.

v v v v v

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **vijito, vilima, wavuvi, viboko, viota, visima**. Waagize wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ________________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 13: Siku ya 2

Wiki ya 13: Siku ya 1 na 2 **Mazingira**

Tamka sauti.

v p f

Soma sauti ya herufi na silabi.

| v e | v i | v u | v a |
|---|---|---|---|
| **ve** | **vi** | **vu** | **va** |

Soma s labi na maneno.

| vi ji to | wa vu vi | vi bo ko | ma de vu |
|---|---|---|---|
| **vijito** | **wavuvi** | **viboko** | **madevu** |

Tamka sauti.

v

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| f o | v o | f e | v e |
|---|---|---|---|
| **fo** | **vo** | **fe** | **ve** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| ya li malizika | a ka wa ita |
|---|---|
| **yalimalizika** | **akawaita** |
| vi ka haribiwa | wa li po kata |
| **vikaharibiwa** | **walipokata** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| hiki ni **ki**jito | hivi ni **vi**jito. |
| hiki ni **ki**lima | hivi ni **vi**lima. |
| hiki ni **ki**boko | hivi ni **vi**boko. |
| hiki ni **ki**ota | hivi ni **vi**ota. |

61

Wiki ya 13: Siku ya 1 na 2 **Mazingira**

Mto umekauka. Wanyama wa majini wamekufa. Ndege wakubwa wanaila mizoga ya wanyama hao.

**Athari za ukataji wa miti**

Kijijini Taita kulikuwa na vijito na vilima.
Vijana wa huko walikuwa wavuvi wa samaki.
Watu walipokata miti, maji yalimalizika vijitoni.
Viboko na samaki wakafa.
Viota vikaharibiwa.
Mzee Madevu akawaita watu na kusema, "Tunahitaji kupanda miti, ili tupate maji visimani."

62

### ▲ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **v**. Tamka sauti ya herufi **/v/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ⬬ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **fo**. Sema kila sauti **/f/ /o/** kisha uunganishe na kusema silabi **fo**. **[U]** Endelea kwa silabi: **vo, fe** na **ve.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **ya li malizika** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **yalimalizika**. **[U]** Endelea na maneno: **vi ka haribiwa (vikaharibiwa), a ka wa ita (akawaita), wa li po kata (walipokata)**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

[N/T/U] Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma sentensi pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Hiki ni **ki**jito | Hivi ni **vi**jito. |
| Hiki ni **ki**lima | Hivi ni **vi**lima. |
| Hiki ni **ki**boko | Hivi ni **vi**boko. |
| Hiki ni **ki**ota | Hivi ni **vi**ota. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **wavuvi, viota** na **viboko**.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Athari za ukataji wa miti"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### ⟐ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Je, watu walikata miti kwa nini?*** *(kutengeneza kuni/ makaa, kujengea nyumba)*
2. ***Je unafikiri watu walifanya vile Mzee Madevu aliwaambia? Tetea jibu lako.*** *(watoto walijibu na kueleza jibu lao)*

### ✍ Kuandika: Imla

Soma maneno **vilima**, **miti**, **samaki**. Wanafunzi wayaandike kisha wajadiliane kuhusu vilima, miti, samaki.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Waagize wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao:

**kijito** - **vijito**
**kilima** - **vilima**

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

Wiki ya 13: Siku ya 3 na 4 **Mazingira**

Tamka sauti.

**sh** **v** **f**

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| sh o | sh e | sh i | sh a |
| **sho** | **she** | **shi** | **sha** |

Soma s labi na maneno.

| | |
|---|---|
| shu le ni | ni sha ni |
| **shuleni** | **nishani** |
| di ri sha ni | m ko ro sho |
| **dirishani** | **mkorosho** |

Tamka sauti.

**Sh** **sh**

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| sh i | s i | sh u | s u |
| **shi** | **si** | **shu** | **su** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a ka simama | wa ka shikana |
| **akasimama** | **wakashikana** |
| wa li washa | wa ka amua |
| **waliwasha** | **wakaamua** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| **neno** | **matumizi ya -ni** |
|---|---|
| shule | shule**ni** |
| dirisha | dirisha**ni** |
| darasa | darasa**ni** |
| kijiji | kijiji**ni** |

63

Wiki ya 13: Siku ya 3 na 4 **Mazingira**

Wasichana wawili wanafagia majani chini ya mti shuleni

### Aisha na Shiko wazawadiwa

Aisha alifika shuleni mapema. Akasimama dirishani na kutazama Shumila akikariri shairi. Mara Shiko akatokea. Wakashikana mikono kwa furaha. Shiko akasema, "Hujambo Aisha?" Aisha akajibu, "Sijambo. U hali gani Shiko?" "Njema," Shiko akajibu. Shumila akasikia kelele akashtuka. Mara akawaona Shiko na Aisha. Shiko akasema, "Pole." Aisha akasema, "Samahani."

Kisha wakaamua kufagia karibu na mkorosho. Baadaye waliwasha majani na takataka moto.

Siku hiyo, mwalimu mkuu aliwapa nishani na shada la maua.

64

**Ufahamu wa fonimu**

N/T/U: Tamka sauti **/sh/**. Taja maneno huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. (**shida, asha). [U]**Endelea kwa maneno: ***shilingi, mpishi, shimo, shona, shuka***.

**Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **sh**. Tamka sauti **/sh/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **sho**. Sema kila sauti **/sh/ /o/** kisha uunganishe na kusema silabi **sho**. **[U]** Endelea kwa silabi **she, shi** na **sha.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U: Tamka silabi **shu le** na **ni** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **shuleni**. **[U]** Endelea na maneno: **dirishani, nishani** na **mkorosho.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **shairi, mkorosho** na **shada**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya "**Aisha na Shiko wazawadiwa"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Aisha alifanya nini alipofika shuleni?*** *(alisimama dirishani na kutazama Shumila akikariri shairi)*
2. ***Mwalimu mkuu aliwapa Shiko na Aisha vitu gani?*** *(aliwapa nishani na shada la maua)*

**Kuandika**

Waagize wanafunzi waandike herufi **sh** mara tatu.

sh sh sh sh sh

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi hizi: **Aisha alifika shuleni; Shumila alikariri shairi; Walifagia karibu na mkorosho; Watoto walipewa nishani**. Waagize wanafunzi wazinakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 13: Siku ya 3 na 4 **Mazingira**

Tamka sauti.

sh v f

Soma sauti ya herufi na silabi.

sh o — **sho**
sh e — **she**
sh i — **shi**
sh a — **sha**

Soma s labi na maneno.

shu le ni — **shuleni**
ni sha ni — **nishani**
di ri sha ni — **dirishani**
m ko ro sho — **mkorosho**

Tamka sauti.

Sh sh

Soma sauti ya herufi na silabi.

sh i — **shi**
s i — **si**
sh u — **shu**
s u — **su**

Soma sehemu za neno na neno lote.

a ka simama — **akasimama**
wa ka shikana — **wakashikana**
wa li washa — **waliwasha**
wa ka amua — **wakaamua**

Sarufi: Soma maneno haya.

| neno | matumizi ya -ni |
|---|---|
| shule | shuleni |
| dirisha | dirishani |
| darasa | darasani |
| kijiji | kijijini |

63

Wiki ya 13: Siku ya 3 na 4 **Mazingira**

Wasichana wawili wanafagia majani chini ya mti shuleni

**Aisha na Shiko wazawadiwa**

Aisha alifika shuleni mapema. Akasimama dirishani na kutazama Shumila akikariri shairi. Mara Shiko akatokea. Wakashikana mikono kwa furaha. Shiko akasema, "Hujambo Aisha?" Aisha akajibu, "Sijambo. U hali gani Shiko?" "Njema," Shiko akajibu. Shumila akasikia kelele akashtuka. Mara akawaona Shiko na Aisha. Shiko akasema, "Pole." Aisha akasema, "Samahani."
Kisha wakaamua kufagia karibu na mkorosho. Baadaye waliwasha majani na takataka moto.
Siku hiyo, mwalimu mkuu aliwapa nishani na shada la maua.

64

### ▲ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **sh**. Tamka sauti ya herufi **/sh/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ⬬ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **shi**. Sema kila sauti **/sh/ /i/** kisha uunganishe na kusema silabi **shi**. **[U]** Endelea kwa silabi: **si, shu** na **su.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **a ka simama** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **akasimama** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **wa li washa (waliwasha), wa ka shikana (wakashikana), wa ka amua (wakaamua).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

[N/T] Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Kisha uyasome pamoja na wanafunzi. Eleza wanafunzi jinsi ya kutumia kielezi wapi. Kwa mfano: Wanafunzi wanafagia wapi? Shuleni. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

shule - shule**ni**
dirisha - disha**ni**
darasa - darasa**ni**
kijiji - kijiji**ni**

### 🕮 Kabla ya kusoma::

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **shairi, mkorosho** na **shada**.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Aisha na Shiko wazawadiwa"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Unafikiri ni kwa nini mwalimu mkuu aliwapa nishani na shada la maua?*** *(kwa sababu walikuwa wasafi/walikuwa watoto wazuri)*
2. ***Kwa nini Shumila alimwambia Aisha samahani?*** *(watoto waeleze sababu ya kuomba msamaha)*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Waagize wanafunzi wayaandike wakiangaza silabi **ni** mwishoni wa kila neno.

| **Neno** | **Ongeza -ni** |
|---|---|
| dirisha | dirishani |
| darasa | ____________ |
| kijiji | ____________ |
| mti | ____________ |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yaliyochanganywa: **shanini, dasha, lenishu, shadiri, irisha**. Waambie wanafunzi wayaandike maneno halisi. Kisha wawasomee wenzao: **Mfano:** irisha - shairi

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 13: Siku ya 5 **Mazingira**

Tamka sauti.

v V f F sh

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: vi bo ko - **vi**bo**ko**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| fo | di | shi | bo | ri | sha | ma |
| ko | ni | ji | to | le | li | vi |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| dereva **ali**simama | madereva **wali**simama. |
| dereva **ali**furahi | madereva **wali**furahi. |
| dereva **ali**ogopa | madereva **wali**ogopa. |
| dereva **ali**lala | madereva **wali**lala. |

Kima wanasukuma gari wakielekeza msituni. Ndani ya gari kuna dereva.

**Dereva na kima**

Siku moja dereva mvivu alisimamisha gari lake karibu na barabara. Akala viazi vitamu na uji. Mara akajifunika kwa vazi lake kisha akalala fofofo. Kima watano wakamvamia. Walisukuma gari lake hadi msituni. Dereva alipoamka alijikuta katikati ya miti msituni. Kima walipoona dereva ameamka wakaogopa na kutorokea msituni.

65

### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(sh)**. Tamka sauti ya herufi **/sh/**. **[U]** Endelea kwa herufi **(v)**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Silabi

**[N]** Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **vi, bo** na **ko** kuandika neno **viboko**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ● Sarufi

[N/T/U] Eleza wanafunzi wasome ukurasa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma sentensi pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Dereva **ali**simama | Madereva **wali**simama. |
| Dereva **ali**furahi | Madereva **wali**furahi. |
| Dereva **ali**ogopa | Madereva **wali**ogopa. |
| Dereva **ali**lala | Madereva **wali**lala. |

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mvivu, vikosi** na **vikamvamia**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Dereva na kima"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Taja mambo aliyoyafanya dereva.*** *(alisimamisha gari/ akala viazi vitamu/alijifunika kwa vazi lake alilala fofofo)*
2. ***Kima watano walifanya nini?*** *(walimvamia, walisukuma gari lake hadi msituni)*
3. ***Kwa nini dereva alilala?*** *(alikuwa ameshiba/alikuwa amechoka)*
4. ***Kwa nini kima walitoroka?*** *(walimwogopa dereva)*

### Hadithi ya mwalimu

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. (*Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

**Chozi na Akinyi**

Palitokea dada wawili. Dada hao walikuwa na tabia nzuri. Shuleni pia walifanya vizuri katika masomo. Walipita mitihani vizuri. Hasa Akinyi alikuwa na bidii sana. Chozi alikuwa katika darasa moja na Akinyi. (***Kwa nini unafikiri dada hawa walifanya vizuri katika masomo yao?)***

Siku moja, Akinyi na dada yake walipanga kwenda porini. Akinyi alifanya kazi zote za nyumbani kama kufua sare zake za shule na kung'arisha chumba chake cha kulala halafu wakaelekea porini. ***(Akinyi na dadake walipanga kwenda wapi?)*** Walitembea wakiwa na woga na wasiwasi.

Mle porini waliona mimea ya matunda, miti, ndege, maua, maembe na mapera. Mara Chozi akaona kanga aliyekuwa na mayai. Akinyi akamwambia wasongee karibu. Kanga yule alikuwa ameanza kuangua vifaranga. Tayari wawili walikuwa wametokea. Akinyi na dadake wakamwacha.(***Kama ni wewe uliyempata kanga huyo ungefanya nini?)***

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiandika: **shuleni, dirishani, viboko, vijito, wavuvi**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Eleza wanafunzi waendelee kuunda maneno zaidi wakitumia silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 14: Siku ya 1

Wiki ya 14: Siku ya 1 na 2 **Sehemu za mwili**

Tamka sauti.

ny v sh

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ny a | ny i | ny e | ny u |
| nya | nyi | nye | nyu |

Sarufi: Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| nyu ki | nya nyi ro |
| nyuki | nyanyiro |
| wa nya ma | nyo ro ro |
| wanyama | nyororo |

Tamka sauti.

ny

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ny a | n a | n e | ny e |
| nya | na | ne | nye |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa ka kaza | wa ka m tafuta |
| wakakaza | wakamtafuta |
| a li kariri | wa ka toroka |
| alikariri | wakatoroka |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mtu aliishi hapa | watu waliishi hapa. |
| mtu alimtafuta sana | watu waliwatafuta sana. |
| mtu alikaza mguu wake | watu walikaza miguu yao. |
| mtu alikariri shairi | watu walikariri mashairi. |

66

Wiki ya 14: Siku ya 1 na 2 **Sehemu za mwili**

Msituni kuna mti mrefu na mzinga wa nyuki juu yake. Chini ya mti kuna mvulana. Mikono yake miwili imefungwa ikielekezwa nyuma. Miguu yake pia imefungwa pamoja. Hana shati. Watu wawili waliovalia nadhifu wanakimbizwa na nyuki.

## Nyamari na nyuki

Nyamari aliishi kijijini Nyanyiro.
Yeye alijua kukariri mashairi.
Alijua mashairi ya wanyama na nyuki.
Watu wabaya wenye nyororo wakaja na kumteka nyara Nyamari.
Wanakijiji wa Nyanyiro walimtafuta hata msituni.Watu wabaya wakakaza mikono na miguu kwa nyororo. Nyamari alikariri shairi la nyuki.
Nyuki wakaja na kuwauma wale watu wabaya.
Wakatoroka huku wakilia.

67

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/ny/.** Taja maneno **(nyoka, ponyoka)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea kwa maneno: **nyuki, foronya, nyama** na **nyanya.**

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **ny**. Tamka sauti **/ny/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **nya**. Sema kila sauti **/ny/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi **nya**. **[U]** Endelea kwa silabi **nyi, nye** na **nyu.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **nyu** na **ki** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **nyuki.** **[U]** Endelea na maneno **Nyanyiro, wanyama** na **nyororo.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kuteka nyara, wakakaza** na **nyororo**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Nyamari na nyuki"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Nyamari aliishi wapi?*** *(aliishi kijijini Nyanyiro)*
2. ***Nyamari alijua kukariri nini?*** *(alijua kukariri mashairi ya wanyama na nyuki)*

### Kuandika

Wanafunzi waandike herufi **ny** mara tatu.

ny ny ny

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **wanyama, nyuki, nyara, nyororo, kuteka**. Wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 14: Siku ya 1 na 2 **Sehemu za mwili**

Tamka sauti.

ny v sh

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ny a | ny i | ny e | ny u |
| nya | nyi | nye | nyu |

Sarufi: Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| nyu ki | nya nyi ro |
| nyuki | nyanyiro |
| wa nya ma | nyo ro ro |
| wanyama | nyororo |

Tamka sauti.

ny

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ny a | n a | n e | ny e |
| nya | na | ne | nye |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa ka kaza | wa ka m tafuta |
| wakakaza | wakamtafuta |
| a li kariri | wa ka toroka |
| alikariri | wakatoroka |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mtu aliishi hapa | watu waliishi hapa. |
| mtu alimtafuta sana | watu waliwatafuta sana. |
| mtu alikaza mguu wake | watu walikaza miguu yao. |
| mtu alikariri shairi | watu walikariri mashairi. |

66

Wiki ya 14: Siku ya 1 na 2 **Sehemu za mwili**

Msituni kuna mti mrefu na mzinga wa nyuki juu yake. Chini ya mti kuna mvulana. Mikono yake miwili imefungwa ikielekezwa nyuma. Miguu yake pia imefungwa pamoja. Hana shati. Watu wawili waliovalia nadhifu wanakimbizwa na nyuki.

**Nyamari na nyuki**

Nyamari aliishi kijijini Nyanyiro.
Yeye alijua kukariri mashairi.
Alijua mashairi ya wanyama na nyuki.
Watu wabaya wenye nyororo wakaja na kumteka nyara Nyamari.
Wanakijiji wa Nyanyiro walimtafuta hata msituni.Watu wabaya wakakaza mikono na miguu kwa nyororo. Nyamari alikariri shairi la nyuki.
Nyuki wakaja na kuwauma wale watu wabaya.
Wakatoroka huku wakilia.

67

▲ **Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **ny**. Tamka sauti ya herufi **/ ny/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

⬬ **Kusoma silabi**

N/T/U: Tamka silabi **nya** ubaoni. Sema kila sauti **/ny/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi **nya**. **[U]** Endelea kwa silabi **na, nye** na **ne**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa ka kaza** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **wakakaza** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **a li kariri (alikariri), wa ka m tafuta (wakamtafuta), wa ka toroka (wakatoroka).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

◆ **Sarufi**

[N/T/U] Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma sentensi kisha uzisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Mtu **a**liishi hapa | - | Watu **wa**liishi hapa. |
| Mtu **a**limtafuta sana | - | Watu **wa**liwatafuta sana. |
| Mtu **a**likaza mguu wake | - | Watu **wa**likaza miguu yao. |
| Mtu **a**likariri shairi | - | Watu **wa**likariri shairi. |

🕮 **Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **kuteka nyara, wakikaza** na **nyororo**.

🕮 **Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Nyamari na nyuki"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

◈ **Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Je, unafikiri watu walimpata Nyanyiro***? *(ndiyo, kwa sababu watu wabaya walitoroka)*
2. ***Je, unafikiri hadithi hii ni ya kweli? Tetea jibu lako.*** *(wanafunzi watoe sababu za majibu yao)*

✍ **Kuandika: Imla**

Soma maneno yafuatayo mara mbili. Wanafunzi wayaandike **nyuki, mti, nyororo**. Wanafunzi wajadiliane kuhusu nyuki, mti, nyororo.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| **a**liishi | - | **wa**liishi |
| **a**limtafuta | - | **wa**limtafuta |
| **a**likaza | - | **wa**likaza |

Waagize wanafunzi wayanakili kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 14: Siku ya 3



Tamka sauti.

dh ny v

Tamka sauti ya herufi na silabi.

dh a dh e dh i dh o

**dha** **dhe** **dhi** **dho**

Soma silabi na maneno.

go dha na bi dha a fe dha dha ha bu

**godhana** **bidhaa** **fedha** **dhahabu**

Tamka sauti.

dh dh

Tamka sauti ya herufi na silabi.

dh u d u dh i d i

**dhu** **du** **dh i** **di**

Soma sehemu za neno na neno lote.

ki na meta meta a ka m pasua

**kinametameta** **akampasua**

a li po fika a ka nunua

**alipofika** **akanunua**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| samaki huyu ni mdogo | samaki hawa ni wadogo. |
| samaki huyu ni mtamu | samaki hawa ni watamu. |
| samaki huyu ni mrefu | samaki hawa ni warefu. |
| samaki huyu ni mzuri | samaki hawa ni wazuri. |





Kijana anapasua samaki upande mmoja kwa kisu juu ya meza. Ameshika kitu kinachometameta huku akiwa anashangaa.

**Godhana atajirika**

Godhana alitaka kununua bidhaa tofauti tofauti.
Siku hiyo hakuwa na fedha za kutosha.
Jioni moja, akanunua samaki mdogo na dania.
Alipofika kwake, alimweka samaki mezani, kisha akampasua.
Godhana akapata kijiwe kidogo ndani ya samaki.
Akakiosha kijiwe mara akaona kinametameta.
Alipojua ni dhahabu alifurahi sana.
Godhana akaiuza dhahabu hiyo, akatajirika.



### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/dh/**. Taja maneno **(dhambi, fedha)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea kwa maneno: **dhahabu, orodha, dhati, udhi, bidhaa** na **fadhili**.

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **dh**. Tamka sauti **/dh/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **dha**. Sema kila sauti **/dh/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi **dha**. **[U]** Endelea kwa silabi **dhe, dhi** na **dho**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **/go/ /dha/ /na/** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **Godhana**. **[U]** Endelea na maneno: **bidhaa, fedha, dhahabu**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **bidhaa, dhahabu** na **fedha**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Godhana atajirika**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Taja vitu ambavyo Godhana alinunua?*** *(alinunua samaki na dania)*
2. ***Ni kitu gani ambacho Godhana alikiona alipopasua samaki?*** *(kijiwe, dhahabu n.k)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **dh** mara tatu.

dh dh dh dh dh

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo:

**Godhana alinunua bidhaa.**
**Godhana hakuwa na fedha.**
**Godhana aliuza dhahabu.**

Wanafunzi wazinakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 14: Siku ya 4

Wiki ya 14: Siku ya 3 na 4 **Vyakula**

Tamka sauti.

dh ny v

Tamka sauti ya herufi na silabi.

dh a dh e dh i dh o

**dha dhe dhi dho**

Soma silabi na maneno.

go dha na bi dha a fe dha dha ha bu

**godhana bidhaa fedha dhahabu**

Tamka sauti.

dh dh

Tamka sauti ya herufi na silabi.

dh u d u dh i d i

**dhu du dh i di**

Soma sehemu za neno na neno lote.

ki na meta meta a ka m pasua

**kinametameta akampasua**

a li po fika a ka nunua

**alipofika akanunua**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| samaki huyu ni mdogo | samaki hawa ni wadogo. |
| samaki huyu ni mtamu | samaki hawa ni watamu. |
| samaki huyu ni mrefu | samaki hawa ni warefu. |
| samaki huyu ni mzuri | samaki hawa ni wazuri. |

68

Wiki ya 14: Siku ya 3 na 4 **Vyakula**

Kijana anapasua samaki upande mmoja kwa kisu juu ya meza. Ameshika kitu kinachometameta huku akiwa anashangaa.

**Godhana atajirika**

Godhana alitaka kununua bidhaa tofauti tofauti.
Siku hiyo hakuwa na fedha za kutosha.
Jioni moja, akanunua samaki mdogo na dania.
Alipofika kwake, alimweka samaki mezani, kisha akampasua.
Godhana akapata kijiwe kidogo ndani ya samaki.
Akakiosha kijiwe mara akaona kinametameta.
Alipojua ni dhahabu alifurahi sana.
Godhana akaiuza dhahabu hiyo, akatajirika.

69

### ▲ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **dh**. Tamka sauti ya herufi **/dh/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ⬬ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **dhu**. Sema kila sauti **/dh/ /u/** kisha uunganishe na kusema silabi **dhu**. **[U]** Endelea kwa silabi: **du, dhi** na **di.**
Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **ki na meta meta** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **kinametameta**. **[U]** Endelea kwa maneno: **a li po fika (alipofika), a ka m pasua (akampasua) a ka nunua (akanunua).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

[N/T] Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma sentensi kisha uzisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Samaki huyu ni **m**dogo | - | Samaki hawa ni **wa**dogo. |
| Samaki huyu ni **m**tamu | - | Samaki hawa ni **wa**tamu. |
| Samaki huyu ni **m**refu | - | Samaki hawa ni **wa**refu. |
| Samaki huyu **ni m**zuri | - | Samaki hawa ni **wa**zuri. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **bidhaa, dhahabu** na **fedha**.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Godhana atajirika"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### ◇ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Kwa nini Godhana alifurahi sana?*** *(kwa sababu alijua kijiwe kilikuwa ni dhahabu)*
2. ***Je, unafikiri Godhana alifanyia nini zile pesa alizopata baada ya kuiuza ile dhahabu?*** *(alijenga nyumba, alinunua gari n.k)*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo.
Wanafunzi waandike wingi wa maneno hayo.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| mdogo | wadogo |
| mtamu | ________ |
| mrefu | ________ |
| mfupi | ________ |
| mzuri | ________ |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yaliyochanganywa: **dhafe, habudha, makisa, niada**. Waagize wanafunzi wayaandike maneno halisi. Kisha wawasomee wenzao. **Mfano:** dhaabi - bidhaa

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 14: Siku ya 5 **Afya na USafi**

Tamka sauti.

ny dh

Tumia s labi kuunda maneno.
Kwa mfano: nyo ro ro **nyororo**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| nyu | nya | ki | ra | nyo | dha | ha |
| ma | si | wa | ro | re | u | bu |

Sarufi: Soma maneno haya.

| umoja | wingi |
|---|---|
| aliugua | waliugua |
| aliwapa | waliwapa |
| alikuwa | walikuwa |
| aliparara | waliparara |

Nyoka ameingia chumbani kichafu. Sakafuni kumetapakaa vitu mbalimbali.

**Usafi**

Watoto wa Shinyanya hawakuwa safi. Hawakuoga wala kusugua meno. Nyayo zao zilipasuka hata zikawa na vidonda. Miili yao pia iliparara. Kwao hakukuwa safi. Nyuki, nyigu, panya na nyoka walihamia huko. Watoto hawa walikuwa na minyoo na waliugua. Nyanya yao aliwapa dawa na kuwashauri wawe safi.

70

### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(ny)**. Tamka sauti ya herufi **/ ny/**. **[U]** Endelea kwa herufi **(dh)**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Silabi

**[N]** Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **nyo, ro** na **ro** kuandika neno **nyororo**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. [N/T/U]: Soma maneno kisha uyasome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **a**liugua | - | **wa**liugua |
| **a**liwapa | - | **wa**liwapa |
| **a**likuwa | - | **wa**likuwa |
| **a**liparara | - | **wa**liparara |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **nyigu, minyoo** na **iliparara**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Usafi"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Tunajuaje watoto wa Shinyanya walikuwa wachafu?*** *(kwa sababu hawakuoga, hawakusugua meno, nyayo zao zilipasuka, miili yao iliparara)*
2. ***Taja wanyama na wadudu waliohamia kwao.*** *(nyuki, nyigu, panya, nyoka)*
3. ***Eleza umuhimu wa kuwa safi.*** *(hutapata magonjwa)*
4. ***Wadudu husababisha magonjwa kama gani?*** *(minyoo, kipindupindu, homa n.k)*

### 🕮 Hadithi ya mwalimu

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. *(Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

**Hadithi ya vidole**

Vidole vya mwanadamu si sawa, ijapokuwa vyote ni vya muhimu sana. Siku moja, vidole viliongea kuhusu ni nani muhimu zaidi kati yao. Kidole cha gumba kikasema, "Bila mimi, nyinyi ni dhaifu kabisa."

Kidole cha kati kikajibu kwa maringo, "Wee, mbilikimo! Huoni mimi ndio mrefu zaidi?"(***Kidole cha kati kiliringa kwa sababu gani?***)

Kidole cha pete kikasema, "Binadamu ananiheshimu sana. Ndio maana yeye hunivisha pete." Kidole cha shahada kikawaza na kusema, "Hamjui mimi ndio alama ya nguvu?" (***Kwa nini kidole hiki kikaitwa cha pete?***)

Mwishowe kile kidole kidogo kikajibu kwa upole na kusema, "Wacheni kusemezana. Mungu alituumba hivi tulivyo ili tuwe funzo kwa wanadamu. Tunastahili kuishi pamoja na kushirikiana ikiwa tutafaulu maishani." (***Kwa nini ni vizuri pawe na ushirikiano baina ya vidole?***)

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiandika**:** **wanyama, nyororo, bidhaa, fedha, dhahabu**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Eleza wanafunzi waendelee kuunda maneno zaidi wakitumia silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Wiki ya 15: Siku ya 1

Wiki ya 15: Siku ya 1 na 2 **Tarakimu**

Tamka sauti.

th ny dh

Soma sauti ya herufi na silabi.

th a th u th i th e
**tha** **thu** **thi** **the**

Soma silabi na maneno.

the la thi ni the ma ni ni
**thelathini** **themanini**
tha ma ni dha ti
**thamani** **dhati**

Tamka sauti.

th

Soma sauti ya herufi na silabi.

th a t a t o th o
**tha** **ta** **to** **tho**

Soma sehemu za neno na neno lote.

a li po jua a me mu ibia
**alipojua** **amemuibia**
ha ja thubutu u ka isha
**hajathubutu** **ukaisha**

Sarufi: Soma maneno haya.

| neno | kinyume |
|---|---|
| lala | amka |
| fupi | refu |
| rafiki | adui |
| keti | simama |

71

Wiki ya 15: Siku ya 1 na 2 **Tarakimu**

Mti mkubwa na juu yake kuna nyoka. Nyoka wanaangaliana na nyati. Angani kuna ndege na mawingu machache.

## Nyati na Nyoka

Nyati na Nyoka walikuwa marafiki wa dhati.
Walikaa pamoja kila wakati.
Nyoka alikuwa na miaka themanini.
Nyati alikuwa na miaka thelathini.
Nyoka alikuwa na vitu vya thamani.
Siku moja nyati akamuibia nyoka.
Nyoka alipojua kuwa nyati amemuibia alikasirika sana.
Hapo hapo urafiki wao ukaisha.
Tangu siku hiyo nyati hajathubutu kukaa karibu na nyoka tena.

72

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/th/**. Taja maneno **(thelathini, athari)** halafu wanafunzi wafanye ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea kwa maneno (**themanini, hadithi, thamani, athari, thuluthi** na **tete**.

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **th**. Tamka sauti **/th/**.
Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **tha**. Sema sauti **/th/ /a/** kisha uunganishe na kusema upesi silabi **tha**. **[U]** Endelea na silabi **thu, thi** na **the.**
Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **the la thi** na **ni** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **thelathini**. **[U]** Endelea na maneno **themanini, thamani** na **dhati**.
Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **dhati, thamani** na **hajathubutu/thubutu**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo.
Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Nyati na Nyoka**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

- ***i. Nyoka alikuwa na miaka mingapi?*** *(themanini)*
- ***ii. Nyoka alikuwa ni vitu vya aina gani?*** *(thamani)*
- ***iii. Nini kilifanyika kwa urafiki wao?*** *(urafiki wao uliisha)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **th** mara tatu.

th th th

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **dhati, themanini, thelathini, thamani, thubutu**. Waagize wanafunzi wayaandike kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 15: Siku ya 1 na 2 **Tarakimu**

Tamka sauti.

th ny dh

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| th a | th u | th i | th e |
| **tha** | **thu** | **thi** | **the** |

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| the la thi ni | the ma ni ni |
| **thelathini** | **themanini** |
| tha ma ni | dha ti |
| **thamani** | **dhati** |

Tamka sauti.

th

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| th a | t a | t o | th o |
| **tha** | **ta** | **to** | **tho** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li po jua | a me mu ibia |
| **alipojua** | **amemuibia** |
| ha ja thubutu | u ka isha |
| **hajathubutu** | **ukaisha** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| neno | kinyume |
|---|---|
| lala | amka |
| fupi | refu |
| rafiki | adui |
| keti | simama |

71

Wiki ya 15: Siku ya 1 na 2 **Tarakimu**

Mti mkubwa na juu yake kuna nyoka. Nyoka wanaangaliana na nyati. Angani kuna ndege na mawingu machache.

### Nyati na Nyoka

Nyati na Nyoka walikuwa marafiki wa dhati.
Walikaa pamoja kila wakati.
Nyoka alikuwa na miaka themanini.
Nyati alikuwa na miaka thelathini.
Nyoka alikuwa na vitu vya thamani.
Siku moja nyati akamuibia nyoka.
Nyoka alipojua kuwa nyati amemuibia alikasirika sana.
Hapo hapo urafiki wao ukaisha.
Tangu siku hiyo nyati hajathubutu kukaa karibu na nyoka tena.

72

**▲ Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **th**. Tamka sauti **/th/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **tha**. Sema sauti **/th/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi kwa upesi **tha**. **[U]** Endelea kwa silabi **ta, to** na **tho**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**★ Kusoma maneno marefu.**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **alipojua** kisha uunganishe sehemu hizo upesi na useme neno **alipojua**. **[U]** Endelea na: **ha ja thubutu (hajathubutu), a me mu ibia (amemuibia), u ka isha (ukaisha).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**◆ Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U. Soma maneno yote.

| **Neno** | | **Kinyume** |
|---|---|---|
| lala | - | amka |
| fupi | - | refu |
| rafiki | - | adui |
| keti | - | simama |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **dhati, thamani** na **hajathubutu/thubutu**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi "**Nyoka na Nyati**" wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome kwa vikundi vya wawili wawili.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

*i.* **Je, unafikiri nyati na nyoka walifanya nini wakati walikuwa wakiketi pamoja?** *(walizungumza/walicheza pamoja n.k)*

*ii.* **Je, unafikiri nyoka alikuwa na vitu gani vya thamani?** *(pesa n.k, wanafunzi wataje vitu mbalimbali)*

*iii.* **Je, ungekuwa nyoka ungefanya nini?** *(ningemshitaki nyati/ ningemsamehe nyati)*

**Kuandika: Imla**

Sema neno **nyoka**. Wanafunzi waliandike kisha wajadiliane kuhusu **nyoka na nyati**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Wanafunzi waandike kinyume.

| | | |
|---|---|---|
| **karibu** | - | **mbali** |
| **mbele** | - | ___________ |
| **rafiki** | - | ___________ |

Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Tamka sauti.

ch th dh

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ch a | ch i | ch o | ch e |
| cha | chi | cho | che |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| chu i | chu ra | cha tu | m che zo |
| chui | chura | chatu | mchezo |

Tamka sauti.

ch

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ch u | j u | h u | ch o |
| chu | ju | hu | cho |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li cheza | a ka hesabu |
| walicheza | akahesabu |
| a ka mweka | a li kasirika |
| akamweka | alikasirika |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | | wingi | |
|---|---|---|---|
| chatu huyu ni mmoja | 1 | chatu hawa ni kumi. | 10 |
| chiriku huyu ni mmoja | 1 | chiriku hawa ni ishirini. | 20 |
| chui huyu ni mmoja | 1 | chui hawa ni hamsini. | 50 |
| chura huyu ni mmoja | 1 | chura hawa ni sitini. | 60 |





Ni usiku. Nje ya nyumba kuna Nyoka mkubwa na chui. Wanamchungulia chura akiwa ndani ya mkebe. Angani kuna nyota na mwezi. Kuna mwangaza ndani ya nyumba.

**Mchezo wa wanyama**

Chatu, Chura na Chui waliishi kwenye kichochoro.
Siku moja walicheza mchezo wa kuhesabu nyota.
Chatu alihesabu na kupata nyota kumi tu.
Chui naye alihesabu kutoka kumi hadi ishirini.
Chura akahesabu kutoka thelathini, arobaini, hamsini, sitini, sabini, themanini, tisini hadi mia moja.
Chui alikasirika sana.
Akamweka Chura kwenye chupa.



### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/ch/**. Taja maneno **(choo, kachero)** halafu wanafunzi wafanye ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea kwa maneno (**fanicha, cheza, chachu, cheka** na **chumba**.

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **ch**. Tamka sauti **/ch/**.
Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma silabi

Andika silabi **cha**. N/T/U: Sema sauti **/ch/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi **cha**. **[U]** Endelea na silabi: **chi, cho** na **che**.
Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **chu** na **i** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **chui**. **[U]** Endelea na maneno **chura, chatu** na **mchezo**.
Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kichochoro, chatu** na **nyota**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo.
Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Mchezo wa wanyama"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

*i.* ***Chura na chui waliishi wapi?*** *(kichorochoroni/kwenye kichochoro)*
*ii.* ***Walicheza mchezo gani?*** *(kuhesabu nyota)*
*iii.* ***Chura alihesabu hadi ngapi?*** *(mia moja)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **ch** mara tatu.

ch ch ch

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo:

i. **Chatu na Chura walicheza.**
ii. **Chui na Chatu waliishi kwa kichochoro.**
iii. **Chui alimweka Chura kwenye chupa.**

Waambie wanafunzi waziandike kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 15: Siku ya 3 na 4 **Tarakimu**

Tamka sauti.

ch th dh

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ch a | ch i | ch o | ch e |
| **cha** | **chi** | **cho** | **che** |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| chu i | chu ra | cha tu | m che zo |
| **chui** | **chura** | **chatu** | **mchezo** |

Tamka sauti.

ch

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ch u | j u | h u | ch o |
| **chu** | **ju** | **hu** | **cho** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li cheza | a ka hesabu |
| **walicheza** | **akahesabu** |
| a ka mweka | a li kasirika |
| **akamweka** | **alikasirika** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | | wingi | |
|---|---|---|---|
| chatu **huyu** ni mmoja | 1 | chatu **hawa** ni kumi. | 10 |
| chiriku **huyu** ni mmoja | 1 | chiriku **hawa** ni ishirini. | 20 |
| chui **huyu** ni mmoja | 1 | chui **hawa** ni hamsini. | 50 |
| chura **huyu** ni mmoja | 1 | chura **hawa** ni sitini. | 60 |

73

Wiki ya 15: Siku ya 3 na 4 **Tarakimu**

Ni usiku. Nje ya nyumba kuna Nyoka mkubwa na chui. Wanamchungulia chura akiwa ndani ya mkebe. Angani kuna nyota na mwezi. Kuna mwangaza ndani ya nyumba.

**Mchezo wa wanyama**

Chatu, Chura na Chui waliishi kwenye kichochoro.
Siku moja walicheza mchezo wa kuhesabu nyota.
Chatu alihesabu na kupata nyota kumi tu.
Chui naye alihesabu kutoka kumi hadi ishirini.
Chura akahesabu kutoka thelathini, arobaini, hamsini, sitini, sabini, themanini, tisini hadi mia moja.
Chui alikasirika sana.
Akamweka Chura kwenye chupa.

74

### ▲ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **ch**. Tamka sauti **/ch/**.
Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ⬬ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **chu**. Sema sauti **/ch/ /u/** kisha uunganishe na kusema silabi **chu**. **[U]** Endelea kwa silabi: **ju, hu** na **cho**.
Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa li cheza** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **walicheza**. **[U]** Endelea na: **a ka hesabu (akahesabu), a ka mweka (akamweka), a li kasirika (alikasirika).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U. Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Chatu **huyu** ni mmoja | Chatu **hawa** ni kumi |
| Chiriku **huyu** ni mmoja | Chiriku **hawa** ni ishirini |
| Chui **huyu** ni mmoja | Chui **hawa** ni hamsini |
| Chura **huyu** ni mmoja | Chura **hawa** ni sitini |

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **kichochoro, chatu** na **nyota**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi **"Mchezo wa wanyama"** wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome kwa vikundi vya wawili wawili.
Mwalimu achague wanafunzi wawili wasimulie hadithi waliyoisoma.

### ⟐ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

i. ***Je, unafikiri wanyama walicheza mchezo wao saa ngapi?*** *(walicheza usiku kwa sababu walihesabu nyota)*
ii. ***Je, unafikiri kwa nini chui alikasirika?*** *(kwa sababu chura alihesabu nyota nyingi)*
iii. ***Je, chui alifanya jambo zuri kumweka mwenzake kwenye chupa?*** *(la au ndio (wanafunzi waeleze majibu yao)*

### Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye tarakimu zifuatazo.
Wanafunzi waziandike tarakimu hizo kwa maneno.

| | |
|---|---|
| 20 | ishirini |
| 30 | ____________ |
| 40 | ____________ |
| 80 | ____________ |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yalichanganywa: **manitha, rachu, tucha, pachu**. Waambie wanafunzi wayaandike maneno halisi kisha wasomee wenzao. **Mfano:** tidha - dhati

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 15: Siku ya 5 Tarakimu

Soma sauti.

th ch

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: the lu ji **theluji**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| the | ni | ji | cha | ra | che |
| ma | lu | tha | i | che | ki |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **wakati uliopita** | **wakati ujao** |
|---|---|
| chui alikasirika | chui atakasirika. |
| chui alimweka | chui atamweka. |
| chatu alihesabu | chatu atahesabu. |
| chura alicheza | chura atacheza. |

Mama mrembo amekaa kitini. Anaangalia mikufu inayoning'inia ukutani. Kando yake kuna meza ndogo.

**Nyororo za dhahabu**

Tabitha alikuwa na nyororo kumi za dhahabu. Chebet akasema, "Ukinipatia nyororo hizi za dhahabu nitazifanya ziwe thelathini." Tabitha akasema, "Hata kama utazifanya ziwe themanini sikupi." Chebet hakuacha kuuliza kuhusu nyororo hizo. Tabitha alijua thamani ya nyororo zake. Kutoka siku hiyo hakuthubutu kuziweka hadharani tena.

75

### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la **(th)**. Tamka sauti ya herufi **/th/**. **[U]** Endelea kwa herufi **(ch)**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Silabi

Soma silabi pamoja zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** na wanafunzi. **[N]** Tumia silabi **the lu** na **ji** kuandika neno **theluji**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U. Soma vifungu hivi.

| **Wakati uliopita** | | **Wakati ujao** |
|---|---|---|
| Chui a**li**kasirika | - | Chui a**ta**kasirika |
| Chui a**li**mweka | - | Chui a**ta**mweka |
| Chatu a**li**hesabu | - | Chatu a**ta**hesabu |
| Chura a**li**cheza | - | Chura a**ta**cheza |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **hadharani, thamani** na **hakuthubutu/thubutu**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Nyororo za dhahabu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

*i.* ***Tabitha alikuwa na nyororo ngapi?*** *(alikuwa na nyororo kumi)*
*ii.* ***Chebet alisema atafanya nyororo ziwe ngapi?*** *(alisema atazifanya ziwe thelathini)*
*iii.* ***Je, unafikiri Chebet alikuwa na nia gani?*** *(alitaka kumdanganya Tabitha)*
*iv.* ***Kwa nini hakuweka nyororo zake hadharani tena?*** *(aliogopa kuwa zitaibiwa)*

### 🕮 Hadithi ya mwalimu

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. (*Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

**Wasafiri Sita**

Wasafiri sita walikuwa wamesafiri kwa muda mrefu. Wakafika ukingoni mwa mto. Mara mvulana akatokea aliyekuwa na mashua. Wakamwomba awape mashua ili wavuke mto. Mvulana akakubali kuwapa mashua. ***(Wasafiri waliomba mashua kufanyia nini?)*** Wale wasafiri wakaingia katika mashua lakini, mashua ikazama. Wale wasafiri wakaogelea hadi ukingoni. Walipofika ng'ambo ya mto, wakataka kujua ikiwa wote walikuwa salama.

Msafiri wa kwanza akagusa kichwa cha kila mtu akiwahesabu, "Mmoja, wawili, watatu, wanne, watano." (***Msafiri huyu alisahau kumhesabu nani?***) Akasahau kujihesabu. Akasema, "Mmoja wetu ametoweka!" Msafiri wapili akasema, "Wewe Hujui kuhesabu. Hebu nihesabu mimi." Naye akagusa mkono wa kila mtu akihesabu," Mmoja, miwili, mitatu, minne, mitano, sita, saba, minane, tisa, kumi." Akasahau kujihesabu. Akamaka na kusema, "Idadi yetu ni watu kumi! Ndio maana mashua ikazama." (***Je, ni kweli walikuwa watu kumi?***)
Mara wakamwona yule mvulana tena. Wakamwambia amtafute msafiri aliyetoweka nao watampa zawadi. Yule mvulana akasema, "Hebu kwanza niwahesabu kabla sijaanza kumtafuta mwenzenu aliyepotea." Aliwahesabu, na kupata wote sita. Akasema, "Nimempata msafiri aliyepotea." Wasafiri walicheka. ***(Wasafiri walimpa yule mvulana zawadi?)***

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara tatu huku wanafunzi wakiandika: **thamani, dhahabu, tabitha, hadharani, chebet**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Eleza wanafunzi waendelee kuunda maneno zaidi wakitumia silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 16: Siku ya 1 na 2 **Mavazi**

Tamka sauti.

gh th ch

Soma sauti ya herufi na silabi.

gh e gh o gh u gh a

ghe gho ghu gha

Soma silabi na maneno.

gho ro fa gha li gha si a gha ra ma

ghorofa ghali ghasia gharama

Tamka sauti.

gh

Soma sauti ya herufi na silabi.

gh i h i g i k i

ghi hi gi ki

Soma sehemu za neno na neno lote.

tu li shangaa wa ka mu umiza

tulishangaa wakamuumiza

ya ka raruka vi li onekana

yakararuka vilionekana

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja -ake | wingi -ao |
|---|---|
| hili ni vazi lake | haya ni mavazi yao. |
| hili ni shati lake | haya ni mashati yao. |
| hili ni koti lake | haya ni makoti yao. |
| hili ni gauni lake | haya ni magauni yao. |

76

Wiki ya 16: Siku ya 1 na 2 **Mavazi**

Polisi wa kike na kiume wamemshika mwizi. Kando kuna tairi, mtungi na mawe. Nguo za mwizi zimeraruka na uso wake umefura. Kiatu chake kimoja kimetoka.

### Adhabu ya mwizi

Kulitokea ghasia kijijini kwetu.
Mimi na wazazi wangu tuliishi katika ghorofa ya tatu.
Tulishangaa kuona mtu akifukuzwa. Polisi walimkamata.
Mavazi yake yakararuka.
Suruali yake ikapasuka vipande vikaanguka.
Kofia na viatu vyake vilionekana kuwa ghali sana.
Baadaye jirani akasema kuwa mwizi huyo alikuwa ameiba vitu sokoni.

77

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/gh/.** Taja maneno **(ghali, magharibi)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]** Endelea kwa maneno **ghala, ghorofa** na **faragha.**

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi ni **gh**. Tamka sauti **/gh/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **ghe**. Sema kila sauti **/gh/ /e/** kisha uunganishe na kusema silabi **ghe**. **[U]** Endelea kwa silabi **gho, ghu** na **gha**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **gho ro fa** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **ghorofa**. **[U]** Endelea na maneno: **ghali, ghasia** na **gharama.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **ghali, ghasia** na **ghorofa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Adhabu ya mwizi"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Wahusika wa hadithi hii waliishi wapi?*** *(waliishi kwenye ghorofa ya tatu, kijijini).*
2. ***Taja mavazi aliyovaa mtu aliyepigwa.*** *(Suruali, shati, kofia na viatu.)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **gh** mara tatu.

gh gh gh

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno haya: **ghasia, ghorofa, ghali, suruali** na **shati**. Waambie wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 16: Siku ya 2

Wiki ya 16: Siku ya 1 na 2 **Mavazi**

Tamka sauti.

gh th ch

Soma sauti ya herufi na silabi.

| gh e | gh o | gh u | gh a |
|---|---|---|---|
| ghe | gho | ghu | gha |

Soma silabi na maneno.

| gho ro fa | gha li | gha si a | gha ra ma |
|---|---|---|---|
| ghorofa | ghali | ghasia | gharama |

Tamka sauti.

gh

Soma sauti ya herufi na silabi.

| gh i | h i | g i | k i |
|---|---|---|---|
| ghi | hi | gi | ki |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| tu li shangaa | wa ka mu umiza |
|---|---|
| tulishangaa | wakamuumiza |
| ya ka raruka | vi li onekana |
| yakararuka | vilionekana |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja -ake | wingi -ao |
|---|---|
| hili ni vazi lake | haya ni mavazi yao. |
| hili ni shati lake | haya ni mashati yao. |
| hili ni koti lake | haya ni makoti yao. |
| hili ni gauni lake | haya ni magauni yao. |

76

Wiki ya 16: Siku ya 1 na 2 **Mavazi**

Polisi wa kike na kiume wamemshika mwizi. Kando kuna tairi, mtungi na mawe. Nguo za mwizi zimeraruka na uso wake umefura. Kiatu chake kimoja kimetoka.

### Adhabu ya mwizi

Kulitokea ghasia kijijini kwetu.
Mimi na wazazi wangu tuliishi katika ghorofa ya tatu.
Tulishangaa kuona mtu akifukuzwa. Polisi walimkamata.
Mavazi yake yakararuka.
Suruali yake ikapasuka vipande vikaanguka.
Kofia na viatu vyake vilionekana kuwa ghali sana.
Baadaye jirani akasema kuwa mwizi huyo alikuwa ameiba vitu sokoni.

77

**▲ Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **gh**. Tamka sauti ya herufi **/gh/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**⬬ Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **ghi**. Sema kila sauti **/gh/ /i/** kisha uunganishe na kusema silabi **ghi**. **[U]** Endelea kwa silabi**: gi, hi** na **ki.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**★ Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **tu li shangaa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **tulishangaa**. **[U]** Endelea na maneno: **ya ka raruka (yakararuka), wa ka mu umiza (wakamuumiza), vi li onekana (vilionekana).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**◆ Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Some sentensi kisha uzisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| **Umoja -ake** | | **Wingi -ao** |
|---|---|---|
| Hili ni vazi **lake** | - | Haya ni **ma**vazi **yao**. |
| Hili ni shati **lake** | - | Haya ni **ma**shati **yao**. |
| Hili ni koti **lake** | - | Haya ni **ma**koti **yao**. |
| Hili ni gauni **lake** | - | Haya ni **ma**gauni **yao**. |

**🕮 Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **ghali, ghasia** na **ghorofa**.

**🕮 Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **Adhabu ya mwizi** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

**◈ Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Ni aina gani ya mavazi huvaliwa na wasichana?*** *(sketi, blauzi, n.k)*
2. ***Je, wizi ni kitu kizuri au kibaya? Eleza jibu lako.*** *(Kibaya kwa sababu, huwa unachukua cha mtu. Unaweza kupigwa na/ama kuuwawa n.k.)*

**✍ Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **ghorofa**, **shati**, **viatu**. Wanafunzi wajadiliane kuhusu **ghorofa**, **shati** na **viatu**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye vifungu:

**vazi lake - mavazi yao**
**shati lake - mashati yao**

Waagize wanafunzi wavinakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Wiki ya 16: Siku ya 3 na 4 **Mavazi**

Tamka sauti.

**ng** **gh** **th**

Soma sauti ya herufi na silabi.

ng e ng u ng o ng a

**nge** **ngu** **ngo** **nga**

Soma silabi na maneno.

we ngi ne shi ngo ni ma ko nge sha nga

**wengine** **shingoni** **makonge** **shanga**

Tamka sauti.

**ng**

Tamka sauti ya herufi na silabi

ng a ng' a g a k a

**nga** **ng'a** **ga** **ka**

Soma sehemu za neno na neno lote.

vi li kuwa ha wa ku vaa

**vilikuwa** **hawakuvaa**

ya me badilika wa li beba

**yamebadilika** **walibeba**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja -angu | wingi -etu |
|---|---|
| huyu ni baba yangu | hawa ni baba zetu. |
| huyu ni babu yangu | hawa ni mababu zetu. |
| huyu ni bibi yangu | hawa ni mabibi zetu. |
| huyu ni mama yangu | hawa ni mama zetu. |

78

Wiki ya 16: Siku ya 3 na 4 **Mavazi**

Wanawake wawili. Mmoja amevalia mavazi ya kitamaduni. Mwingine amevalia mavazi ya kisasa.

**Mavazi ya zamani**

Zamani mababu na mabibi zetu hawakuvaa mavazi ya bei ghali.
Walivaa nguo za ngozi kiunoni.
Pia walivaa shanga za rangi mbalimbali shingoni.
Viatu vyao vilikuwa vya miti, ngozi na mkonge.
Wengine walibeba rungu ili kuonyesha cheo au heshima.
Siku hizi mambo yamebadilika.
Watu wanavaa watakavyo.
Mavazi hayana heshima wala kujali utamaduni wetu.

79

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/ng/**. Taja maneno **(ngano, mwanga)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]**Endelea na maneno ***ngoja*, *ingia*, *nguo*, *ngao*** *na* ***nyingi***.

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi ni **ng**. Tamka sauti **/ng/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **nge**. Sema kila sauti **/ng/ /e/** kisha uunganishe na kusema silabi **nge**. **[U]** Endelea kwa silabi**: ngu, ngo** na **nga.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **we ngi ne** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **wengine**. **[U]** Endelea kwa maneno: **shingoni, makonge** na **shanga.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **shanga, ngozi** na **utamaduni**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Mavazi ya zamani"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Babu na bibi zetu walivaa mavazi gani kiunoni?*** *(nguo za ngozi)*
2. ***Babu na bibi zetu walivaa mavazi gani miguuni?*** *(viatu vya miti, ngozi na makonge)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **ng** mara tatu.

ng ng ng

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo: **walivaa shanga za rangi; viatu vyao ni vya ngozi; wengine walibeba rungu**. Waambie wanafunzi wazinakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 16: Siku ya 3 na 4 **Mavazi**

Tamka sauti.

ng gh th

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng e | ng u | ng o | ng a |
| nge | ngu | ngo | nga |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| we ngi ne | shi ngo ni | ma ko nge | sha nga |
| wengine | shingoni | makonge | shanga |

Tamka sauti.

ng

Tamka sauti ya herufi na silabi

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng a | ng' a | g a | k a |
| nga | ng'a | ga | ka |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| vi li kuwa | ha wa ku vaa |
| vilikuwa | hawakuvaa |
| ya me badilika | wa li beba |
| yamebadilika | walibeba |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja -angu | wingi -etu |
|---|---|
| huyu ni baba yangu | hawa ni baba zetu. |
| huyu ni babu yangu | hawa ni mababu zetu. |
| huyu ni bibi yangu | hawa ni mabibi zetu. |
| huyu ni mama yangu | hawa ni mama zetu. |

78

Wiki ya 10: Siku ya 3 na 4 **Siku za Wiki**

Mtu aliyevalia suti amesimama juu ya gari lililofunguliwa dau. Amezingirwa na askari na anahutubia umati wa watu sokoni akitumia kipaza sauti.

**Ziara ya Rais**

Ilikuwa siku ya Jumatatu mwezi wa Januari Rais alipotutembelea. Rais wetu alikuja kijijini kukutana na raia.
Gari lake lilisimama barabarani.
Rais akasema, "Nawasihi mkae kwa amani na watu wote."
Siku hiyo, wanakijiji walikuwa na furaha sana.
Akimalizia ziara yake, mara tukasikia radi.
Watu wakatorokea madukani.
Kesho yake barabara ilikuwa imejaa maji.

49

### ▲ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi ni **ng**. Tamka sauti ya herufi **/ng/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ⬬ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **nga**. Sema kila sauti **/ng/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi **nga**. **[U]** Endelea kwa silabi: **ng'a, ga** na **ka.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **vi li kuwa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **vilikuwa** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **ya me badilika (yamebadilika), ha wa ku vaa (hawakuvaa), wa li beba (walibeba).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

[N/T/U] Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma sentensi kisha uzisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| **Umoja - angu** | | **Wingi - etu** |
|---|---|---|
| Huyu ni baba **yangu** | - | Hawa ni baba **zetu**. |
| Huyu ni babu **yangu** | - | Hawa ni mababu **zetu**. |
| Huyu ni bibi **yangu** | - | Hawa ni mabibi **zetu**. |
| Huyu ni mama **yangu** | - | Hawa ni mama **zetu**. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **shanga, ngozi** na **utamaduni**.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Mavazi ya zamani"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### ⟐ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Kuna tofauti ipi kati ya mavazi ya zamani na ya kisasa?*** *(ya kisasa hayazingatii utamaduni kama yale ya zamani)*
2. ***Ni mavazi gani yanaruhusiwa shuleni?*** *(sare za shule, nguo za michezo na mazoezi)*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye vifungu vifuatavyo. Wanafunzi waandike wingi wa vifungu hivyo.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **nguo ya ngozi** | **-** | **nguo za ngozi** |
| **ushanga wa rangi** | **-** | ______________ |
| **kiatu cha mti** | **-** | ______________ |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yaliyochanganywa: **zingo, ongu, kongema, ngasha**. Wanafunzi wayaandike maneno halisi kisha wawasomee wenzao: **Mfano:** ngira - rangi

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Wiki ya 16: Siku ya 5 **Mavazi**

Soma sauti.

ng gh

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: ngo zi **ngozi**.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| gha | sha | li | o | ngo | ra |
| nga | ru | ngu | zi | ngi | ndi |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

1. nili**kula** chumbani.
2. nili**cheza** uani.
3. nili**keti** ghalani.
4. nili**kimbia** shuleni.

Sehemu ya kuanika nguo. Wanawake wawili. Mmoja anafua nguo na mwingine anaanika.

**Mavazi ya mama Fatuma**

Fatuma alikuwa chumbani. Mvua ikaanza kunyesha kwa ghafla. Kukawa na gharika. Mama alikuwa ghalani akitoa nafaka. Mavazi yake yalikuwa uani. Nikakimbia na kutoa rinda, gauni, sketi, kamisi na blauzi ya mama. Kwa kawaida mavazi ya mama huwa ghali sana.

80

■ **Majina ya herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(ng)**. Tamka sauti ya herufi **/ng/**. **[U]** Endelea kwa herufi **(gh)**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

★ **Silabi**

**[N]** Soma silabi zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **ngo** na **zi** kuandika neno **ngozi**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

● **Sarufi**

**[N]** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. **[T]** Zisome sentensi pamoja na wanafunzi. Eleza jinsi ya kutumia vitenzi kama **kula**.**[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

Nili**kula** chumbani.
Nili**cheza** uani.
Nili**keti** ghalani.
Nili**kimbia** shuleni.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **gharika, ghalani** na **ghafla**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Mavazi ya Mama Fatuma"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Fatuma na mama walikuwa wapi?*** *(Fatuma alikuwa chumbani/Mama alikuwa ghalani akitoa nafaka).*
2. ***Eleza kilichotendeka?*** *(mvua ilinyesha/kukawa na gharika).*
3. ***Ni mavazi gani ya mama yalikuwa uani?*** *(rinda, gauni, sketi, kamisi na blausi ya mama.)*
4. ***Taja mavazi ambayo huvaliwa na wanaume?*** *(shati, suruali, soksi n.k)*

**Hadithi ya mwalimu**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. *(Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

**Nasibu abahatika**

Nasibu aliishi na jamii ya Kamau ijapokuwa yeye hakuwa mtoto wa Mzee Kamau. Mzee Kamau alikuwa na watoto kumi na wawili. (***Mzee Kamau alikuwa na watoto wangapi?***) Wote walikuwa wasichana. Mzee Kamau, aliamua kuwa Nasibu pia angerithi mali yake. Wale wasichana kumi na wawili wakakasirika sana. Wakaamua kuwa hawangemruhusu Nasibu kurithi mali ya baba yao.

Siku moja walianza kumtusi Nasibu. Usiku mmoja, watu wote walienda kulala. Watoto wa Kamau wakaona watafute njia ya kumfukuza Nasibu kutoka pale nyumbani kwao. Wakaenda mtoni. Wakajaza karai kumi na mbili za siafu. Kisha wakafungua dirisha na kummwagia Nasibu hao siafu.Siafu waligeuka kuwa pesa!(***Kwa nini wasichana hawa wakatumia siafu?)***

Asubuhi ilipofika, Nasibu akajikuta amefunikwa na noti za pesa chumbani mwake. Kisha akawaita wale wasichana waje wamsaidie kuzihesabu. Kutoka siku hiyo Nasibu alikuwa tajiri sana. (***Je, unafikiri wasichana hawa walifurahia bahati ya nasibu?***)

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiandika: **ghasia**, **gharama**, **ghali**, **ngozi**, **shanga**, **ngozi**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Eleza wanafunzi waendelee kuunda maneno zaidi wakitumia silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 17: Siku ya 1 na 2 — **Wanyama**

Tamka sauti.

**ng'** gh ng

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng' a | ng' i | ng' u | ng' o |
| **ng'a** | **ng'i** | **ng'u** | **ng'o** |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng'o mbe | ng'a mbo | Ng'a ng'a | se ng'e nge |
| **ng'ombe** | **ng'ambo** | **Ng'ang'a** | **seng'enge** |

Tamka sauti.

**ng'**

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng' a | ng a | ng' e | ng e |
| **ng'a** | **nga** | **ng'e** | **nge** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku hudhuria | a ka ng'oa |
| **kuhudhuria** | **akang'oa** |
| ku ng'a ra | a li nunua |
| **kung'ara** | **alinunua** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| ndama huyu ni mweusi | ndama hawa ni weusi. |
| nyati huyu ni mweusi | nyati hawa ni weusi. |
| duma huyu ni mweupe | duma hawa ni weupe. |
| ngamia huyu ni mweupe | ngamia hawa ni weupe. |

81

Wiki ya 17: Siku ya 1 na 2 — **Wanyama**

Mzee anavusha ng'ombe wawili wanene mto. Amevalia kofia, buti na ana fimbo ndefu.

**Ng'ang'a auza ng'ombe**

Ng'ang'a aliishi peke yake ng'ambo ya mto.
Siku moja, alitaka kuhudhuria maonyesho ya kilimo sokoni.
Siku hiyo alivaa nguo nyeupe za kung'ara.
Alipofika mtoni, aling'oa mti ili apime kina cha maji.
Alipovuka mto, Ng'ang'a aliuza ng'ombe wake.
Baadaye alinunua seng'enge na bidhaa mbalimbali.
Alirudi kwake akiwa na furaha nyingi.

82

### Ufahamu wa fonimu

N/T/U: Tamka sauti **/ng'/**. Taja neno **(ng'ombe)** huku wanafunzi wakifanya ishara waliokubaliana. **[U]**Endelea kwa maneno **seng'enge, ung'eng'e, *ng'ambo, ng'amua, ng'onda*** na ***ng'ang'ana.***

### Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **ng'**. Tamka sauti **/ng'/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **ng'a**. Sema kila sauti **/ng'/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi **ng'a**. **[U]** Endelea kwa silabi**: ng'i, ng'u** na **ng'o**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **ng'o mbe** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **ng'ombe**. **[U]** Endelea na maneno ***ng'ambo*, ng'ang'a** na **seng'enge**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kung'ara, ng'ambo** na **aling'oa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Ng'ang'a auza ng'ombe**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Ng'ang'a aliishi wapi?*** *(Ng'ang'a aliishi ng'ambo ya mto)*
2. ***Ng'ang'a alipofika ng'ambo ya mto alifanya nini?*** *(aliuza ng'ombe wake/alinunua bidhaa mbalimbali)*

### Kuandika

Waagize wanafunzi waandike herufi **ng'** mara tatu.

ng' ng' ng'

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno haya: **ng'ambo, akang'oa, zakung'ara, ng'ombe, seng'enge**. Waagize wanafunzi wayanakili. Kisha baadaye wawasomee wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kitu cha muhimu zaidi katika mradi wa KUSOMA ni kuhakikisha wanafunzi wote wanaweza kusoma vizuri wakimaliza mwaka huu. Je, umeweza kuwasaidia wasome vilivyo?

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 17: Siku ya 2

Wiki ya 17: Siku ya 1 na 2 **Wanyama**

Tamka sauti.

**ng'** **gh** **ng**

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng' a | ng' i | ng' u | ng' o |
| **ng'a** | **ng'i** | **ng'u** | **ng'o** |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng'o mbe | ng'a mbo | Ng'a ng'a | se ng'e nge |
| **ng'ombe** | **ng'ambo** | **Ng'ang'a** | **seng'enge** |

Tamka sauti.

**ng'**

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng' a | ng a | ng' e | ng e |
| **ng'a** | **nga** | **ng'e** | **nge** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku hudhuria | a ka ng'oa |
| **kuhudhuria** | **akang'oa** |
| ku ng'a ra | a li nunua |
| **kung'ara** | **alinunua** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| ndama huyu ni **mw**eusi | ndama hawa ni **w**eusi. |
| nyati huyu ni **mw**eusi | nyati hawa ni **w**eusi. |
| duma huyu ni **mw**eupe | duma hawa ni **w**eupe. |
| ngamia huyu ni **mw**eupe | ngamia hawa ni **w**eupe. |

81

Wiki ya 17: Siku ya 1 na 2 **Wanyama**

Mzee anavusha ng'ombe wawili wanene mto. Amevalia kofia, buti na ana fimbo ndefu.

**Ng'ang'a auza ng'ombe**

Ng'ang'a aliishi peke yake ng'ambo ya mto.
Siku moja, alitaka kuhudhuria maonyesho ya kilimo sokoni.
Siku hiyo alivaa nguo nyeupe za kung'ara.
Alipofika mtoni, aling'oa mti ili apime kina cha maji.
Alipovuka mto, Ng'ang'a aliuza ng'ombe wake.
Baadaye alinunua seng'enge na bidhaa mbalimbali.
Alirudi kwake akiwa na furaha nyingi.

82

### ▲ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi ni **ng'**. Tamka sauti ya herufi **/ng'/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ⬬ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **ng'a**. Sema kila sauti **/ng'/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi **ng'a**. **[U]** Endelea kwa silabi**: nga, ng'e** na **nge**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **ku hudhuria** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **kuhudhuria** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: ***ku ng'a ra* (*kung'ara*), a ka ngo'a (akango'a), a li nunua (alinunua).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

[N/T/U] Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma sentensi. **[T]** Zisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Ndama huyu ni **mwe**usi | - | Ndama hawa ni **we**usi. |
| Nyati huyu ni **mwe**usi | - | Nyati hawa ni **we**usi. |
| Duma huyu ni **mwe**upe | - | Duma hawa ni **we**upe. |
| Ngamia huyu ni **mwe**upe | - | Ngamia hawa ni **we**upe. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno ***kung'ara***, **akango'a** na **ng'ambo**.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **Ng'ang'a auza ng'ombe** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Nini kinaonyesha siku hiyo ilikuwa ya kufana?*** *(alirudi nyumbani akiwa na furaha sana)*
2. ***Kwa nini Ng'ang'a alinunua seng'enge?*** *(kuzungusha kwenye shamba lake)*

### ✍ Kuandika: Imla

Soma neno **ng'ombe**. Wanafunzi waliandike kisha wajadiliane kuhusu **ng'ombe, paka** na **mbuzi**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye vifungu vifuatavyo:

**nguo nyeusi**

**nguo nyeupe**

**nguo nyekundu**

Waambie wanafunzi wavinakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 17: Siku ya 3 na 4 — **Shuleni**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| i a | o a | e a | u a |
|---|---|---|---|
| **ia** | **oa** | **ea** | **ua** |

Soma silabi na maneno.

| a li zo e a | ha ku tii | a ka m zu i a |
|---|---|---|
| **alizoea** | **hakutii** | **akamzuia** |
| ku zo a | u o ngo | zo e a |
| **kuzoa** | **uongo** | **zoea** |

Soma sauti ya herufi na silabi.

| a o | u i | a e | a u |
|---|---|---|---|
| **ao** | **ui** | **ae** | **au** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| ha ku tii | a ka futwa |
|---|---|
| **hakutii** | **akafutwa** |
| a ka m zuia | a ka puuza |
| **akamzuia** | **akapuuza** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja -ake | wingi -ao |
|---|---|
| yule ni mwalimu wake | wale ni walimu wao. |
| yule ni mtumishi wake | wale ni watumishi wao. |
| yule ni mshirika wake | wale ni washirika wao. |

83

Wiki ya 17: Siku ya 3 na 4 — **Shuleni**

Mtu amelala chini ya mti na amefunika uso wake kwa kofia. Kando yake kuna ufagio, toroli (wheelbarrow) na reki. Nyasi ni refu sana.

**Juma Mvivu**

Juma alikuwa mfanyikazi shambani mwa shule. Msimamizi wake akasema, "Acha uvivu." Juma hakutii. Msimamizi akamzuia kuzoa takataka shambani. Juma akasema uongo ili apewe kazi yake tena. Msimamizi wake akasema asubiri uamuzi wa kamati ya shule. Juma bado alipuuza maagizo. Mwalimu mkuu alimfuta kazi.

84

### ■ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **ia**. Sema kila sauti **/i/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi **ia**. **[U]** Endelea kwa silabi **oa**, **ea** na **ua**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ● Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **a li zo e a**. kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **alizoea**. **[U]** Endelea kwa maneno: **hakutii**, **akamzuia**, **kuzoa**, **uongo** na **zoea.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mvivu**, **kamati** na **uongo**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Juma mvivu**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**.** **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Juma alikuwa amezoea kufanya nini?*** *(alizoea kuwa mvivu)*
2. ***Kwa nini Juma alisema uongo?*** *(alisema uongo ili arudishiwe kazi tena).*

### ✍ Kuandika

Waagize wanafunzi waandike silabi **oa**, **ea**, **ua**.

oa ea ua

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo:

**Juma alizoea kuwa mvivu.**

**Msimamizi alimzuia.**

**Juma alisema uongo.**

**Juma alipuuza maagizo.**

Waambie wanafunzi wazinakili. Baadaye wawasomee wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Ni muhimu kutathmini jinsi kila mwanafunzi anavyoendelea mara mbili kila muhula. Kusudi ni kuimarisha ufasaha wake wa kusoma na ufahamu. Kwa hivyo, ni bora kutathmini wanafunzi watatu kila siku.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 17: Siku ya 4

Wiki ya 17: Siku ya 3 na 4 **Shuleni**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| i a | o a | e a | u a |
| **ia** | **oa** | **ea** | **ua** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| a li zo e a | ha ku tii | a ka m zu i a |
| **alizoea** | **hakutii** | **akamzuia** |
| ku zo a | u o ngo | zo e a |
| **kuzoa** | **uongo** | **zoea** |

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a o | u i | a e | a u |
| **ao** | **ui** | **ae** | **au** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ha ku tii | a ka futwa |
| **hakutii** | **akafutwa** |
| a ka m zuia | a ka puuza |
| **akamzuia** | **akapuuza** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja -ake | wingi -ao |
|---|---|
| yule ni **m**walimu wake | wale ni **wa**limu wao. |
| yule ni **m**tumishi wake | wale ni **wa**tumishi wao. |
| yule ni **m**shirika wake | wale ni **wa**shirika wao. |

83

Wiki ya 17: Siku ya 3 na 4 **Shuleni**

Mtu amelala chini ya mti na amefunika uso wake kwa kofia. Kando yake kuna ufagio, toroli (wheelbarrow) na reki. Nyasi ni refu sana.

**Juma Mvivu**

Juma alikuwa mfanyikazi shambani mwa shule.
Msimamizi wake akasema, "Acha uvivu." Juma hakutii.
Msimamizi akamzuia kuzoa takataka shambani.
Juma akasema uongo ili apewe kazi yake tena.
Msimamizi wake akasema asubiri uamuzi wa kamati
ya shule. Juma bado alipuuza maagizo. Mwalimu mkuu
alimfuta kazi.

84

### ▲ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **ao**. Sema kila sauti **/a/ /o/** kisha uunganishe na kusema silabi **ao**. **[U]** Endelea kwa silabi **ae, au** na **ui.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ⬬ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **ha ku tii** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **hakutii** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **a ka m zuia (akamzuia), a ka futwa (akafutwa), a ka puuza (akapuuza).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Sarufi

[N/T/U] Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma sentensi kisha uzisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| **Umoja -ake** | | **Wingi -ao** |
|---|---|---|
| Yule ni **m**walimu wake | - | Wale ni **wa**limu wao. |
| Yule ni **m**tumishi wake | - | Wale ni **wa**tumishi wao. |
| Yule ni **m**shirika wake | - | Wale ni **wa**shirika wao. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **mvivu, uongo** na **kamati.**

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Juma mvivu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Kwa nini Juma alifutwa kazi?*** *(alipuuza maagizo ya kamati)*
2. ***Tunajifunza nini kutokana na hadithi hii?*** *(kuwa mvivu si vizuri/tufanye kazi kwa bidii/tusipuuze maagizo)*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye vifungu vifuatavyo. Wanafunzi waviandike kwa wingi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| msimamizi **wangu** | - | **wa**simamizi **wetu** |
| msimamizi **wako** | - | ____________ |
| msimamizi **wake** | - | ____________ |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yaliyochanganywa: **zoaku, ngouo, gizaamo, vivuu**. Waagize wanafunzi wayaandike maneno halisi. Kisha wawasomee wenzao. **Mfano**: zoaku - kuzoa

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 17: Siku ya 5 **Ndege na Wanyama**

Tamka sauti.

ng Ng'

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: si ki a **sikia**.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ng'o | ng'a | ki | a | ri | ma |
| mbo | mbe | si | sa | fa | nge |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| wakati uliopo | wakati uliopita |
|---|---|
| juma **ana**zoea | juma **ali**zoea |
| king'ori **ana**enda | king'ori **ali**enda |
| marangi **ana**elekea | marangi **ali**elekea |

Kuku ameangua mayai. Kifaranga mmoja ameshatoka kwenye yai. Wawili wanaendelea kutoka kwa mayai.

**Marangi aenda kwa King'ori**

Marangi alifunga safari kwenda kwa King'ori. Yeye na King'ori wakala mayai ya kukaanga. Walipomaliza, walielekea eneo la wazi kulikokuwa na maua. Walitoa mkeka na kuulalia. Waliwaona kuku waliokuwa wameangua vifaranga. Mwewe alipowakaribia, walimtimua.

85

### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(ng')**. Tamka sauti ya herufi **(ng)**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Silabi

**[N]** Soma silabi pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **si, ki** na **a** kuandika neno **sikia**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ● Sarufi

[N/T/U] Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma sentensi kisha uzisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

| **Wakati uliopo** | | **Wakati uliopita** |
|---|---|---|
| Juma **ana**zoea | - | Juma **ali**zoea |
| King'ori **ana**enda | - | King'ori **ali**enda |
| Marangi **ana**elekea | - | Marangi **ali**elekea |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kufunga safari**, **walimtimua** na **wameangua**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Marangi aenda kwa King'ori"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ◇ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Marangi alisafiri kuelekea wapi?*** *(aliend kwa King'ori)*
2. ***Marangi na King'ori walikula nini?*** *(walikula mayai ya kukaanga)*
3. ***Kwa nini walimtimua mwewe?*** *(mwewe alitaka kula vifaranga n.k)*
4. ***Je, unafikiri mayai waliyokula yalitoka wapi?*** *(mayai yalitoka kwa kuku/kuku alitaga mayai)*

### 🕮 Hadithi ya mwalimu

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. *(Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

**Lokono na Chatu**

Lokono aliamua kwenda kisimani kuchota maji aoge. Kisimani, akasikia sauti. Chatu alikuwa amekwama kisimani. Chatu alimwomba Lokono amsaidie. Lokono akamtoa Chatu kisimani. Walipotoka tu, Chatu akataka kumla Lokono. (***Lokono alienda kisimani kufanya nini?***)

Punde tu Ng'ombe akaja. Wakamuuliza Ng'ombe atoe uamuzi. Akasema, "Lokono hana wema. Kazi yake ni kukama maziwa na kula nyama ya ng'ombe. Afadhali aliwe na chatu."

Wakakutana na Punda wakamuuliza. Punda akasema, "Lokono hana wema. Humbebesha punda mizigo mingi bila kujali afya yake. Aliwe."

Baadaye wakakutana na Sungura. Sungura akasema angetaka kujua yaliyotokea. Lokono akaeleza kilichotokea. Sungura akawashauri warudi kwenye kisima. ***(Taja wanyama waliotajwa kwenye hadithi hii).***

Akamwambia chatu arudi ndani ya kisima ili apate kujua ni nini Lokono alichokifanya. Chatu alipoingia ndani ya kisima, Lokono na Sungura wakatoroka. (***Kati ya ng'ombe, punda na sungura, nani alikuwa rafiki ya Lokono?***)

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **nguo, ng'ambo, kung'ara, maagizo, uongo**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Eleza wanafunzi waendelee kuunda maneno zaidi wakitumia silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 18: Siku ya 1 na 2 — Darasani

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a o | i o | e e | u o |
| ao | io | ee | uo |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u ba o | mwe u si | ki cho nge o |
| ubao | mweusi | kichongeo |
| Ne re a | ki fu ti o | shi ka moo |
| Nerea | kifutio | shikamoo |

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| e o | o u | o i | o e |
| eo | ou | oi | oe |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a ki ingia | a na itwa |
| akiingia | anaitwa |
| hu mu amkua | hu tumia |
| humuamkua | hutumia |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| hiki ni kitabu cheusi. | hivi ni vitabu vyeusi. |
| hiki ni kifutio cheusi. | hivi ni vifutio vyeusi. |
| hiki ni kichongeo cheupe. | hivi ni vichongeo vyeupe. |
| hiki ni kitabu cheupe. | hivi ni vitabu vyeupe. |

86

Wiki ya 18: Siku ya 1 na 2 — Darasani

Darasani kuna madawati. Juu ya ubao kuna saa. Kando ya ubao kuna chati unayoonyesha maumbo. Mlango wa darasa umefungwa.

### Darasa la Maria

Maria yuko katika darasa la kwanza.
Mwalimu wake anaitwa Nerea.
Nerea akiingia darasani, wanafunzi humuamkua,
"Shikamoo?" Mwalimu hujibu, "Marahaba wanafunzi."
Darasa lao ni kubwa.
Kwenye kuta kuna saa ya duara na chati. Kwenye chati kuna michoro yenye maumbo mbalimbali. Kwa mfano, pembe tatu, mraba na duara.
Darasa lina ubao mweusi wa umbo la mstatili.
Mwalimu wao hutumia chaki kuandikia ubaoni.
Kila mwanafunzi huwa na kitabu, kalamu, kifutio na pia kichongeo.

87

■ **Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **ao**. Sema kila sauti **/a/ /o/.** Kisha uunganishe na kusema silabi **ao. [U]** Endelea kwa silabi **io, ee** na **uo.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

● **Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U: Tamka silabi **u ba o** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **ubao. [U]** Endelea na maneno: **mweusi, kichongeo, Nerea, kifutio** na **shikamoo.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kichongeo, kifutio** na **shikamoo**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya "**Darasa la Maria**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Wanafunzi humuamkua mwalimu vipi?*** *("shikamoo")*
2. ***Taja vitu ambavyo wanafunzi huwa navyo wakiwa darasani?*** *(kila mwanafunzi huwa na kitabu, kalamu, kifutio na kichongeo)*

**Kuandika**

Soma maneno **ubao, darasa** na **kwao** wanafunzi waandike.

ubao

darasa

kwao

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

Kamilisha somo kwa wimbo: **Nasikia sauti**.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **ubao, chati, kitabu, kalamu, kifutio, chaki**. Waambie wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wazazi wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati unapojitayarisha kwa somo, ni muhimu kusoma na kutafakari kuhusu vidokezo vya mwalimu kwenye mwongozo.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a o | i o | e e | u o |
| ao | io | ee | uo |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u ba o | mwe u si | ki cho nge o |
| ubao | mweusi | kichongeo |
| Ne re a | ki fu ti o | shi ka moo |
| Nerea | kifutio | shikamoo |

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| e o | o u | o i | o e |
| eo | ou | oi | oe |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a ki ingia | a na itwa |
| akiingia | anaitwa |
| hu mu amkua | hu tumia |
| humuamkua | hutumia |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| hiki ni kitabu cheusi. | hivi ni vitabu vyeusi. |
| hiki ni kifutio cheusi. | hivi ni vifutio vyeusi. |
| hiki ni kichongeo cheupe. | hivi ni vichongeo vyeupe. |
| hiki ni kitabu cheupe. | hivi ni vitabu vyeupe. |

86



Darasani kuna madawati. Juu ya ubao kuna saa. Kando ya ubao kuna chati unayoonyesha maumbo. Mlango wa darasa umefungwa.

**Darasa la Maria**

Maria yuko katika darasa la kwanza.
Mwalimu wake anaitwa Nerea.
Nerea akiingia darasani, wanafunzi humuamkua,
"Shikamoo?" Mwalimu hujibu, "Marahaba wanafunzi."
Darasa lao ni kubwa.
Kwenye kuta kuna saa ya duara na chati. Kwenye chati kuna michoro yenye maumbo mbalimbali. Kwa mfano, pembe tatu, mraba na duara.
Darasa lina ubao mweusi wa umbo la mstatili.
Mwalimu wao hutumia chaki kuandikia ubaoni.
Kila mwanafunzi huwa na kitabu, kalamu, kifutio na pia kichongeo.

87

### ▲ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **eo**. Sema kila sauti **/e//o/**. Kisha uunganishe na kusema silabi **eo**. **[U]** Endelea kwa silabi**: ou, oi, oe**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ⬬ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **a ki ingia** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **akiingia**. **[U]** Endelea kwa maneno: **hu mu amkua (humuamkua), a na itwa (anaitwa), hu tumia (hutumia)**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Sarufi

[N/T] Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma sentensi. Kisha uzisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Hiki ni **ki**tabu **che**usi | - | Hivi ni **vi**tabu **vye**usi. |
| Hiki ni **ki**futio **che**usi | - | Hivi ni **vi**futio **vye**usi. |
| Hiki ni **ki**chongeo **che**upe | - | Hivi ni **vi**chongeo **vye**upe. |
| Hiki ni **ki**tabu **che**upe | - | Hivi ni **vi**tabu **vye**upe. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **kichongeo, kifutio** na **shikamoo.**

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Darasa la Maria"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Mwalimu hujibu vipi wanafunzi wanaposema, "Shikamoo mwalimu."*** *(hujibu marahaba watoto)*
2. ***Taja vitu vingine vinavyopatikana darasani.*** *(dawati, kabati n.k)*

### ✍ Kuandika: Imla

Soma neno **kitabu**. Wanafunzi waliandike kisha wajadiliane kuhusu **kitabu, ubao, kalamu** na **kifutio**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo:

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **kitabu** | - | **vitabu** |
| **kifutio** | - | **vifutio** |
| **kichongeo** | - | **vichongeo** |
| **kiti** | - | **viti** |

Waambie wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 18: Siku ya 3 na 4 **Darasani**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| b a | d a | p a | b o |
| **ba** | **da** | **pa** | **bo** |

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| Ki o ko | ta bi a |
| **Kioko** | **tabia** |
| wa na tu li a | ki ra nja |
| **wanatulia** | **kiranja** |

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| b e | b u | p e | p u |
| **be** | **bu** | **pe** | **pu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li kusanya | a li hakikisha |
| **alikusanya** | **alihakikisha** |
| a li furahishwa | wa li po chagua |
| **alifurahishwa** | **walipochagua** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| wakati uliopo | wakati uliopita |
|---|---|
| anampenda | alimpenda |
| anafurahisha | alifurahisha |
| anahakikisha | alihakikisha |
| anachagua | alichagua |

88

Wiki ya 18: Siku ya 3 na 4 **Darasani**

Wanafunzi wamepiga foleni. Mmoja wao anawahutubia huku ameshika kitabu mkononi.

**Kiranja wetu**

Kioko alikuwa kiranja wa darasa la kwanza.
Alihakikisha wanafunzi wanatulia darasani.
Alikusanya na kumsaidia mwalimu kubeba vitabu vya wanafunzi.
Kabla ya mwalimu kuingia darasani, Kioko alihakikisha wanafunzi wametulia.
Mwalimu alifurahishwa na kazi ya Kioko.
Wanafunzi pia walimpenda kwani alikuwa na tabia nzuri.
Kila walipochagua kiranja, Kioko alichaguliwa.

89

## ■ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **ba**. Sema kila sauti **/b/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi **ba. [U]** Endelea kwa silabi: **da**, **pa**, **bo**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

## ● Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **Ki o ko** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **Kioko**. **[U]** Endelea kwa maneno: **wanatulia**, **tabia** na **kiranja**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

## Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **tabia nzuri, kiranja** na **kuchaguliwa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

## Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **kiranja wetu** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

## Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Kioko alikuwa kiranja wa darasa gani?*** *(alikuwa kiranja wa darasa la kwanza)*
2. ***Kwa nini Kioko alichaguliwa kama kiranja kila wakati?*** *(wanafunzi walimpenda/kioko alikuwa na tabia nzuri)*

## Kuandika: Imla

Soma maneno yafuatayo mara mbili kisha wanafunzi waandike.

| |
|---|
| wanatulia |
| tabia |
| kiranja |
| ubao |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

## Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo:

**Kioko alikuwa kiranja.**

**Kioko alichaguliwa.**

**Kioko humbebea mwalimu vitabu.**

Waagize wanafunzi wazinakili. Baadaye wawasomee wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Ni wajibu wa mwalimu kuhakikisha anawapongeza wanafunzi kila wakati wanapojibu maswali sahihi. Pia ni muhimu kusaidia wale wanaokosa kutoa jibu sahihi na kuwatia moyo.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 18: Siku ya 3 na 4 **Darasani**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| b a | d a | p a | b o |
| **ba** | **da** | **pa** | **bo** |

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| Ki o ko | ta bi a |
| **Kioko** | **tabia** |
| wa na tu li a | ki ra nja |
| **wanatulia** | **kiranja** |

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| b e | b u | p e | p u |
| **be** | **bu** | **pe** | **pu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li kusanya | a li hakikisha |
| **alikusanya** | **alihakikisha** |
| a li furahishwa | wa li po chagua |
| **alifurahishwa** | **walipochagua** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| wakati uliopo | wakati uliopita |
|---|---|
| anampenda | alimpenda |
| anafurahisha | alifurahisha |
| anahakikisha | alihakikisha |
| anachagua | alichagua |

88

Wiki ya 18: Siku ya 3 na 4 **Darasani**

Wanafunzi wamepiga foleni. Mmoja wao anawahutubia huku ameshika kitabu mkononi.

### Kiranja wetu

Kioko alikuwa kiranja wa darasa la kwanza.
Alihakikisha wanafunzi wanatulia darasani.
Alikusanya na kumsaidia mwalimu kubeba vitabu vya wanafunzi.
Kabla ya mwalimu kuingia darasani, Kioko alihakikisha wanafunzi wametulia.
Mwalimu alifurahishwa na kazi ya Kioko.
Wanafunzi pia walimpenda kwani alikuwa na tabia nzuri.
Kila walipochagua kiranja, Kioko alichaguliwa.

89

**▲ Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **be**. Sema kila sauti **/b/ /e/** kisha uunganishe na kusema silabi **be**. **[U]** Endelea kwa silabi: **bu, pe** na **pu.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**⬬ Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **a li kusanya** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **alikusanya** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **a li hakikisha (alihakikisha), a li furahishwa (alifurahishwa) wa li po chagua (walipochagua).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**★ Sarufi**

[N/T] Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma maneno. Kisha uyasome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| Wakati uliopo | Wakati uliopita |
|---|---|
| **ana**mpenda | **ali**mpenda |
| **ana**furahisha | **ali**furahisha |
| **ana**nakikisha | **ali**hakikisha |
| **ana**chagua | **ali**chagua |

**📖 Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **tabia nzuri, kiranja** na **kuchaguliwa** .

**📖 Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Kiranja wetu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**.** **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

**◈ Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Kazi ya kiranja wa darasa ni nini?*** *(kuhakikisha kuwa wanafunzi wametulia/kualiandika majina ya watu wapigao kelele)*
2. ***Je, kiranja wenu anafanya kazi gani?*** *(wanafunzi walijibu wakieleza kazi mbalimbali za kiranja)*

**✍ Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Kisha wanafunzi wayaandike katika wakati uliopita.

| Wakati uliopo | | Wakati uliopita |
|---|---|---|
| anampenda | - | alimpenda |
| anahakikisha | - | __________ |
| anachagua | - | __________ |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yaliyochanganywa: **ticha, njakira, atabi, limwamu**. Waagize wanafunzi wayaandike maneno halisi kisha wawasomee wenzao.

**Kwa mfano:** radasa - darasa

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

# Wiki ya 18: Siku ya 5

Wiki ya 18: Siku ya 5 **Darasani**

Soma sauti za herufi na silabi.

i a — **ia**   o o — **oo**   i o — **io**   e a — **ea**   u a — **ua**

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: u ba o - **ubao**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| o | ba | bu | li | mu |
| pi | u | ki | ta | bi |
| da | ti | wa | fu | cha |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

1. judi ali**soma** kitabu.
2. rono ali**chonga** penseli.
3. njoki ali**futa** ubao.
4. bari ali**chora** chati.

Wanafunzi wameketi kwenye zulia. Kuna redio iliyowekwa juu ya stuli.

**Somo la wanyama**

Ijumaa iliyopita, wanafunzi wa darasa la kwanza walisoma kuhusu wanyama. Mwalimu alitumia chati ya wanyama kufunzia somo hilo. Kwenye chati kulichorwa ngamia, kondoo, ng'ombe, mbuzi na jimbi au jogoo. Wanafunzi waliimba wimbo kuhusu wanyama tofauti. Baadaye mwalimu aliwaletea redio. Wakasikiza somo la redio. Wanafunzi walifurahi sana.

90

### ■ Kusoma silabi

N/T/U: Andika herufi **ia**. Sema kila sauti **/i/ /a/** kisha uunganishe na kusema **ia**. **[U]** Endelea kwa herufi**: ia, oo, io, ea,** na **ua**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Silabi

**[N]** Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **u**, **ba** na **o** kuandika neno **ubao**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U. Soma sentensi hizi na ueleze wanafunzi jinsi ya kutumia vitenzi vyepesi katika sentensi. Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

**Sentensi**
Judi **ali**soma kitabu.
Rono **ali**chonga penseli.
Njoki **ali**futa ubao.
Bari **ali**chora chati.

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **chati, ngamia** na **jimbi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Somo la Wanyama"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Ijumaa iliyopita wanafunzi walisoma kuhusu nini?*** *(walisoma kuhusu wanyama)*
2. ***Taja wanyama waliochorwa kwenye chati.****(ngamia, kondoo, ng'ombe, mbuzi na jogoo)*
3. ***Ni wanyama gani wengine ambao hufugwa nyumbani?*** *(kuku, nguruwe n.k)*
4. ***Ni wimbo gani wa wanyama unaoujua?*** *(watoto waimbe nyimbo za wanyama kwa muda mfupi)*

### 🕮 Hadithi ya mwalimu

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. *(Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

**Mgeni darasani**

Siku moja, mgeni alitembelea darasa letu. Mwalimu wetu akampa Kendi nafasi ili amtajie mgeni vitu mbalimbali pale darasani. Pia amueleze manufaa ya kila kitu. Mwanzo Kendi akataja ubao na kusema hutumiwa kutufundishia mambo mbalimbali. Baadaye alitaja kifutio cha kufuta maandishi ubaoni. (***Kendi alitaja vitu gani?***)

Halafu mwalimu akampa Kiptoo nafasi ataje vitu zaidi. Kiptoo alitaja meza ya mwalimu pamoja na kiti chake. Vilevile akataja madawati na viti vya wanafunzi. (***Viti vya wanafunzi hutumiwa kufanya nini?***) Akamuelezea mgeni kuwa tunavitumia kukalia na kuandikia.

Alimuonyesha kabati iliyoko pale nyuma ya darasa. Akasema mwalimu pamoja wanafunzi huweka vitabu pale viwe salama. Kisha akataja vitabu mbalimbali ambavyo anapenda kuvisoma. (***Nitajieni vitabu ambavyo mnapenda kuvisoma.***)

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **ubao, kifutio, tabia, darasa, kiranja, vitabu, chati, ngamia, jimbi.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Eleza wanafunzi waendelee kuunda maneno zaidi wakitumia silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 19: Siku ya 1 na 2 — **Sokoni**

Tamka sauti.

m t s p

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | a | e |
| ta | sa | pa | me |
| mta | msa | mpa | mme |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m ku li ma | mi go mba | cha mbo |
| **mkulima** | **migomba** | **chambo** |
| m vu vi | Ka je mbe | mi e mbe |
| **mvuvi** | **Kajembe** | **miembe** |

Tamka sauti.

m f b k v

Soma silabi hizi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | u | u |
| fa | ba | ku | vu |
| mfa | mba | mku | mvu |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li penda | a li tumia |
| **alipenda** | **alitumia** |
| a li kuwa | a li ji funga |
| **alikuwa** | **alijifunga** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| huyu ni **m**zee | hawa ni **wa**zee. |
| huyu ni **m**kulima | hawa ni **wa**kulima. |
| huyu ni **m**vuvi | hawa ni **wa**vuvi. |
| huyu ni **mwa**limu | hawa ni **wa**limu. |
| huyu ni **mwa**nafunzi | hawa ni **wa**nafunzi. |

91

Wiki ya 19: Siku ya 1 na 2 — **Sokoni**

Mzee aliyevaa kilemba ameketi kando ya mto. Ameshikilia ndoano. Kando yake kuna ndoo iliyo na samaki.

**Kajembe**

Mzee Kajembe aliishi katika kijiji cha Mbalambala.
Kajembe alikuwa mkulima na mvuvi hodari sana. Kila siku alijifunga kilemba na kuelekea mtoni.
Akiwa mtoni, Kajembe alipenda kuimba na kucheza na firimbi yake.
Mto huo ulikuwa na samaki na mamba wengi sana.
Mara nyingi alitumia chambo na fimbo kuvua samaki.
Pia alikuwa na shamba la migomba na miembe.
Mzee Kajembe husafirisha samaki hadi sokoni. Kule sokoni yeye huuza samaki kwa wateja wengi.

92

■ **Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **m**. Tamka sauti **/m/**. **[U]** Endelea na herufi **t, s** na **p**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

● **Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **a**. Soma sauti hiyo **/a/.** Ongeza sauti **/t/** kisha uunganishe na kusema silabi **ta**. Ongeza sauti **/m/** kisha uunganishe na kusema silabi **mta**. **[U]** Endelea kwa silabi **a, sa, msa; a, pa, mpa; e, me, mme.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

▬ **Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U: Tamka silabi **m ku li ma** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mkulima**. **[U]** Endelea na maneno: **migomba, chambo, mvuvi, Kajembe** na **miembe.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **migomba, chambo** na **mamba**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya "**Kajembe**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Taja mimea ambayo Kajembe alipanda.*** *(migomba, miembe, mbaazi)*
2. ***Alitumia nini kuvua samaki?*** *(alitumia fimbo na chambo)*

**Kazi ya Kuandika: Imla**

Soma maneno yafuatayo kisha wanafunzi wayaandike:

| |
|---|
| chambo |
| mvuvi |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **mgomba, chambo, mvuvi, mkulima, mamba**. Waambie wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 19: Siku ya 1 na 2 — Sokoni

Tamka sauti.

m t s p

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | a | e |
| ta | sa | pa | me |
| mta | msa | mpa | mme |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m ku li ma | mi go mba | cha mbo |
| mkulima | migomba | chambo |
| m vu vi | Ka je mbe | mi e mbe |
| mvuvi | Kajembe | miembe |

Tamka sauti.

m f b k v

Soma silabi hizi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | u | u |
| fa | ba | ku | vu |
| mfa | mba | mku | mvu |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li penda | a li tumia |
| alipenda | alitumia |
| a li kuwa | a li ji funga |
| alikuwa | alijifunga |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| huyu ni **m**zee | hawa ni **wa**zee. |
| huyu ni **m**kulima | hawa ni **wa**kulima. |
| huyu ni **m**vuvi | hawa ni **wa**vuvi. |
| huyu ni **mwa**limu | hawa ni **wa**limu. |
| huyu ni **mwa**nafunzi | hawa ni **wa**nafunzi. |

91

Wiki ya 19: Siku ya 1 na 2 — Sokoni

Mzee aliyevaa kilemba ameketi kando ya mto. Ameshikilia ndoano. Kando yake kuna ndoo iliyo na samaki.

Kajembe

Mzee Kajembe aliishi katika kijiji cha Mbalambala.
Kajembe alikuwa mkulima na mvuvi hodari sana. Kila siku alijifunga kilemba na kuelekea mtoni.
Akiwa mtoni, Kajembe alipenda kuimba na kucheza na firimbi yake.
Mto huo ulikuwa na samaki na mamba wengi sana.
Mara nyingi alitumia chambo na fimbo kuvua samaki.
Pia alikuwa na shamba la migomba na miembe.
Mzee Kajembe husafirisha samaki hadi sokoni. Kule sokoni yeye huuza samaki kwa wateja wengi.

92

▲ **Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **m**. Tamka sauti **/m/**. **[U]** Endelea na herufi **f, b, k** na **v.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

⬬ **Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **a**. Soma sauti hiyo **/a/.** Ongeza sauti **/f/** kisha uunganishe na kusema silabi **fa**. Ongeza sauti **/m/** kisha uunganishe na kusema silabi **mfa**. **[U]** Endelea kwa silabi:**a, ba, mba; u, ku, mku; u, vu, mvu.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **a li penda** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **alipenda** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **a li tumia (alitumia), a li kuwa (alikuwa), a li ji funga (alijifunga).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

◆ **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma sentensi. Kisha uzisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Huyu ni **m**zee | Hawa ni **wa**zee |
| Huyu ni **m**kulima | Hawa ni **wa**kulima |
| Huyu ni **m**vuvi | Hawa ni **wa**vuvi |
| Huyu ni **mwa**limu | Hawa ni **wa**limu |
| Huyu ni **mwa**nafunzi | Hawa ni **wa**nafunzi |

🕮 **Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **migomba, chambo** na **mamba**.

🕮 **Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Kajembe"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

◈ **Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Ni vifaa gani hutumiwa shambani?*** *(Upanga/Reki/Sururu).*
2. ***Unafikiri ni kwa nini kajembe alijifunga kilemba?*** *(kwa sababu ya jua wakati akilima/Alipenda kufunga kilemba n.k.)*

✍ **Kuandika:**

Soma neno **mgomba**. Wanafunzi waliandike kisha wajadiliane kuhusu **mgomba, mamba, firimbi, jembe**.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye vifungu vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **mzee huyu** | - | **wazee hawa** |
| **mkulima huyu** | - | **wakulima hawa** |
| **mvuvi huyu** | - | **wavuvi hawa** |

Waambie wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

# Wiki ya 19: Siku ya 3

Wiki ya 19: Siku ya 3 na 4 — **Sokoni**

Tamka sauti.

n d j z

Soma silabi hizi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | a | e |
| da | ja | za | de |
| **nda** | **nja** | **nza** | **nde** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ki ba nda | hu pe nda | bo nde |
| **kibanda** | **hupenda** | **bonde** |
| ki wa nda | ma a nda zi | ki na nda |
| **kiwanda** | **maandazi** | **kinanda** |

Tamka sauti.

t m ch b

Soma silabi hizi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | i | i |
| ta | ba | ti | chi |
| **nta** | **mba** | **mti** | **nchi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| i li yo kuwa | ku li kuwa |
| **iliyokuwa** | **kulikuwa** |
| zi li zo shika | ni li enda |
| **zilizoshika** | **niliendo** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| hili ni bonde | haya ni **ma**bonde. |
| hili ni andazi | haya ni **ma**andazi. |
| hili ni gari | haya ni **ma**gari. |
| hili ni banda | haya ni **ma**banda. |

93

Wiki ya 19: Siku ya 3 na 4 — **Sokoni**

Msichana anatembea njia yenye matope kuelekea nyumbani.

## Kaka Banda

Ndugu yangu Banda anaishi kwenye kibanda karibu na bonde la nzi, karibu na soko la Suswa.
Banda hufanya kazi katika kiwanda cha mwananchi.
Kila asubuhi yeye hupenda kula maandazi kwa supu ya kunde. Yeye hupata vyakula hivi sokoni.
Juzi nilienda nyumbani kwake.
Huko niliona kitanda, kinanda na kalenda iliyokuwa na picha ya bundi. Vifaa hivi vilitengenezwa na rafiki yake Janda. Janda ni fundi maarufu huko Bondeni. Kule Bondeni kulikuwa na matope yaliyoshikana kama gundi.

94

### ■ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **n**. Tamka sauti **/n/**. **[U]** Endelea na herufi: **d, j** na **z**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ● Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **a**. Soma sauti hiyo **/a/**. Ongeza sauti **/d/** kisha uunganishe na kusema silabi **da**. Ongeza sauti **/n/** kisha uunganishe na kusema silabi **nda**. **[U]** Endelea kwa silabi: **a, ja, nja; a, za, nza; e, de, nde**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ▬ Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **ki ba nda** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **kibanda**. **[U]** Endelea na maneno: **kiwanda, hupenda, maandazi, bonde** na **kinanda.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **bonde, kalenda** na **gundi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Kaka Banda**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Banda hula nini kila asubuhi?*** *(Maandazi na supu ya kunde)*
2. ***Nyumbani kwa Banda kuna vitu gani?*** *(Kuna kinanda, kitanda, kalenda)*

### Kuandika

Soma maneno yafuatayo kisha wanafunzi wayaandike.

| |
|---|
| bonde |
| gundi |
| maandazi |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo:

**Atieno alipitia karibu na bonde.**
**Kalenda hii inapendeza.**
**Kibanda chake ni kidogo sana.**
**Maandazi haya ni matamu sana.**

Waagize wanafunzi wazinakili. Baadaye wawasomee wenzao:

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Tamka sauti.

n d j z

Soma silabi hizi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | a | e |
| da | ja | za | de |
| nda | nja | nza | nde |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ki ba nda | hu pe nda | bo nde |
| kibanda | hupenda | bonde |
| ki wa nda | ma a nda zi | ki na nda |
| kiwanda | maandazi | kinanda |

Tamka sauti.

t m ch b

Soma silabi hizi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | i | i |
| ta | ba | ti | chi |
| nta | mba | mti | nchi |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| i li yo kuwa | ku li kuwa |
| iliyokuwa | kulikuwa |
| zi li zo shika | ni li enda |
| zilizoshika | nilienda |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| hili ni bonde | haya ni mabonde. |
| hili ni andazi | haya ni maandazi. |
| hili ni gari | haya ni magari. |
| hili ni banda | haya ni mabanda. |

93



Msichana anatembea njia yenye matope kuelekea nyumbani.

**Kaka Banda**

Ndugu yangu Banda anaishi kwenye kibanda karibu na bonde la nzi, karibu na soko la Suswa.
Banda hufanya kazi katika kiwanda cha mwananchi.
Kila asubuhi yeye hupenda kula maandazi kwa supu ya kunde. Yeye hupata vyakula hivi sokoni.
Juzi nilienda nyumbani kwake.
Huko niliona kitanda, kinanda na kalenda iliyokuwa na picha ya bundi. Vifaa hivi vilitengenezwa na rafiki yake Janda. Janda ni fundi maarufu huko Bondeni. Kule Bondeni kulikuwa na matope yaliyoshikana kama gundi.

94

▲ **Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **t**. Tamka sauti **/t/**. **[U]** Endelea na herufi: **m, ch** na **b**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

● **Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **a**. Soma sauti hiyo **/a/.** Ongeza sauti **/t/** kisha uunganishe na kusema silabi **ta**. Ongeza sauti **/n/** kisha uunganishe na kusema silabi **nta. [U]** Endelea kwa silabi: **a, ba, mba; i, ti, mti; i, chi, nchi.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **i li yo kuwa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **iliyokuwa**. **[U]** Endelea kwa maneno: **zi li zo shika (zilizoshika), ku li kuwa (kulikuwa), ni li enda (nilienda).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

◆ **Sarufi**

**[N]** Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma sentensi. **[T]** Zisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Hili ni bonde | - | Haya ni **ma**bonde. |
| Hili ni andazi | - | Haya ni **ma**andazi. |
| Hili ni gari | - | Haya ni **ma**gari. |
| Hili ni banda | - | Haya ni **ma**banda. |

📖 **Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **bonde, kalenda** na **gundi**.

📖 **Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Kaka Banda"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Unafikiria vitu alivyokuwa navyo banda hutumiwa kufanyia nini?*** *(kinanda-kuchezea muziki/kitanda-kulalia/kalenda-kujua tarehe).*
2. ***Kwa nini Banda aliishi kwenye kibanda karibu na bonde?*** *(kwa sababu hakuwa na pesa za kutosha/kwa sababu hapo ndipo kwao n.k.)*

✍ **Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatazo kisha wanafunzi wayaandike mwa wingi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| bonde | - | mabonde |
| gari | - | ____________ |
| banda | - | ____________ |
| pipa | - | ____________ |
| pera | - | ____________ |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yaliyochanganywa: **ndebo, lendaka, ndigu, ndazimaa, nandaki**. Waambie wanafunzi wayaandike maneno halisi. Kisha wawasomee wenzao. **Mfano:** ndebo - bonde

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 19: Siku ya 5 — Sokoni

Tamka sauti.

ng gh

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: ngo zi **ngozi**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| gha | sha | li | o | ngo | ra |
| nga | fo | ngu | fa | zi | ngi |
| ndi | ghe | gho | ru | ni | mbu |

Sarufi: Soma maneno haya.

| neno | matumizi ya "ni" |
|---|---|
| uwanja | uwanjani |
| nyumba | nyumbani |
| shamba | shambani |
| kiwanda | kiwandani |

Fundi ameketi chini akishona viatu.

### Umuhimu wa Mbuzi

Mbuzi ni mnyama mwenye manufaa mengi kwa wafugaji. Mbolea ya mbuzi ni nzuri kwa ukulima. Ngozi ya mbuzi hutumiwa kutengenezea viatu na mikoba. Mbuzi wa kike hutoa maziwa yanayofaidi mwili wa binadamu. Nyama yake ni tamu sana. Watu wengine huchoma na kupika nyama ya mbuzi. Wengine huwauza sokoni ili kupata pesa. Ni muhimu sana kutunza mbuzi na wanyama wote wa kufugwa.

95

#### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi majina ya herufi ndogo na kubwa **(ng)**. Tamka sauti ya herufi **/ng/gh/**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

#### ★ Silabi

**[N]** Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **ngo** na **zi** kuandika neno **ngozi**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia silabi. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

#### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U. Soma maneno haya ukionyesha jinsi ya kutumia **ni** kuonyesha mahali. Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

| **Neno** | | **mahali** |
|---|---|---|
| Uwanja | - | uwanja**ni** |
| Nyumba | - | nyumba**ni** |
| Shamba | - | shamba**ni** |
| Kiwanda | - | kiwanda**ni** |

#### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **manufaa,mbolea** na **kutunza**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

#### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Umuhimu wa mbuzi**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

#### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Mbuzi ni mnyama ambaye hufaidi nani?*** *(mbuzi hufaidi wafugaji)*
2. ***Ni manufaa gani ambayo mbuzi hutupa?*** *(wanafunzi watoe majibu mbalimbali)*
3. ***Ni mnyama gani mwingine ambaye hutupa nyama?*** *(ngombe, kondoo, sungura n.k)*
4. ***Tunaweza kutunza vipi wanyama wa kufugwa?*** *(kuwalisha vyema, kuwapa maji, kuwapa dawa n.k.)*

#### 🕮 Hadithi ya mwalimu

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. (*Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

### Panya Nyumbani

Baada ya kutoka safari, Karimi na mamake walikuta godoro, mto na foronya zimeliwa na panya. Walishangaa sana wakajiuliza, “Huyu ni panya wa namna gani ambaye anakula hata godoro?” (***Je, wangapi wanajua panya?***)

Wakatamani kunywa chai. Hapo ndipo mama ya Karimi akachemsha maji jikoni. Wakati maji yakiendelea kuchemka, wakaona ni heri wamtafute huyo panya. Karimi akachukua mwiko na mamake akachukua upanga. Kabla waanze kutafuta Karimi akamwambia mamake, “Ni lazima tutafute mwanya alioingilia panya.”(***Mama alichukua nini kumtafutia panya?***)

Wakazunguka nyumba nzima. Mara wakaona shimo kubwa ambalo hata mtoto mchanga anaweza kuingilia. Mamake Karimi akasema, “Hata kama huyo panya ni mkubwa kiasi gani, hawezi kutushinda. Sisi tuko na mwiko na upanga.” (***Je, unafikiri Karimi na mamake walimuua panya?***)

#### ✍ Kuandika – Imla:

Soma maneno haya huku wanafunzi wakiyaandika: **nguo, ng’ambo, kung’ara, nyeupe, maagizo, uongo.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

#### Kazi ya ziada

Eleza wanafunzi waendelee kuunda maneno zaidi wakitumia silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 20: Siku ya 1 na 2 — **Sokoni**

Tamka sauti.

y v p

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | o | a | u |
| ya | yo | ya | yu |
| vya | vyo | pya | vyu |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| vi pya | o vyo o vyo | vyu ma |
| vipya | ovyoovyo | vyuma |
| vyu ngu | m guu | pi ngu |
| vyungu | mguu | pingu |

Tamka sauti.

m f p

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | |
|---|---|---|
| a | a | a |
| ya | ya | ya |
| mya | fya | pya |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li m funga | i ka mu umiza |
| walimfunga | ikamuumiza |
| ha ku tarajia | wa ka fyatua |
| hakutarajia | wakafyatua |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| huyu ni mtu mzuri | hawa ni watu wazuri. |
| huyu ni mbuzi mzuri | hawa ni mbuzi wazuri. |
| huyu ni mnyama mbaya | hawa ni wanyama wabaya. |
| huyu ni kondoo mbaya | hawa ni kondoo wabaya. |

96

Wiki ya 20: Siku ya 1 na 2 — **Dukani**

Kuna mwanamume anachungulia akiwa nyuma ya dirisha lenye vyuma.

**Jambazi akamatwa**

Oga alikuwa jambazi hatari.
Aliiba vitu vipya na kuviuza ovyoovyo.
Siku moja, Oga aliingia dukani kimyakimya na kuiba vyuma na vyungu vya dhahabu.
Alipoingia tu, king'ora kikaanza kulia.
Oga hakutarajia hayo.
Akaanza kutoroka. Polisi wakafyatua risasi ikamuumiza mguu.
Wakamkamata na kumpeleka hospitalini.
Baadaye walimfunga pingu na kumfungia seli.

97

### ■ Jina la herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **y.** Tamka sauti **/y/.** Endelea kwa herufi **v, p**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ● Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **a**. Soma sauti hiyo **/a/.** Ongeza herufi **y** kisha uunganishe na kusema silabi **ya**. Ongeza herufi **v** kisha uunganishe na kusema silabi **vya. [U]** Endelea kwa silabi: **o, yo, vyo; a, ya, pya; u, yu, vyu.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ▬ Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **vi pya** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **vipya**. **[U]** Endelea na maneno **ovyoovyo, vyuma, vyungu, mguu** na **pingu.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **dhahabu, king'ora** na **fyatua**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Jambazi akamatwa**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

*i.* **Nani alikuwa jambazi sugu?** *(Oga)*
*ii.* **Oga aliiba nini?** *(vyungu na vyuma vya dhahabu)*
*iii.* **Polisi walimpeleka wapi Oga?** *(hospitalini)*

### Kuandika: Imla

Soma maneno haya kisha wanafunzi wayaandike.

| |
|---|
| vipya |
| vyuma |
| oga |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **vipya, ovyoovyo, kimya, vyuma, vyungu, king'ora**. Waagize wanafunzi waandike kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Wiki ya 20: Siku ya 1 na 2 — Sokoni

Tamka sauti.

y v p

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | o | a | u |
| ya | yo | ya | yu |
| vya | vyo | pya | vyu |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| vi pya | o vyo o vyo | vyu ma |
| vipya | ovyoovyo | vyuma |
| vyu ngu | m guu | pi ngu |
| vyungu | mguu | pingu |

Tamka sauti.

m f p

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | |
|---|---|---|
| a | a | a |
| ya | ya | ya |
| mya | fya | pya |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li m funga | i ka mu umiza |
| walimfunga | ikamuumiza |
| ha ku tarajia | wa ka fyatua |
| hakutarajia | wakafyatua |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| huyu ni mtu mzuri | hawa ni watu wazuri. |
| huyu ni mbuzi mzuri | hawa ni mbuzi wazuri. |
| huyu ni mnyama mbaya | hawa ni wanyama wabaya. |
| huyu ni kondoo mbaya | hawa ni kondoo wabaya. |

96

Wiki ya 20: Siku ya 1 na 2 — Dukani

Kuna mwanamume anachungulia akiwa nyuma ya dirisha lenye vyuma.

Jambazi akamatwa

Oga alikuwa jambazi hatari.
Aliiba vitu vipya na kuviuza ovyoovyo.
Siku moja, Oga aliingia dukani kimyakimya na kuiba vyuma na vyungu vya dhahabu.
Alipoingia tu, king'ora kikaanza kulia.
Oga hakutarajia hayo.
Akaanza kutoroka. Polisi wakafyatua risasi ikamuumiza mguu.
Wakamkamata na kumpeleka hospitalini.
Baadaye walimfunga pingu na kumfungia seli.

97

**▲ Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **m**. Tamka sauti **/m/**. Endelea kwa herufi **f** na **p.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**⬬ Kusoma silabi**

N/T/U: Andika herufi **a**. Soma sauti hiyo **/a/.** Ongeza herufi **y** kisha uunganishe na kusema silabi **ya**. Ongeza herufi **m** kisha uunganishe na kusema silabi **mya**. **[U]** Endelea kwa silabi: **a, ya, fya; a, ya, pya.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**★ Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa li m funga** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **walimfunga**. **[U]** Endelea na maneno: **ha ku tarajia (hakutarajia), i ka mu umiza (ikamuumiza), wa ka fyatua (wakafyatua).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**◆ Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U. Soma sentensi hizi. Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Huyu ni **m**tu **m**zuri | - | Hawa ni **wa**tu **wa**zuri. |
| Huyu ni mbuzi **m**zuri | - | Hawa ni mbuzi **wa**zuri. |
| Huyu ni **m**nyama **m**baya | - | Hawa ni **wa**nyama **wa**baya. |
| Huyu ni kondoo **m**baya | - | Hawa ni kondoo **wa**baya. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **dhahabu, king'ora** na **fyatua**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi **"Jambazi akamatwa"** wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome kwa vikundi vya wawili wawili.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

i. ***Je, unafikiri kwa nini Oga aliingia dukani kimyakimya?*** *(hakutaka watu wajue/alikuwa mwizi)*
ii. ***Je, unafikiri polisi walifanya jambo jema kufyatua risasi?*** *(ndio au la - wanafunzi watoe sababu)*
iii. ***Je, ungekuwa wewe ungempeleka Oga hospitalini?*** *(ndio au la - wanafunzi watoe sababu)*

**Kuandika: Imla**

Wanafunzi wayaandike sawa maneno haya **bastola** na **bunduki** wanafunzi wayaandike kisha wajadiliane kuhusu bastola na bunduki. (mwalimu awaonyeshe wanafunzi modeli ya bunduki na bastola)

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie kadi za breli zenye maneno yafuatayo:

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| mtu | - | watu |
| mzuri | - | wazuri |
| mnyama | - | wanyama |
| mbaya | - | wabaya |

Waagize wanafunzi wayanakili. Baadaye wawasomee wenzao:

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 20: Siku ya 3 na 4 **Mazingira**

Soma sauti.

w k t b

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | a | a |
| wa | wa | wa | wa |
| kwa | twa | mwa | bwa |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m bwa | m ku bwa | mi chu ngwa |
| mbwa | mkubwa | michungwa |
| bwa wa | ku nywa | ja ngwa ni |
| bwawa | kunywa | jangwani |

Soma sauti.

w sh z ny ng

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | a | a |
| wa | wa | wa | wa |
| shwa | zwa | nywa | ngwa |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a ki bweka | i li po pulizwa |
| akibweka | ilipopulizwa |
| a ka tuzwa | a ka twa a |
| akatuzwa | akatwaa |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mbwa huyu ni mkubwa | mbwa hawa ni wakubwa. |
| mamba huyu ni mkubwa | mamba hawa ni wakubwa. |
| mbwa huyu ni mkali | mbwa hawa ni wakali. |
| mnyama huyu ni mdogo | wanyama hawa ni wadogo. |

98

Wiki ya 20: Siku ya 3 na 4 **Mazingira**

Vijana ambao wamevalia sare za kufanana wakikimbia njiani huku mmoja wao ameinua mwenge.

### Mashindano ya mbio

Punde tu firimbi ilipopulizwa, Sanaipei alipewa mwenge ndipo tukaanza mbio. Mbio zilianza uwanjani, kupitia mtoni kuelekea jangwani.
Njiani tuliona michungwa, miembe na mipera.
Pia tuliona mbwa mkubwa akibweka karibu na bwawa la maji.
Tulitamani kunywa maji, kwa sababu tulihisi kiu.
Mwalimu akatuambia bwawa lilikuwa na mamba wengi.
Tukatoroka kuelekea jangwani.
Sanaipei akawa wa kwanza.
Akatuzwa medali ya dhahabu.

99

■ **Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Wakumbushe wanafunzi jina la herufi **w.** Tamka sauti **/w/**. Endelea kwa **k, t** na **b**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

● **Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **/a/**. Soma sauti **/a/**. Ongeza sauti **/w/** kisha uunganishe na kusema silabi **wa**. Ongeza sauti **/k/** kisha uunganishe na kusema silabi **kwa**. **[U]** Endelea kwa silabi: **a, wa, twa; a, wa, mwa; a, wa, bwa**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

▬ **Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U: Tamka silabi **m bwa** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mbwa**. **[U]** Endelea na maneno **mkubwa, michungwa, bwawa, kunywa** na **jangwani.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **jangwani, mwenge** na **bwawa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya "**Mashindano ya mbio**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

*i.* **Sanaipei alipewa nini ndipo mbio zikaanza?** (mwenge)

*ii.* **Njiani wakimbiaji waliona nini?** (michungwa, mbwa akibweka)

*iii.* **Sanaipei alituzwa nini?** (medali ya dhahabu)

**Kuandika: Imla**

Soma maneno kisha wanafunzi wayaandike.

| |
|---|
| mkubwa |
| mwenge |
| bwawa |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo:

i. **Tuliona michungwa.**
ii. **Tuliona mbwa mkubwa.**
iii. **Tuliona bwawa la maji.**
iv. **Tulitamani kunywa maji.**

Wanafunzi wazinakili. Baadaye wawasomee wenzao:

Tarehe: ________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Wiki ya 20: Siku ya 3 na 4 — **Mazingira**

Soma sauti.

w k t b

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | a | a |
| wa | wa | wa | wa |
| kwa | twa | mwa | bwa |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m bwa | m ku bwa | mi chu ngwa |
| mbwa | mkubwa | michungwa |
| bwa wa | ku nywa | ja ngwa ni |
| bwawa | kunywa | jangwani |

Soma sauti.

w sh z ny ng

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | a | a |
| wa | wa | wa | wa |
| shwa | zwa | nywa | ngwa |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a ki bweka | i li po pulizwa |
| akibweka | ilipopulizwa |
| a ka tuzwa | a ka twa a |
| akatuzwa | akatwaa |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mbwa huyu ni mkubwa | mbwa hawa ni wakubwa. |
| mamba huyu ni mkubwa | mamba hawa ni wakubwa. |
| mbwa huyu ni mkali | mbwa hawa ni wakali. |
| mnyama huyu ni mdogo | wanyama hawa ni wadogo. |

98

Wiki ya 20: Siku ya 3 na 4 — **Mazingira**

Vijana ambao wamevalia sare za kufanana wakikimbia njiani huku mmoja wao ameinua mwenge.

### Mashindano ya mbio

Punde tu firimbi ilipopulizwa, Sanaipei alipewa mwenge ndipo tukaanza mbio. Mbio zilianza uwanjani, kupitia mtoni kuelekea jangwani.

Njiani tuliona michungwa, miembe na mipera.

Pia tuliona mbwa mkubwa akibweka karibu na bwawa la maji.

Tulitamani kunywa maji, kwa sababu tulihisi kiu.

Mwalimu akatuambia bwawa lilikuwa na mamba wengi.

Tukatoroka kuelekea jangwani.

Sanaipei akawa wa kwanza.

Akatuzwa medali ya dhahabu.

99

▲ **Jina la herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **w**. Tamka sauti **/W/**. Endelea na **sh, z, ny** na **ng.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

⬬ **Kusoma silabi**

N/T/U: Andika herufi **a**. Soma sauti hiyo **/a/.** Ongeza sauti **/w/** kisha uunganishe na kusema silabi **wa**. Ongeza sauti **/sh/** kisha uunganishe na kusema silabi **shwa**. **[U]** Endelea kwa silabi: **a, wa, zwa; a, wa, nywa; a, wa, ngwa.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **a ki bweka** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **akibweka**. **[U]** Endelea na maneno: **a ka tuzwa (akatuzwa), i li po pulizwa (ilipopulizwa), a ka twambia (akatwambia).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

◆ **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U. Soma sentensi hizi. Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Mbwa huyu ni **m**kubwa | - | Mbwa hawa ni **wa**kubwa. |
| Mamba huyu ni **m**kubwa | - | Mamba hawa ni **wa**kubwa. |
| Mbwa huyu ni **m**kali | - | Mbwa hawa ni **wa**kali. |
| Mnyama huyu ni **m**dogo | - | Wanyama hawa ni **wa**dogo. |

📖 **Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **jangwani, mwenge** na **bwawa**.

📖 **Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi "**Mashindano ya mbio**" wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome kwa vikundi vya wawili wawili.

Mwalimu achague wanafunzi wawili wasimulie hadithi waliyoisoma.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

i. ***Kwa nini mwalimu aliwakataza kunywa maji?*** *(kwa sababu mamba ni hatari sana)*

ii. ***Kwa nini walitamani kunywa maji?*** *(walikuwa na kiu/ walihisi kiu)*

iii. ***Je, ungekuwa wa kwanza ungetamani zawadi gani?*** *(medali, kikombe, pesa n.k)*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye vifungu vifuatavyo kisha wanafunzi waviandike kwa wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| mbwa mkubwa | mbwa wakubwa |
| mamba mdogo | ____________ |
| mnyama mkali | ____________ |

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yaliyochanganywa kisha wanafunzi waandike maneno halisi. Baadaye wasomee wenzao. **mfano:** ngwanija - jangwani

**ngwanija, ngemwe, bwamku, wabwa, nzakwa.**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 20: Siku ya 5 **Usafi na Afya**

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: che nza - chenza

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ku | mbwa | ma | ngu | che | wa | nza | ngwa |
| nywa | vyu | na | bwa | chu | zwa | ja | shwa |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| hiki ni chumba kidogo | hivi ni vyumba vidogo. |
| hiki ni cheti kikubwa | hivi ni vyeti vikubwa. |
| hiki ni choo kirefu | hivi ni vyoo virefu. |
| hiki ni chakula kingi | hivi ni vyakula vingi. |

Msichana na mvulana wameshikilia vifyekeo wakipanguza jasho. Wako kwa sehemu yenye nyasi ndefu.

**Mvua ya mawe**

Siku moja, kulinyesha mvua ya mawe. Watoto wakafurahia kumumunya na kuchezea barafu kimyakimya. Barafu iliwaletea kikohozi. Mama akawasikia watoto wakikohoa. Akawaita nyumbani. Akawapa adhabu ya kufyeka nyasi. Walifyeka nyasi hadi vipaji vyao vikajaa jasho. Baadaye waliomba msamaha. Pia waliahidi kuwa hawangerudia kosa hilo tena.

100

★ **Silabi**

Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. **[N]** Tumia silabi **che** na **nza** kuandika neno **chenza.** **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

● **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U. Soma sentensi hizi. Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Hiki ni **ch**umba kidogo | - | Hivi ni **vy**umba vidogo. |
| Hiki ni **ch**eti kikubwa | - | Hivi ni **vy**eti vikubwa. |
| Hiki ni **ch**oo kirefu | - | Hivi ni **vy**oo virefu. |
| Hiki ni **ch**akula kingi | - | Hivi ni **vy**akula vingi. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kumumunya, kufyeka** na **barafu**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya "**Mvua ya mawe"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

***i.*** ***Watoto walifurahi kufanya nini?*** *(walifurahia kumumunya na kucheza na barafu)*
***ii.*** ***Barafu iliwaletea watoto nini?*** *(iliwaletea kikohozi)*
***iii.*** ***Kwa nini watoto walitokwa na jasho?*** *(walifanya kazi ngumu/walifyeka nyasi)*
***iv.*** ***Nini kilichofanyika baadaye?*** *(waliomba msamaha, waliahidi kutorudia makosa hayo tena)*

**Hadithi ya mwalimu**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. *(Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

**Tumbili na Simba**

Ulikuwa wakati wa mwezi wa Juni. Kulikuwa na baridi kali sana. Tumbili alijificha pangoni akaanza kula ndizi. (***Tumbili alifanya nini?***) Muda si muda, Simba naye akaingia mle pangoni. Tumbili akaona maisha yake yamo hatarini. Simba huenda akamla. Akafikiria sana. Mara akapata jibu.

Simba alipomuona tumbili akanguruma, "Grrrrr! Warowarowao!"Tumbili akashika paa la pango na kusema, "Simba, nisaidie kushika hili paa. Harakisha! Linaanguka! Huoni nimeacha ndizi zangu? Tusipofanya hivyo litatuangukia sote tufe." (***Unafikiri simba alimuamini Tumbili?***)

Simba akanyosha miguu yake na kulishika paa. Kisha Tumbili akamwambia, "Simba, wewe una nguvu kuliko mimi. Naomba uendelee kushika hili paa. Nitaenda kuleta gogo ili tutumie kushikilia paa la pango."

Simba, kwa upumbavu, akaendelea kushika paa. Tumbili huyo, akakimbilia kichakani na hakurudi pale pangoni tena. Toka siku hiyo Simba anamtafuta Tumbili.(***Kwa nini Simba anamtafuta Tumbili?***)

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara tatu huku wanafunzi wakiandika: **mvua, kimya, fyeka, vyao, mumunya, vipaji.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Eleza wanafunzi waendelee kuunda maneno zaidi wakitumia silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 21: Siku ya 1 **Shuleni**

Soma sauti.

p f v sh

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: shu le - **shule**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| shu | vu | pa | m | fu |
| ka | jaa | a | pi | le |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| darasa moja | 1 | madarasa sita | 6 |
| | | madarasa matano | 5 |
| kanisa moja | 1 | makanisa mawili | 2 |
| | | makanisa saba | 7 |

Kuna shule na sehemu moja iko na mabati yaliyong'oka.
Kuna bendera inapepea mbele ya madarasa.

**Paa la shule yetu**

Kuna shule moja tu kijijini mwetu.
Wiki jana, upepo mkali uliharibu paa la darasa letu.
Hivi sasa, sote tunasomea kanisani.
Lakini shida hii ni ya muda mfupi tu.
Mheshimiwa mbunge wetu, ametuma bahasha ya pesa.
Wazazi nao watakuja kesho shuleni kuchanga pesa zaidi.
Watanunua vifaa na kurekebisha paa hilo.

101

**Vidokezo vya Mwalimu**

Wakati wa kufunza msamiati, unaweza kutumia lugha inayoeleweka na wanafunzi. Pia vitu halisi, picha na maelezo pamoja na kutumia neno kwenye sentensi ni mbinu itakayowasaidia wanafunzi kuelewa vyema.

### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(p)**. Tamka sauti ya herufi **/p/**. **[U]** Endelea kwa herufi **f, v** na **sh.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Silabi

**[N]** Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **shu** na **le** kuandika neno **shule**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U. Soma maneno yote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| darasa moja | 1 | madarasa sita | 6 |
| | | madarasa matano | 5 |
| kanisa moja | 1 | makanisa mawili | 2 |
| | | makanisa saba | 7 |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **paa, bahasha** na **vifaa.** Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Paa la shule yetu**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

- ***i. Upepo mkali uliharibu sehemu gani ya nyumba?*** *(paa)*
- ***ii. Wiki jana kulifanyika nini?*** *(upepo mkali uliharibu paa la darasa)*
- ***iii. Wazazi watakuja shuleni kufanya nini?*** *(watanunua vifaa, watarekebisha paa la shule)*

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **bahasha, shule, shida, mfupi, kijijini, mbunge.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Waambie wanafunzi waandike maneno matano zaidi kutokana na silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** na wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 21: Siku ya 2 **Usafi na Afya**

Soma sauti.

ny dh ch th

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: che ma - **chema**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| che | ta | si | nyo | na |
| ma | cha | ku | m | ka |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

1. kitabu kiko **juu ya** meza. 2. kiatu kiko **chini ya** kiti.

Msichana mdogo amevaa sare ya shule. Amebeba mfuko. Amesimama huku akionekana mchangamfu.

Chebet

Chebet ni msichana nadhifu. Yeye havai nguo za bei ghali. Anatamani saa ya dhahabu inayometameta kama nyota. Kila siku Chebet huoga na kuchana nywele mara moja, mbili, hata tatu. Yeye habaki nyuma kwa usafi, masomo na michezo. Vilevile, yeye hula lishe bora. Anajua uchafu unaweza kumdhuru. Kila mara akitoka chooni, Chebet hunawa mikono mara nyingi.

102

**Vidokezo vya Mwalimu**

Wakati wa kusoma hadithi (zamu yangu), hakikisha kuwa unasoma kwa mwendo wako na sio mwendo wa wanafunzi ili waweze kuelewa. Ni kwa njia hii pia wanafunzi watajua jinsi ya kusoma kwa haraka.

### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **(ny)**. Tamka sauti ya herufi **/ny/**. **[U]** Endelea kwa herufi **dh, ch** na **th.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **che,** na **ma** kuandika neno **chema**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome majibu katika ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U. Soma maswali haya. Eleza wanafunzi jinsi ya kutumia vihusishi kama **kando ya**. Uliza maswali yafuatayo.

**Kitabu kiko wapi?**

**Kiatu kiko wapi?**

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **nadhifu, ghali** na **lishe**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Chebet"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

*i.* ***Chebet hakuvaa nguo za aina gani?*** *(nguo za bei ghali)*

*ii.* ***Chebet alioga mara ngapi?*** *(mara moja, mbili na tatu/ mara nyingi)*

*iii.* ***Chebet alifanya nini akitoka chooni?*** *(hunawa mikono mara nyingi sana)*

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili kwa sauti huku wanafunzi wakiandika: **Chebet, nadhifu, ghali, lishe, michezo, dhahabu.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Waambie wanafunzi waandike maneno matano zaidi kutokana na silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** na wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 21: Siku ya 3 na 4 — Jinsia

Soma sauti.

gh ng ng'

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: si ku - **siku**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| gha | me | tu | ku | a |
| si | wa | li | gha | ni |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja - **hii** | wingi - **hizi** |
|---|---|
| nyumba **hii** ya ghorofa | nyumba **hizi** za ghorofa. |
| bendera **hii** imezeeka | bendera **hizi** zimezeeka. |
| pazia **hii** ni ghali | pazia **hizi** ni ghali. |
| sakafu **hii** ni chafu | sakafu **hizi** ni chafu. |

Wanaume wawili na wanawake wawili wamevalia nadhifu. Mwanamke mmoja anafungua mlango wenye rangi ya kijani kibichi huku wenzake wakishangilia.

### Nyumba ya ghorofa

Mwakio alisema, "Nyumba hii ya ghorofa imezeeka. Lakini pazia hii ni ghali na maua haya yanang'ara. Bendera inayopepea kwenye paa ilitoka ng'ambo." Aliendelea, "Leo ni siku ya kung'ang'ania ugavana. Nitautoa ufunguo huu kwa yule atakayeshinda." Kendi alishinda. Akapewa ufunguo. Akafungua nyumba na kutulia mezani, huku watu wakishangilia.

103

**Vidokezo vya Mwalimu**

Mwalimu mzuri ni yule anayechukua mda kujiyatarisha kabla ya somo. Ni vizuri kuliangalia somo kabla ya kulifunza. Kujitayarisha vyema kunafanya somo liwe zuri na la kupendeza.

### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi. Tamka sauti ya herufi **/gh/**. **[U]** Endelea kwa herufi **ng** na **ng'**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Soma silabi zote zilizo kurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **si,** na **ku** kuandika neno **siku**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U. Soma sentensi hizi.

| Umoja - hii | Wingi - hizi |
|---|---|
| Nyumba **hii** ni ya ghorofa | Nyumba **hizi** ni za ghorofa. |
| Bendera **hii** imezeeka | Bendera **hizi** zimezeeka. |
| Pazia **hii** ni ghali | Pazia **hizi** ni ghali. |
| Sakafu **hii** ni chafu | Sakafu **hizi** ni chafu. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **ghorofa, ng'ara** na **ng'ang'ania**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Nyumba ya ghorofa"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

- ***i.*** ***Kiilu alisema nyumba ilikuwa vipi?*** *(imezeeka)*
- ***ii.*** ***Bendera ilitoka wapi?*** *(ilitoka ng'ambo)*
- ***iii.*** ***Kendi aliposhinda alifanya nini?*** *(alifungua nyumba na kutulia)*

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya kwa sauti huku wanafunzi wakiandika: **ghorofa, zulia, ng'ara, kiilu, udiwani, bendera.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Waambie wanafunzi waandike maneno matano zaidi kutokana na silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** na wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 21: Siku ya 3 na 4 **Sokoni**

Tamka sauti.

**m** **b** **n** **d**

Soma sauti ya herufi na silabi.

m b a n d a n d e n d i

**mba** **nda** **nde** **ndi**

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: nda ni - **ndani**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ndi | tu | zi | nda | li |
| le | mba | ni | ye | mu |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja -angu | wingi -etu |
|---|---|
| **hiki** ni **ki**tanda changu. | **hivi** ni **vi**tanda vyetu. |
| **hiki** ni **ki**banda changu. | **hivi** ni **vi**banda vyetu. |
| **hiki** ni **ki**wanda changu. | **hivi** ni **vi**wanda vyetu. |
| **hiki** ni **ki**faa changu. | **hivi** ni **vi**faa vyetu. |

Mwanamume akiwa nje ameshika kifaa cha kutengenezea vyombo vya mbao. Kando yake kuna kiti na kabati. Pia kuna kisanduku, msumeno na nyundo.

**Fundi hodari**

Mjomba wangu ni fundi hodari sana. Alianza kazi yake punde tu alipotoka India. Yeye ana ujuzi wa kujenga nyumba, vibanda vya duka na hata viwanda. Pia mjomba huunda vitanda, meza hata na kabati. Katika ujenzi wake, yeye hutumia vifaa kama vile nyundo, misumeno, misumari, randa na gundi.

104

**Vidokezo vya Mwalimu**
Ni wajibu wa mwalimu kuhakikisha anawapongeza wanafunzi kila wakati wanapojibu maswali sahihi. Pia ni muhimu kusaidia wale wanaokosa kutoa jibu sahihi na kuwatia moyo.

### ■ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **m**. Tamka sauti ya herufi **/m/**. **[U]** Endelea kwa herufi **b, n** na **d.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ★ Silabi

**[N]** Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **nda** na **ni** kuandika neno **ndani**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U. Soma sentensi zote.

| **Umoja -angu** | | **Wingi -etu** |
|---|---|---|
| **Hiki** ni **ki**tanda changu. | - | **Hivi** ni **vi**tanda vyangu. |
| **Hiki** ni **ki**banda changu. | - | **Hivi** ni **vi**banda vyangu. |
| **Hiki** ni **ki**wanda changu. | - | **Hivi** ni **vi**wanda vyangu. |
| **Hiki** ni **ki**faa changu. | - | **Hivi** ni **vi**faa vyangu. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **hodari, randa,** na **gundi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Fundi hodari"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ⟐ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

*i.* ***Mjomba alianza kazi lini?*** *(alianza kazi punde tu alopotoka India)*

*ii.* ***Ana ujuzi wa kujenga nini?*** *(ana ujuzi wa kujenga nyumba, vibanda na viwanda)*

*iii.* ***Katika ujenzi wake yeye hutumia nini?*** *(hutumia vifaa kama nyundo, randa, misumeno na misumari)*

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili kwa sauti huku wanafunzi wakiandika: **bendera, kibanda, alishinda, waya, sebuleni.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Waambie wanafunzi waandike maneno matano zaidi kutokana na silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** na wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 21: Siku ya 5

Wiki ya 21: Siku ya 5 **Vyakula**

Tamka sauti.

| w | sh | t | m |
|---|---|---|---|

Tamka silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | e | a | e |
| wa | we | wa | we |
| shwa | gwe | twa | mwe |

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: shwa ri - **shwari**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| shwa | nga | twa | i | ma |
| po | ha | nda | ri | we |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| ini liko wapi? | maini yako wapi? |
| andazi liko wapi? | maandazi yako wapi? |
| dirisha liko wapi? | madirisha yako wapi? |
| pengo liko wapi? | mapengo yako wapi? |

Mama akiwa ndani ya chumba. Kuna vitanda viwili. Kwa kitanda kimoja kuna mvulana na kwa kingine kuna msichana ambao wameamka. Mama amesimama katikati ya vitanda.

**Asubuhi**

Asubuhi na mapema tuliitwa na mama. Anga ilikuwa shwari. Jua lilikuwa limechomoza. Mama akatwambia tuende kupatia kuku wishwa na kufungia mbwa. Tukamwambia mama kuwa hatujapata kiamshakinywa. Hapo ndipo mama alitupatia mkate mweupe. Kisha tukanywa chai kwa maharagwe. Tuliposhiba tukaelekea nje na kufanya kazi tuliyopewa na mama.

105

■ **Majina ya herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **w**. Tamka sauti ya herufi **/w/**: Endelea kwa: **sh, t** na **m**. Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

★ **Silabi**

**[N]** Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **shwa** na **ri** kuandika neno **shwari**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia silabi kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

● **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U. Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Ini liko wapi? | - | Maini yako wapi? |
| Andazi liko wapi? | - | Maandazi yako wapi? |
| Dirisha liko wapi? | - | Madirisha yako wapi? |
| Pengo liko wapi? | - | Mapengo yako wapi? |

🕮 **Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **shwari, chomoza** na **wishwa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

🕮 **Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya "**Asubuhi**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

◈ **Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

*i.* ***Mama alitutuma tufanye nini?*** *(kupatia kuku wishwa/ kufungia mbwa)*

*ii.* ***Mama alitupatia mkate wa rangi gani?*** *(mkate mweupe, chai, maharagwe)*

*iii.* ***Baada ya kiamsha kinywa watoto walifanya nini?*** *(walielekea nje/walifanya kazi waliyopewa na mama)*

🕮 **Hadithi ya mwalimu**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Hadithi hii ni ya mwalimu. Eleza wanafunzi kuwa utawauliza maswali baada ya kusoma hadithi. *(Mara ya kwanza mwalimu ataisoma hadithi bila kikomo. Mara ya pili mwalimu ataisoma hadithi huku akiuliza wanafunzi maswali.)*

**Kima na Papa**

Hapo zamani za kale, Kima alifanya urafiki na Papa. Siku moja Papa na Kima wakakutana karibu na bahari. Papa akamsihi Kima aende kumtembelea kule kwao anakoishi baharini. Kima alikubali. (***Papa aliishi wapi?***)

Papa akambeba Kima mgongoni wakaanza safari baharini. Walipofika katikati ya bahari Papa akasema, “Rafiki yangu Kima, Malkia wetu ni mgonjwa na inasemekana dawa yake ni moyo wa Kima!” Kima akatabasamu na kujibu, “Rafiki yangu, ili kumsaidia Malkia wenu, ni lazima turudi kwa ghala ya mioyo ya kima tumchukulie moyo.” (***Je, unafikiri Papa alikuwa akisema ukweli?***)

Papa akamrudisha Kima kando ya bahari. Kwa haraka Kima aliruka na kutoroka.

Papa akauliza, “Vipi rafiki yangu?” Huku akiwa amekasirika. Kima akamjibu, “Uongo haufai. Wewe ulitaka kuniua.” Kutoka siku hiyo urafiki wa Kima na Papa ukaisha. ***(Je, ungekuwa Kima ungemuamini Papa?)***

✍ **Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili kwa sauti huku wanafunzi wakiyaandika: **kinanda, bendera, ghorofa, ng'ara, udiwani, dhahabu, nadhifu, mfupi, mbunge, bahasha.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Waambie wanafunzi waandike maneno matano zaidi kutokana na silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** na wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

Soma sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| b u | ch u | d u | f u |
| **bu** | **chu** | **du** | **fu** |

Soma s labi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| du ka ni | su ka ri | ma ja ni |
| **dukani** | **sukari** | **majani** |
| m ka te | mi che zo | cha i |
| **mkate** | **michezo** | **chai** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li m tembelea | a ka mu uliza |
| **alimtembelea** | **akamuuliza** |
| ni li vyo ku tuma | li li po tua |
| **nilivyokutuma** | **lilipotua** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **wakati uliopita** | **wakati ujao** |
|---|---|
| naitore alimtembelea | naitore atamtembelea. |
| babu alimuuliza | babu atamuuliza. |
| mama alituamsha | mama atatuamsha. |
| omari aliugua | omari ataugua. |





Wasichana wawili na wavulana wawili wako kwa uwanja. Mvulana mmoja anaruka kamba, wenzake wakimtazama.

### Dukani

Siku moja, Naitore alimtembelea babu yake kijijini. Babu akamtuma Naitore dukani. Babu alitaka aletewe sukari, majani chai na mkate. Njiani, Naitore alikutana na marafiki wake. Walifurahi kuonana. Wakacheza michezo mbalimbali. Naitore akasahau kwenda dukani. Jua lilipotua, Naitore alirudi kwa babu. Babu akamuuliza, "Naitore, unatoka wapi? Wapi vitu nilivyokutuma?" Naitore alishtuka, "Oo, babu! Samahani. Nilicheza njiani hata nikasahau kufika dukani. Sitafanya hivyo tena"



**Kusoma silabi**

N/T/U: Andika silabi **bu**. Sema kila sauti **/b//u/** kisha uunganishe na kusema silabi **bu**. **[U]** Endelea kwa silabi **chu, du** na **fu.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U: Tamka silabi **du ka** na **ni** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **dukani**. **[U]** Endelea kwa maneno **sukari, majani, mkate, michezo** na **chai.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **jua lilipotua, samahani** na **alishtuka**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Dukani"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Babu alimtuma Naitore nini?*** *(alimtuma alete sukari, majani chai na mkate)*
2. ***Eleza mambo ambayo Naitore alifanya na rafiki zake.*** *(walicheza michezo mbali mbali)*
3. ***Naitore aliporudi nyumbani alimwambiaje babu?*** *(Oo, babu, samahani! Nilicheza njiani hata nikasahau. Sitafanya hivyo tena.)*

**Kuandika: Imla**

Soma maneno haya huku wanafunzi wakiyaandika: **dukani, sukari, majani, chai, mchezo, mkate, samahani.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wanafunzi waandike maneno walioyaandika darasani tena kisha wawasomee wenzao: **dukani, sukari, majani, chai, mchezo, mkate, samahani.**

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kabla ya kusoma hadithi mwalimu huzungumza kuhusu msamiati, husoma kichwa cha hadithi, hujadili picha na wanafunzi hatimaye hutoa utabiri.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Wiki ya 22: Siku ya 1 na 2 — Sokoni/Dukani

Soma sauti na silabi.

| b u | ch u | d u | f u |
|---|---|---|---|
| **bu** | **chu** | **du** | **fu** |

Soma s labi na maneno.

| du ka ni | su ka ri | ma ja ni |
|---|---|---|
| **dukani** | **sukari** | **majani** |
| m ka te | mi che zo | cha i |
| **mkate** | **michezo** | **chai** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li m tembelea | a ka mu uliza |
|---|---|
| **alimtembelea** | **akamuuliza** |
| ni li vyo ku tuma | li li po tua |
| **nilivyokutuma** | **lilipotua** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **wakati uliopita** | **wakati ujao** |
|---|---|
| naitore a**li**mtembelea | naitore a**ta**mtembelea. |
| babu a**li**muuliza | babu a**ta**muuliza. |
| mama a**li**tuamsha | mama a**ta**tuamsha. |
| omari a**li**ugua | omari a**ta**ugua. |

106

Wiki ya 22: Siku ya 1 na 2 — Sokoni/Dukani

Wasichana wawili na wavulana wawili wako kwa uwanja. Mvulana mmoja anaruka kamba, wenzake wakimtazama.

## Dukani

Siku moja, Naitore alimtembelea babu yake kijijini. Babu akamtuma Naitore dukani. Babu alitaka aletewe sukari, majani chai na mkate. Njiani, Naitore alikutana na marafiki wake. Walifurahi kuonana. Wakacheza michezo mbalimbali. Naitore akasahau kwenda dukani. Jua lilipotua, Naitore alirudi kwa babu. Babu akamuuliza, "Naitore, unatoka wapi? Wapi vitu nilivyokutuma?" Naitore alishtuka, "Oo, babu! Samahani. Nilicheza njiani hata nikasahau kufika dukani. Sitafanya hivyo tena"

107

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **a li m tembelea** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **alimtembelea** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **a ka mu uliza (akamuuliza), ni li vyo ku tuma (nilivyokutuma), li li po tua (lilipotua).**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| **Wakati uliopita** | | **Wakati ujao** |
|---|---|---|
| Naitore a**li**mtembelea | - | Naitore a**ta**mtembelea. |
| Babu a**li**muuliza | - | Babu a**ta**muuliza. |
| Mama a**li**tuamsha | - | Mama a**ta**tuamsha. |
| Omari a**li**ugua | - | Omari a**ta**ugua. |

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **lilipotua/jua lilipotua**, **samahani** na **alishtuka**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Dukani"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Kwa nini Naitore alishtuka?*** *(kwa sababu alikuwa amesahau)*
2. ***Unafikiri Babu alifanya nini baada ya Naitore kuomba msamaha?*** *(alimsamehe)*
3. ***Unafikiri Naitore na rafiki zake walicheza michezo gani?*** *(kati, kalongo n.k)*

### Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi na maneno: **sukari, majani, mkate** na **samahani**. Wanafunzi watumie maneno hayo kukamilisha sentensi walizopewa.

i. Babu alitaka aletewe sukari.
ii. Babu alitaka aletewe __________.
iii. Babu alitaka aletewe __________.
iv. Naitore akasema __________.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **alimtembelea, anamuuliza, alimtuma, anakutana**. Waambie wanafunzi wayanakili. Baadaye watunge sentensi wakitumia maneno hayo kisha wawasomee wenzao:

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 22: Siku ya 3

Wiki ya 22: Siku ya 3 na 4 — **Shuleni**

Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| s u | sh u | v i | f i |
| **su** | **shu** | **vi** | **fi** |

Tamka silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| su ru a li | wa si cha na | ma shu ja a |
| **suruali** | **wasichana** | **mashujaa** |
| so k si | b la u zi | s ke ti |
| **soksi** | **blauzi** | **sketi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu wa ambia | wana funzi |
| **huwaambia** | **wanafunzi** |
| i na itwa | ma shujaa |
| **inaitwa** | **mashujaa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **umoja** | **wingi** |
|---|---|
| mtoto **yuko** nje ya ofisi. | watoto **wako** nje ya ofisi. |
| mdudu **yuko** chini ya meza. | wadudu **wako** chini ya meza. |
| mgonjwa **yuko** juu ya kitanda. | wagonjwa **wako** juu ya vitanda. |
| mwanafunzi **yuko** karibu na darasa. | wanafunzi **wako** karibu na madarasa. |

108

Wiki ya 22: Siku ya 3 na 4 — **Shuleni**

Wasichana na wavulana wakiwa kwa uwanja wa shule wakiruka kamba.

**Sare ya shule**

Shule yetu inaitwa Mashujaa. Shule hii ina watoto wengi sana. Ina watoto wavulana na wasichana. Wao huvaa sare maridadi. Wasichana huvaa sketi nyekundu. Wanavaa pia blauzi ya samawati na soksi nyeupe. Wavulana huvaa suruali fupi. Wao pia huvaa soksi za kijivu na shati za samawati. Wanafunzi wote huvaa sweta za samawati na viatu vyeusi. Kila mara mwalimu mkuu hutuambia, "Someni kwa bidii."

109

### ● Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **su**. Sema kila sauti **/s//u/** kisha uunganishe na kusema silabi **su**. **[U]** Endelea kwa silabi: **shu, vi, fi.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ▬ Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **su ru a li** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **suruali**. **[U]** Endelea kwa maneno: **wasichana, mashujaa, soksi, sketi** na **blauzi.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **sketi, blauzi** na **soksi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu "**Sare ya shule**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Eleza sare za wasichana.*** *(sketi nyekundu, blauzi ya samawati na soksi nyeupe)*
2. ***Eleza sare za wavulana.*** *(suruari fupi, shati za samawati, soksi za kijivu)*
3. ***Ni mavazi gani ambayo huvaliwa na wanafunzi wote?*** *(sweta za samawati na viatu vyeusi)*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **sketi, blauzi, samawati, soksi, suruali fupi, sweta.**

i. Wasichana huvaa ____________ na ____________.

ii. Wavulana huvaa ____________na ____________.

iii. Wanafunzi wote huvaa ____________ za ____________.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Eleza wanafunzi watunge sentensi kutumia maneno haya: **nyekundu, blauzi, samawati, wavulana, wasichana, sweta**.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Ufahamu wa fonimu huzingatia kufunza sauti za herufi. Wakati wa kufunza sauti, mwalimu hapaswi kuandika herufi hizi ubaoni.Kipindi hiki ni cha mazungumzo pekee.

Tarehe: ____________________ Muda: ____________________ Idadi: ____________________

Wiki ya 22: Siku ya 3 na 4 — Shuleni

Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| s u | sh u | v i | f i |
| **su** | **shu** | **vi** | **fi** |

Tamka silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| su ru a li | wa si cha na | ma shu ja a |
| **suruali** | **wasichana** | **mashujaa** |
| so k si | b la u zi | s ke ti |
| **soksi** | **blauzi** | **sketi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu wa ambia | wana funzi |
| **huwaambia** | **wanafunzi** |
| i na itwa | ma shujaa |
| **inaitwa** | **mashujaa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mtoto **yuko** nje ya ofisi. | watoto **wako** nje ya ofisi. |
| mdudu **yuko** chini ya meza. | wadudu **wako** chini ya meza. |
| mgonjwa **yuko** juu ya kitanda. | wagonjwa **wako** juu ya vitanda. |
| mwanafunzi **yuko** karibu na darasa. | wanafunzi **wako** karibu na madarasa. |

108

Wiki ya 22: Siku ya 3 na 4 — Shuleni

Wasichana na wavulana wakiwa kwa uwanja wa shule wakiruka kamba.

**Sare ya shule**

Shule yetu inaitwa Mashujaa. Shule hii ina watoto wengi sana. Ina watoto wavulana na wasichana. Wao huvaa sare maridadi. Wasichana huvaa sketi nyekundu. Wanavaa pia blauzi ya samawati na soksi nyeupe. Wavulana huvaa suruali fupi. Wao pia huvaa soksi za kijivu na shati za samawati. Wanafunzi wote huvaa sweta za samawati na viatu vyeusi. Kila mara mwalimu mkuu hutuambia, "Someni kwa bidii."

109

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **hu wa ambia (huwaambia)** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **huwaambia**. **[U] wana funzi (wanafunzi), i na itwa (inaitwa), ma shujaa (mashujaa).**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

◆ **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **M**toto **yuko** nje ya ofisi | - | **Wa**toto **wako** nje ya ofisi. |
| **M**dudu **yuko** chini ya meza | - | **Wa**dudu **wako** chini ya meza. |
| **M**gonjwa **yuko** juu ya kitanda | - | **Wa**gonjwa **wako** juu ya vitanda. |
| **M**wanafunzi **yuko** karibu na darasa | - | **Wa**nafunzi **wako** karibu na madarasa. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **sketi, blauzi** na **soksi**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Sare ya shule"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Shule yenu inaitwaje?*** *(wanafunzi wataje jina la shule yao)*
2. ***Wanafunzi wa shule yenu huvaa sare ya aina gani?*** *(wanafunzi waeleze sare za shule)*
3. ***Someni hadithi huku mkitumia rangi za mazavi ya shule yenu.***

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo. Wanafunzi waziandike.

i. **shule yetu inaitwa mashujaa**
ii. **wasichana huvaa sketi nyekundu**
iii. **kiranja wetu ni mkoji**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **Mtoto, mvulana, mwanafunzi, mashujaa**. Waambie watunge sentensi kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 22: Siku ya 5 **Shuleni**

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: du ka ni - **dukani**

| | | | |
|---|---|---|---|
| du | su | ka | ku |
| fi | ri | ki | shu |
| le | ni | si | ra |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| **ni**nalala chini ya mti | **tu**nalala chini ya miti. |
| **ni**nacheza karibu na nyumba | **tu**nacheza karibu na nyumba. |
| ndege **yu**ko juu ya paa | ndege **wa**ko juu ya mapaa. |
| mpira **u**ko kando ya njia | mipira **i**ko kando ya njia. |

Rafiki Kalulu

Vijana wawili wamelala chini ya mti. Kando yake kuna mpira na kamba ya kuruka. Nyumba zinaonekana kwa umbali.

110

★ **Silabi**

**[N]** Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **du, ka**, na **ni** kuandika neno **dukani**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

● **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma katika umoja na wingi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **Ni**nalala chini ya mti | - | **Tu**nalala chini ya miti. |
| **Ni**nacheza karibu na nyumba | - | **Tu**nacheza karibu na nyumba. |
| Ndege **yu**ko juu ya paa | - | Ndege **wa**ko juu ya mapaa. |
| Mpira **u**ko kando ya njia | - | Mipira **i**ko kando ya njia. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya msamiati **sebule, kochi, televisheni**. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Eleza wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya "**Rafiki Kalulu**" huku wanafunzi wakisikiliza kwa makini.

**Rafiki Kalulu**

Jana rafiki yangu Kalulu alikuja kwetu kunitembelea. Nilifurahi sana kumwona. Nilimkaribisha sebuleni kwetu. Tukakaa kwenye kochi lililokuwa karibu na televisheni. Tukaburudika kutazama kipindi cha watoto. (***Kalulu alikaribishwa wapi?***)

Baadaye tukaenda nje. Tukakaa chini ya miembe. Tukacheza michezo mbalimbali. Tuliruka kamba, tukacheza kati au bano na kalongo pamoja na kibe. Tulirudi sebuleni kula chakula. Lo! Kilikuwa kitamu mno. (***Unafikiri walicheza mchezo gani mwingine?***)

Baada ya chakula tulienda nje tena. Tuliendelea kucheza chini ya miembe. Tukahisi tumechoka. Punde si punde, tukaanza kusinzia. Mwishowe tukalala pale pale chini ya miembe. Jioni,Kalulu akatuaga na kuelekea kwao. Ama kweli siku hiyo ilikuwa ya kufana sana. (***Kalulu na rafikiye walilala wapi?***)

**Baada ya kusoma**

[N/T/U] Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Taja mahali Kalulu na rafiki yake waliketi.*** *(sebuleni)*
2. ***Taja michezo waliyocheza.*** *(kati, bano, kalongo, kibe)*
3. ***Ni nini kinachoonyesha kuwa watoto hawa walikuwa wamechoka?*** *(walisinzia na kulala)*
4. ***Ni michezo gani unaopenda kucheza na marafiki zako?***

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiandika:

**majani, shule, wavulana, mtoto, sare, sukari, jioni, dukani, sketi, nyekundu.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Waambie wanafunzi waandike maneno matano zaidi kutokana na silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** na wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

Wiki ya 23: Siku ya 1 na 2 — Afya na Usafi

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ma wa i dha | ma a ru fu | m jo mba |
| **mawaidha** | **maarufu** | **mjomba** |
| vi ru si | kwa nza | u ki mwi |
| **virusi** | **kwanza** | **ukimwi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ku ji kinga | wa si ambukizwe | hu fundisha |
| **kujikinga** | **wasiambukizwe** | **hufundisha** |
| a me ji funza | a na ishi | hu saidia |
| **amejifunza** | **anaishi** | **husaidia** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| umoja | wingi |
|---|---|
| amejifunza | wamejifunza |
| amejikinga | wamejikinga |
| ameishi | wameishi |
| amesaidia | wamesaidia |

111

Wiki ya 23: Siku ya 1 na 2 — Afya na Usafi

Wavulana watatu wamevaa sare za shule na wameshikana mikono. Wanaonekana nadhifu na wenye furaha.

**Hadithi ya Toili**

Huyu ni Toili. Yuko katika darasa la kwanza. Toili anaishi na mjomba wake. Mjomba wake ni maarufu sana kijijini. Yeye husaidia wanakijiji kwa kuwapa mawaidha. Mawaidha haya huwasaidia kujikinga na virusi vya UKIMWI. Pia hufundisha watu jinsi ya kuisha na virusi vya UKIMWI. Toili amejifunza mambo mengi kutoka kwa mjomba wake.

112

### Kusoma maneno kwa silabi:

Tamka kila silabi **ma wa i dha** kisha uunganishe silabi na useme neno lote **mawaidha**. N/T/U: Endelea kwa maneno **maarufu, mjomba, virusi, kwanza** na **ukimwi.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

Wanafunzi waeleze maana ya maneno **virusi**, **mawaidha**. **[N]** Eleza wanafunzi maana ya msamiati **virusi, mawaidha** na **kujikinga**. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Eleza wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma "**Hadithi ya Toili"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya wanafunzi wawili.

### Maswali

N/T/U:] Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Toili yuko darasa la ngapi?*** *(Toili yuko darasa la kwanza)*
2. ***Toili anaishi na nani?*** *(anaishi na mjomba wake)*
3. ***Mjomba wake ni maarufu kwa nini?*** *(husaidia wanakijiji kwa mawaidha ya kujikinga na maradhi ya UKIMWI./ hufundisha watu jinsi ya kuishi na virusi vya UKIMWI)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **mjomba, maarufu, ukimwi, virusi, kwanza, mawaidha**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Waambie wanafunzi wayanakili maneno waliyoandika tena kisha baadaye wawasomee wenzao: **mjomba, maarufu, ukimwi, virusi, kwanza, mawaidha**.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Hakikisha umejiandaa vyema kabla ya kwenda darasani. Panga kadi za herufi utakazotumia kwenye mfuko wa herufi kabla ya kuanza kufunza. Hii itasaidia kuokoa wakati.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 23: Siku ya 1 na 2 — Afya na Usafi

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ma wa i dha | ma a ru fu | m jo mba |
| **mawaidha** | **maarufu** | **mjomba** |
| vi ru si | kwa nza | u ki mwi |
| **virusi** | **kwanza** | **ukimwi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ku ji kinga | wa si ambukizwe | hu fundisha |
| **kujikinga** | **wasiambukizwe** | **hufundisha** |
| a me ji funza | a na ishi | hu saidia |
| **amejifunza** | **anaishi** | **husaidia** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| umoja | wingi |
|---|---|
| amejifunza | wamejifunza |
| amejikinga | wamejikinga |
| ameishi | wameishi |
| amesaidia | wamesaidia |

111

Wiki ya 23: Siku ya 1 na 2 — Afya na Usafi

Wavulana watatu wamevaa sare za shule na wameshikana mikono. Wanaonekana nadhifu na wenye furaha.

Hadithi ya Toili

Huyu ni Toili. Yuko katika darasa la kwanza. Toili anaishi na mjomba wake. Mjomba wake ni maarufu sana kijijini. Yeye husaidia wanakijiji kwa kuwapa mawaidha. Mawaidha haya huwasaidia kujikinga na virusi vya UKIMWI. Pia hufundisha watu jinsi ya kuishi na virusi vya UKIMWI. Toili amejifunza mambo mengi kutoka kwa mjomba wake.

112

### ★ Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno **ku ji kinga** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote. N/T/U: Endelea kwa maneno**: wa si ambukizwe (wasiambukizwe), hu fundisha (hufundisha), a me ji funza (amejifunza), a na ishi (anaishi), hu saidia (husaidia).**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma katika umoja na wingi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **ame**jifunza | – | **wame**jifunza |
| **ame**jikinga | – | **wame**jikinga |
| **ame**ishi | – | **wame**ishi |
| **ame**saidia | – | **wame**saidia |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

[N/T/U] Wakumbushe wanafunzi maana ya msamiati **virusi, mawaidha** na **kujikinga**).

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma "**Hadithi ya Toili**". **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### ◈ Maswali

**[U]** Uliza maswali yafuatayo:

1. ***Je, unajua nini kuhusu ukimwi?*** *(wanafunzi waeleze wanachokijua kuhusu ukimwi)*
2. ***Taja mambo ambayo Toili amejifundisha.*** *(wanafunzi wataje mambo mazuri aliyojifunza Toili)*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waziandike sentensi kikamilifu: **mjomba, kwanza, mawaidha, maarufu.**

i) Toili yuko darasa la ________.

ii) Yeye anaishi na ________ wake.

iii) Toili ni ________ sana shuleni.

iv) Mwalimu aliwapatia wanafunzi ________.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi zenye maneno: **kijiji, vyao, kitabu, chake**. Waambie wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno hayo kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Wiki ya 23: Siku ya 3 na 4 **Afya na Usafi**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| vya ku la | tha ma ni | cha ku la |
| **vyakula** | **thamani** | **chakula** |
| mi ka te | mbo ga | ma tu nda |
| **mikate** | **mboga** | **matunda** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| u ta shangaa | na vi tamani |
| **utashangaa** | **navitamani** |
| hu ta kataa | vya tapakaa |
| **hutakataa** | **vyatapakaa** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| -ako | -enu |
|---|---|
| kalamu **yako** | kalamu **zenu** |
| kitabu **chako** | vitabu **vyenu** |
| mtoto **wako** | watoto **wenu** |
| jino **lako** | meno **yenu** |

113

Wiki ya 23: Siku ya 3 na 4 **Afya na Usafi**

Kuna chumba cha maamkuli. Kuna meza na viti viwili. Juu ya meza kuna bakuli iliyo na nyama na mboga, sahani ingine iliyo na ugali, glasi ya maji na embe.

**Lishe bora**

Nina shairi jamani, ni fupi utashangaa
La vyakula vya thamani, ukipewa hutakataa
Vyote navitamani, naviona vyatapakaa
**Chakula sio utamu, sisitiza lishe bora**

Lishe bora sio ghali, ni vyakula vya kawaida
Vya mikate na ugali, na mboga zenye faida
Matunda kwa kila hali, mafuta bila ziada
**Chakula sio utamu, sisitiza lishe bora**

114

**Kusoma maneno kwa silabi:**

Tamka kila silabi **vya ku la** kisha uunganishe silabi na useme neno lote **vyakula**. N/T/U: Endelea kwa maneno **mikate, thamani, mboga, chakula, matunda.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kabla ya kusoma:**

Wanafunzi waeleze maana ya maneno **thamani, lishe bora**. **[N]** Eleza wanafunzi maana ya msamiati **thamani, lishe bora** na **mafuta bila ziada**. Soma kichwa cha shairi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Eleza wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma shairi**

**[N]** Imba au kariri "**Shairi la lishe bora**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya wanafunzi wawili.

**Maswali:**

N/T/U:] Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Lishe bora ni nini?*** *(ni vyakula vya thamani/ni vyakula vya kawaida/sio vyakula ghali)*
2. ***Ni vyakula gani vya kawaida?*** *(mikate, ugali, mboga, matunda, mafuta)*
3. ***Ni mstari gani uliorudiwa katika shairi hili?*** *(Chakula sio utamu, sisitiza lishe bora)*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **matunda, mkate, vyakula.**

1. **__________ hivi ni vitamu.**
2. **Mimi napenda kula __________.**
3. **Kila asubuhi mimi hula chai kwa __________.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **vyakula, thamani, mikate, matunda, mafuta,sisitiza**. Waambie wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno hayo kisha wawasomee wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati unapouliza maswali ya ufahamu yenye majibu kwenye hadithi, hakikisha kuwa wanafunzi wanaangalia jawabu kwenye hadithi kabla ya kujibu swali.

Tarehe: ____________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

Wiki ya 23: Siku ya 3 na 4 — Afya na Usafi

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| vya ku la | tha ma ni | cha ku la |
| vyakula | thamani | chakula |
| mi ka te | mbo ga | ma tu nda |
| mikate | mboga | matunda |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| u ta shangaa | na vi tamani |
| utashangaa | navitamani |
| hu ta kataa | vya tapakaa |
| hutakataa | vyatapakaa |

Sarufi: Soma maneno haya.

| -ako | -enu |
|---|---|
| kalamu yako | kalamu zenu |
| kitabu chako | vitabu vyenu |
| mtoto wako | watoto wenu |
| jino lako | meno yenu |

113

Wiki ya 23: Siku ya 3 na 4 — Afya na Usafi

Kuna chumba cha maamkuli. Kuna meza na viti viwili. Juu ya meza kuna bakuli iliyo na nyama na mboga, sahani ingine iliyo na ugali, glasi ya maji na embe.

Lishe bora

Nina shairi jamani, ni fupi utashangaa
La vyakula vya thamani, ukipewa hutakataa
Vyote navitamani, naviona vyatapakaa
**Chakula sio utamu, sisitiza lishe bora**

Lishe bora sio ghali, ni vyakula vya kawaida
Vya mikate na ugali, na mboga zenye faida
Matunda kwa kila hali, mafuta bila ziada
**Chakula sio utamu, sisitiza lishe bora**

114

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **u ta shangaa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **utashangaa**. **[U]**Endelea kwa maneno: **hu ta kataa (hutakataa), na vi tamani (navitamani), vya tapakaa (vyatapakaa).**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

◆ **Sarufi**

[N/T] Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Kisha uzisome. Eleza matumizi ya vimilikishi kama **yako** – **yenu**. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| -ako | | -enu |
|---|---|---|
| kalamu **yako** | - | kalamu **zenu** |
| kitabu **chako** | - | vitabu **vyenu** |
| mtoto **wako** | - | watoto **wenu** |
| jino **lako** | - | meno **yenu** |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **thamani, lishe bora** na **mafuta bila ziada.**

**Kusoma shairi**

**[N]** Soma au kariri "**Shairi la lishe bora**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Taja vyakula ambavyo ni lishe bora.*** *(wanafunzi wataje mchanganyiko wa vyakula ambavyo ni lishe bora)*
2. ***Taja matunda unayoyajua.*** *(maembe, machungwa, mapera, mananasi)*
3. ***Ni mboga gani unazozipenda?*** *(sukumawiki, kabeji n.k.)*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo. Wanafunzi wanakili.

1. **kuna vyakula aina nyingi**
2. **vyakula hivi ni kama vile mikate ugali mboga na matunda**
3. **wewe unapenda matunda gani**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye vifungu vifuatavyo. Wanafunzi waandike wingi wakitumia **enu**.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Chakula chako | Vyakula vyako |
| 2. Kiatu chako | ____________ |
| 3. Nyumba yako | ____________ |
| 4. Yai lako | ____________ |

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 23: Siku ya 5 **Afya na Usafi**

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: shu ka - **shuka**

| | | | |
|---|---|---|---|
| du | le | ni | ku |
| su | ri | ra | shu |
| fi | ki | si | ka |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| wakati uliopo | wakati ujao |
|---|---|
| athumani **ana**kula | athumani **ata**kula. |
| omboga **ana**lia | omboga **ata**lia. |
| kalulu **ana**lala | kalulu **ata**lala. |
| toili **ana**ishi | toili **ata**ishi. |

**Vyakula mbalimbali**

Msichana na mvulana wakiwa jikoni wakiosha matunda. Kuna mfereji wa maji na beseni. Kuna aina nyingi ya matunda yakiwa kwa kikapu.

115

**★ Silabi**

**[N]** Soma silabi zilizo kurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **shu** na **ka** kuandika neno **shuka**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

**● Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma katika nyakati mbalimbali.

| Wakati Uliopo | | Wakati Ujao |
|---|---|---|
| Athumani **ana**kula. | - | Athumani **ata**kula. |
| Omboga **ana**lia. | - | Omboga **ata**lia. |
| Kalulu **ana**lala. | - | Kalulu **ata**lala. |
| Toili **ana**ishi. | - | Toili **ata**ishi. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya msamiati **kupona, kukua** na **mchicha**. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Eleza wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Vyakula mbalimbali"** huku wanafunzi wakisikiliza kwa makini.

**Vyakula mbalimbali**

Chakula ni muhimu sana kwa mwili wa mtu. Mtu asipokula vizuri hatakuwa na afya nzuri. Hatakuwa na nguvu za kufanya kazi. Atashikwa na magonjwa na hatapona haraka. Chakula pia hutusaidia kukua na kuwa wakubwa. ***(Mtu asiyekula vizuri atapata shida gani?)***

Kuna vyakula vya aina mbalimbali. Kuna vyakula vya kujenga mwili. Vyakula hivi ni kama vile nyama, mayai, maziwa, maharagwe na samaki.(***Ni vyakula gani vya kujenga mwili?***)

Pia kuna vyakula vya kulinda mwili. Vyakula hivi huzuia watu kuwa na magonjwa mbalimbali. Vyakula hivi ni mboga kama kabeji, sukumawiki, mchicha na karoti. Matunda ni kama maembe, machungwa, ndizi na ndimu.

Watoto wazuri hula vyakula wakipewa. Watoto wabaya hutupa mboga na kuchagua vipande vya nyama na mayai. Wakipewa matunda wao hula bila kuyaosha. Watoto wazuri hukataa chakula wanachopewa na mtu wasiyemjua. (***Kwa nini tusichukue chakula tunachopewa na mtu tusiyemjua?***)

**Baada ya kusoma**

[N/T/U] Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Mtu asiyekula chakula vizuri hawi na nini?*** *(afya nzuri)*
2. ***Taja vyakula vya kuujenga mwili?*** *(nyama, mayai, maziwa)*
3. ***Kulingana na hadithi hii watoto wabaya hufanya nini?*** *(hutupa mboga na kuchagua vipande vya nyama na mayai)*
4. ***Taja chakula ukipendacho.*** *(wanafunzi wataje vyakula mbalimbali)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **mjomba, maarufu, ukimwi, vyakula, mikate, matunda.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Eleza wanafunzi watumie silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kuandika maneno yanayohusu vyakula mbalimbali. Kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| z i | s i | b a | p a |
| **zi** | **si** | **ba** | **pa** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| zi wa ni | ku m la | ki to we o |
| **ziwani** | **kumla** | **kitoweo** |
| ba ku li | ba ta | kwe li |
| **bakuli** | **bata** | **kweli** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku ku tembelea | a me nenepa |
| **kukutembelea** | **amenenepa** |
| a m tembelee | a ka mwa lika |
| **amtembelee** | **akamwalika** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| bata **huyu** ni **m**zuri | bata **hawa** ni **wa**zuri. |
| dubu **huyu** ni **m**kali | dubu **hawa** ni **wa**kali. |
| kuku **huyu** ni **m**dogo | kuku **hawa** ni **wa**dogo. |
| nyoka **huyu** ni **m**refu | nyoka **hawa** ni **wa**refu. |

116



Mnyama mkubwa aliye na manyoya mengi mwilini. Ana makucha marefu. Ameketi kwenye ukingo wa mto. Kuna bata anaelea majini karibu na yule mnyama mkubwa.

### Dubu na Bata

Dubu alimuona bata barabarani. Akawaza, "Siku hizi bata amenenepa kuliko kuku!" Siku ya pili akakutana na bata ziwani. Dubu akamualika bata amtembelee. Lakini bata alielewa nia ya dubu ni kumla. Bata akasema, "Kwaa, kwaa, kwaa! Kukutembelea wewe ni kama kuweka kitoweo katika bakuli lako." Dubu akasema, "Kwa kweli, leo bata umenikataa. Siku moja nitakupata."

117

### ● Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **zi**. Sema kila sauti **/z/ /i/** kisha uunganishe na kusema silabi **zi**. **[U]** Endelea kwa maneno **si, ba** na **pa.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ▬ Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **zi wa ni** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **ziwani**. **[U]** Endelea na maneno: **bakuli, bata, kitoweo, kweli** na **kumla.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **Dubu, amenenepa** na **kitoweo**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu "**Dubu na Bata"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Dubu na Bata walikutana wapi?*** *(walikutana barabarani/ walikutana ziwani).*
2. ***Dubu aliwaza nini kuhusu Bata?*** *(aliwaza kuwa amenenepa sana).*
3. ***Bata alimjibu dubu vipi?*** *(Kwaa! Kwaa! Kwaa! Kututembelea wewe ni kama kuweka kitoweo kwa bakuli lako).*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno tofauti. Wanafunzi wayanakili. **dubu, amenenepa, kitoweo, bata, bakuli, ziwani**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike maneno walionakili tena kisha wawasomee wenzao: **dubu, amenenepa, kitoweo, bata, bakuli, ziwani**.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kiswahili ni lugha ya kupendeza sana. Mwalimu lazima ajifunze kutamka maneno sawasawa ili aweze kuongoza wanafunzi kuyatamka vyema.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| z i | s i | b a | p a |
| **zi** | **si** | **ba** | **pa** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| zi wa ni | ku m la | ki to we o |
| **ziwani** | **kumla** | **kitoweo** |
| ba ku li | ba ta | kwe li |
| **bakuli** | **bata** | **kweli** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku ku tembelea | a me nenepa |
| **kukutembelea** | **amenenepa** |
| a m tembelee | a ka mwa lika |
| **amtembelee** | **akamwalika** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| bata **huyu** ni mzuri | bata **hawa** ni wazuri. |
| dubu **huyu** ni mkali | dubu **hawa** ni wakali. |
| kuku **huyu** ni mdogo | kuku **hawa** ni wadogo. |
| nyoka **huyu** ni mrefu | nyoka **hawa** ni warefu. |





Mnyama mkubwa aliye na manyoya mengi mwilini. Ana makucha marefu. Ameketi kwenye ukingo wa mto. Kuna bata anaelea majini karibu na yule mnyama mkubwa.

### Dubu na Bata

Dubu alimuona bata barabarani. Akawaza, "Siku hizi bata amenenepa kuliko kuku!" Siku ya pili akakutana na bata ziwani. Dubu akamualika bata amtembelee. Lakini bata alielewa nia ya dubu ni kumla. Bata akasema, "Kwaa, kwaa, kwaa! Kukutembelea wewe ni kama kuweka kitoweo katika bakuli lako." Dubu akasema, "Kwa kweli, leo bata umenikataa. Siku moja nitakupata."



**★ Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **ku ku tembelea** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **kukutembelea**. **[U]** Endelea kwa maneno: **a me nenepa (amenenepa), a m tembelee (amtembelee), a ka mwalika (akamwalika).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**◆ Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Bata **huyu** ni mzuri | - | Bata **hawa** ni wazuri. |
| Dubu **huyu** ni mkali | - | Dubu **hawa** ni wakali. |
| Kuku **huyu** ni mdogo | - | Kuku **hawa** ni wadogo. |
| Nyoka **huyu** ni mrefu | - | Nyoka **hawa** ni warefu. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **dubu, amenenepa** na **kitoweo**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Dubu na Bata"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Je, unafikiri ni kwa nini dubu alimwalika bata nyumbani kwake? Tueleze sababu.*** *(alitaka kumla, alitaka wawe marafiki n.k).*
2. ***Kama ungekuwa Dubu ungefanya nini?*** *(ningemkamata bata n.k).*
3. ***Je, unafikiri hadithi hii ni ya kweli au la?*** *(wanafunzi wajibu huku wakitoa sababu zao).*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **amenenepa, kitoweo, barabarani, umenikataa, bata.**

1. Dubu alimwona bata __________.
2. Dubu alitaka kumfanya kuku __________.
3. Bata __________ kuliko kuku.
4. Leo __________ umenikataa.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno haya: **bata huyu, dubu wale, kuku huyu.** Wanafunzi watunge sentensi wakitumia hayo maneno kisha wasomee wenzao.

Tarehe: ________________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 24: Siku ya 3 na 4 **Mazingira**

Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| t e | v e | w e | y e |
| **te** | **ve** | **we** | **ye** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m bwa | ng'o mbe | nga mi a |
| **mbwa** | **ng'ombe** | **ngamia** |
| mbu zi | ngu ru we | si mba |
| **mbuzi** | **nguruwe** | **simba** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li shangazwa | wa li ishi |
| **walishangazwa** | **waliishi** |
| ha ku wapa | wa li kuja |
| **hakuwapa** | **walikuja** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| mimi | yeye |
|---|---|
| ninapenda paka. | anapenda paka. |
| ninataka bata. | anataka bata. |
| ninapenda dubu. | anapenda dubu. |
| ninafuga mbuzi. | anafuga mbuzi. |

118

Wiki ya 24: Siku ya 3 na 4 **Ndege na Wanyama**

Kijana ambaye amesimama kwa mguu mmoja akiwa ameshikilia fimbo. Karibu naye kuna simba ambaye amelala. Kuna ng'ombe wawili wanaokula nyasi hapo karibu.

**Siri ya Otonglo**

Mzee Otonglo aliishi katika kijiji cha Mitimbili. Yeye alikuwa tajiri sana. Otonglo alikuwa maarufu kwa ufugaji wa wanyama. Katika zizi lake alifuga mbuzi, kondoo, na ngamia. Wanakijiji walishangazwa na Otonglo. Yeye alifuga fisi na simba pia. Wanyama hawa waliishi pamoja kwa amani. Watu walikuja kutoka sehemu mbalimbali za nchi. Walikuja ili wajue siri yake. Otonglo hakuwapa siri hiyo.

119

### ★ Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **te**. Sema kila sauti **/t//e/** kisha uunganishe na kusema silabi **te**. **[U]** Endelea kwa silabi: **ve, we** na **ye.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **m bwa** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mbwa**. **[U]** Endelea kwa maneno: **mbuzi, ng'ombe, nguruwe, ngamia** na **simba.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **zizi, maarufu** na **siri**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu "**Siri ya Otonglo**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Taja wanyama waliokuwa katika zizi la mzee Otonglo.*** *(mbuzi, kondoo na ngamia)*
2. ***Ni nini kilishangaza watu kuhusu mzee Otonglo?*** *(kwa sababu alifuga fisi na simba pia)*
3. ***Kwa nini watu walikuja kwa Otonglo*** *(walitaka kujua siri ya Otonglo/walitaka kujua siri yake)*

### Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **zizi, nguruwe, maarufu.**

1. **__________ hili ni kubwa sana.**
2. **Mzee huyu ni __________ kwa ufugaji.**
3. **__________ huyu amenona sana.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **zizi, ng'ombe, mbuzi, nguruwe, maarufu**. Waambie wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno hayo kisha wawasomee wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati mwalimu anasoma hadithi mara ya kwanza, hakikisha wanafunzi wanasoma au wanafuatilia anachosoma mwalimu kwa kidole.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 24: Siku ya 4

Wiki ya 24: Siku ya 3 na 4 **Mazingira**

Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| t e | v e | w e | y e |
| **te** | **ve** | **we** | **ye** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m bwa | ng'o mbe | nga mi a |
| **mbwa** | **ng'ombe** | **ngamia** |
| mbu zi | ngu ru we | si mba |
| **mbuzi** | **nguruwe** | **simba** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li shangazwa | wa li ishi |
| **walishangazwa** | **waliishi** |
| ha ku wapa | wa li kuja |
| **hakuwapa** | **walikuja** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| mimi | yeye |
|---|---|
| ninapenda paka. | anapenda paka. |
| ninataka bata. | anataka bata. |
| ninapenda dubu. | anapenda dubu. |
| ninafuga mbuzi. | anafuga mbuzi. |

118

Wiki ya 24: Siku ya 3 na 4 **Ndege na Wanyama**

Kijana ambaye amesimama kwa mguu mmoja akiwa ameshikilia fimbo. Karibu naye kuna simba ambaye amelala. Kuna ng'ombe wawili wanaokula nyasi hapo karibu.

**Siri ya Otonglo**

Mzee Otonglo aliishi katika kijiji cha Mitimbili. Yeye alikuwa tajiri sana. Otonglo alikuwa maarufu kwa ufugaji wa wanyama. Katika zizi lake alifuga mbuzi, kondoo, na ngamia. Wanakijiji walishangazwa na Otonglo. Yeye alifuga fisi na simba pia. Wanyama hawa waliishi pamoja kwa amani. Watu walikuja kutoka sehemu mbalimbali za nchi. Walikuja ili wajue siri yake. Otonglo hakuwapa siri hiyo.

119

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa li shangazwa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **walishangazwa** kwa upesi. [U] Endelea kwa maneno: **ha ku wapa (hakuwapa), wa li ishi (waliishi), wa li kuja (walikuja).**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma sentensi hizi katika nafsi mbalimbali.

| Mimi | | Yeye |
|---|---|---|
| **Ni**napenda paka | - | **A**napenda paka. |
| **Ni**nataka bata | - | **A**nataka bata. |
| **Ni**napenda dubu | - | **A**napenda dubu. |
| **Ni**nafuga mbuzi | - | **A**nafuga mbuzi. |

### Kabla ya kusoma:

[N] Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **zizi, maarufu** na **siri**.

### Kusoma hadithi

[N] Soma hadithi ya **"Siri ya Otonglo"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Kwa nini watu walishangaa?*** *(kwa sababu kwa kawaida simba na fisi hula wanyama kama vile mbuzi na kondoo).*
2. ***Taja wanyama wanaofugwa nyumbani.*** *(kondoo, mbuzi, ng'ombe, kuku n.k).*
3. ***Je, unafikiri hadithi hii ni ya kweli? Eleza sababu yako.*** *(wanafunzi wajibu huku wakieleza sababu yao).*

### Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo. Wanafunzi wanakili.

**mzee otonglo alikuwa tajiri sana**

**otonglo alifuga nini zizini**

**mzee otonglo alifuga mbuzi kondoo na ngamia**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **ninataka, anaishi, ninapenda, anacheza**. Wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno hayo kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 24: Siku ya 5 **Ndege na Wanyama**

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: nga mi a - **ngamia**

| | | | |
|---|---|---|---|
| ka | ga | ta | nga |
| mbe | ng'o | pu | mi |
| nda | zi | mbu | a |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| **wewe una**muona dubu | **nyinyi mna**waona dubu. |
| **wewe una**muona kuku | **nyinyi mna**waona kuku. |
| **wewe una**muona sungura | **nyinyi mna**waona sungura. |
| **wewe una**muona fisi | **nyinyi mna**waona fisi. |

Umoja wa siafu

Kuna tundu ardhini na siafu kwenye mlango wa tundu hilo.

120

### ★ Silabi

**[N]** Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **nga**, **mi** na **a** kuandika neno **ngamia**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi wakitumia silabi kwenye vitabu vyao.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma sentensi hizi katika umoja na wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **Wewe una**muona dubu | **Nyinyi mna**waona dubu. |
| **Wewe una**muona kuku | **Nyinyi mna**waona kuku. |
| **Wewe una**muona sungura | **Nyinyi mna**waona sungura. |
| **Wewe una**muona fisi | **Nyinyi mna**waona fisi. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya msamiati **kustaajabisha, vibarua** na **hushambulia**. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Eleza wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Umoja wa siafu**" huku wanafunzi wakisikiliza kwa makini.

**Umoja wa Siafu**

Siafu ni wadudu wadogo wa kustaajabisha. Kwa kawaida siafu huishi kwa starehe katika vijiji vyao. Siku zote utawaona wakifanya kazi kwa bidii usiku na mchana. Siafu wana mpango mzuri sana wa kugawana kazi. Kwa mfano, wako askari walinzi, vibarua, wachukua mzigo na wawindaji watafutao chakula. ***(Siafu hufanya kazi saa ngapi?)***

Kwenye kijiji cha siafu kila mmoja ni mfanyikazi; hakuna anayejifanya mkubwa kuliko wenzake. Hata malkia wao ambaye ni mkuu wa jamii ana kazi maalum. Yeye hutaga mayai. Adui akiingia kijijini na kuwaharibia starehe au wakikutana naye njiani basi wote kwa pamoja hushambulia vikali. ***(Malkia hufanya kazi gani?)***

Sheria moja ya siafu ni kwamba, wanapokuwa safarini hakuna ruhusa ya kutawanyika. Wote husafiri pamoja. Ndio maana kundi lao siku zote huwa kubwa sana. Kweli siafu hujua ya kwamba umoja ni nguvu. ***(Kundi la siafu linaweza kuwa na siafu wangapi?)***

### ◈ Baada ya kusoma

[N/T/U] Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Taja aina mbalimbali za siafu.*** *(askari, vibarua)*
2. ***Kazi ya malkia siafu ni nini?*** *(kutaga mayai)*
3. ***Taja sheria moja ya siafu.*** *(kutotawanyika)*
4. ***Siafu wanatufunza nini?*** *(umoja ni nguvu)*

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **msichana, mchafu, nywele, marafiki, kudumisha, kichwani, kwapani, mwishowe, ikafura, wakatoweka.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Eleza wanafunzi watumie silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kuandika maneno yanayohusu wanyama. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 25: Siku ya 1 na 2 — Afya na Usafi

Tamka sauti na silabi.

| | |
|---|---|
| a | e |
| wa | we |
| nywa | nywe |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m si cha na | ku du mi sha | ku cha na |
| msichana | kudumisha | kuchana |
| m cha fu | nywe le | ku su gu a |
| mchafu | nywele | kusugua |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ha ku penda | ku m penda |
| hakupenda | kumpenda |
| wa ka m toroka | a ka furahi |
| wakamtoroka | akafurahi |

Soma maneno haya.

| neno | kinyume |
|---|---|
| safi | chafu |
| enda | rudi |
| juu | chini |
| kubwa | ndogo |
| lia | cheka |

121

Wiki ya 25: Siku ya 1 na 2 — Afya na Usafi

Msichana amekaa kitini. Nywele ni chafu. Nguo ni chafu na anaonekana hajaoga.

## Msichana mchafu

Kando ya mto Mara, paliishi msichana aliyekuwa mchafu sana. Hakupenda kuoga, kusugua meno wala kuchana nywele zake. Kucha na nguo zake zilikuwa chafu sana. Siku moja, akaanza kujikuna kwa sababu ya chawa na uchafu. Wazazi wake, ndugu na marafiki wakamtoroka. Akabaki peke yake. Ndipo akaamua kuoga, kusugua meno, kuchana nywele na kukata kucha zake. Jamii na marafiki wakarudi na kumpenda tena. Msichana akafurahi sana na kuahidi kudumisha usafi.

122

### ● Kusoma silabi

N/T/U: Andika herufi **a**. Soma sauti hiyo **/a/.** Ongeza herufi **w** kisha uunganishe na kusema silabi **wa**. Ongeza herufi **ny** kisha uunganishe na kusema silabi **nywa**. **[U]** Endelea kwa herufi: **e, we, nywe.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ▬ Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **m si cha na** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **msichana**. **[U]** Endelea kwa maneno **mchafu, kudumisha, nywele, kuchana** na **kusugua.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya vifungu hivi vya maneno **kusugua meno, kuchana nywele** na **kukata kucha**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu "**Msichana mchafu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Taja mambo ambayo msichana kwenye hadithi hakupenda kufanya.*** *(Hakupenda kuoga, kusugua meno wala kuchana nywele.)*
2. ***Ni watu gani waliomtoroka msichana huyu?*** *(wazazi wake, ndugu na marafiki)*
3. ***Baada ya watu kutoroka, msichana alifanya nini?*** *(aliamua kuoga, kusugua meno, kuchana nywele zake na kukata kucha)*

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika kwenye madaftari yao: **msichana, mchafu, nywele, marafiki, kudumisha.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike maneno walioyaandika tena. Kisha wawasomee wenzao: **msichana, mchafu, nywele, marafiki, kudumisha.**

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati wanafunzi wanaposoma, tembea darasani ili uweze kujua wasioweza kusoma. Utawasaidia hawa wanafunzi kusoma.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 25: Siku ya 1 na 2 — Afya na Usafi

Tamka sauti na silabi.

| | |
|---|---|
| a | e |
| wa | we |
| nywa | nywe |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m si cha na | ku du mi sha | ku cha na |
| msichana | kudumisha | kuchana |
| m cha fu | nywe le | ku su gu a |
| mchafu | nywele | kusugua |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ha ku penda | ku m penda |
| hakupenda | kumpenda |
| wa ka m toroka | a ka furahi |
| wakamtoroka | akafurahi |

Soma maneno haya.

| neno | kinyume |
|---|---|
| safi | chafu |
| enda | rudi |
| juu | chini |
| kubwa | ndogo |
| lia | cheka |

121

Wiki ya 25: Siku ya 1 na 2 — Afya na Usafi

Msichana amekaa kitini. Nywele ni chafu. Nguo ni chafu na anaonekana hajaoga.

### Msichana mchafu

Kando ya mto Mara, paliishi msichana aliyekuwa mchafu sana. Hakupenda kuoga, kusugua meno wala kuchana nywele zake. Kucha na nguo zake zilikuwa chafu sana. Siku moja, akaanza kujikuna kwa sababu ya chawa na uchafu. Wazazi wake, ndugu na marafiki wakamtoroka. Akabaki peke yake. Ndipo akaamua kuoga, kusugua meno, kuchana nywele na kukata kucha zake. Jamii na marafiki wakarudi na kumpenda tena. Msichana akafurahi sana na kuahidi kudumisha usafi.

122

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **ha ku penda** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **hakupenda**. **[U]** Endelea kwa maneno: **wa ka m toroka (wakamtoroka), ku m penda (kumpenda), a ka furahi (akafurahi).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

◆ **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma maneno na kinyume chake.

| **Neno** | | **Kinyume** |
|---|---|---|
| safi | - | chafu |
| enda | - | rudi |
| juu | - | chini |
| kubwa | - | ndogo |
| lia | - | cheka |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya vifungu hivi vya maneno **kusugua meno, kuchana nywele** na **kukata kucha**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Msichana mchafu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Kwa nini watu walimtoroka msichana aliyezungumziwa kwenye hadithi?*** *(kwa sababu alikuwa mchafu sana/kwa sababu alikuwa ananuka/kwa sababu alikuwa na chawa)*
2. ***Ni nini umuhimu wa kuweka mwili wako ukiwa safi?*** *(utakinga magonjwa/utakuwa na afya nzuri)*
3. ***Taja vitu ambavyo hutumiwa kwa kuchana nywele ___________, kuoga ___________ na kusugua meno ___________.***

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **kuoga, mchafu, kudumisha**.

1. **Msichana alikuwa** _______________.
2. **Hakupenda** _______________.
3. **Msichana aliahidi** _______________ **usafi.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | **Msichana** | **Mvulana** |
| 2. | **Chafu** | _______________ |
| 3. | **Rafiki** | _______________ |

Waambie wanafunzi waandike kinyume cha maneno hayo, kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 25: Siku ya 3 na 4 — Afya na Usafi

Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| i | i | a | a |
| wi | wi | wa | wa |
| **kwi** | **mwi** | **chwa** | **mwa** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u so ni | ki chwa ni | mwi sho we |
| **usoni** | **kichwani** | **mwishowe** |
| kwa pa ni | ma go ti ni | mi guu ni |
| **kwapani** | **magotini** | **miguuni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa ka tu uma | tu me lala |
| **wakatuuma** | **tumelala** |
| wa ka toweka | tu li kuwa |
| **wakatoweka** | **tulikuwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| sentensi | kinyume |
|---|---|
| savida **alichafua** rinda | savida **alisafisha** rinda. |
| mkoji **alianika** nguo | mkoji **alianua** nguo. |
| flora **alitega** mtego | flora **alitegua** mtego. |
| malenya **alipanga** vyombo | malenya **alipangua** vyombo. |

123

Wiki ya 25: Siku ya 3 na 4 — Afya na Usafi

Kuna tundu ardhini na kando yake kuna siafu wanaotembea.

**Siafu**

Siku moja, siafu walikuja kwetu. Sote tulikuwa tumelala. Siafu wakatuuma kila mahali. Miili yetu ikafura. Walituuma usoni na kichwani. Pia wakatuuma mabegani, kwapani, mikononi na magotini. Mwishowe wakatuuma miguuni hata nyayoni. Jamii nzima ikalia kwa uchungu. Tulikuwa na maumivu kwa sababu ya kuumwa na siafu. Ilipofika asubuhi, siafu wote wakatoweka.

124

● **Kusoma silabi**

N/T/U: Andika herufi **i**. Soma sauti hiyo **/i/**. Ongeza herufi **w** kisha uunganishe na kusema silabi **wi**. Ongeza herufi **k** kisha uunganishe na kusema silabi **kwi**. **[U]** Endelea kwa herufi: **i, wi, mwi; a, wa, chwa; a, wa, mwa.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

▬ **Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U: Tamka silabi **u so ni** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **usoni**. **[U]** Endelea kwa maneno: **kichwani, kwapani, mwishowe, magotini** na **miguuni.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kwapani, ikafura/kufura** na **wakatoweka**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Siafu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Taja sehemu za mwili ambazo siafu waliuma watu.*** *(usoni,kichwani, mabegani, kwapani, mikononi na magotini,miguuni na nyayoni)*
2. ***Kwa nini watu walilia?*** *(kwa sababu walikuwa na maumivu/waliumwa na siafu)*
3. ***Imbeni wimbo wa viungo: kichwa mabega, (magoti, vidole) x3*** *(Kichwa mabega magoti vidole, pua mdomo masikio) au wimbo wowote kuhusu sehemu za mwili.*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **kichwani, ikafura, wakatoweka**

1. **Siafu walituuma _____________.**
2. **Miili yetu _____________ sana.**
3. **Siafu wote _____________.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **kichwani, kwapani, mwishowe, ikafura, wakatoweka**. Waambie wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno hayo kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ________________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| i | i | a | a |
| wi | wi | wa | wa |
| **kwi** | **mwi** | **chwa** | **mwa** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u so ni | ki chwa ni | mwi sho we |
| **usoni** | **kichwani** | **mwishowe** |
| kwa pa ni | ma go ti ni | mi guu ni |
| **kwapani** | **magotini** | **miguuni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa ka tu uma | tu me lala |
| **wakatuuma** | **tumelala** |
| wa ka toweka | tu li kuwa |
| **wakatoweka** | **tulikuwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| sentensi | kinyume |
|---|---|
| savida **alichafua** rinda | savida **alisafisha** rinda. |
| mkoji **alianika** nguo | mkoji **alianua** nguo. |
| flora **alitega** mtego | flora **alitegua** mtego. |
| malenya **alipanga** vyombo | malenya **alipangua** vyombo. |





Kuna tundu ardhini na kando yake kuna siafu wanaotembea.

**Siafu**

Siku moja, siafu walikuja kwetu. Sote tulikuwa tumelala. Siafu wakatuuma kila mahali. Miili yetu ikafura. Walituuma usoni na kichwani. Pia wakatuuma mabegani, kwapani, mikononi na magotini. Mwishowe wakatuuma miguuni hata nyayoni. Jamii nzima ikalia kwa uchungu. Tulikuwa na maumivu kwa sababu ya kuumwa na siafu. Ilipofika asubuhi, siafu wote wakatoweka.



**★ Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa ka tu uma** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **wakatuuma**. **[U]** Endelea kwa maneno: **wa ka toweka (wakatoweka), tu me lala (tumelala), tu li kuwa (tulikuwa).**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**◆ Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma sentensi kisha uzisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wazisome peke yao.

| Sentensi | | Kinyume |
|---|---|---|
| Savida **alichafua** rinda | - | Savida **alisafisha** rinda. |
| Mkoji **alianika** nguo | - | Mkoji **alianua** nguo. |
| Flora **alitega** mtego | - | Flora **alitegua** mtego. |
| Malenya **alipanga** vyombo | - | Malenya **alipangua** vyombo. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **kwapani, ikafura/kufura** na **wakatoweka**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Siafu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

Mwalimu achague wanafunzi wawili wasimulie hadithi walioisoma.

**◇ Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Siafu walikuja wakati gani? Unajuaje?*** *(Walikuja wakati wa usiku. Kwa sababu watu walikuwa wamelala/Kwa sababu ilipofika asubuhi siafu walikuwa wametoweka.)*
2. ***Ukiumwa na siafu utafanya nini?*** *(nitapaka dawa/ nitaenda hospitali; Nitamuua, nitalia n.k.)*
3. ***Ni wadudu gani wengine ambao huuma watu?*** *(mbu, nyuki, nyigu n.k.)*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo. Wanafunzi wanakili.

**siafu walikuja kwetu**

**siafu walituuma mabegani mikononi na magotini**

**umewahi kuumwa na siafu**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **amekuja, wamelala, amepika, wametoa**. Waambie wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno haya. Kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 25: Siku ya 5

Wiki ya 25: Siku ya 5 — Afya na Usafi

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: si a fu - **siafu**

| | | | |
|---|---|---|---|
| m | si | cha | mu |
| ngu | fu | na | le |
| **a** | o | **wa** | te |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| **nina**furahi sana | **tuna**furahi sana. |
| **nina**weza kusoma | **tuna**weza kusoma. |
| **nina**tafuta nyota | **tuna**tafuta nyota. |

Mafumbo ya maumbo

Mwalimu akiwa kwa darasa na wanafunzi wameketi kwa madawati wakichora maumbo.

125

★ **Silabi**

[N] Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **si, a** na **fu** kuandika neno **siafu**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

● **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **Nina**furahi sana | - | **Tuna**furahia sana. |
| **Nina**weza kusoma | - | **Tuna**weza kusoma. |
| **Nina**tafuta nyota | - | **Tuna**tafuta nyota. |

**Kabla ya kusoma:**

[N] Eleza wanafunzi maana ya msamiati na uonyeshe maumbo **pembe tatu, mraba, nyota, mstatili, duara dufu** na **mviringo duara**. Soma kichwa cha mafumbo. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu maelezo, kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

[N] Soma **"Mafumbo ya maumbo"** huku wanafunzi wakiyajibu. Jibu fumbo la kwanza. Kisha wanafunzi wajibu mafumbo mengine.

**Mafumbo ya maumbo**

1. Nina pembe tatu, ni mfano wa samosa. Mimi ni nani? Pembe tatu
2. Sina pembe yoyote. Nina umbo la yai. Mimi ni nani?
3. Nina pembe nne. Ni mfano wa ubao darasani. Mimi ni nani?
4. Sina pembe yoyote. Nimefanana na shilingi. Mimi ni nani?
5. Nina pembe nne. Pande zote zinatoshana. Mimi ni nani?
6. Nina pembe nyingi. Ninametameta usiku. Mimi ni nani?

**Majibu**

| | |
|---|---|
| 1. umbo la pembe tatu | 2. umbo la duara dufu |
| 3. umbo la mstatili | 4. umbo la mviringo au duara |
| 5. umbo mraba | 6. umbo la nyota |

**Kuandika**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **msichana, mchafu, nywele, marafiki, kudumisha, kichwani, kwapani, mwishowe, ikafura, wakatoweka**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Eleza wanafunzi watumie silabi waliopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kuandika maneno yanayohusu wadudu au usafi. Baadaye wawasomee wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati mwalimu anasoma hadithi mara ya kwanza, hakikisha wanafunzi wanasoma au wanafuatilia anachosoma mwalimu kwa kidole.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Tamka sauti na silabi.

| | |
|---|---|
| u | i |
| vu | vi |
| mvu | mvi |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u pi nde | m vu a | nye ku ndu |
| upinde | mvua | nyekundu |
| ma chu ngwa | ma nja no | sa ma wa ti |
| machungwa | manjano | samawati |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| tu ka unda | tu ka shindana |
| tukaunda | tukashindana |
| tu li po kuwa | ki ka shinda |
| tulipokuwa | kikashinda |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| rangi **yangu** ni nyekundu | rangi **zetu** ni nyekundu. |
| sare **yangu** ni nyeupe | sare **zetu** ni nyeupe. |
| sketi **yangu** ni nyeusi | sketi **zetu** ni nyeusi. |
| kaptula **yangu** ni hudhurungi | kaptula **zetu** ni hudhurungi. |





Kuna upinde wa mvua unaonekana nyuma ya milima miwili. Mawingu mazito yametanda. Kuna mto mbele ya mlima.

## Upinde wa mvua

Jana tulipokuwa shuleni kulinyesha mvua ya rasharasha. Mara tukaona upinde wa mvua angani. Upinde ulikuwa na rangi nzuri za kupendeza. Kwa kawaida, upinde wa mvua una rangi saba. Mimi na marafiki zangu tukashindana kutaja rangi za upinde wa mvua. Tukaunda makundi mawili. Ndipo tukataja rangi hizo kwa haraka. Kikundi changu kikataja rangi tano: nyekundu, machungwa, manjano, kijani kibichi, na samawati. Kikundi changu kikashinda.



### ● Kusoma silabi

N/T/U: Andika herufi **u**. Soma sauti hiyo **/u/**. Ongeza herufi **v** kisha uunganishe na kusema silabi **vu**. Ongeza herufi **m** kisha uunganishe na kusema silabi **mvu**. **[U]** Endelea kwa silabi **i, vi, mvi**.

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ▬ Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **u pi nde** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **upinde**. **[U]** Endelea kwa maneno: **mvua, nyekundu, machungwa, manjano** na **samawati.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya vifungu hivi vya maneno **upinde wa mvua, rangi ya manjano** na **rangi ya machungwa**. Eleza wanafunzi maana ya vifungu hivi. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Upinde wa mvua"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Upinde wa mvua una rangi ngapi?*** *(Upinde wa mvua una rangi saba.)*
2. ***Eleza marafiki walifanya nini?*** *(Waliunda makundi mawili na kushindana kutaja rangi za upinde wa mvua.)*
3. ***Taja rangi zilizotajwa kwenye hadithi.*** *(Nyekundu, machungwa, manjano, kijani kibichi, samawati.)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **mvua, nyekundu, machungwa, upinde, rasharasha**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike maneno waliyoyaandika tena kisha wawasomee wenzao: **mvua, nyekundu, machungwa, upinde, rasharasha**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 26: Siku ya 1 na 2 — **Rangi**

Tamka sauti na silabi.

| | |
|---|---|
| u | i |
| vu | vi |
| **mvu** | **mvi** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u pi nde | m vu a | nye ku ndu |
| **upinde** | **mvua** | **nyekundu** |
| ma chu ngwa | ma nja no | sa ma wa ti |
| **machungwa** | **manjano** | **samawati** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| tu ka unda | tu ka shindana |
| **tukaunda** | **tukashindana** |
| tu li po kuwa | ki ka shinda |
| **tulipokuwa** | **kikashinda** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| rangi **yangu** ni nyekundu | rangi **zetu** ni nyekundu. |
| sare **yangu** ni nyeupe | sare **zetu** ni nyeupe. |
| sketi **yangu** ni nyeusi | sketi **zetu** ni nyeusi. |
| kaptula **yangu** ni hudhurungi | kaptula **zetu** ni hudhurungi. |

126

Wiki ya 26: Siku ya 1 na 2 — **Rangi**

Kuna upinde wa mvua unaonekana nyuma ya milima miwili. Mawingu mazito yametanda. Kuna mto mbele ya mlima.

**Upinde wa mvua**

Jana tulipokuwa shuleni kulinyesha mvua ya rasharasha. Mara tukaona upinde wa mvua angani. Upinde ulikuwa na rangi nzuri za kupendeza. Kwa kawaida, upinde wa mvua una rangi saba. Mimi na marafiki zangu tukashindana kutaja rangi za upinde wa mvua. Tukaunda makundi mawili. Ndipo tukataja rangi hizo kwa haraka. Kikundi changu kikataja rangi tano: nyekundu, machungwa, manjano, kijani kibichi, na samawati. Kikundi changu kikashinda.

127

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **tu ka unda** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **tukaunda**. **[U]** Endelea kwa maneno: **tu li po kuwa (tulipokuwa), tu ka shindana (tukashindana), ki ka shinda (kikashinda).**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

◆ **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Rangi **yangu** ni nyekundu | - | Rangi **zetu** ni nyekundu. |
| Sare **yangu** ni nyeupe | - | Sare **zetu** ni nyeupe. |
| Sketi **yangu** ni nyeusi | - | Sketi **zetu** ni nyeusi. |
| Kaptura **yangu** ni hudhurungi | - | Kaptura **zetu** ni hudhurungi. |

📖 **Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya vifungu hivi vya maneno **upinde wa mvua, rangi ya manjano** na **rangi ya machungwa**.

📖 **Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Upinde wa Mvua"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

◇ **Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Je, unajua rangi zipi za upinde wa mvua?*** *(nyekundu, samawati, kijani kibichi)*
2. ***Kunaponyesha ni vitu gani huonekana angani?*** *(mawingu, upinde n.k.)*
3. ***Ni rangi gani ambazo watoto kwenye hadithi hawakuzitaja?*** *(nili na urujuani)*

✍ **Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **rasharasha, nyekundu, rangi**.

1. **Upinde wa mvua una ____________ saba**
2. **Kulinyesha mvua ya __________________.**
3. **Tuliona rangi ______________.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **rangi zetu, rafiki yangu, shule yangu**. Waagize wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno hayo kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Tamka sauti na silabi.

| ng u | ng a | ng o | ng e |
|---|---|---|---|
| **ngu** | **nga** | **ngo** | **nge** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| be nde ra | hi s to ri a | nye u si |
| **bendera** | **historia** | **nyeusi** |
| u ku mbu sho | ma e nde le o | n chi |
| **ukumbusho** | **maendeleo** | **nchi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu tu kumbusha | tu ki pigania |
| **hutukumbusha** | **tukipigania** |
| i li yo mwagika | wa lio pigania |
| **iliyomwagika** | **waliopigania** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| rangi **hii** ni nyekundu | rangi **hizi** ni nyekundu. |
| nguo **hii** ni nyeupe | nguo **hizi** ni nyeupe. |
| ngao **hii** ni nyeusi | ngao **hizi** ni nyeusi. |
| ngazi **hii** ni nyeusi | ngazi **hizi** ni nyeusi. |





Bendera ya Kenya. Ina rangi nyeusi, nyeupe, nyekundu na kijani kibichi. Katikati kuna ngao na mikuki miwili.

## Rangi za bendera yetu

Bendera yetu ni ukumbusho wa historia yetu. Rangi nyeusi kama ngozi yetu hutukumbusha mashujaa wetu waliopigania uhuru. Nyekundu hutukumbusha damu iliyomwagika wakati tukipigania uhuru wetu. Rangi ya kijani kibichi ni ukumbusho wa uzuri wa nchi yetu. Nyeupe ni ya amani. Amani ambayo hutufanya tuishi pamoja. Hii ndiyo nguvu, ngao, nguzo na ngazi ya maendeleo.



### ● Kusoma silabi

N/T/U: Andika silabi **ngu**. Sema kila sauti **/ng//u/** kisha uunganishe na kusema silabi **ngu**. **[U]** Endelea kwa silabi **nga, ngo** na **nge.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ▬ Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **be nde ra** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **bendera**. **[U]** Endelea kwa maneno: **ukumbusho, historia, maendeleo, nyeusi** na **nchi.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **ngao, ukumbusho** na **uhuru**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Rangi ya bendera"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Bendera yetu ya Kenya inatukumbusha nini?*** *(historia yetu)*
2. ***Taja rangi za bendera yetu.*** *(nyeusi, nyekundu, nyeupe, na kijani kibichi)*
3. ***Rangi nyekundu ni ya nini?*** *(damu iliyomwagika tukipigania uhuru)*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **bendera, ukumbusho** na **uhuru.**

1. **Bendera ni ________ wa uhuru wetu.**
2. **Mashujaa walipigania ________.**
3. **________ ina rangi nne.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **historia, maendeleo, ngao, ukumbusho** na **uhuru.** Kisha watunge sentensi wakitumia maneno hayo. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 26: Siku ya 4

Wiki ya 26: Siku ya 3 na 4 **Rangi**

Tamka sauti na silabi.

| ng u | ng a | ng o | ng e |
|---|---|---|---|
| **ngu** | **nga** | **ngo** | **nge** |

Soma silabi na maneno.

| be nde ra | hi s to ri a | nye u si |
|---|---|---|
| **bendera** | **historia** | **nyeusi** |
| u ku mbu sho | ma e nde le o | n chi |
| **ukumbusho** | **maendeleo** | **nchi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu tu kumbusha | tu ki pigania |
|---|---|
| **hutukumbusha** | **tukipigania** |
| i li yo mwagika | wa lio pigania |
| **iliyomwagika** | **waliopigania** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| rangi **hii** ni nyekundu | rangi **hizi** ni nyekundu. |
| nguo **hii** ni nyeupe | nguo **hizi** ni nyeupe. |
| ngao **hii** ni nyeusi | ngao **hizi** ni nyeusi. |
| ngazi **hii** ni nyeusi | ngazi **hizi** ni nyeusi. |

128

Wiki ya 26: Siku ya 3 na 4 **Rangi**

Bendera ya Kenya. Ina rangi nyeusi, nyeupe, nyekundu na kijani kibichi. Katikati kuna ngao na mikuki miwili.

**Rangi za bendera yetu**

Bendera yetu ni ukumbusho wa historia yetu. Rangi nyeusi kama ngozi yetu hutukumbusha mashujaa wetu waliopigania uhuru. Nyekundu hutukumbusha damu iliyomwagika wakati tukipigania uhuru wetu. Rangi ya kijani kibichi ni ukumbusho wa uzuri wa nchi yetu. Nyeupe ni ya amani. Amani ambayo hutufanya tuishi pamoja. Hii ndiyo nguvu, ngao, nguzo na ngazi ya maendeleo.

129

**★ Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **hu tu kumbusha** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **hutukumbusha**. **[U]** Endelea kwa maneno: **tu ki pigania (tukipigania), i li yo mwagika (iliyomwagika), wa li o pigania (waliopigania).**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**◆ Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Rangi **hii** ni nyekundu | — | Rangi **hizi** ni nyekundu. |
| Nguo **hii** ni nyeupe | — | Nguo **hizi** ni nyeupe. |
| Ngao **hii** ni nyeusi | — | Ngao **hizi** ni nyeusi. |
| Ngazi **hii** ni nyeusi | — | Ngazi **hizi** ni nyeusi. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **ngao, ukumbusho** na **uhuru**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **Bendera Yetu** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Taja vitu vingine vilivyo kwenye bendera ya nchi*** *(ngao, mkuki)*
2. ***Je, unajua majina ya mashujaa wa nchi ya Kenya?*** *(Kenyatta Mzee, Ochieng' Aneko, Mekatilili)*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo. Wanafunzi wanakili.

1. **bendera yetu ni ukumbusho**
2. **je bendera hukukumbusha nini**
3. **amani ndiyo nguvu ngao nguzo na ngazi ya maendeleo**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **rangi hii, ngao hizi.** Wanafunzi watunge sentensi kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 26: Siku ya 5

Wiki ya 26: Siku ya 5 **Rangi**

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: nye u pe - **nyeupe**

| | | | |
|---|---|---|---|
| ja | ku | su | nja |
| ni | nye | si | no |
| ma | ndu | ki | pe |

Sarufi: Soma maneno haya.

| neno | kinyume |
|---|---|
| mkarimu | mchoyo |
| mzuri | mbaya |
| mrefu | mfupi |
| mkubwa | mdogo |
| mnene | mwembamba |

**Vitendawili**

1. nyumba yangu ni kubwa lakini mlango mdogo.
2. mama nieleke.
3. nawaka nateketea.
4. tik tak tik tak.
5. nikimpiga mwanangu watu hucheza.
6. bubu mwenye maneno mengi.
7. popote niendapo hunifuata.
8. akija kila mtu analia.
9. kipo lakini sikioni.
10. wazungu wawili wamechungulia mlangoni.
11. nyumba yangu haina taa.
12. bak bandika bak bandua.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| kifo | chupa | kitabu | ngoma | nyayo | kitanda | kivuli |
| mshumaa | kaburi | mate | saa | makamasi | kisogo | bunduki |

130

★ **Silabi**

[N] Soma silabi zote zilizo katika ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **nye u** na **pe** kuandika neno **nyeupe**. [T] Soma neno pamoja na wanafunzi. [U] Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

● **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma maneno na kinyume chake.

| **Neno** | | **Kinyume** |
|---|---|---|
| Mkarimu | | mchoyo |
| mzuri | - | mbaya |
| mrefu | - | mfupi |
| mkubwa | - | mdogo |
| mnene | - | mwembamba |

**Kabla ya kutega na kutegua vitendawili**

**N** - Kwa mfano - Kitendawili

**T** - Tega

**N** - Mama nieleke

**T** - Kitanda

Wanafunzi wakishindwa mwalimu atoe mji.

**N** - Nipe mji

**T** - Wanafunzi watoe miji kisha wategue vitendawili

[N] Mwalimu atege vitendawili. Wanafunzi wategue. Wape wanafunzi nafasi wategе vitendawili vyao, huku wakifuata utaratibu wa kutegua ikiwa wenzao wameshindwa.

**Vitendawili**

1. Nyumba yangu ni kubwa lakini mlango mdogo (chupa).
2. Mama nieleke (Kitanda).
3. Nawaka nateketea (mshumaa).
4. Tik tak tik tak (saa).
5. Nikimpiga mwanangu watu hucheza (ngoma).
6. Bubu mwenye maneno mengi (kitabu).
7. Popote niendapo hunifuata (kivuli).
8. Akija kila mtu analia (kifo).
9. Kipo lakini sikioni (kisogo).
10. Wazungu wawili wamechungulia mlangoni (makamasi).
11. Nyumba yangu haina taa (kaburi).
12. Bak bandika bak bandua (Nyayo).

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **Mvua, nyekundu, machungwa, upinde, rasharasha, historia, maendeleo, ngao, ukumbusho** na **uhuru**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Eleza wanafunzi wafanye utafiti wa vitendawili vitano. Waviandike na wamletee mwalimu asahihishe siku itakayofuata. Kisha watege na wategue na wenzao

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 27: Siku ya 1 na 2 **Familia**

Tamka s labi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | i | a | i |
| ha | si | wa | pi |
| mha | msi | njwa | spi |

Soma s labi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| mu u gu zi | wa ki li | ma ju mba |
| **muuguzi** | **wakili** | **majumba** |
| m ha ndi si | mwa li mu | re di o ni |
| **mhandisi** | **mwalimu** | **redioni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu fundisha | a nge penda |
| **hufundisha** | **angependa** |
| hu hudumia | a tangaze |
| **huhudumia** | **atangaze** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

1. kima yuko nyuma ya gari.
2. mwalimu yuko mbele ya darasa.

131

Wiki ya 27: Siku ya 1 na 2 **Familia**

Msichana amekaa kitini. Mbele yake kuna kitabu kilichofunguliwa juu ya dawati. Anafikiria kuhusu mtangazaji fulani.

**Jamaa ya Guyatu na kazi zao**

Baba ya Guyatu ni mwalimu. Yeye hufundisha watoto wa shule ya msingi. Kaka yake ni muuguzi. Yeye huhudumia wagonjwa hospitalini. Mama yake ni mhandisi. Yeye hujenga barabara na majumba makubwa. Dada yake ni wakili. Yeye hutetea watu mahakamani. Guyatu angependa kuwa mwanahabari ili atangaze redioni na kwenye runinga. Wewe ungependa kuwa nini baada ya masomo yako?

132

**● Kusoma silabi**

N/T/U: Andika herufi **a**. Soma sauti hiyo **/a/**. Ongeza herufi **h** kisha uunganishe na kusema silabi **ha**. Ongeza herufi **m** kisha uunganishe na kusema silabi **mha**. **[U]** Endelea kwa silabi: **i, si, msi; a, wa, njwa; i, pi, spi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**▬ Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U: Tamka silabi **mu u gu zi** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **muuguzi**. **[U]** Endelea na maneno: **mhandisi, wakili, mwalimu, majumba, redioni.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **wakili, mhandisi** na **runinga**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **Jamaa ya Guyatu na kazi zao** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Eleza kazi ambazo jamii ya Guyatu hufanya.*** *(Baba ni mwalimu/kaka ni muuguzi/mama ni mhandisi).*
2. ***Guyatu angetaka kuwa nini?*** *(angetaka kuwa mwanahabari).*
3. ***Eleza kazi ya muuguzi.*** *(huhudumia wagonjwa kwa hospitali).*

**Kuandika**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **mhandisi, wakili, mwalimu, muuguzi, runinga**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **mhandisi, wakili, mwalimu, muuguzi, runinga**. Wanafunzi wayanakili kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 27: Siku ya 2

Wiki ya 27: Siku ya 1 na 2 — **Familia**

Tamka s labi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | i | a | i |
| ha | si | wa | pi |
| mha | msi | njwa | spi |

Soma s labi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| mu u gu zi | wa ki li | ma ju mba |
| **muuguzi** | **wakili** | **majumba** |
| m ha ndi si | mwa li mu | re di o ni |
| **mhandisi** | **mwalimu** | **redioni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu fundisha | a nge penda |
| **hufundisha** | **angependa** |
| hu hudumia | a tangaze |
| **huhudumia** | **atangaze** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

1. kima yuko nyuma ya gari.
2. mwalimu yuko mbele ya darasa.

131

Wiki ya 27: Siku ya 1 na 2 — **Familia**

Msichana amekaa kitini. Mbele yake kuna kitabu kilichofunguliwa juu ya dawati. Anafikiria kuhusu mtangazaji fulani.

**Jamaa ya Guyatu na kazi zao**

Baba ya Guyatu ni mwalimu. Yeye hufundisha watoto wa shule ya msingi. Kaka yake ni muuguzi. Yeye huhudumia wagonjwa hospitalini. Mama yake ni mhandisi. Yeye hujenga barabara na majumba makubwa. Dada yake ni wakili. Yeye hutetea watu mahakamani. Guyatu angependa kuwa mwanahabari ili atangaze redioni na kwenye runinga. Wewe ungependa kuwa nini baada ya masomo yako?

132

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **hu fundisha** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **hufundisha** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **hu hudumia (huhudumia), a nge penda (angependa), a tangaze (atangaze).**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma sentensi hizi. Eleza wanafunzi jinsi ya kutumia vihusishi kama **nyuma ya**.

Kima yuko **nyuma ya** gari.

Mwalimu yuko **mbele ya** darasa.

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **wakili, mhandisi** na **runinga.**

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **Jamaa ya Guyatu na kazi zao** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Mhandisi hufanya kazi gani?*** *(Mhandisi, hujenga barabara na majumba makubwa).*
2. ***Baada ya masomo ungependa kufanya kazi gani?*** *(wanafunzi waleze kuhusu kazi mbalimbali).*
3. ***Toa maelezo kuhusu kazi uipendayo.***

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **mhandisi, huhudumia, muuguzi**.

1. **Kaka ya Guyatu ni ______________________**
2. **Mama ya Guyatu ni __________________**
3. **Daktari ______________ wagonjwa hospitalini.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno:: **Wakili, muuguzi, mhandisi na mwalimu.** Eleza wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno haya kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ________________________ Muda: ________________ Idadi: _________________

Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | a | a |
| za | ja | wa | ta |
| nza | nja | kwa | kta |

Tamka s labi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| nje ma | kwa nza | u da k ta ri |
| njema | kwanza | udaktari |
| la zi ma | mwa shi | o g le |
| lazima | mwashi | ogle |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ni nge penda | ni ta saidia |
| ningependa | nitasaidia |
| ni fundishe | ni fanikiwe |
| nifundishe | nifanikiwe |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| yule ni mwanamuziki | wale ni wanamuziki. |
| yule ni mwanahabari | wale ni wanahabari. |
| yule ni mwashi | wale ni waashi. |
| yule ni mwalimu | wale ni walimu. |





Chumba cha wagonjwa. Mgonjwa yuko kitandani. Daktari anampima na kifaa cha kupima wagonjwa.

**Kazi nizipendazo**

Mimi ni Ogle. Niko katika darasa la kwanza. Nikimaliza masomo ningependa kufanya kazi mbalimbali. Ningependa kuwa mwalimu kama dada yangu ili nifundishe watoto kusoma. Mama yangu alisema ninaweza kuwa mwashi, nijenge majumba ya kifahari. Baba alisema udaktari pia ni kazi nzuri. Nitasaidia wagonjwa kupata nafuu. Ninajua kuwa ili nifanikiwe katika kazi yoyote ni lazima nisome kwa bidii.



### ● Kusoma silabi

N/T/U: Andika herufi **a**. Soma sauti hiyo **/a/**. Ongeza herufi **z** kisha uunganishe na kusema silabi **za**. Ongeza herufi **n** kisha uunganishe na kusema silabi **nza**. **[U]** Endelea kwa silabi: **a, ja, nja; a, wa, kwa; a, ta, kta.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ▬ Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **nje ma** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **njema**. **[U]** Endelea kwa maneno: **kwanza, mwashi, udaktari, lazima, Ogle.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mwashi, nafuu** na **kifahari**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **Kazi nizipendazo** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Ogle yuko darasa la ngapi?*** *(Ogle yuko darasa la kwanza).*
2. ***Ogle angependa kuwa nini? Eleza sababu yake?*** *(Mwalimu/Mwashi/Daktari).*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: (**mwashi, nafuu** na **kifahari**)

1. **__________ hujenga majumba.**
2. **Majumba hayo huwa ya __________.**
3. **Daktari hutusaidia kupata __________.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **kwanza, mwashi, udaktari, nafuu** na **kifahari.** Eleza wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno hayo. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 27: Siku ya 3 na 4 **Familia**

Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | a | a |
| za | ja | wa | ta |
| nza | nja | kwa | kta |

Tamka s labi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| nje ma | kwa nza | u da k ta ri |
| njema | kwanza | udaktari |
| la zi ma | mwa shi | o g le |
| lazima | mwashi | ogle |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ni nge penda | ni ta saidia |
| ningependa | nitasaidia |
| ni fundishe | ni fanikiwe |
| nifundishe | nifanikiwe |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| yule ni mwanamuziki | wale ni wanamuziki. |
| yule ni mwanahabari | wale ni wanahabari. |
| yule ni mwashi | wale ni waashi. |
| yule ni mwalimu | wale ni walimu. |

133

Wiki ya 27: Siku ya 3 na 4 **Familia**

Chumba cha wagonjwa. Mgonjwa yuko kitandani. Daktari anampima na kifaa cha kupima wagonjwa.

**Kazi nizipendazo**

Mimi ni Ogle. Niko katika darasa la kwanza. Nikimaliza masomo ningependa kufanya kazi mbalimbali. Ningependa kuwa mwalimu kama dada yangu ili nifundishe watoto kusoma. Mama yangu alisema ninaweza kuwa mwashi, nijenge majumba ya kifahari. Baba alisema udaktari pia ni kazi nzuri. Nitasaidia wagonjwa kupata nafuu. Ninajua kuwa ili nifanikiwe katika kazi yoyote ni lazima nisome kwa bidii.

134

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **ni nge penda** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **ningependa**. **[U]** Endelea kwa maneno: **ni fundishe (nifundishe), ni ta saidia (nitasaidia), ni fanikiwe (nifanikiwe).**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma sentensi hizi

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Yule ni **mwa**namuziki | - | Wale ni **wa**namuziki. |
| Yule ni **mwa**nahabari | - | Wale ni **wa**nahabari. |
| Yule ni **mwa**shi | - | Wale ni **wa**ashi. |
| Yule ni **mwa**limu | - | Wale ni **wa**limu. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **mwashi, nafuu** na **kifahari**.

### 🕮 Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Kazi nizipendazo"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### ◈ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Dada ya Ogle anafanya kazi gani? Eleza sababu yake.*** *(Ualimu).*
2. ***Kazi ya mwalimu ni gani?*** *(mwalimu hufundisha watoto kusoma).*
3. ***Ili mtu afanikiwe katika kazi zote ni lazima afanye nini?*** *(Ni lazima asome kwa bidii).*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo. Wanafunzi wazinakili.

1. **kaka ya eda ni muuguzi**
2. **mama ya eda hujenga barabara nyumba na majumba makuu**
3. **wewe ungependa kuwa nini baada ya masomo**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno: **mwanahabari, waashi, mwalimu, wanariadha.** Wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno hayo kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 27: Siku ya 5 **Familia**

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: fu ndi - fundi

| | | | |
|---|---|---|---|
| ndi | to | mu | o |
| mwa | li | na | ndi |
| fu | nzi | shi | wa |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| ninaenda sokoni | tunaenda sokoni. |
| ninaenda barabarani | tunaenda barabarani. |
| ninaenda nyumbani | tunaenda nyumbani. |
| ninaenda shuleni | tunaenda shuleni. |
| ninaenda dukani | tunaenda dukani. |

**Mafumbo ya Wanyama**

1. Kuku kumi waliangalia mwewe angani. Ni macho mangapi yalimuona mwewe? (Macho kumi, kuku huangalia juu kutumia jicho moja).
2. Kuna ndege kumi mtini. Ukirusha jiwe moja ni wangapi watabaki? (Wote watatoroka).
3. Mabaharia watano waliingia majini. Walipotoka, nywele zao hazikuwa na maji. Je, ni kwa sababu gani? (Mabaharia walikuwa na vipara).
4. Mwenye kuzaa hana miguu, mwenye kuzaliwa ana miguu. (Yai na vifaranga).

135

**Mafumbo ya wanyama**

1. Kuku kumi waliangalia mwewe angani. Ni macho mangapi yalimuona mwewe? ***(Macho kumi, kuku huangalia juu kwa kutumia jicho moja)***
2. Ndege kumi wako kwenye mti. Ukirusha jiwe moja ni wangapi watabaki? ***(Wote watatoroka)***
3. Mabaharia watano walizama majini. Walipotoka nywele zao hazikuwa na maji. Je, ni kwa sababu gani? ***(Mabaharia walikuwa na vipara)***
4. Mwenye kuzaa hana miguu, mwenye kuzaliwa ana miguu. ***(Yai na vifaranga)***

**✍ Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika:
**mhandisi, wakili, mwalimu, muuguzi, runinga, mwashi, udaktari**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Eleza wanafunzi watumie silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kuunda maneno kuhusu kazi mbalimbali. Baadaye wawasomee wenzao.

**★ Silabi**

**[N]** Soma silabi zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **fu** na **ndi** kuandika neno **fundi**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

**● Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma katika umoja na wingi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **Nina**enda sokoni | - | **Tuna**enda sokoni. |
| **Nina**enda barabarani | - | **Tuna**enda barabarani. |
| **Nina**enda nyumbani | - | **Tuna**enda nyumbani. |
| **Nina**enda shuleni | - | **Tuna**enda shuleni. |
| **Nina**enda dukani | - | **Tuna**enda dukani. |

**Kabla ya kufumba na kufumbua mafumbo**

Eleza wanafunzi wafunge vitabu vyao. **[N]** Mwalimu afumbe mafumbo. Wanafunzi wafumbue. Wape wanafunzi nafasi wafumbue mafumbo yao, huku wakifuata utaratibu wa kufumbua ikiwa wenzao wameshindwa.

Mafumbo manne yametayarishwa tayari kwenye kitabu.

**Vidokezo vya Mwalimu**

Wakati wa kuunda maneno kutoka kwa jedwali, kumbusha wanafunzi kuwa wanaweza tu kutengeneza haya maneno wakitumia sauti au silabi zilizo kwenye jedwali. Maneno hayo ni sharti yawe maneno halisi yenye maana.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 28: Siku ya 1 na 2 **Mazingira**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| vi pe pe o | ku ngu ni | pa nzi |
| **vipepeo** | **kunguni** | **panzi** |
| chu ngu | m chwa | nzi ge |
| **chungu** | **mchwa** | **nzige** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| mbali mbali | wa karibia |
| **mbalimbali** | **wakaribia** |
| a li ye umba | ku haribia |
| **aliyeumba** | **kuharibia** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| neno | kinyume |
|---|---|
| wanene | wembamba |
| wakubwa | wadogo |
| kasi | polepole |
| ugumu | urahisi |
| uchungu | utamu |
| mwerevu | mjinga |

136

Wiki ya 28: Siku ya 1 na 2 **Mazingira**

Bustani la maua yenye rangi ya poda na nyuki wametua kwenye hayo maua.

### Wadudu

Shairi nina kariri, la wadudu mbalimbali,
Wabaya nao wazuri, la nyuki wenye asali,
Vipepeo wa rangi nzuri, na chungu kila mahali,
**Wadudu nao viumbe, ni Mungu aliyeumba.**

Wengine wakaribia, kwa uchafu ulo ndani,
Mende na panzi pia, chawa nao kunguni,
Mchwa kuharibia, panzi na nzige shambani,
**Wadudu nao viumbe, ni Mungu aliyeumba.**

137

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **vi pe pe o** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **vipepeo**. **[U]** Endelea kwa maneno: **chungu, kunguni, mchwa, panzi, nzige.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kariri, nzige** na **panzi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma shairi

**[N]** Soma au kariri shairi kuhusu "**Wadudu**" huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Ni wadudu gani wametajwa kwenye shairi?*** *(nyuki, vipepeo, chungu, mende, chawa, kunguni, panzi, nzige).*
2. ***Ni wadudu gani wenye rangi za kupendeza?*** *(vipepeo).*
3. ***Ni wadudu gani hupenda uchafu?*** *(mende, chawa, kunguni).*

### Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo: **chungu, kunguni, mchwa, nzi, panzi, nzige, nyuki.** Wanafunzi wanakili.

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike maneno waliyoyaandika tena kisha wawasomee wenzao: **chungu, kunguni, mchwa, nzi, panzi, nzige, nyuki.**

**Vidokezo vya Mwalimu**

Wakati wa kufunza msamiati, sharti utumie lugha inayoeleweka na wanafunzi. Pia vitu halisi, picha na maelezo pamoja na kutumia neno kwenye sentensi ni mbinu itakayowasaidia wanafunzi kuelewa vyema.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 28: Siku ya 2

Wiki ya 28: Siku ya 1 na 2 **Mazingira**

Soma silabi na maneno.

| vi pe pe o | ku ngu ni | pa nzi |
|---|---|---|
| **vipepeo** | **kunguni** | **panzi** |
| chu ngu | m chwa | nzi ge |
| **chungu** | **mchwa** | **nzige** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| mbali mbali | wa karibia |
|---|---|
| **mbalimbali** | **wakaribia** |
| a li ye umba | ku haribia |
| **aliyeumba** | **kuharibia** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| neno | kinyume |
|---|---|
| wanene | wembamba |
| wakubwa | wadogo |
| kasi | polepole |
| ugumu | urahisi |
| uchungu | utamu |
| mwerevu | mjinga |

136

Wiki ya 28: Siku ya 1 na 2 **Mazingira**

Bustani la maua yenye rangi ya poda na nyuki wametua kwenye hayo maua.

**Wadudu**

Shairi nina kariri, la wadudu mbalimbali,
Wabaya nao wazuri, la nyuki wenye asali,
Vipepeo wa rangi nzuri, na chungu kila mahali,
**Wadudu nao viumbe, ni Mungu aliyeumba.**

Wengine wakaribia, kwa uchafu ulo ndani,
Mende na panzi pia, chawa nao kunguni,
Mchwa kuharibia, panzi na nzige shambani,
**Wadudu nao viumbe, ni Mungu aliyeumba.**

137

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **mba li mba li** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **mbalimbali** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **a li ye umba (aliyeumba), wa karibia (wakaribia), ku haribia (kuharibia).**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

◆ **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma maneno haya na kinyume chake. N/T/U:

| Neno | | Kinyume |
|---|---|---|
| wanene | - | wembamba |
| wakubwa | - | wadogo |
| kasi | - | polepole |
| ugumu | - | urahisi |
| uchungu | - | utamu |
| mwerevu | - | mjinga |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **kariri, nzige** na **panzi**.

**Kusoma shairi**

**[N]** Soma au kariri shairi kuhusu **wadudu** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi maswali yafuatayo:

1. ***Nyuki wana faida gani?*** *(nyuki hutupatia asali)*
2. ***Ni wadudu gani wengine unaowajua?*** *(wanafunzi wataje wadudu mbalimbali)*
3. ***Mbali na wadudu, ni viumbe gani vingine ambavyo unajua?*** *(watu, wanyama, samaki n.k)*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **nyuki, kariri, vipepeo**.

1. **Nina ____________________ shairi.**
2. **___________________ wana asali.**
3. **_______________ wana rangi nzuri.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Wanafunzi waandike kinyume cha maneno hayo, kisha wawasomee wenzao.

| | Sentensi | Kinyume |
|---|---|---|
| 1. | Wadudu hawa ni wadogo | __________________ |
| 2. | Kunguni hawa ni wanene | __________________ |
| 3. | Vipepeo hawa ni wembamba | __________________ |

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| wa du du | ka dhaa | ma fu pi |
| **wadudu** | **kadhaa** | **mafupi** |
| ma ba wa | hu fa ri ki | ma ya i |
| **mabawa** | **hufariki** | **mayai** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa na pendeza | hu penda |
| **wanapendeza** | **hupenda** |
| hu patikana | hu fariki |
| **hupatikana** | **hufariki** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| -ake | -ao |
|---|---|
| yai **lake** limevunjika | mayai **yao** yamevunjika. |
| nguo **yake** imeraruka | nguo **zao** zimeraruka. |
| mpira **wake** umepotea | mipira **yao** imepotea. |
| kioo **chake** kimepasuka | vioo **vyao** vimepasuka. |





Vipepeo wa rangi tofauti wanapepea angani. Wengine wametua kwenye matawi ya miti.

### Vipepeo

Vipepeo ni aina ya wadudu ambao wanapendeza sana. Hii ni kwa sababu ya rangi kwenye mabawa yao. Maisha ya wadudu hawa huwa ni mafupi sana. Wao huishi kwa wiki kadhaa tu. Kwa kawaida vipepeo wa kike hutaga mayai, halafu hufariki. Je wajua kwa nini vipepeo hupenda maua? Chakula cha kipepeo hupatikana kwenye maji ya maua.



### Kusoma maneno kutumia silabi

**N/T/U:** Tamka silabi **wa du du** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **wadudu**. **[U]** Endelea kwa maneno: **mabawa, kadhaa, hufariki, mafupi, mayai.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mabawa, hutaga mayai** na **hufariki**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma taarifa

**[N]** Soma taarifa kuhusu **"Vipepeo"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Kwa nini vipepeo hupendeza sana?*** *(kwa sababu ya rangi kwenye mabawa)*
2. ***Eleza sababu inyofanya vipepeo kupenda maua.*** *(chakula cha vipepeo ni maji ya maua)*
3. ***Kawaida ya vipepeo wa kike ni ipi?*** *(wao hutaga mayai kisha baadaye hufa/hufariki)*

### Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **(mabawa, mafupi, mayai).**

**Vipepeo wana ___________.**
**Vipepeo hutaga ___________.**
**Maisha ya vipepeo ni ___________ sana.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno hayo kisha wawasomee wenzao: **mabawa, kadhaa, hufariki, mafupi, mayai.**

**Vidokezo vya Mwalimu**

Ni muhimu kutathmini kila mwanafunzi mara mbili kila muhula. Hii itakuwezesha kufahamu jinsi mwanafunzi anavyoendelea. Kusudi ni kuimarisha ufasaha wake wa kusoma na ufahamu. Kwa hivyo, ni bora kutathmini wanafunzi watatu kila siku.

Tarehe: __________________ Muda: _____________ Idadi: _____________

# Wiki ya 28: Siku ya 4

Wiki ya 28: Siku ya 3 na 4 **Mazingira**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| wa du du | ka dhaa | ma fu pi |
| **wadudu** | **kadhaa** | **mafupi** |
| ma ba wa | hu fa ri ki | ma ya i |
| **mabawa** | **hufariki** | **mayai** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa na pendeza | hu penda |
| **wanapendeza** | **hupenda** |
| hu patikana | hu fariki |
| **hupatikana** | **hufariki** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| -ake | -ao |
|---|---|
| yai **lake** limevunjika | mayai **yao** yamevunjika. |
| nguo **yake** imeraruka | nguo **zao** zimeraruka. |
| mpira **wake** umepotea | mipira **yao** imepotea. |
| kioo **chake** kimepasuka | vioo **vyao** vimepasuka. |

138

Wiki ya 28: Siku ya 3 na 4 **Mazingira**

Vipepeo wa rangi tofauti wanapepea angani. Wengine wametua kwenye matawi ya miti.

Vipepeo

Vipepeo ni aina ya wadudu ambao wanapendeza sana. Hii ni kwa sababu ya rangi kwenye mabawa yao. Maisha ya wadudu hawa huwa ni mafupi sana. Wao huishi kwa wiki kadhaa tu. Kwa kawaida vipepeo wa kike hutaga mayai, halafu hufariki. Je wajua kwa nini vipepeo hupenda maua? Chakula cha kipepeo hupatikana kwenye maji ya maua.

139

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa na pendeza** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **wanapendeza** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **hu patikana (hupatikana), hu penda (hupenda), hu fariki (hufariki).**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma sentensi kisha ueleze matumizi ya vimilikishi kama **lake** - **yao**.

| **Sentensi** | | **Kukanusha** |
|---|---|---|
| Yai **lake** limevunjika | - | Mayai **yao** yamevunjika. |
| Nguo **yake** imeraruka | - | Ngu **zao** zimeraruka. |
| Mpira **wake** umepotea | - | Mipira **yao** imepotea. |
| Kioo **chake** kimepasuka | - | Vioo **vyao** vimepasuka. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **mabawa, hutaga mayai** na **hufariki**.

### 🕮 Kusoma taarifa

**[N]** Soma taarifa ya **vipepeo** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### ⟐ Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Taja mdudu unayemjua na chakula anachokula.*** *(nzi - kinyesi, nyuki - maua)*
2. ***Ni wadudu gani wengine ambao wana rangi za kupendeza?*** *(nyigu, nyuki n.k)*
3. ***Vipepeo hupatikana wapi?*** *(vipepeo hupatikana kwenye maua)*

### ✍ Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo. Wanafunzi wanakili.

**umewahi kuona vipepeo wakipepea karibu na maua**
**kuna wadudu kama vile nzi nzige na mbu.**
**miti ya nyumba ya kakolo ililiwa na mchwa**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Waagize wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno haya: **anataga, hatagi, anapatikana, hapatikani.** Kisha wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 28: Siku ya 5 **Mazingira**

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: m bu - **mbu**

| | | | |
|---|---|---|---|
| wa | vi | pa | fu |
| pe | o | nzi | m |
| cha | ge | nza | bu |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| wakati uliopo | wakati ujao |
|---|---|
| kiwavi **ana**taga | kiwavi **ata**taga. |
| kipepeo **ana**vuka | kipepeo **ata**vuka. |
| siafu **ana**toroka | siafu **ata**toroka. |
| mende **ana**lala | mende **ata**lala. |

Hadithi ya Nzi

Mwanamke ameketi karibu na jiko la mawe tatu. Anatia chai kwenye kikombe kytoka kwa birika.

140

★ **Silabi**

**[N]** Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **m** na **bu** kuandika neno **mbu**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

● **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma katika nyakati mbalimbali.

| **Wakati uliopo** | | **Wakati ujao** |
|---|---|---|
| Kiwavi **ana**taga | - | Kiwavi **ata**taga. |
| Kipepeo **ana**vuka | - | Kipepeo **ata**vuka |
| Siafu **ana**toroka | - | Siafu **ata**toroka. |
| Mende **ana**lala | - | Mende **ata**lala. |

📖 **Kabla ya kusoma:**

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya msamiati **kikateleza, kinyonga** na **mjusi**. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Eleza wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

📖 **Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Nzi"** huku wanafunzi wakisikiliza kwa makini.

**Hadithi ya Nzi**

Mama ya Roda aliamka asubuhi na mapema. Akapika chai na kuiweka kwenye kikombe. Nzi akavuma na kuruka kwenye uso wake. Kikombe kikateleza na kuanguka.

Kulikuwa na kuku nyumbani. Aliposikia kikombe kikianguka, akaogopa. Akatorokea mlangoni. Mlangoni akakutana na mtoto akicheza. Akapita katikati ya miguu yake.

Mtoto akaogopa na kulia. Akaruka na kuangukia paka. Paka akaogopa sana. Akaruka nje ya ua. Akakutana na kinyonga. Kinyonga alipoona paka akaogopa sana. Akaruka na kuanguka kwenye mgongo wa mbuzi.

Mbuzi akaogopa. Akatorokea nyumbani. Nyumbani, mbuzi alimkuta baba Roda kwenye zizi akikama ng'ombe. Mbuzi akamgonga baba ya Roda akaanguka.

Ng'ombe alipoona Baba Roda yuko chini akaogopa sana. Akagonga mkebe wa maziwa ukaanguka. Maziwa yote yakamwagika. Nzi akaja na kulamba maziwa.

Mara mjusi akatokea. Nzi alipoona mjusi akaogopa. Akapaa na kuingia kwenye nyumba tena.

◇ **Baada ya kusoma**

[N/T/U] Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Taja wanyama waliotajwa kwenye hadithi hii.*** *(paka, kinyonga n.k.)*
2. ***Mama Roda aliamka saa ngapi?*** *(asubuhi na mapema)*
3. ***Kama ungekuwa Mama Roda ungefanya nini?***
4. ***Unafikiri ni kitu gani kitafanyika tena?***

✍ **Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika:
**chungu, kunguni, mchwa, nzi, panzi, nzige, nyuki, mabawa, kadhaa, mayai.**
Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Eleza wanafunzi watumie silabi zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kuunda maneno kuhusu **wadudu mbalimbali**. Baadaye wawasomee wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati unapojitayarisha kwa somo, ni muhimu kusoma na kutafakari kuhusu vidokezo vya mwalimu kwenye mwongozo.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 29: Siku ya 1 na 2 **Anga**

Soma s labi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| vi pa wa | ma ba di li ko | vyu ra |
| **vipawa** | **mabadiliko** | **vyura** |
| ku ta bi ri | ki a nga zi | m vu a |
| **kutabiri** | **kiangazi** | **mvua** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| he wa | u pe po | jo to | hu hi si |
| **hewa** | **upepo** | **joto** | **huhisi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu ongezeka | u ta wa sikia |
| **huongezeka** | **utawasikia** |
| ha wa onekani | wa ki imba |
| **hawaonekani** | **wakiimba** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **yule** | **wale** |
|---|---|
| mwalimu **yule** ni mzuri | walimu **wale** ni wazuri. |
| mwanafunzi **yule** ni mwerevu | wanafunzi **wale** ni werevu. |
| dereva **yule** ni hodari | madereva **wale** ni hodari. |
| mtoto **yule** ni mtiifu | watoto **wale** ni watiifu. |

141

Wiki ya 29: Siku ya 1 na 2 **Anga**

Maua yamemea majini. Vyura wawili wamekaa juu ya majani na mmoja anaruka.

### Utabiri wa hali ya hewa: Sehemu ya kwanza

Wanyama na wadudu wana vipawa vya kutabiri hali ya hewa. Wao huhisi mabadiliko ya hewa kama vile joto na upepo.
Vyura hawaonekani kwa urahisi wakati wa kiangazi. Wakati wa mvua, wadudu huwa wengi sana. Vyura nao huongezeka na kula wadudu hao. Ndio maana utawasikia vyura wakiimba kabla ya mvua kunyesha.

142

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **vi pa wa** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **vipawa**. **[U]** Endelea kwa maneno: **kutabiri, mabadiliko, kiangazi, vyura, mvua.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **vipawa, kutabiri** na **kiangazi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma taarifa

**[N]** Soma taarifa kuhusu **"Utabiri wa hali ya hewa: Sehemu ya kwanza"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Wanyama na wadudu huhisi nini?*** *(huhisi mabadiliko ya hewa kama vile joto na upepo)*
2. ***Eleza wakati ambao vyura huonekana kwa urahisi.*** *(Vyura huonekana kwa urahisi wakati wa unyevunyevu)*
3. ***Eleza kinachofanyika wakati wa kiangazi.*** *(Vyura hawaonekani kwa urahisi)*

### Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Wanafunzi wanakili. **Vipawa. Anga, kutabiri, mabadiliko, kiangazi.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike maneno waliyoyaandika tena kisha wawasomee wenzao: **vipawa, anga, kutabiri, mabadiliko, kiangazi.**

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kitu cha muhimu zaidi katika mradi wa KUSOMA ni kuhakikisha wanafunzi wote wanaweza kusoma vizuri wakimaliza huu mwaka. Je, umeweza kuwasaidia wasome vilivyo?

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 29: Siku ya 1 na 2 **Anga**

Soma s labi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| vi pa wa | ma ba di li ko | vyu ra |
| **vipawa** | **mabadiliko** | **vyura** |
| ku ta bi ri | ki a nga zi | m vu a |
| **kutabiri** | **kiangazi** | **mvua** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| he wa | u pe po | jo to | hu hi si |
| **hewa** | **upepo** | **joto** | **huhisi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu ongezeka | u ta wa sikia |
| **huongezeka** | **utawasikia** |
| ha wa onekani | wa ki imba |
| **hawaonekani** | **wakiimba** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **yule** | **wale** |
|---|---|
| mwalimu **yule** ni mzuri | walimu **wale** ni wazuri. |
| mwanafunzi **yule** ni mwerevu | wanafunzi **wale** ni werevu. |
| dereva **yule** ni hodari | madereva **wale** ni hodari. |
| mtoto **yule** ni mtiifu | watoto **wale** ni watiifu. |

141

Wiki ya 29: Siku ya 1 na 2 **Anga**

Maua yamemea majini. Vyura wawili wamekaa juu ya majani na mmoja anaruka.

**Utabiri wa hali ya hewa: Sehemu ya kwanza**

Wanyama na wadudu wana vipawa vya kutabiri hali ya hewa. Wao huhisi mabadiliko ya hewa kama vile joto na upepo.

Vyura hawaonekani kwa urahisi wakati wa kiangazi. Wakati wa mvua, wadudu huwa wengi sana. Vyura nao huongezeka na kula wadudu hao. Ndio maana utawasikia vyura wakiimba kabla ya mvua kunyesha.

142

**★ Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **hu ongezeka** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **huongezeka** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **u ta wa sikia (utawasikia), ha wa onekani (hawaonekani), wa ki imba (wakiimba).** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**◆ Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. **N/T/U**: Soma sentensi hizi kisha ueleze matumizi ya vionyeshi kama **yule** - **wale**. Soma pamoja na wanafunzi. Wanafunzi wasome peke yao.

| Yule | Wale |
|---|---|
| Mwalimu **yule** ni mzuri | Walimu **wale** ni wazuri. |
| Mwanafunzi **yule** ni mwerevu | Wanafunzi **wale** ni werevu. |
| Dereva **yule** ni hodari | Madereva **wale** ni hodari. |
| Mtoto **yule** ni mtiifu | Watoto **wale** ni watiifu. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **vipawa, kutabiri** na **kiangazi.**

**Kusoma taarifa**

**[N]** Soma taarifa kuhusu **"Utabiri wa hali ya hewa"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Unafikiri vyura hula chakula gani?*** *(vyura hula wadudu)*
2. ***Kwa nini vyura huimba kabla ya mvua kunyesha?*** *(kwa sababu wanapenda mvua/kwa sababu wanajua watapata chakula/kwa sababu wadudu huongezeka na vyura hupata chakula)*
3. ***Mbali na vyura, ni wanyama gani hupenda maji?*** *(kaa, samaki, kiboko n.k.)*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **(kiangazi, vipawa)**.

1. **Wanyama wana ___________ vya kutabiri.**
2. **Vyura hawaonekani wakati wa ___________.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo. Wanafunzi waziandike katika wingi kisha wasomee wenzao.

1. **Mtoto yule ni mwerevu** **Watoto wale ni werevu.**
2. **Bibi yule ni mwaminifu** ______________________________
3. **Mwalimu yule ni mrefu** ______________________________
4. **Shangazi yule ni mzuri** ______________________________

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

Wiki ya 29: Siku ya 3 na 4 **Anga**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ba a dhi | ki wa ngo | ku twa |
| **baadhi** | **kiwango** | **kutwa** |
| u ta a la mu | m cha na | nzi ge |
| **utaalamu** | **mchana** | **nzige** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku tembelea | i me karibia |
| **kutembelea** | **imekaribia** |
| wa me ji ficha | wa me somea |
| **wamejificha** | **wamesomea** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| neno | kinyume |
|---|---|
| mchana | usiku |
| baridi | joto |
| funga | fungua |
| nzito | nyepesi |
| rahisi | ngumu |
| vaa | vua |

143

Wiki ya 29: Siku ya 3 na 4 **Anga**

Mwanamume amevalia kabuti ya rangi nyeupe. Ana vifaa vya kutabiri hali ya anga.

### Utabiri wa hali ya hewa: Sehemu ya pili

Kwa kawaida, wadudu kama vile vipepeo hupenda kutembelea maua mchana kutwa. Mara tu unapoona wamejificha upande wa chini wa majani, mvua huwa imekaribia. Je, wajua kwamba nyenje nao huimba sana usiku.

Nchi yetu ina watu ambao wamesomea utaalamu wa kutabiri hali ya hewa. Wao wana ujuzi wa kupima kiwango cha mvua na joto. Wataalamu hawa huitwa watabiri wa hali ya hewa.

144

**Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U: Tamka silabi **ba a dhi** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **baadhi**. **[U]** Endelea kwa maneno: **utaalamu, kiwango, mchana, kutwa, nzige.** Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **utaalamu, kiwango** na kifungu cha maneno **mchana kutwa.** Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma taarifa**

**[N]** Soma taarifa kuhusu **"Utabiri wa hali ya hewa: Sehemu ya pili"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Vipepeo hupenda kufanya nini?*** *(Vipepeo hupenda kutembelea maua mchana kutwa).*
2. ***Ukiona vipepeo vimejificha chini ya majani ni nini kitafanyika?*** *(mvua huwa imekaribia).*
3. ***Watabiri wa hali ya hewa wana ujuzi gani?*** *(wana ujuzi wa kupima kiwango cha joto na mvua).*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **(utaalam, nzige, maua).**

**i)** **Vipepeo hupenda _________.**
**ii)** **_________ nao huimba wakati wa kiangazi.**
**iii)** **Watu wamesomea _________ wa kutabiri hali ya hewa.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno hayo kisha wawasomee wenzao: **upande, utaalam, kiwango, mchana kutwa, nzige.**

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kabla ya wanafunzi kutabiri, hakikisha wamesoma kichwa cha hadithi, na kueleza wanachokiona kwenye picha iliyoko kwa hadithi.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 29: Siku ya 4



Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ba a dhi | ki wa ngo | ku twa |
| **baadhi** | **kiwango** | **kutwa** |
| u ta a la mu | m cha na | nzi ge |
| **utaalamu** | **mchana** | **nzige** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku tembelea | i me karibia |
| **kutembelea** | **imekaribia** |
| wa me ji ficha | wa me somea |
| **wamejificha** | **wamesomea** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| neno | kinyume |
|---|---|
| mchana | usiku |
| baridi | joto |
| funga | fungua |
| nzito | nyepesi |
| rahisi | ngumu |
| vaa | vua |





Mwanamume amevalia kabuti ya rangi nyeupe. Ana vifaa vya kutabiri hali ya anga.

### Utabiri wa hali ya hewa: Sehemu ya pili

Kwa kawaida, wadudu kama vile vipepeo hupenda kutembelea maua mchana kutwa. Mara tu unapoona wamejificha upande wa chini wa majani, mvua huwa imekaribia. Je, wajua kwamba nyenje nao huimba sana usiku.

Nchi yetu ina watu ambao wamesomea utaalamu wa kutabiri hali ya hewa. Wao wana ujuzi wa kupima kiwango cha mvua na joto. Wataalamu hawa huitwa watabiri wa hali ya hewa.



### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U: Tamka sehemu za neno **ku tembelea** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **kutembelea** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **i me karibia (imekaribia), wa me somea (wamesomea), wa me ji ficha (wamejificha).**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### ◆ Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma katika kinyume.

| Neno | Kinyume |
|---|---|
| mchana | usiku |
| baridi | joto |
| funga | fungua |
| nzito | nyepesi |
| rahisi | ngumu |
| vaa | vua |

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **utaalamu, kiwango** na kifungu cha maneno **mchana kutwa**.

### Kusoma taarifa

**[N]** Soma taarifa ya **"Utabiri wa hali ya hewa"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

### Maswali

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Watu wanaotabiri hali ya anga hupata vipi ujuzi huu?*** *(wao husoma hali ya hewa)*
2. ***Je, wewe hutambua vipi kuwa mvua inataka kunyesha?*** *(joto huongezeka)*

### Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo. Wanafunzi wanakili.

1. **je wajua kuwa nzige huimba sana wakati wa kiangazi**
2. **watu wanaosomea utaalamu wa hali ya hewa hufanya kazi gani**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Eleza wanafunzi watafute maneno sita mengine na kinyume chake. Wanafunzi wayaandike na baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 29: Siku ya 5 **Anga**

Tumia silabi kuunda maneno.

Kwa mfano: u pe po - **upepo**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ju | vu | pe | u | to | wa |
| m | jo | a | po | pa | he |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mdudu utamsikia | wadudu mtawasikia. |
| mdudu unamsikia | wadudu mnawasikia. |
| mdudu ulimsikia | wadudu mliwasikia. |
| mdudu umemsikia | wadudu mmewasikia. |

Ndovu na Sungura

Kuna ndovu na sungura msituni. Mbele yao moto mkubwa unawaka.

145

### ★ Silabi

[N] Soma silabi zote zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **u, pe** na **po** kuandika neno **upepo**. [T] Soma neno pamoja na wanafunzi. [U] Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia silabi kwenye vitabu vyao.

### ● Sarufi

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma katika umoja na wingi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Mdudu **uta**msikia | - | Wadudu **mta**wasikia. |
| Mdudu **una**sikia | - | Wadudu **mna**wasikia. |
| Mdudu **uli**msikia | - | Wadudu **mli**wasikia. |
| Mdudu **ume**msikia | - | Wadudu **mme**wasikia. |

### 🕮 Kabla ya kusoma:

[N] Eleza wanafunzi maana ya msamiati **manyoya, lahaula** na **vumilia**. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. [U] Eleza wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### 🕮 Kusoma hadithi

[N] Soma hadithi ya **Ndovu na Sungura** huku wanafunzi wakisikiliza kwa makini.

**Ndovu na Sungura**

Hapo zamani za kale Sungura alikuwa na viatu vizuri vya kupendeza. Ndovu alikuwa na manyoya mengi sana mwilini. Kwa muda mrefu Ndovu alitamani viatu vya Sungura. Akamuuliza Sungura mahali alinunua viatu vyake. Sungura akasema alivinunua motoni.

Bila kufikiria Ndovu akaingia kwenye moto. Muda si muda, moto ukaanza kumchoma. Lakini hakuwa amepata viatu. Ndovu akaita, "Sungura, sivioni viatu ulivyoniambia." Sungura akajibu, "Tulia. Viatu bado vinaundwa kwenye moto."

Ndovu akajibu, "Haya! Kwa vile navitaka viatu kama vyako, nitavumilia tu." Sungura akamwambia, "Vumilia tu viatu vinakuja. Viatu maridadi vimeanza kutokea. Tazama viatu vizuri kuliko vyangu! Lahaula! Ni vizuri sana. Rafiki yangu vumilia tu!"

Ndovu alichomeka na manyoya yake yote yakatoka. Sungura alimvuta mkia na kumtoa motoni huku akimcheka. Tangu siku hiyo, Ndovu hana manyoya mengi mwilini.

### ◈ Baada ya kusoma

[N/T/U] Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Ndovu alitamani kitu gani kutoka kwa Sungura?*** *(viatu)*
2. ***Je, Sungura alimwambia Ndovu ukweli? Eleza jibu lako.*** *(hapana)*
3. ***Kwa nini Sungura alimvuta ndovu kutoka motoni?*** *(hakutaka afe)*
4. ***Kama wewe ungekuwa Ndovu ungefanya nini?*** *(ningemuua Sungura, n.k.)*

### ✍ Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **utaalam, kiwango, mchana, nzige, hewa, vipawa, anga, kiangazi.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Eleza wanafunzi watumie silabi zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** kuunda maneno kuhusu wanyama mbalimbali. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

Wiki ya 30: Siku ya 1 na 2 **Ndege na Wanyama**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m ku li ma | ngu ru we | ma zi wa |
| **mkulima** | **nguruwe** | **maziwa** |
| ng'o mbe | Na li a ka | a su bu hi |
| **ng'ombe** | **Naliaka** | **asubuhi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li o nona | ku wa patia |
| **walionona** | **kuwapatia** |
| a li furahi | wa li endelea |
| **alifurahi** | **waliendelea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| ng'ombe **aliye**nona | ng'ombe **wali**onona. |
| nguruwe **aliye**nona | nguruwe **wali**onona. |
| kuku **aliye**nona | kuku **wali**onona. |
| ng'ombe **aliye**konda | ng'ombe **wali**okonda. |

146

Wiki ya 30: Siku ya 1 na 2 **Ndege na Wanyama**

Msichana analisha kuku uwani. Kando kuna nyumba ya kuku.

**Mifugo ya Naliaka: Sehemu ya kwanza**

Naliaka alikuwa mkulima hodari sana. Alifuga ng'ombe, kuku na nguruwe walionona sana. Kila asubuhi Naliaka alisema, "Kuku mweusi nitagie mayai ili nipate kiamshakinywa." Kila mara kuku mweusi alitaga mayai madogo na matamu. Ng'ombe naye alitoa maziwa ya kupikia chai. Naliaka alifurahi na kuwapatia kuku na ng'ombe chakula kingi zaidi. Wote waliendelea kukua vizuri.

147

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U: Tamka silabi **m ku li ma** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mkulima. [U]** Endelea kwa maneno: **ng'ombe, nguruwe, Naliaka, asubuhi, maziwa.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kutaga/nitagie** na **kiamshakinywa, mkulima hodari**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mifugo ya Naliaka Sehemu ya Kwanza"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

### Maswali

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Mkulima Naliaka alifuga wanyama gani?*** *(alifuga ng'ombe, nguruwe na kuku)*
2. ***Kila asubuhi mkulima Naliaka alifanya nini?*** *(alimuuliza kuku amtagie mayai ili apate kutengeneza kiamsha kinywa)*

### Kuandika

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Wanafunzi wayanakili. **ng'ombe, kuku, nguruwe, walionona, asubuhi, maziwa.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike maneno waliyoyaandika tena kisha wawasomee wenzao: **ng'ombe, kuku, nguruwe, walionona, asubuhi, maziwa.**

**Vidokezo vya Mwalimu**
Hakikisha kuwasaidia watoto ambao hawajui kusoma. Wape mazoezi ya kusoma sauti, silabi na maneno mepesi. Baada ya muda mfupi wataanza kusoma kama wengine.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 30: Siku ya 1 na 2 **Ndege na Wanyama**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m ku li ma | ngu ru we | ma zi wa |
| **mkulima** | **nguruwe** | **maziwa** |
| ng'o mbe | Na li a ka | a su bu hi |
| **ng'ombe** | **Naliaka** | **asubuhi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li o nona | ku wa patia |
| **walionona** | **kuwapatia** |
| a li furahi | wa li endelea |
| **alifurahi** | **waliendelea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| ng'ombe **ali**yenona | ng'ombe **wali**onona. |
| nguruwe **ali**yenona | nguruwe **wali**onona. |
| kuku **ali**yenona | kuku **wali**onona. |
| ng'ombe **ali**yekonda | ng'ombe **wali**okonda. |

146

Wiki ya 30: Siku ya 1 na 2 **Ndege na Wanyama**

Msichana analisha kuku uwani. Kando kuna nyumba ya kuku.

**Mifugo ya Naliaka: Sehemu ya kwanza**

Naliaka alikuwa mkulima hodari sana. Alifuga ng'ombe, kuku na nguruwe walionona sana. Kila asubuhi Naliaka alisema, "Kuku mweusi nitagie mayai ili nipate kiamshakinywa." Kila mara kuku mweusi alitaga mayai madogo na matamu. Ng'ombe naye alitoa maziwa ya kupikia chai. Naliaka alifurahi na kuwapatia kuku na ng'ombe chakula kingi zaidi. Wote waliendelea kukua vizuri.

147

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa li o nona** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **walionona** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **a li furahi (alifurahi), ku wa patia (kuwapatia), wa li endelea (waliendelea)**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

◆ **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma katika umoja na wingi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Ng'ombe **ali**yenona. | - | Ng'ombe **wali**onona. |
| Nguruwe **ali**yenona. | - | Nguruwe **wali**onona. |
| Kuku **ali**yenona. | - | Kuku **wali**onona. |
| Ng'ombe **ali**yekonda. | - | Ng'ombe **wali**okonda. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **kutaga** na **kiamsha kinywa** na **mkulima hodari.**

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mifugo ya Naliaka: Sehemu ya kwanza"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Kwa nini Mkulima Naliaka alifurahi na kumpatia kuku chakula kingi?*** *(Kwa sababu kuku alitaga mayai)*
2. ***Ng'ombe hula chakula gani?*** *(majani, nyasi n.k)*
3. ***Unafikiri hadithi hii itaendeleaje?*** *(Wanafunzi wajibu njia tofauti za kuendeleza hadithi)*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **hodari, ng'ombe, alitaga.**

1. **Naliaka alikuwa mkulima __________ sana.**
2. **Naliaka alifuga __________ aliyenona.**
3. **Kuku mweusi __________ mayai.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo. Wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno hayo kisha wawasomee wenzao: **nguruwe aliyenona, kuku walionona, ng'ombe aliyekonda.**

Tarehe: ________________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 30: Siku ya 3 na 4 **Ndege na Wanyama**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| gha la ni | mwe u si |
| **ghalani** | **mweusi** |
| so se ji | ni u a we |
| **soseji** | **niuawe** |
| m ku ta no | dha ti |
| **mkutano** | **dhati** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li kuwa | ni me anza |
| **walikuwa** | **nimeanza** |
| a ka lalamika | a ka fikiria |
| **akalalamika** | **akafikiria** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mimi **nina**zeeka | sisi **tuna**zeeka. |
| mimi **nina**choka | sisi **tuna**choka. |
| mimi **nina**waza | sisi **tuna**waza. |
| mimi **nina**sema | sisi **tuna**sema. |

148

Wiki ya 30: Siku ya 3 na 4 **Ndege na Wanyama**

Kuna kijumba cha kuhifadhi nafaka. Mbele yake kuna nguruwe ameketi. Kuku amesimama mbele ya nguruwe huku wakizungumza. Kando kuna shimo la taka.

**Mifugo ya Naliaka: Sehemu ya pili**

Kuku mweusi na baba nguruwe walikuwa marafiki wa dhati. Siku moja wakawa na mkutano ghalani karibu na shimo la taka. Kuku mweusi akalalamika, "Mimi nimeanza kuzeeka. Nimechoka kutaga mayai kila siku. Mbona wewe hutoi hata angalau soseji moja kwa Naliaka?"
Baba Nguruwe akafikiria kisha akasema kwa huzuni, "Rafiki yangu, kwako wewe kutaga yai ni rahisi sana. Ili mimi nitoe soseji ni lazima niuawe."

149

**Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U: Tamka silabi **gha la ni** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **ghalani**. **[U]** Endelea kwa maneno: **soseji, mkutano, mweusi, niuawe, dhati.**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **ghalani, dhati** na **soseji**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. **[U]** Waulize wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mifugo ya Naliaka: Sehemu ya pili"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. ***Kuku alilalamika kwa nguruwe kuhusu nini?*** *(Mbona wewe hutoi hata angalau soseji moja kwa binadamu?")*
2. ***Nguruwe alimjibu kuku vipi?*** *(Rafiki yangu, kwako wewe kutaga yai ni rahisi sana. Ili mimi nitoe soseji ni lazima nife.")*
3. ***Mbona kuku hakulalamika kwa ng'ombe?*** *(kwa sababu ng'ombe alitoa maziwa kila asubuhi)*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zilizo na mapengo na maneno ya kujaza hayo mapengo. Waagize wanafunzi waandike sentensi kamilifu: **soseji, mweusi, dhati.**

- **i) Kuku ________ alitaga mayai.**
- **ii) Kuku na nguruwe walikuwa marafiki wa ________.**
- **iii) Tafadhali naomba unipikie ________.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye maneno yafuatayo: **soseji, mkutano, mweusi, nimeanza, kuzeeka, dhati**. Wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno hayo kisha wawasomee wenzao.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kitu cha muhimu zaidi katika mradi wa KUSOMA ni kuhakikisha wanafunzi wote wanaweza kusoma vizuri wakimaliza huu mwaka. Je, umeweza kuwasaidia wasome vilivyo?

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 30: Siku ya 3 na 4 **Ndege na Wanyama**

Soma silabi na maneno.

gha la ni
**ghalani**

mwe u si
**mweusi**

so se ji
**soseji**

ni u a we
**niuawe**

m ku ta no
**mkutano**

dha ti
**dhati**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa li kuwa
**walikuwa**

ni me anza
**nimeanza**

a ka lalamika
**akalalamika**

a ka fikiria
**akafikiria**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| umoja | wingi |
|---|---|
| mimi **nina**zeeka | sisi **tuna**zeeka. |
| mimi **nina**choka | sisi **tuna**choka. |
| mimi **nina**waza | sisi **tuna**waza. |
| mimi **nina**sema | sisi **tuna**sema. |

148

Wiki ya 30: Siku ya 3 na 4 **Ndege na Wanyama**

Kuna kijumba cha kuhifadhi nafaka. Mbele yake kuna nguruwe ameketi. Kuku amesimama mbele ya nguruwe huku wakizungumza. Kando kuna shimo la taka.

**Mifugo ya Naliaka: Sehemu ya pili**

Kuku mweusi na baba nguruwe walikuwa marafiki wa dhati. Siku moja wakawa na mkutano ghalani karibu na shimo la taka. Kuku mweusi akalalamika, "Mimi nimeanza kuzeeka. Nimechoka kutaga mayai kila siku. Mbona wewe hutoi hata angalau soseji moja kwa Naliaka?"

Baba Nguruwe akafikiria kisha akasema kwa huzuni, "Rafiki yangu, kwako wewe kutaga yai ni rahisi sana. Ili mimi nitoe soseji ni lazima niuawe."

149

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa li kuwa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **walikuwa** kwa upesi. **[U]** Endelea kwa maneno: **a ka lalamika (akalalamika), ni me anza (nimeanza), a ka fikiria (akafikiria).**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

◆ **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Soma katika umoja na wingi. N/T/U:

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Mimi **nina**zeeka | - | Sisi **tuna**zeeka. |
| Mimi **nina**choka | - | Sisi **tuna**choka. |
| Mimi **nina**waza | - | Sisi **tuna**waza. |
| Mimi **nina**sema | - | Sisi **tuna**sema. |

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **ghalani, dhati** na **soseji**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Mifugo ya Naliaka: Sehemu ya pili"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili.

**Maswali**

[N/T/U] Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Unafikiri ni kwa nini mkutano ulifanyika kwenye ghala karibu na pipa la taka?*** *(kwa sababu nguruwe anapenda takataka/nguruwe anakula uchafu)*
2. ***Kwa nini Nguruwe aliona ugumu kutoa soseji?*** *(Alisema kwake kutoa soseji ni lazima afe)*
3. ***Je, hadithi hii ni ya kweli au la?*** *(wanafunzi wajibu wakitoa sababu zao)*

**Kuandika**

Wapatie wanafunzi kadi za breli zenye sentensi zifuatazo. Wanafunzi wanakili.

1. **mbona hutoi hata soseji**
2. **rafiki yangu kwako wewe kutaga mayai ni rahisi sana**
3. **naliaka alifuga ng'ombe kuku na nguruwe**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Waagize wanafunzi watunge sentensi wakitumia vifungu hivi: **mimi nimechoka, sisi tumewaza; mimi nimesema**. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 30: Siku ya 5 **Ndege na Wanyama**

Tumia silabi kuunda maneno.
Kwa mfano: chu ra - **chura**.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| si | chu | ga | vu | ra |
| ndo | nya | ngu | ti | ku |
| twi | su | i | swa | mba |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| neno | kinyume |
|---|---|
| haraka | polepole |
| ndani | nje |
| tajiri | masikini |
| juu | chini |

Mfalme Simba na Sungura

Wanyama wengi wamekusanyika mtoni. Simba mwenye krauni na sungura wamesimama juu ya daraja. Twiga, pundamilia, nyati na swara wanawatazama.

150

★ **Silabi**

[N] Soma silabi zote zilizo ukurasa ***[ukurasa wa breli unaolingana]*** pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **chu** na **ra** kuandika neno **chura**. [T] Soma neno pamoja na wanafunzi. [U] Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia silabi zilizo ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***.

● **Sarufi**

Eleza wanafunzi wasome kwenye ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. N/T/U: Soma neno na kinyume.

| Neno | | Kinyume |
|---|---|---|
| haraka | - | polepole |
| ndani | - | nje |
| tajiri | - | masikini |
| juu | - | chini |

📖 **Kabla ya kusoma:**

[N] Eleza wanafunzi maana ya msamiati **zamani, aliwatesa** na **akaogelea**. Soma kichwa cha hadithi. Wasomee wanafunzi maelezo. [U] Eleza wanafunzi wajadiliane kuhusu maelezo kisha watoe utabiri wao.

📖 **Kusoma hadithi**

[N] Soma hadithi ya **"Mfalme Simba na Sungura"** huku wanafunzi wakisikiliza kwa makini.

### Mfalme Simba na Sungura

Hapo zamani za kale, Simba alikuwa mfalme wa wanyama wote. Simba alikuwa mkali sana. Aliwatesa na kuwala wanyama wengine. Siku moja wanyama waliamua kutafuta mfalme mwingine. Wanyama wote walikataa kuchukua ufalme. ***Kwa nini wanyama waliamua kumtafuta mfalme mwingine?***

Sungura alijitokeza na kusema, "Mimi niko tayari. Nina mpango wa kuwaokoa. Bora tu mniruhusu niwatawale." Wanyama wote walikubali.

Siku iliyofuata, Sungura alimuambia Simba, "Kuna Simba mwingine mtoni ambaye alitaka kuchukua ufalme wako." Simba alikimbia haraka mtoni bila kufikiria. ***Kwa nini Simba alikimbia mtoni?***

Alipofika juu ya daraja, akatazama chini mtoni. Mara, akaona sura ya Simba majini. Akamrukia. Alijaribu kuogelea lakini akabebwa na maji hadi nchi nyingine ambayo haikuwa na mfalme.

Tangu siku hiyo Sungura akawa mfalme wa wanyama wote. ***Kati ya Simba na Sungura, wewe ungependa kuwa mnyama gani? Kwa nini?***

◈ **Baada ya kusoma**

[N/T/U] Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. ***Mfalme simba aliwafanyia nini wanyama wengine?*** *(aliwatesa na kuwala)*
2. ***Ni nani aliwaokoa wanyama wote?*** *(Sungura)*
3. ***Simba alidanganyika vipi?*** *(watoto waeleze vile Simba alivyodanganyika)*
4. ***Je, unafikiri Sungura alikuwa mfalme mzuri? Eleza jibu lako.***

✍ **Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **ghalani, soseji, ng'ombe, nguruwe, mweusi, dhati, kuzeeka, kuku, asubuhi, chakula**

Hakikisha wanafunzi wanaandika wakizingatia sheria za breli.

**Kazi ya ziada**

Eleza wanafunzi waendelee kuunda maneno zaidi wakitumia silabi walizopewa ukurasa wa ***[ukurasa wa breli unaolingana]***. Baadaye wawasomee wenzao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kiswahili 1

## Mwongozo wa Mwalimu

### Utohozi kwa Walimu wa Wanafunzi wenye Ulemavu wa Kuona

Kitabu hiki cha Kiswahili kimetayarishwa na kuchapishwa chini ya mradi wa TUSOME. Kimeandikwa kufuatia mwongozo wa mawanda na mfuatano uliofanyiwa utafiti wa hali ya juu kwa miaka mitatu katika mradi wa kuboresha ujuzi wa hisabati na usomaji nchini. Utafiti huu uliegemea kubuni njia mwafaka za kufunza usomaji na ufahamu.

Vipengele muhimu na vya kipekee kuhusu hiki kitabu ni:

- Kitabu hiki kinafuata mtaala wa taifa la Kenya.
- Mazoezi ya somo yamefuata mpangilio wa mantiki kutokana na utafiti wa njia bora za kufunza Kiswahili katika darasa la kwanza na la pili.
- Masomo katika kitabu hiki hujumuisha vijenzi vyote vya lugha ambavyo ni; kusikiza, kuongea, kusoma na kuandika.
- Mpangilio wa kitabu hiki umekusudia kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa uzoefu kwa sababu kinawapatia nafasi ya kukumbana na vijenzi vyote vya kusoma.

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.

Juni 2016